# UTAIFA WA JAMII YA AKAMBA KATIKA NYIMBO PENDWA ZA KEN WA MARIA

**MUNYAO JOSEPHINE KANINI**

**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Shule ya Mafuzu kwa Minajili ya Kutosheleza baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili na Mawasiliano, Chuo Kikuu cha Laikipia**

**OKTOBA, 2025**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi……………………………………. Tarehe…………………………

**Munyao Josephine Kanini**

**MDK32/2586/19**

## IDHINI YA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Laikipia.

Sahihi ……………………………………………. Tarehe…………………………….

**Prof. Wendo Nabea**

**Idara ya Usomilugha na Mawasiliano**

**Chuo Kikuu cha Laikipia**

Sahihi ……………………………………………. Tarehe…………………………….

**Prof. Sheila Pamela Wandera-Simwa**

**Idara ya Usomilugha na Mawasiliano**

**Chuo Kikuu cha Laikipia**

## HAKIMILIKI

**@2025, Munyao Josephine Kanini**

Haki zote zimehifadhiwa. Huruhusiwi kuiga, kunakili, kupigisha chapa, kutafsiri au kutoa sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Laikipia kwa niaba ya mwandishi.

## TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu Peter Munyao Ndolo, Naomi Itumbi Munyao na Lilian Wambui Wahome, mume wangu Wahome Kimondo na wanangu Leon, Wambui na Wahome. Mwanzo wa ngoma ni lele.

## SHUKRANI

Ninamshukuru Rabuka ambaye ameniwezesha kufanikisha kazi hii. Tasnifu hii ni zao la mchango wa wahusika kadhaa. Sina budi kuwatambua baadhi yao ambao walifanikisha kazi hii. Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu mahiri, Maprofesa Wendo Nabea na Sheila Wandera Simwa. Nisitosahau kikao chetu cha kwanza. Nilikuwa nimetamauka lakini mkanipa moyo nizidi kupiga hatua. Nawashukuru kwa stahamala yenu, uelekezi, nasaha na kule kujitolea kwenu katika kuisahihisha kazi yangu hadi tukafika ukingoni. Mlinipa moyo kwa uelekezi wenu wa kila mara ambao uliifaa kazi hii. Subira yenu haimithilishwi na chochote. Mwenyezi Mungu awazidishie baraka na siha njema, mwafae wengine kama mlivyonifaa mimi.

Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Laikipia kwa kunipa fursa kwa mara ya pili kukiendeleza kisomo changu chuoni humo. Wahadhiri wangu ambao tulitangamana nao darasani na nje ya darasa pokeeni shukrani zangu. Hawa ni pamoja na Profesa Felicia Yieke, Profesa James Ogola Onyango, Dkt. Muthoka Mutie na wengineo. Nasaha na uelekezi wenu kwa hakika ulinitia makali na kuwezesha kufanikisha kazi hii. Dkt. Severina Mwirichia (KeMU), mchango wako hauwezi kamwe kusahaulika.

Ninawashukuru masahibu wangu wasomi ambao tulihimizana, kucheka, kulizana na kufarijiana pamoja tulipokuwa katika safari hii. Kila mara tulikumbushana kuwa safari ya hatua nyinyi huanza kwa hatua moja. Tumestahimili mengi na hakika mlichangia kwa njia kuu kazi hii. Sitawasahau Dkt. Kimathi Mwembu, Dkt. Julius Chepkwony, Bw. Chomba Mugane, Emmanuel Kiio, Cecilia Gikong’a, Carolyne Ng’etich, Jacqueline Wanjiku na wengineo. Geoffrey Ndichu, asante kwa kuhakikisha kuwa niliwasilisha kazi yangu kwa wakati. Pia, sitaisahau familia yangu ambayo ilinitia moyo kila mara wakati nikiandaa kazi hii. Ilikuwa vigumu lakini mkaifanya kuwa nyepesi. Laazizi wangu Kimondo Wahome, asante sana kwa kuhakikisha kuwa wanetu hawakukosa penzi na uelekezi wa mzazi wakati nilipokuwa nimezamia kazi hii. Wanangu Leon Mwendwa, Wambui Kimondo na David Wahome, utulivu wenu na uelewa mlipokosa uwepo wa mama haumithilishwi. Kwa wazazi wangu wapendwa, asanteni sana kwa kunishajiisha kila mara nifuate ndoto yangu. Kazi hii ni yenu. Njooni tusherehekee pamoja.

# IKISIRI

Utaifa wa jamii ni mambo yanayowaunganisha watu kuwa taifa moja. Ni hali ya watu kuishi katika nchi moja na kuunganika kutokana na matukio ya kihistoria, mfumo wa kiuchumi na kiutamaduni chini ya serikali moja. Utaifa wa jamii hujitokeza katika tanzu mbalimbali za sanaa. Wanadamu hutumia fasihi yao kuendeleza utaifa wa jamii ili kuelezea asili yao, changamoto zinazowakabili, maadili ya jamii yao, maono na ushindi wao. Mwanamuziki kama kiwakilishi cha jamii yake hutumia mtindo wa kipekee wa lugha kuendeleza maudhui ambayo huelezea falsafa ya jamii na matamanio ya jamii yake yakiwemo suala la utaifa wa jamii. Hata hivyo, fasihi simulizi imechukuliwa kama finyu na ni wanazuoni wachache ambao wameipa uzito wa kifasihi kueleza suala la utaifa wa jamii. Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza jinsi nyimbo pendwa za mwanamuziki Ken wa Maria zinavyoendeleza utaifa wa jamii ya Akamba. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza arki za utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria, kuhakiki mbinu za kimtindo zinazotumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria na kupambanua changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba kwa mujibu wa nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; kwanza ni nadharia ya utaifa iliyoasisiwa na David Smith. Nadharia ya utaifa hueleza kwamba ili utaifa wa jamii uwepo lazima jamii hiyo iweze kumiliki utamaduni mmoja, lugha, imani ya dini na historia. Utafiti huu pia ulielekezwa na nadharia ya umitindo iliyoasisiwa na Leech pamoja na Short. Nadharia ya umitindo huchunguza namna msanii wa fasihi hutumia lugha kwa namna ya kipekee ili kumwezesha kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Mihimili ya nadharia hizi ndiyo iliyoelekeza utafiti huu wakati wa kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha data kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Utafiti huu ni wa kimaelezo. Utafiti huu ulifanyiwa katika maktaba ili kupata data. Sampuli ya kimakusudi ilitumika ili kupata nyimbo 24 ambazo zilipakuliwa kutoka mtandao wa *YouTube* na *Mdundo.com*. Nyimbo hizi zilitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kisha kuchanganuliwa ili kubainisha arki za utaifa wa jamii ya Akamba, mbinu za kimtindo alizotumia msanii Ken wa Maria na changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba. Data ilichanganuliwa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti huu na matokeo yake kufafanuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Uwasilishaji wa data ya utafiti ulifanywa kwa njia ya kimaelezo. Utafiti huu ulibaini kwamba kunazo arki za utaifa katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria kama vile utambulisho wa kiuana na kijamii, utamaduni, historia na ikolojia. Pia, utafiti huu ulionyesha jinsi mbinu za kimtindo kama vile jazanda, methali, istiari na aforisimu zinavyotumiwa na msanii kujenga utaifa wa jamii ya Akamba. Isitoshe, utafiti huu ulibainisha kuwa utaifa wa jamii ya Akamba unakumbwa na changamoto kama vile kuzuka kwa utambulisho mpya na utandawazi. Utafiti huu ulionyesha nafasi ya nyimbo pendwa katika makuzi ya utaifa wa jamii. Utafiti huu utaongezea maarifa ya kinadharia kuhusu kipera cha nyimbo katika fasihi simulizi. Pia, utawafaidi watafiti wa fasihi simulizi katika kutambua mchango wa nyimbo pendwa katika fasihi simulizi. Aidha, utafaidi mashirika ya kikatiba yaliyopewa jukumu la kuendeleza maadili ya kitaifa na utamaduni tajiri wa Kenya kama vile Makavazi ya Kitaifa ya Kenya na Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano wa Kenya, katika kutambua umuhimu wa nyimbo pendwa katika kukuza maadili ya kitaifa na kuhifadhi tamaduni za kikabila.

## ABSTRACT

Ethno-nationalism is the identification with one's own ethnic nation. It is a shared attachment amongst people of one ethnic group based on governance, history, economic and cultural activities. Ethno-nationalism manifests itself through different genres of art. The Ethno-nation uses literature to express their common origin, threats, values, vision and achievements. The artist, being the mouthpiece of a community uses stylistic devices to develop themes which communicate the community's philosophy and nationalistic aspirations. However, oral literature has been stereotyped as a rural concept and few scholars have given it serious literary attention to express ethnonationalism. The aim of this study was to investigate how selected popular songs by Ken wa Maria promote ethno-nationalism among the Akamba community. The specific objectives of the study were: To explore elements of ethno-nationalism in Ken wa Maria's popular songs, to examine literary devices used by Ken wa Maria in his popular music to promote ethno-nationalism among the Akamba and to analyze the challenges facing Kamba nationalism in selected Ken wa Maria's popular songs. This study was guided by two theories; nationalism theory whose proponent is David Smith. The theory argues that for ethno-nationalism to develop, the community must have a shared culture, religious beliefs, history and language. The study also adopted the stylistics theory whose proponent is Leech and Short. The stylistics theory holds that language is a significant ingredient in literature. It also argues that the writer uses unique language style to convey the message to the audience. The tenets of these theories were used in collecting and analyzing data in regard to the research objectives. The study was descriptive library-based research. The researcher used purposive sampling to identify 24 popular songs by Ken wa Maria which were downloaded from *YouTube* and *Mdundo.com.* The songs were transcribed and translated to Kiswahili. An analysis of the elements of ethno-nationalism, stylistic devices and challenges of ethno-nationalism were conducted. Data was analyzed qualitatively in view of the research objectives. This study established that there were elements of ethno-nationalism in Ken wa Maria's songs such as Kamba cultural practices, gendered identity, history and geographical mapping. The study also revealed how the stylistic choices in contextual usage contribute to the promotion of ethno-nationalism among the Akamba. Additionally, the study revealed that the Akamba ethno-nationalism is facing a number of challenges such as emerging new identities, globalization and internal oppression. The findings of this research illuminate the significance of popular music in the development of ethno-nationalism. The study will contribute to the theory of music in oral literature. It will benefit scholars of oral literature to establish the emerging themes in popular music. It is also bound to benefit constitutional bodies mandated to promote national values and Kenya's rich culture such as the National Museums of Kenya and the National Cohesion and integration Commission of Kenya in establishing the significance of popular songs in the promotion of national values and conservation of ethnic cultures.

# YALIYOMO

UNGAMO ..................................................................................................... ii
IDHINI YA WASIMAMIZI ..................................................................................... ii
HAKIMILIKI .............................................................................................................. iii
TABARUKU ................................................................................................................ iv
SHUKRANI.................................................................................................................. v
IKISIRI ........................................................................................................................ vi
ABSTRACT ................................................................................................................. vii
AKRONIMU NA VIFUPISHO VYA MANENO ................................................ xi
UFAFANUZI WA ISTILAHI .................................................................................... xii
SURA YA KWANZA.................................................................................................. 1
UTANGULIZI............................................................................................................... 1
1.1 Usuli wa Mada ........................................................................................................ 1
1.1.1 Nyimbo na Utaifa.................................................................................................. 3
1.2 Suala la Utafiti ........................................................................................................ 8
1.3 Madhumuni ya Utafiti ............................................................................................ 8
1.4 Maswali ya Utafiti .................................................................................................. 8
1.5 Umuhimu wa Utafiti............................................................................................... 9
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ..................................................................................... 10
SURA YA PILI............................................................................................................. 12
MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA ............................ 12
2.1 Utangulizi................................................................................................................ 12
2.2 Arki za Utaifa ......................................................................................................... 12
2.3 Mbinu za Kimtindo ................................................................................................ 16
2.4 Changamoto za Utaifa............................................................................................ 21
2.5 Misingi ya Nadharia ............................................................................................... 23
2.5.1 Nadharia ya Utaifa ............................................................................................... 24
2.5.2 Nadharia ya Umitindo .......................................................................................... 25
2.6 Hitimisho ................................................................................................................ 27
SURA YA TATU.......................................................................................................... 28
MBINU ZA UTAFITI.................................................................................................. 28
3.1 Utangulizi................................................................................................................ 28
3.2 Muundo wa Utafiti ................................................................................................. 28
3.3 Eneo la Utafiti......................................................................................................... 28
3.4Walengwa wa Utafiti .............................................................................................. 29

**3.5 Uteuzi wa Sampuli ..... 29**
**3.6 Ukusanyaji Data ..... 30**
**3.7 Uchanganuzi wa Data ..... 30**
**3.8 Uwasilishaji wa Data ..... 31**
**3.9 Maadili Wakati wa Utafiti ..... 31**
**SURA YA NNE ..... 32**
**UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA ..... 32**
**4.1 Utangulizi ..... 32**
**4.2 Usawiri wa Arki za Utaifa wa Jamii ya Akamba ..... 33**
**4.2.1 Arki ya Utamaduni ..... 33**
**4.2.1.1 Usawiri wa Ndoa ..... 34**
**4.2.1.2 Imani za Kijamii ..... 44**
**4.2.1.3 Vyakula ..... 49**
**4.2.1.4 Shughuli za Kiuchumi ..... 53**
**4.2.2 Arki ya Utambulisho ..... 56**
**4.2.3 Arki ya Siasa na Uongozi ..... 60**
**4.2.4 Arki ya Jiografia ..... 67**
**4.2.5 Arki ya Historia ..... 69**
**4.3 Uhakiki wa Mbinu za Kimtindo Zinazojenga Utaifa wa Jamii ya Akamba ..... 75**
**4.3.1 Usimulizi ..... 77**
**4.3.2 Takriri ..... 85**
**4.3.3 Chuku ..... 90**
**4.3.4 Misemo ..... 91**
**4.3.5 Methali ..... 95**
**4.3.6 Jazanda ..... 96**
**4.3.7 Aforisimu ..... 103**
**4.3.8 Taswira ..... 105**
**4.3.9 Mbinu ya Ulinganuzi na Mgotanisho ..... 110**
**4.3.10 Majazi ..... 111**
**4.3.11 Matumizi ya Motifu ..... 113**
**4.4 Changamoto Zinazokumba Utaifa wa Jamii ya Akamba ..... 115**
**4.4.1 Kuzuka kwa Utambulisho Mpya ..... 116**
**4.4.2 Athari za Utandawazi ..... 120**
**4.4.3 Uhamiaji ..... 123**

**4.4.4 Ukandamizwaji wa Ndani ........................................................................... 125**
**4.4.5 Ukosefu wa Usemi Mkuu Kisiasa................................................................ 126**
**4.4.6 Ukosefu wa Umoja wa Kijamii................................................................... 127**
**4.4.7 Siasa za Utengano ....................................................................................... 129**
**4.4.8 Usaliti wa Kisiasa........................................................................................ 131**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..................................................... 133**
**5.1 Utangulizi.......................................................................................................... 133**
**5.2 Muhtasari wa Tasnifu ...................................................................................... 133**
**5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ................................................................... 134**
**5.4 Hitimisho .......................................................................................................... 137**
**5.5 Mapendekezo.................................................................................................... 138**
**MAREJELEO ........................................................................................................... 140**
**VIAMBATISHO ........................................................................................................ 156**
**KIAMBATISHO 1: BARUA YA UTAFITI ............................................................ 156**
**KIAMBATISHO 2: KIBALI CHA NACOSTI ......................................................... 157**
**KIAMBATISHO 3: NYIMBO PENDWA ZA KEN WAMBUA NGUNZE (Ken wa Maria)……………………………………………………………………………………..158**

## AKRONIMU NA VIFUPISHO VYA MANENO

**AF** –Aforisimu

**AR** – Arki za utaifa

**CH** – Changamoto za ujenzi wa utaifa

**Ch** – Chuku

**H** – Historia

**J** – Jiografia

**JZ** – Jazanda

**M -** Mshororo

**MB** – Mbinu za kimtindo

**MJ** – Majazi

**MO** – Motifu

**MS** –Misemo

**MT**- Methali

**S** – Siasa na uongozi

**SL** – Usaliti wa kisiasa

**SM** – Usimulizi

**T** – Takriri

**TS**- Taswira

**U**- Utamaduni

**UH -** Uhamiaji

**UJ** – Ukosefu wa umoja wa kijamii

**UK** – Ukandamizwaji wa ndani

**UM -** Ulinganiisho na Mgotanisho

**US-** Ukosefu wa usemi mkuu kisiasa

**UT** – Utambulisho

**UTM** – Utambulisho mpya

**UZ -** Athari za utandawazi

**W** – Wimbo

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

**Arki za Utaifa:** Vipengele vinavyojenga utaifa wa jamii kama vile lugha, utamaduni, historia ya Pamoja, jiografia, siasa na uongozi na uchumi.

**Changamoto za utaifa:** Masuala au vikwazo ambavyo vinaathiri maendeleo ya umoja wa jamii ya Akamba.

**Nyimbo pendwa**: Ni aina ya muziki unaosambazwa kwa wingi kupitia njia mbalimbali za mawasiliano na vyombo vya habari, unaolenga kuvutia hadhira kubwa na husheheni maudhui mepesi na ya moja kwa moja. Muziki huu hujulikana kwa urahisi wa kueleweka na kuimbika, na huwa sehemu ya utamaduni maarufu unaoakisi mitindo, maadili, na changamoto za kijamii za kizazi fulani

**Taifa:** Jamii ya watu wanaoishi katika nchi moja na wanaoungana kupitia matukio ya kihistoria, mfumo wa uchumi na utamaduni chini ya uongozi wa serikali moja. Ni mfumo wa ndani ulioendelea wa mawasiliano ambao hujenga hisia ya utambulisho sawa miongoni mwa watu tofauti. Jamii ya Akamba ni taifa.

**Utaifa:** Mambo ya mila, lugha, dini na utamaduni, ambayo yanawaunganisha watu kuwa taifa moja.

**Utaifa wa jamii (ethno-nationalism)**: Ni uzalendo wa watu katika jamii unaohusisha utiifu kwa jamii ambalo mtu lazima awe na asili nalo. Ni utaifa unaotokana na ufahamu wa pamoja wa kibinafsi ambapo watu hujiona kuwa sehemu ya kitu kikubwa zaidi. Katika utafiti huu, istilahi hii imetumiwa kurejelea utaifa wa jamii ya Akamba. Msamiati ukabila umeepukwa kwa sababu unaweza kuzua hisia hasi ambazi hazilengwi na utafiti wenyewe.

**Utamaduni:** Mila, desturi, asili, imani na itikadi za jamii ya Akamba

**Utambulisho:** Ni sifa, hisia ama imani ambazo humtofautisha Mkamba na mwenzake

**Uzalendo:** Mapenzi makubwa aliyonayo mtu kwa jamii yake: utashi wa pamoja wa kutetea kitu au jambo lenye maslahi ya jamii ya Akamba

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Pana watu wengi ulimwenguni wanaoishi katika mataifa mbalimbali. Watu hawa huwa na ukuruba kupitia misingi ya damu, rangi ya ngozi, tamaduni zao, asili, dini na maeneo wanayoishi. Ingawa wote ni waja wa ulimwengu pana, suala la utaifa huweza kuunganisha baadhi yao na wakati huo huo kuwatenganisha na watu wengine. Kwa mfano, pana watu wengi ulimwenguni ambao huwa na mnasaba kupitia dhamani fulani katika jamii.

Utaifa ni jambo muhimu kwa sababu ndio huleta mshikamano miongoni mwa watu. Ni mchakato ambao huleta pamoja watu wa itikadi, tamaduni, imani, kabila na tabaka tofauti tofauti ili kuunda taifa moja. Utaifa ni hali ya jamii kuwa na amani, usawa na ufahamu juu ya kitambulisho kimoja baina ya wananchi. Hii inachukuliwa kuwa hata watu wawe na makabila, dini, maeneo na ndimi tofauti tofauti, bado ni kitu kimoja. Jamii ambayo imetangamana pamoja aghalabu hufurahi kuishi kwa amani, uthabiti, maendeleo na utendaji kazi mwema.

Utaifa ni mambo ya: Mila, lugha, dini, siasa, uchumi na elimu ambayo huwaunganisha watu na kuwafanya kuwa taifa moja. Vilevile, utaifa unajitokeza katika watu wakati wanapokuwa na utashi wa pamoja wa kutetea kitu au jambo lenye maslahi yao. Hivi ni kusema kwamba, ujenzi wa utaifa hushirikisha vipengele chungu nzima, vikiwemo nyimbo pendwa na waimbaji wake, mradi tu nyimbo husika ziwe zinatumika kuwaunganisha watu ili wawe na mielekeo sawa kuhusu taifa lao; huku zikiwatia utashi wa kupenda na kutetea maslahi yao. Utaifa ni suala changamano kwa kuwa huwa na sura nyingi. Ni mchanganyiko wa historia, tamaduni na utambulisho ambao hujidhihirisha kwa njia tofauti tofauti (Smith, 2010).

Utaifa unaweza kuainishwa katika makundi mawili makuu katika mataifa yaliyowahi kutawaliwa na wakoloni; utaifa wa kimaeneo na utaifa wa kikabila. Utaifa wa kimaeneo una sura mbili; utaifa kabla ya uhuru na baada ya uhuru. Utaifa wa kabla ya uhuru ulinuia kuwaondoa wakoloni ili kujenga taifa jipya. Utaifa baada ya uhuru uliazimia kuleta makabila yote pamoja ili kujenga jamii moja ya kisiasa au nchi huru. Utaifa wa kikabila

pia umetokea kwa njia mbili kabla na baada ya uhuru. Katika utaifa wa kikabila kabla ya uhuru, makabila yalijitenga na kila kabila likajenga utaifa wao binafsi. Baada ya uhuru, makabila yaliyojitenga yalipanua mahusiano yao kwa kuwajumuisha watu wa kabila lao walioishi nje ya maeneo yao ili kukuza zaidi utaifa wa kikabila (Smith, 2010).

Kuna uhusiano kati ya utaifa na taifa. Utaifa ndio unaowajumuisha watu wote wa taifa moja ili kuwa kitu kimoja. Ni mvuto wa kuwaleta pamoja watu wa matabaka mbalimbali na kuishi kwa amani kama jamii moja (Mung'ala, 2020). Taifa ni jamii ya watu wanaoishi katika nchi moja na wanaoungana kupitia matukio ya kihistoria, mfumo wa uchumi na utamaduni chini ya uongozi wa serikali moja. Ni jamii ya watu wenye historia moja, fasihi simulizi sawa, utamaduni mmoja, wenye njia sawa za kiuchumi na majukumu bainifu na haki sawa kwa kila mwanajamii. Aidha, taifa ni mfumo wa ndani ulioendelea wa mawasiliano ambao hujenga hisia ya utambulisho sawa miongoni mwa watu tofauti (Breuilly, 1995). Jamii yenye utaifa huwa imezinduka kisiasa na huweza kuwasiliana wenyewe kwa wenyewe iwapo watu wako mbali na karibu kuhusu masuala mbalimbali. Uwezo wa kuwasiliana hufaulu sana iwapo jamii itatumia lugha moja, dini na imani sawa, kumbukumbu ya kihistoria inayolingana pamoja na utamaduni sawa.

Kuna aina mbili za taifa. Kwanza kuna taifa la kisiasa ambalo linajengwa kupitia kwa nia au maamuzi huru na unyenyekevu wa raia kwa taifa yaani demokrasia. Kwa mfano Ufaransa, Marekani na Uingereza ambapo raia hujitambulisha kwa chama cha kisiasa. Pili ni taifa kupitia urathi wa utamaduni. Wasomi kama vile Ozkirimli (2010), Smith (2010), na Llobera (1999), wanaonyesha kwamba utaifa hujengwa kupitia masuala mbalimbali. Haya ni pamoja na lugha ambayo watu wanatumia katika eneo moja. Vile vile wanaweza kuwa na historia moja kupitia visasili vyao. Kadhalika, wanaweza kuwa ni sehemu ya kijiografia wanakoishi na kukabiliana na hali za kimazingira ziwe nzuri au mbaya. Vilevile, utaifa utaunaweza kujengwa kupitia sanaa kama vile fasihi.

Mojawapo ya vipera muhimu vya fasihi ambavyo hujenga utaifa wa jamii ni nyimbo. Hii ni kwa sababu nyimbo zinahamasisha watu katika umoja wao. Japo nyimbo ni za aina mbalimbali, mojawapo ya aina za nyimbo ambazo hujenga utaifa ni nyimbo pendwa. Licha ya nyimbo kuwa na mafunzo na burundani, ni kigezo muhimu cha kujenga utaifa miongoni mwa jamii mbalimbali. Hata hivyo, pana data finyu kuhusu jinsi nyimbo zimechangia

katika suala hilo. Utafiti huu ulinuia kuchunguza nyimbo za Ken wa Maria kama vijenzi vya utaifa miongoni mwa jamii ya Akamba.

### 1.1.1 Nyimbo na Utaifa

Nyimbo ni mojawapo wa kipera kikuu katika utanzu wa ushairi simulizi (Wamitila, 2003). Nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka, hutungwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya taswira na mapigo ya silabi. Nyimbo huchukua sehemu kubwa katika miviga ya jamii mbalimbali, hivyo ni muhimu sana katika jamii yoyote ile. Kando na hayo, Wamitila (keshatajwa), anasema kuwa nyimbo huwa na mawazo mazito yanayotumiwa kudhihirisha uhusiano wa kijamii, mgogoro, kejeli, kuliwaza na kutumbuiza. Akishadidia kauli hii, Kanyange (2015), anasema kuwa yamkini shughuli zote za binadamu ziwe za kiuchumi, kisiasa au kijamii huandamana na nyimbo. Msomi huyu anaendelea kusema kuwa, kila shughuli huwa na aina yake ya nyimbo maalum. Owino (2011), anaongezea kuwa wimbo ni muungano wa sauti zenye athari changamano kwa msikilizaji. Sauti hizi zina uwezo wa kueleza yaliyopo na kudokeza yajayo. Nyimbo pia, huwasilisha hisia mbalimbali kama vile upendo, chuki, ukandamizwaji, umoja, utambulisho na ukombozi wa jamii fulani. Nyimbo hujikita katika utamaduni mahususi unaozingatiwa na jamii yenye idadi fulani ya watu katika eneo fulani. Wasanii wanaotunga nyimbo huwa ni sehemu ya jamii kwa hivyo, hujinasibisha na jamii husika.

Ngugi (2000), anafafanua nyimbo kwa kusema kuwa, kama ilivyo fasihi kwa jumla, lengo kuu la nyimbo ni kuelimisha na pia kutoa burudani kwa wanajamii. Msomi huyu anaendelea kueleza kuwa nyimbo huwa na fursa kubwa ya kufikia watu wengi ikilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi. Hii ni kwa sababu wasanii wengi wa utanzu huu hutumia lugha za kiasili kupitisha ujumbe. Vilevile, Ngugi (keshatajwa), anaeleza kuwa vyombo vya habari nchini Kenya vimeipa fasihi hii nafasi kubwa sana, hivyo basi kupanua hadhira yake. Aidha, msomi huyu anaeleza kuwa nchini Kenya, wanamuziki wamegawanyika katika makundi mbalimbali ambayo ni: watendaji wa muziki wa bendi, kwaya, taarabu na watendaji wa muziki wa kiasili. Anasisitiza kwamba karibu kila kundi hutumia lugha ya Kiswahili linapokuwa na ujumbe maalam kwa wananchi wote nchini. Maoni haya yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa nyimbo za msanii Ken wa Maria

zilizochunguzwa ni zile huimba kwa Kikamba anapotaka kuwasilisha dhana ya utaifa kwa jamii ya Akamba.

Akizungumzia suala la nyimbo, Musembi (2016), anaesema kuwa ni kipera cha fasihi simulizi kinachotekeleza majukumu muhimu katika jamii zaidi ya kipera kingine chochote cha fasihi simulizi. Akishadidia kauli hii, Mbarwa (1989), anasema kwamba nyimbo zinatekeleza dhima muhimu katika jamii kwa kupitisha ujumbe kuhusu maoni fulani, mitazamo na mielekeo ya watu kuhusu masuala mbalimbali yanayogusa jamii. Mbarwa (keshatajwa) anaendelea kufafanua kwamba nyimbo ni ala muhimu za mawasiliano ambazo hutumia maneno katika muundo wa tamathali za usemi ili kupitisha ujumbe kwa walengwa wake. Kwa mujibu wa Mbiti (1991), nyimbo, methali na hekeya hupatikana katika jamii nyingi za Kiafrika. Fani hizi hutokea katika kipindi maalum zikiwa zimebeba ujumbe bainifu. Msomi huyu anaendelea kushikilia kwamba nyimbo husheheni maudhui mahususi kuhusiana na nyanja mahususi za maisha.

Nyimbo ni chombo kinachotumika na wanajamii kueleza fikra na hisia, na pia kufafanua yaliyomo katika nyoyo ili kutoa hisia zitokanazo na kadhia zinazotokea katika jamii. Kadhia hizi ni pamoja na matukio ya furaha, mateso, migogoro, utangamano, ujenzi wa utaifa na maendeleo ya jamii kwa jumla (Silau, 2003). Msomi huyu anashikilia kuwa, nyimbo huvutia mwimbaji pamoja na hadhira yake, kiasi kwamba hutekenya nyoyo zao na kuacha alama kwenye akili zao ambayo haiwezi kufutika vivi hivi.

Wakizungumzia kuhusu dhima ya nyimbo, Njogu na Chimerah (1999), wanadahili kwamba nyimbo na mashairi simulizi ndiyo yalikuwa vitabu na magazeti ya wanajamii ambao hawakuwa na maandishi. Wataalamu hawa wanaendelea kuhoji kwamba, nyimbo na mashairi ni vipera viwili vya fasihi simulizi ambavyo vilitumiwa kwa wingi kuhifadhi sheria, historia, jiografia na sosholojia. Vipera hivi vilifanya hivi kwa kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (keshatajwa), amali muhimu za kijamii kama vile majukumu ya kiuana, kashfa, ndoa, na masuala ya kimapenzi yalihifadhiwa katika kipera cha nyimbo. Kauli hii inashadidiwa na Musembi (keshatajwa), anaposema kwamba, nyimbo huchukua sehemu kubwa ya maisha ya binadamu. Mtaalamu huyu anashikilia kuwa takriban shughuli zote za maisha ya binadamu kama kulima,

kuvuna, kujenga, kubembeleza mtoto, kupasha tohara na kutambulisha jamii huandamana na nyimbo.

Ngure (2003), anafafanua sifa za nyimbo na vipengele vinavyozingatiwa na watunzi wa nyimbo ili kupitisha ujumbe kwa hadhira husika. Kulingana na mwanafasihi huyu, nyimbo hubeba mawazo, fikra, falsafa na hisia za msanii katika kuziwasilisha kwa walengwa wake. Ngure (keshatajwa), anaendelea kuhoji kuwa wimbo unaweza kuhusiana na hali za kawaida za maisha, utamaduni, siasa, dini, elimu na mazingira. Vipengele hivi ni muhimu katika uchanganuzi wa ujumbe wa mwimbaji. Wakiunga mkono kauli hii, King'ei na Kisovi (2005), wanasema kuwa nyimbo zimeenea miongoni mwa jamii mbalimbali na huimbwa kuambatana na shughuli tofauti. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, nyimbo zimegawika katika makundi mawili makuu: nyimbo za kimapokezi na zile za kisasa. Nyimbo za kimapokezi hupokezwa kizazi hadi kingine. Nyimbo pendwa huwa chini ya kundi kuu la nyimbo za kisasa. Nyimbo za kisasa huwa na lengo kuu ambalo ni kuchuma mali. Wasomi hawa wanaendelea kusema kuwa nyimbo za kisasa zina uwazi mwingi, maneno yasiyo na adabu na midudo yake imesheheni ucheshi si haba.

Nyimbo pendwa ni aina ya nyimbo zinazopendwa na umma kwa wingi. Ni sehemu ya sanaa pendwa ambayo huwasilishwa kwa njia inayoifanya ipendwe na kushabikiwa na watu (TUKI, 2006). Kwa mujibu wa Coates (2003), nyimbo pendwa huwa mojawapo wa sehemu ya nyimbo zinazoimbwa kwa mitindo maarufu na inayoheshimiwa kama vile muziki wa roki. Akifafanua nyimbo pendwa, Keightley (2001) analinganisha hadhi ya nyimbo pendwa na zile za roki, ambapo anahitimisha kwamba nyimbo pendwa huchukuliwa kulenga masuala ya utamaduni huku nyimbo za roki zikifikiriwa kuwa na ujumi zaidi, hivyo kuonekana kuwa na thamani zaidi ya nyimbo pendwa. Akishadidia kauli hii, Silau (keshatajwa) anasema kuwa watu hushabikia nyimbo mbalimbali kwa kutegemea kile kinachowaridhisha na kuwafurahisha kutokana na nyimbo husika. Msomi huyu anaendelea kuhoji kwamba nyimbo pendwa hushabikiwa na kupendwa na watu wengi, ndiyo maana hujulikana kwa jina 'nyimbo pendwa'. Maoni ya wataalamu hawa yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu yalitoa mwanga kuhusu dhima ya nyimbo pendwa kwa kutambua kuwa zinalenga masuala ya kitamaduni ambayo yanajumuisha mojawapo wa arki zinazojenga utaifa wa jamii ya Akamba.

Nyimbo pendwa husaidia wasikilizaji na waimbaji wake kukabiliana na changamoto na shinikizo za maisha. Wanajamii hupata fursa ya kujifahamisha mambo kadha wa kadha ambayo yanashirikisha ujenzi wa utaifa. Mambo haya ni pamoja na kujifunza namna ya kupinga na kukataa kwa dhati matakwa yanayolazimishiwa jamii fulani. Vilevile, nyimbo pendwa hutumiwa kujenga jamii yenye utaifa imara (Fritzsche, 2004; Weekes, 2004). Katika hali hii, nyimbo pendwa huwa chombo muhimu cha kutambulisha wanajamii husika kwa njia iliyo madhubuti na yenye heshima. Maoni ya wataalamu hawa yalikuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kuwa yalisaidia mtafiti kuelewa jinsi utaifa wa jamii ya Akamba unavyojengwa kupitia nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria.

Akizungumzia nyimbo pendwa, Acres (2014), anasema kwamba ni aina ya nyimbo zinazopambwa na vitu vingi vilivyo nje ya kiini chake. Mtaalamu huyu anaendelea kuhoji kuwa nyimbo pendwa hupambwa na maleba, utendaji, mazingira ya kijiografia, usuli wa msanii na historia ya jamii kwa jumla. Hivi ni kusema kwamba, kama ilivyo fasihi nyingine, nyimbo pendwa huwa ni zao la mchakato mzima wa binadamu wa kupambana na hali mbalimbali za maisha. Acres (keshatajwa), anajaribu kuweka mpaka baina ya nyimbo pendwa na muziki pendwa kwa kusema kuwa chanzo cha muziki pendwa ni nyimbo pendwa; bila nyimbo pendwa hakuna muziki pendwa. Maoni ya msomi huyu yanaungwa mkono na Szekely (2006) kwa kusema kuwa wataalamu hawapaswi kuuliza swali ikiwa wimbo ni wimbo pendwa au la, lakini waulize ni kwa kiasi gani kipengele cha muziki pendwa kinadhihirika katika wimbo fulani. Maoni ya wataalamu hawa yanatuelekeza kufahamu kwamba utengano baina ya dhana ya nyimbo pendwa na muziki pendwa upo katika vile vinyago na mapambo ya kila aina yanayoshirikisha muziki pendwa. Vinyago na mapambo haya hubadilika kutoka muziki pendwa mmoja hadi mwingine, na kutoka wakati na kizazi kimoja hadi kiingine, ilhali wimbo pendwa hubakia kuwa wimbo pendwa (Tagg, 1994).

Ngugi (2000) katika makala yake ya nafasi ya muziki uliopendwa katika fasihi ya Kiswahili anaeleza kuwa, muziki uliopendwa uliibuka katika kipindi cha majilio ya wazungu wakati Kenya ilishuhudia nyimbo nyingi za kutoka nje na ambazo zilianza kuonewa fahari. Hii ni kwa sababu wazungu walipofika, walimdhalilisha mwafrika na kumteka kimawazo asiweze kuonea fahari nyimbo zake. Jambo hili lilifanya nyimbo

zilizopendwa kuwa ni zile zilizoimbwa kwa lugha ya Kiingereza. Nyimbo hizi hata hivyo zilisikilizwa tu na watu wachache waliofahamu lugha ya Kiingereza. Waimbaji kadhaa waliendelea kutumia lugha ya Kiswahili katika nyimbo zao mathalani Fadhili William, Daudi Kabaka, John mwale na wengine (Kanyange, 2015).

Kwa mujibu wa Kanyange (keshatajwa), baadaye, watu walianza kubadili msimamo wao wa kupendelea nyimbo zilizopembwa kwa lugha ya Kiingereza na kuanza kuenzi zile zilizoimbwa kwa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kiasili. Kupendwa kwa nyimbo hizi kulitokana na sababu kwamba zilitungwa na kuimbwa katika lugha za kiasili. Akishadidia kauli hii, Musembi (2016) anasema kuwa watu wa jamii ya Akamba walipendelea sana nyimbo zao za kiasili kuliko zile za kigeni, hadi wakati wasanii wao walipoanza kutunga na kuimba nyimbo zilizotumia mitindo tofauti na zile za kiasili kwa kutumia lugha ya Kikamba. Hatua hii ilizifanya nyimbo za waimbaji hawa kujulikana kama nyimbo zilizopendwa hadi sasa. Mfano wa wasanii wa mwanzo katika jamii ya Akamba kutunga na kuimba nyimbo zilizopendwa ni pamoja na Kakai Kilonzo, Jacob William Maunda, Bosco Mulwa, Kalambya Sisters na Kalambya Brothers (King'ei na Kisovi, 2005). Ngugi (keshatajwa), anaeleza kwamba nyimbo pendwa zitaendelea kukua kufuatana na mabadiliko ya kihistoria na kifani hivyo basi, nyimbo hizi lazima zichukuliwe kama sehemu moja ya fasihi ya Waafrika. Katika hali hii, wataalamu hawana budi kuchunguza mchango wake wa kimaudhui na kifani. Maoni haya yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu yalimsaidia mtafiti kukita mizizi katika mada ya utafiti huu. Hii ni kwa sababu utafiti ulihusu uchanganuzi wa jinsi nyimbo pendwa za Ken wa Maria zinavyojenga utaifa wa jamii ya Akamba, suala ambalo lilitokana na mchango wa kimaudhui na kifani wa nyimbo husika.

Mojawapo ya dhima muhimu ya nyimbo pendwa ni ujenzi wa utaifa. Hili linatokana na sababu kwamba wimbo ni muungano wa sauti ambazo zinaweza kusababisha taharuki na kuamsha hisia kama vile: vitisho, kuliwaza, kuongoa na hisia za kimapenzi. Kwa vile mawazo na hisia zinazowakilishwa katika nyimbo pendwa ni rahisi kueleweka, nyimbo pendwa huwa ndiyo njia bora ya kuwasiliana na umma. Nyimbo pendwa zina uwezo wa kupitisha hisia za utaifa kwa jamii. Utafiti kuhusu ujenzi wa utaifa katika fasihi ya Kiswahili ni finyu. Pana pengo kuhusu jinsi hakika nyimbo pendwa zinajenga utaifa hasa

katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Utafiti huu unakusudia kujaza pengo hilo. Utafiti huu ulichunguza utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

### 1.2 Suala la Utafiti

Fasihi simulizi imekuwepo tangu zama. Si ajabu imefanyiwa tafiti kadha wa kadha katika usomaji wa fasihi ya Kiswahili. Tafiti hizi zimejikita katika uainishaji wa nyimbo, maudhui, mtindo, muundo na uumbuji kwa jumla. Hata hivyo, suala la utaifa wa jamii katika fasihi simulizi hasa katika kipera cha nyimbo halijashughulikiwa kwa kina ili liwekwe wazi kitaaluma. Aidha, hamna data ya kutosha kuhusu utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za jamii ya Akamba. Vile vile, kwa muda mrefu usomi wa fasihi simulizi umejikita katika ujumi na burudani huku kigezo cha utaifa wa jamii kikitiwa kapuni. Utafiti huu ulichunguza jinsi nyimbo pendwa zinavyotambulisha na kujenga utaifa wa jamii ya Akamba kupitia nyimbo pendwa teule za msanii Ken wa Maria.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga:

(i) Kuchunguza arki za utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria.

(ii) Kuhakiki mbinu za kimtindo zinazotumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria.

(iii) Kupambanua changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba kwa mujibu wa nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo:

(i) Ni arki gani zinazotumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria?

(ii) Msanii Ken wa Maria ametumia mbinu zipi za kimtindo katika nyimbo pendwa teule ili kujenga utaifa wa jamii ya Akamba?

(iii) Utaifa wa jamii ya Akamba unakumbwa na changamoto zipi kwa mujibu wa nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kipera cha nyimbo pendwa kinaendelea kukua na kupata umaarufu katika jamii mbalimbali. Kwa mfano, katika jamii ya Akamba, hadhira ya nyimbo pendwa ni pana mno. Wasanii hupitisha jumbe tofauti tofauti kupitia nyimbo hizi (Daniel, 2020). Wahakiki wengi na wasomi duniani kote wamekuwa na mvuto kwa nyimbo pendwa tangu kuibuka kwake tangu miaka ya awali ya 1950. Tafiti nyingi zilizofanyiwa nyimbo za Akamba zimeshughulikia maudhui na mtindo bila kushughulikia arki za utaifa katika nyimbo. Utafiti huu ulikuwa muhimu katika kubainisha arki za utaifa katika nyimbo pendwa za Akamba.

Umaarufu wa nyimbo pendwa umechangiwa na mbinu mbalimbali za kimtindo ambazo zimo katika utanzu wa fasihi. Utafiti huu unatambua nyimbo pendwa za jamii ya Akamba kama uwanda mpana ambao unastahili kuangaziwa na kutafitiwa. Nyimbo pendwa za Akamba zinasheheni maudhui mbalimbali kama vile usuli, siasa, utaifa na hata dini. Utafiti huu ulikuwa muhimu kwa kuonyesha jinsi mtindo anaotumia msanii wa nyimbo pendwa unavyojenga utaifa katika jamii ya Akamba na jamii zingine kwa jumla.

Mshikamano wa kijamii miongoni mwa jamii ya Akamba unaendelea kufifia kutokana na utandawazi. Hali ya maisha inaendelea kubadilika kutokana na wanajamii kuhamia mijini katika harakati za kuzalisha mali na kutafuta riziki. Wakamba wanahamia nchi zingine kwa ajili ya kazi na masomo. Hali hii inasababisha kupungua kwa mshikamano miongoni mwa wanajamii. Hivyo basi, utafiti huu ulikuwa muhimu kwa kuwa ulichunguza na kuweka wazi changamoto za utaifa wa jamii ya Akamba.

Utafiti huu utaongeza maarifa katika nadharia na mbinu za uhakiki wa nyimbo katika utanzu wa fasihi simulizi nchini Kenya kwa kuweka wazi aina za utaifa, vitambulisho vya utaifa na jinsi vinavyojitokeza katika nyimbo pendwa. Isitoshe, utafiti huu utakuwa malighafi kwa wasomi wengine kwani utatoa mchango mkubwa katika kipera cha nyimbo katika utanzu wa fasihi simulizi na kutajirisha maktaba ya Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya.

Matokeo ya utafiti huu yatatumika kuonyesha jinsi nyimbo pendwa za Ken wa Maria zinavyokuwa kiungo muhimu cha kuleta utaifa wa jamii au taifa husika. Hii ni kwa sababu

nyimbo katika jamii ya Akamba ni muhimu kwa kuwa hufungamanishwa na historia, utamaduni, amali, mielekeo, imani na itikadi za jamii. Kwa njia moja au nyingine, matokeo ya utafiti huu yalichangia kuelewa jinsi jamii ya Akamba inavyotumia nyimbo pendwa kuunganisha watu ili kupambana na vitisho vinavyotokana na majanga kama vile ukame, uraibu wa dawa za kulevya, magonjwa, vita, misukosuko ya kisiasa na kiuchumi pamoja na vurugu za kijamii.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Kuna aina nyingi ya nyimbo ambazo zinaweza kutumiwa kupitisha maudhui ya utaifa katika jamii ya Akamba. Kuna nyimbo za tohara, za kitamaduni, pendwa na hata za kidini. Utafiti huu ulichunguza nyimbo pendwa ambazo zilikisiwa kudhihirisha utaifa katika jamii ya Akamba. Nyimbo pendwa zilichaguliwa kwa sababu zinashabikiwa na watu wengi; wazee kwa vijana, wanawake kwa wanaume ikilinganishwa na aina nyingine za nyimbo (Daniel, 2020). Sababu nyingine ni kwamba husambazwa kwa wingi kupitia njia mbalimbali za mawasiliano, hulenga kuvutia hadhira kubwa na huwa zimesheheni maudhui mepesi ya moja kwa moja. Nyimbo pendwa pia huwa sehemu ya utamaduni maarufu unaoakisi mitindo, maadili na changamoto za kijamii.

Eneo la Ukambani lina wasanii wengi ambao huimba nyimbo pendwa kwa lugha ya Kikamba. Hata hivyo, mtafiti alizingatia nyimbo pendwa zilizoimbwa na msanii Ken wa Maria. Sababu za kumchagua msanii huyu ni kwamba ni msanii ambaye ni maarufu katika eneo la Ukambani na amefanya mawasilisho mengi katika hafla nyingi kama mikutano ya kisiasa, sherehe za harusi na hata sherehe za kuadhimisha sikukuu za kitaifa. Msanii huyu anathamini lugha za kiasili: huimba nyimbo katika lugha ya Kiswahili, Kikamba, Kikuyu na hata Kijaluo. Nyimbo zake huwa zimejaa tamathali za lugha ithibati ya mapenzi yake kwa lugha. Isitoshe, nyimbo zake husheheni maudhui mbalimbali kama vile maudhui ya mapenzi na ndoa, siasa, uzalendo na masuala ya kiuchumi. Zaidi ya hayo, Ken wa Maria ana wasikilizaji wengi katika mtandao wa *YouTube* akilinganishwa na wasanii wengine. Vilevile, nyimbo zake huchezwa kwa wingi katika vituo vya redio katika eneo la Ukambani (Sang'u, 2021).

Msanii Ken wa Maria ana kanzi kubwa ya nyimbo pendwa. Msanii huyu ametunga na kurekodi zaidi ya nyimbo 450 kwa lugha ya Kikamba, Kiswahili, Kikikuyu na Kijaluo;

nyimbo ambazo zimeshabikiwa kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita kwenye nyimbo pendwa 24 zilizokisiwa kuwa na maudhui ya utaifa. Idadi hii ndiyo ambayo ingeweza kukidhi malengo ya utafiti huu. Nyimbo zilizochunguzwa ni zile alizoimba kwa lugha ya Kikamba. Vilevile, nyimbo hizi zimechezwa kwa mara nyingi katika vituo vya redio vinavyotangaza katika lugha ya Kikamba.

Kuna mambo mengi ambayo yangeweza kuchunguzwa katika nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria. Hata hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza kipengele cha utaifa wa Akamba katika nyimbo pendwa zinazolenga jamii ya Akamba. Zaidi ya hayo, utafiti huu ulichanganua mbinu za kimtindo zilizotumika kujenga utaifa katika nyimbo pendwa teule za msanii Ken wa Maria katika jamii ya Akamba.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Mapitio ya maandishi yalichangia katika kuelewa mada ya utafiti huu ya kuchunguza utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria. Mapitio ya maandishi humshirikisha mtafiti kutoa matokeo ya tafiti zikaribiazo utafiti unaonuiwa kufanywa. Rossman (2006), anasema kuwa mapitio ya maandishi husaidia kuziba mianya iliyoachwa na tafiti zingine. Katika utafiti huu, mapitio ya maandishi yalifanywa kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza ilizingatia kusoma kazi kuhusiana na arki za utaifa wa jamii ya Akamba. Awamu ya pili ilihusu kupitia maandishi kuhusu mbinu za kimtindo zilizotumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba. Hatimaye, katika awamu ya tatu, mtafiti aliangazia maandishi kuhusiana na changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba. Aidha, katika sura hii mtafiti alibainisha misingi na nguzo za nadharia zilizoongoza utafiti huu.

## 2.2 Arki za Utaifa

Smith (1991), katika makala yake ya *Nadharia, Itikadi na Historia*, anakuli kwamba utaifa wa jamii hauwezi kufafanuliwa kwa namna moja tu kwa sababu unajidhihirisha kupitia vipengele vingi vinavyoshirikiana. Anauona kama mchanganyiko wa historia ya kijamii, tamaduni na utambulisho wa pamoja unaojengwa kwa muda mrefu. Kwa mujibu wa Smith (keshatajwa), utaifa wa jamii una mizizi katika hadithi za asili, kumbukumbu za kihistoria, alama za kitamaduni, na thamani za pamoja zinazounganisha watu katika hisia ya kuwa taifa. Maoni ya msomi huyu yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile yalitupa ufafanuzi bayana wa dhana ya utaifa wa jamii. Isitoshe, yaliweka wazi baadhi ya arki za utaifa wa jamii kama vile historia ya jamii, utambulisho na utamaduni. Hizi ni mojawapo wa arki zinazojenga utaifa wa jamii ya Akamba ambazo mtafiti wa utafiti huu alilenga kuchunguza katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Katika makala yake ya *Nadharia ya Utaifa*, Smith (keshatajwa), amefafanua taifa kama jamii ya watu walio na historia moja, wanaoishi eneo moja, wenye asili moja, njia sawa za uzalishaji na kuendeleza uchumi na ambao wana utamaduni sawa. Isitoshe, amefafanua sifa za utaifa wa jamii kama: kuwepo kwa jina linalowatambulisha kama kabila, asili moja, historia moja, lugha moja na utamaduni unaofanana. Maelezo haya yaliongoza utafiti huu

katika kubainisha jamii ya Akamba kama taifa. Hii ni kwa sababu wana asili moja kwa mujibu wa historia ya usuli wa Wabantu nchini Kenya, wanaishi katika eneo moja linalojulikana kama Ukambani, wana njia sawa za uzalishaji na kuendeleza uchumi na wanafuata tamaduni za Kikamba (Mutisya, 2022). Pia, maelezo ya Smith (keshatajwa) yaliongoza utafiti huu kutambua kwamba jamii ya Akamba ina utaifa wa jamii kwa kuwa wana jina linalowatambulisha kama kabila la Akamba na huzungumza lugha ya Kikamba. Maelezo ya msomi huyu yaliusaidia utafiti huu kwa kuainisha arki za utaifa wa jamii kama vile utamaduni, lugha, historia moja, jiografia pamoja na shughuli za kiuchumi. Utafiti huu ulilenga kuchunguza arki za utaifa wa Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Ozkirimli (2010), ameainisha utaifa katika makundi matano. Makundi haya ni pamoja na utaifa wa kibinadamu, utaifa wa Jacobin, utaifa wa kijadi, utaifa huria na utaifa jumuishi. Anafafanua utaifa wa kibinadamu kama utaifa ulioendelezwa na wanasiasa ili kukuza demokrasia, utabaka na utamaduni. Kuhusu utaifa wa Jacobin, anasema kwamba ni utaifa uliozuka kupinga utaifa wa kibinadamu. Utaifa huu ulitumia mabavu kwa wale walioupinga. Uliendeleza maadili yasiyo na uhalisia. Utaifa wa jadi ulianzishwa baada ya vuguvugu la mapinduzi ya Ufaransa. Ulipinga utaifa wa awali wa Jacobin. Ulihimiza watu kufuata mila zao. Utaifa huria ulipinga vita baina ya jamii; ulihimiza nchi zote kubuni serikali za kisiasa zilizoongozwa na katiba. Kwa upande mwingine, utaifa jumuishi uliendelezwa kwa sera za serikali, nguvu za serikali na ulihimiza wananchi wake kuwa waadilifu na kulipatia taifa nafasi ya kwanza katika kazi zao. Utaifa huu ulihimiza uzalendo kwa nchi. Maelezo ya Ozkirimli (keshatajwa) ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile yanatubainishia wazi aina za utaifa na sifa zake, suala ambalo ni la umuhimu kwa utafiti huu.

Akizungumzia kuhusu utaifa, Llobera (1999), anasema kwamba kila jamii huwa na utaifa wa awali. Utaifa awali huchukulia kwamba kila kikundi lazima kijitambulishe. Aidha, katika jamii mbalimbali kuna mahusiano ya kiukoo au damu, rangi, lugha, dini na mahusiano ya kimaeneo. Mahusiano haya japo hayaelezeki, ni ya lazima. Haya ni mahusiano ambayo yamekolea kwa muda mrefu. Mataifa ya kisasa pamoja na yale yanayoendelea yamejaa utambulisho wa awali yaani ukabila. Utambulisho wa kikabila umekita mizizi katika historia ndefu ya binadamu na hauwezi kuepukwa. Mawazo haya ya

Llobera (Keshatajwa) yalikuwa malighafi muhimu ya utafiti huu kwani yanathibitisha kwamba kuna utaifa wa jamii ambao ndio wa awali kwa hivyo, jamii ya Akamba ina utaifa. Pia yanabainisha arki za utaifa wa jamii kuwa lugha, dini, jiografia, siasa na utawala, historia pamoja na utambulisho, ambazo mtafiti katika utafiti huu alichunguza. Utafiti huu ulilenga kuchunguza arki zinazojenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Coulter (2020), alishughulikia utambulisho wa wasichana kupitia nyimbo pendwa. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa kinyume na jinsi watu wanavyoamini kuwa wasichana hawapendi nyimbo pendwa, hali si hivyo. Msomi huyu anaonyesha kwamba wasichana hupenda nyimbo pendwa na huzitumia kujenga taadhima yao, kujenga umoja miongoni mwao na pia kujitambulisha na kikundi fulani. Maelezo ya utafiti huu yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu yanalenga suala la utambulisho. Utafiti huu ulihusu ujenzi wa utaifa ambao mara nyingi huhusisha kutafuta utambulisho wa jamii husika katika nchi fulani. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa ulilenga kuangazia utambulisho wa wasichana kupitia muziki pendwa ilhali utafiti huu unahusu ujenzi wa utaifa wa Akamba kupitia nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria.

Fisher (2012), alichunguza jinsi viongozi wa jamii ya Chagga inayoishi karibu na Mlima Kilimanjaro walivyounda na kuendeleza kitambulisho cha kikabila kutoka enzi za ukoloni hadi sasa. Wakoloni waliwapa Wachagga sifa kama vile wenye bidi na wachapa kazi. Walikuwa na uongozi wa kifalme chini ya chifu mkuu ambao ulionekana kama ishara ya utaifa wa jamii. Utafiti wa Fisher (keshatajwa ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa umebainisha baadhi ya arki za utaifa wa jamii kama vile jiografia, utawala, utambulisho na historia ya jamii ambavyo utafiti huu ulidhamiria kuchunguza. Hata hivyo, utafiti wake ulichunguza vitambulisho vya utaifa wa Wachagga huku utafiti huu ukilenga utaifa wa jamii ya Akamba.

Mutisya (2022), alitafitia thamani ya ujumi katika nyimbo za michezo ya watoto katika jamii ya Akamba. Utafiti wake uligundua kwamba nyimbo za michezo ya watoto za Kikamba zimejikita katika misingi ya utamaduni wa jamii ya Akamba. Utafiti wake pia ulibaini kuwa nyimbo hizi husheheni vipengele vya kiujumi kama vile urafiki, umoja wa wanajamii, uwajibikaji, bidii kazini, vyakula vya kitamaduni, mfumo wa kiukoo, pamoja

na undugu miongoni mwa wanajamii. Utafiti wake uliufaa utafiti huu kwa vile ulitafitia suala la nyimbo kutoka jamii ya Akamba. Isitoshe, matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha kwamba nyimbo husheheni vipengele vinavyojenga utaifa wa jamii ya Akamba kama vile undugu, shughuli za kiuchumi, mifumo ya kiukoo, na vyakula vya kitamaduni, ambazo ni baadhi za arki za utaifa utafiti huu ulilenga kuchunguza katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria. Mtafiti aliona kwamba nyimbo kutoka jamii ya Akamba zina jukumu la kuleta umoja miongoni mwa wanajamii, suala ambalo utafiti huu ulikuwa ukichunguza. Hata hivyo, utafiti wa Mutisya (keshatajwa), ulikuwa tofauti na utafiti huu kwa vile utafiti wake ulichunguza suala thamani za kiujumi katika nyimbo za michezo ya watoto huku utafiti huu ukilenga kuchunguza arki za utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Mung’ala (2020), alichunguza uundaji wa vitambulisho vya utaifa katika tamthilia ya Mstahiki Meya. Utafiti huu ulibaini kuwa kuna aina mbili za taifa: taifa la kisiasa ambalo hujengwa kupitia nia na maamuzi huru ya kidemokrasia, na taifa la kitamaduni ambalo huundwa kupitia kwa urathi wa kitamaduni kama vile lugha, makazi, dini, mila na historia sawa. Utafiti wa Mung’ala (keshatajwa), uliufaa utafiti huu kwa vile ulisaidia kuweka wazi aina za utaifa na utambulisho wa kijamii. Utafiti wa Mung’ala uliongozwa na nadharia ya utaifa ambayo iliufaa utafiti huu. Hata hivyo utafiti wake ni tofauti na huu kwa sababu ulishughulikia kipera cha tamthilia ambacho hupatikana katika utanzu wa fasihi andishi ilhali utafiti huu ulishughulikia kipera cha nyimbo ambacho hujikita katika fasihi simulizi.

Maelo (2014), alichunguza ujenzi wa utaifa wa Wabukusu kupitia simulizi za matanga zinazojulikana kama *Khuswala Kumuse*. Utafiti wake uligundua kwamba simulizi ya *Khuswala Kumuse* imejaa vipengele vya kijamii, kisiasa na kiuchumi ambavyo hujenga utaifa wa Wabukusu. Utafiti wake uliufaa utafiti huu kwa vile ulitafitia kuhusu utaifa wa jamii suala ambalo utafiti huu ulikuwa ukichunguza. Tofauti na utafiti huu, utafiti wa Maelo ulichunguza ujenzi wa utaifa wa jamii ya Abukusu kupitia simulizi za matanga *Khuswala Kumuse* huku utafiti huu ukichunguza ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba kupitia nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Sang (2014), alishughulikia utaifa katika nyimbo pendwa za kabila la Kalenjin. Utafiti wake ulichunguza jinsi nyimbo pendwa zinazochezwa katika vituo vya redio huendeleza

utaifa wa jamii ya Wakalenjin. Kulingana na msomi huyu, nyimbo pendwa ziliweza kukuza utambulisho wa utaifa. Vile vile, utafiti wake ulibainisha kuwa vituo vya redio vya lugha za kikabila vilichangia kukuza utaifa wa Wakalenjin. Utafiti huu wa Sang ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu ulimwezesha mtafiti kubaini jinsi nyimbo za Ken wa Maria zinavyotambulisha jamii ya Akamba. Kwa upande mwingine, utafiti wa Sang ulishughulikia utaifa wa jamii ya Wakalenjini ilhali utafiti huu ulichunguza utaifa katika jamii ya Akamba.

Kwa mujibu wa Mburu (2014), nyimbo huwa na mawazo mazito na hutumiwa kuonyesha uhusiano wa jamii, migogoro, kukejeli, kuliwaza, kubembeleza na kuburudisha. Anaendelea kukuli kwamba nyimbo huchukua sehemu kubwa ya maisha ya binadamu kama vile kulima, kujenga, kupasha tohara, kufua, kujenga, kuoa, kulea na kuvuna. Utafiti wa Mburu (keshatajwa) uliufaa utafiti huu kwa vile shughuli ambazo msomi huyu ametaja zinaonyesha uhusiano dhahiri wa nyimbo na arki za utaifa.

Musyoka (2011), alitafitia nyimbo pendwa za Kikamba huku akichunguza utendaji katika nyimbo za Kennedy Wambua na Bosco Mulwa. Utafiti wake ulibaini kuwa kupitia utendaji masuala kama vile mapenzi, ndoa, uhamaji na utamaduni wa jamii ya Akamba yanapitishwa kupitia nyimbo pendwa za wasanii hawa. Utafiti wake ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile ulitafitia nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria ambaye utafiti huu ulitafitia. Isitoshe, baadhi ya matokeo ya utafiti wa Musyoka yalibainisha kuwepo kwa vipengele ambavyo vinahusishwa katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba kama vile utamaduni ambavyo viliufaa utafiti huu.

### 2.3 Mbinu za Kimtindo

Leech na Short (1981), katika kitabu chao *Style in Fiction*, wameshughulikia mtindo. Wamejadili nadharia ya umitindo kwa kina. Katika kazi yao wana maoni kuwa mtindo na maudhui huhusiana. Kazi yao pia imeanisha viwango vya kuchanganua mtindo ambavyo ni kiwango cha msamiati, grafolojia, semantiki, sintaksia na fonolojia. Utafiti huu uliongozwa na maoni haya makuu ya Leech na Short (keshatajwa) kwani tulilenga kiwango cha kisemantiki kwa vile tuliangalia maana zinazojitokeza katika tamathali za usemi na jinsi maana hizo zinachangia katika kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui ya utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria. Maelezo ya Leech na Short

haswa katika kipengele cha ukiushi katika kiwango cha semantiki yaliufaa utafiti huu kwani madhumuni ya utafiti huu yalilenga hapo kwa kuzingatia tamathali za usemi za chuku, sitiari, tashbihi, jazanda, usimulizina misemo.

Ali (2020), alifanya utafiti linganishi ambapo alichunguza mtindo na dhamira katika riwaya za Euphrase Kezilahabi na Mohamed Suleiman. Utafiti wake ulilenga kubainisha mbinu za kimtindo katika riwaya teule za waandishi hawa, kulinganua mbinu za kimtindo katika riwaya teule na kulinganua dhamira zinazojitokeza katika riwaya husika. Utafiti wake uligundua kuwa waandishi wanatofautiana na kufanana katika mbinu za kimtindo na dhamira zilizotumika kujenga kazi zao za sanaa. Utafiti wa Ali (Keshatajwa) ulikuwa malighafi muhimu ya kazi hii katika kuafikia malengo ya utafiti huu kwa sababu uliongozwa na nadharia ya umitindo ambayo ndiyo iliyotumiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wa Ali ulikuwa tofauti na huu kwa vile ulishughulikia suala la mtindo na dhamira katika riwaya huku utafiti huu ukilenga kubainisha mbinu za kimtindo zilizotumiwa na msanii katika nyimbo pendwa ili kujenga utaifa wa jamii.

Abdalla (2018), alichunguza dhamira na fani katika nyimbo za taarab asilia za Shakila Saidi Khamisi. Utafiti wake ulilenga kubainisha mbinu za kisanaa zinazojitokeza katika nyimbo teule za msanii husika. Utafiti wake ulibaini kuwa kulikuwa na mbinu za kisanaa katika nyimbo za taarab asilia za Shakila Saidi. Miongoni mwa mbinu hizo za kisanaa ni tamathali za semi kama vile chuku, jazanda, majazi na taswira. Utafiti wa Abdala (keshatajwa ) uliufaa utafiti huu kwa vile ulichunguza suala la matumizi ya fani katika nyimbo katika kutekeleza dhamira ya msanii, suala ambalo utafiti huu ulichunguza.

Mbinu ya usimulizi kama mtindo katika fasihi simulizi imechunguzwa na Aboge (2021) katika utafiti wake. Alichunguza vipengele vya usimulizi katika nyimbo teule za Bahati Bukuku. Aboge (keshatajwa), aliona kuwa nyimbo huwa na mbinu za kimtindo ambazo huwasilisha jinsi maudhui yanavyojitokeza katika nyimbo hizo. Utafiti wake ulibaini kuwa nyimbo za Bahati Bukuku zimesheheni aina mbalimbali za usimulizi kama vile usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya pili na usimulizi wa nafsi ya tatu. Utafiti wake ulikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwa vile ulichangia katika uelewa wa aina za usimulizi

katika fasihi simulizi na usimulizi kama mtindo unaotumiwa katika ujenzi wa utaifa wa jamii.

Mwangi na wengine (2017), walichunguza mtindo na maudhui katika nyimbo za kisiasa za msanii John De'Mathew nchini Kenya. Utafiti wao ulifafanua namna msanii anavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe aliodhamiria kupitia mtindo. Isitoshe, utafiti huo ulidhamiria kubainisha mitindo inayotumiwa na mwanamuziki De'Mathew katika kuwasilisha ujumbe wa kisiasa. Utafiti huu ulibaini kuwa nyimbo hutumika nyakati mbalimbali kufafanua masuala anuwai yanayomwathiri binadamu. Utafiti wao uligundua kuwa msanii ametumia mitindo mbalimbali kama vile jazanda, tanakali za sauti, tashihisi, balagha, chuku, tashbihi, methali, misemo na uzungumzi nafsia katika kuwasilisha ujumbe wa kisiasa wa nyimbo zake. Utafiti wao ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile ulibainisha baadhi ya mbinu za kimtindo alizotumia msanii kupitisha ujumbe wa kisiasa ambazo zilichanganuliwa katika utafiti huu. Hata hivyo, tofauti ni kuwa utafiti wao ulilenga nyimbo za kisiasa za msanii De'Mathew ilhali utafiti huu ulidhamiria kuchunguza mbinu za kimtindo anazotumia msanii Ken wa Maria kupitisha ujumbe wa utaifa wa jamii ya Akamba.

Nyandiwa (2015), alishughulikia uchanganuzi wa kimtindo katika *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu*. Lengo kuu la utafiti wake lilikuwa kuchunguza matumizi ya sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora katika tamthilia husika. Mtafiti alichochewa na ufahamu kwamba mtindo na dhana ya maudhui ni vitengo muhimu vya fasihi ambavyo huandamana na kutegemeana ili kufanikisha dhamira ya mwandishi kwa wasomaji wa kazi yake, mawazo ambayo yaliufaa utafiti huu.. Mtafiti aliona kwamba matumizi ya tamathali za usemi huondoa uchapwa katika kazi za sanaa pamoja na kuwa matumizi ya tamathali za usemi si ya kiajali ila hutumika kimakusudi. Utafiti wake uligundua kuwa matumizi ya vipengele vya tamathali za usemi vya sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora vilichangia katika kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui katika tamthilia zilizohusika. Mtafiti aliona kuwa msanii hutawala lugha kiufundi ili kuonyesha tofauti kati ya lugha ya fasihi na lugha ya kawaida. Licha ya utafiti huu kuchunguza mbinu za kimtindo zilizochangia kuibuka kwa maudhui katika kazi za kifasihi alizochunguza mtafiti, utafiti wake ulitofautiana na utafiti huu kwa vile mtafiti

alichunguza utanzu wa fasihi andishi ilihali utafiti huu ulichunguza nyimbo pendwa ambazo zipo katika utanzu wa fasihi simulizi. Isitoshe, utafiti huu ulilenga kuhakiki namna mbinu za kimtindo katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria zilivyotumika katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

Murumba (2013), alitafiti mtindo katika *Watu wa Gehenna*. Katika utafiti wake alitumia nadharia ya umitindo na kubainisha jinsi vipengele vya mtindo vilivyotumika katika matini hiyo na jinsi vilivyoathiri muundo. Katika utafiti wake alionyesha jinsi maana tofauti hujitokeza katika ukiushi wa kisemantiki. Utafiti wake Murumba (keshatajwa) uliufaa utafiti huu kwani alifafanua dhana ya viwango vya umitindo na kwa hivyo kuuupa mwelekeo utafiti huu haswa katika kipengele cha ukiushi wa kisemantiki. Tofauti na utafiti wake ambao ulijikita katika utanzu wa fasihi andishi, utafiti huu ulihakiki mbinu za kimtindo zilizotumika katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Utafiti wa Muriuki (2013), ulichunguza mtindo katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai. Utafiti wake uliainisha aina mbalimbali za nyimbo suala ambalo liliufaa utafiti huu. Mtafiti aliweka wazi nguzo za nadharia ya umitindo suala ambalo lilikuwa na manufaa kwa utafiti huu. Isitoshe, utafiti wake ulibaini kuwa nyimbo za kazi za jamii ya Warabai zinasheheni mitindo mbalimbali kama vile takriri, chuku, tashbihi, ukariri, misemo jazanda na methali. Hili liliusaidia utafiti huu katika kuhakiki mbinu za kimtindo zilizotumika katika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria.

Mwanzia (2007), alitafitia mtindo wa nyimbo za chekechea za Kikamba kwa kuongozwa na mhimili wa semantiki wa nadharia ya umitindo. Utafiti wake ulibainisha kuwa nyimbo za chekechea zilikuwa na mtindo wa matumizi ya misimu, takriri, tashbihi na kuchanganya ndimi. Isitoshe, nyimbo za chekechea zilitungwa kutegemea hadhira. Utafiti wake uliufaidi utafiti huu kwa vile utafiti wake ulichunguza vipengele vya kimtindo ambavyo utafiti huu ulitafitia. Utafiti wake hata hivyo, ulichunguza mtindo katika kipera cha nyimbo za chekechea tofauti na utafiti huu ambao ulichunguza namna mbinu za kimtindo katika nyimbo pendwa zinavyotumika katika uwasilishaji wa maudhui ya utaifa wa jamii.

Wathome (2009), alishughulikia mitindo katika nyimbo za tohara za jamii ya Akamba. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya umitindo katika kuchunguza mabadiliko ya mitindo katika nyimbo za tohara za Wakamba. Utafiti wa Wathome ulibainisha kuwa mabadiliko ya mtindo wa tohara yalitokea katika tamathali za semi. Utafiti huu uliufaidi utafiti huu kwa vile ulichunguza suala la mitindo katika nyimbo suala ambalo utafiti huu ulichunguza. Isitoshe, utafiti wake uliongozwa na nadharia ya umitindo ambayo iliongoza utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na huu kwa vile wake ulijikita katika nyimbo za tohara ilihali utafiti huu ulichunguza utaifa katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Wambua (2001), alichunguza mtindo katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Alichunguza uteuzi wa maneno na mbinu za kuwasilisha maudhui. Utafiti wake ulibainisha kwamba uelewekaji na ukubalifu wa maudhui hutegemea mtindo wa msanii. Mtafiti alibaini kuwa Kakai Kilonzo ametumia jazanda, tashbihi, chuku, methali, takriri na misemo ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Utafiti wake, kama ilivyo katika utafiti huu, uliongozwa na nadharia ya umitindo ambayo ni mojawapo wa nadharia zilizoongoza utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti wake ulikuwa tofauti na wetu kwa vile ulitafitia suala la mitindo katika nyimbo za Kaikai Kilonzo huku wetu ukichunguza utaifa wa jamii ya Akamba kupitia nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Kamau (1992), alichunguza mtindo katika riwaya za Mohammed Said Abdullah. Kamau (keshatajwa), aliongozwa na nadharia ya umitindo katika utafiti wake. Aliona kwamba mhakiki ni sharti azingatie mambo yanayofanya kazi fulani ivutie bali si kushughulikia maudhui tu. Mtafiti anakuli kwamba nadharia ya umitindo imeegemea zaidi katika umuhimu wa lugha ya kuvutia katika kuwasilisha ujumbe. Anaendelea kusema kuwa mbinu za kimtindo humwezesha mwandishi wa riwaya kutoa ujumbe kwa nguvu. Alibainisha kwamba mwandishi Mohammed Said Abdallah alitumia mbinu za takriri, mazungumzo, tashbihi, methali na tanakali za sauti ili kuwasilisha ujumbe wake. Ingawa utafiti wake ulitumia nadharia ya umitindo kama ilivyo katika utafiti huu, tofauti ni kwamba utafiti wake ulilenga kubainisha ufundi aliotumia mwandishi katika riwaya. Zaidi ya hayo, utafiti huu ulipania kuchunguza namna mbinu za kimtindo zinavyojenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

## 2.4 Changamoto za Utaifa

Utaifa umo hatarini ya kutoweka. Hobsbawn (1990), akinukuliwa na Smith (2010), anasema kwamba utaifa wa mataifa huru uliopo kwa sasa utaangamizwa kutokana na kubuniwa kwa miungano mikubwa ya jamii. Anasema kwamba ingawa utaifa utaendelea nafasi yake itakuwa duni. Smith (2010), anasema kuwa utaifa wa taifa huru unatishiwa na: mabadiliko ya kiuchumi, kuvumbuliwa kwa zana hatari za vita, kuingizwa kwa sarafu mpya zilizo na uwezo mkuu wa kibiashara kuliko fedha za nchi huru pamoja na kuibuka na kupanuka kwa makampuni ya uwekezaji yaliyo na nguvu za kifedha na ujuzi kuliko nchi zenyewe. Vilevile, anasema kwamba kubuniwa kwa miungano mikubwa ya kiuchumi na kijeshi inayoshirikisha mataifa mengi kunahatarisha kuendelea kwa utaifa wa mataifa huru. Msomi huyu vilevile anasema kwamba utambulisho wa utaifa umo hatarini kutokana na ndoa mseto, ukimbizi, utalii na utandawazi. Baadhi ya watu wana utambulisho wa mataifa mengi na hivyo kuathiri utambulisho wa utaifa wao. Aidha utamaduni kama arki ya utaifa umo hatarini ya kuangamia kutokana na kuenea kwa utamaduni tandavu unaoenezwa na vyombo vya habari. Mawazo ya Smith ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile yanaweka wazi baadhi ya changamoto za utaifa wa jamii ambazo utafiti huu ulishughulikia.

Nielsen (2022), katika makala yake kuhusu *Nyimbo na Utaifa* alionyesha jinsi mataifa hutumia nyimbo kama chombo cha kisiasa. Aidha, alionyesha namna jamii hutumia nyimbo katika kupinga utambulisho wa kitaifa na kukashifu utaifa wa taifa. Utafiti wake uliufaa utafiti huu kwa kuwa ulibainisha changamoto ambazo zinaweza kukumba utaifa wa jamii yoyote ile. Utafiti wake ulionyesha namna nyimbo zinavyoweza kuwa chombo cha kijamii cha kuendeleza au kupinga utaifa, suala ambalo utafiti huu ulichunguza.

Aslack (2020), ametafitia jamii ya Sami wanaoishi sehemu ya Kaskazini mwa Uswizi na Norway. Jamii ya Sami ni wafugaji ambao hufuga paa. Hata hivyo, utamaduni wao ambao ni arki ya kitaifa unadhalilishwa na shughuli za kimaendeleo za serikali kama vile ujenzi wa mabwawa ya nguvu za umeme ambayo yanazuia utamaduni wa ufugaji. Hii inathibitisha kuwepo kwa udhalilishwaji wa utaifa wa jamii. Utafiti wake ulikuwa wa manufaa kwa utafiti huu kwa vile ulibainisha kwamba utaifa wowote ule hukumbwa na changamoto. Hata hivyo utafiti wake ulikuwa tofauti na utafiti huu kwa vile Aslack

(keshatajwa), alichunguza changamoto katika utaifa wa taifa huku utafiti huu ukipambanua changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba.

Utafiti wa Gibb (2013), ulichunguza hali ambayo huwafanya raia wa Uganda kufuata au kupuuza sheria na taratibu za kisheria, hasa katika masuala ya ardhi. Utafiti wake ulibaini kuwa raia hufuata sheria pale ambapo serikali huwapa motisha za kiuchumi na kuzipuuza iwapo utekelezaji wake ni ghali au hauna manufaa kwao. Haki salama za umiliki wa mali ni msingi wa biashara hivyo, Waganda huanzisha taasisi za kienyeji ambazo ni nafuu, rahisi kufikika na zinazowiana na mahusiano ya kijamiiili kulinda mali zao. Aliendelea kusema kuwa ingawa taasisi hizi ambazo si rasmi huwa na changamoto zake, hudhihirisha hitaji la kimsingi la umiliki salama wa mali. Utafiti wa Gibb (keshatajwa ) ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwani ulidhihirisha kwamba utaifa wa jamii hukumbwa na changamoto kadha kama vile sheria za kukandamiza wanajamii, changamoto za kisiasa Pamoja na za kiuchumi suala ambalo utafiti huu ulidhamiria kupambanua.

Marsella (2011), anatambua ubeberu wa Magharibi ambao huwa na nguvu za uharibifu kama mojawapo wa changamoto za utaifa katika taifa. Anakuli kwamba utofauti wa kiutamaduni kama rasilimali ya kuendeleza maisha unaweza kupatikana kupitia kupunguza utandawazi wa kiubeberu na kuunda usawa katika kila fursa. Hili litaleta matokeo ambapo wanajamii wote watathamini na kulinda mshikamano wa kijamii. Utafiti wa Marsella (keshatajwa) uliongoza utafiti huu katika kubainisha na kupambanua changamoto ambazo vinakumba ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Tofauti na utafiti huu, utafiti wake ulichunguza utaifa wa kitaifa ilhali huu ukichunguza changamoto za utaifa wa jamii ya Akamba.

Sande (2018), katika utafiti wake alichunguza changamoto za utaifa nchini Kenya tangu uhuru. Utafiti wake ulibaini kwamba masuala kama vile ukabila, uongozi mbaya, ukosefu wa demokrasia, uhamaji, ufisadi, ukosefu wa usawa na utengwaji yalichangia katika udhalilishaji wa utaifa wa nchi. Matokeo ya utafiti wake yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile yalibainisha changamoto za utaifa wa taifa, suala ambalo liliupa mwelekeo utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wa Sande ulitofautiana na utafiti huu kwani uliangazia utaifa wa kitaifa huku utafiti huu ukiangazia utaifa wa jamii ya Akamba.

Katika makala yake kuhusu Utaifa wa Kikabila: Mfano wa Jamii ya Kalenjin, Sang, (2014) anasema kwamba msanii wa nyimbo pendwa huweza kutambua changamoto ambazo huikumba jamii yake. Mojawapo ya changamoto hizo ni suala la mabadiliko. Anaendelea kusema kuwa wanasiasa wanaweza kuwa kikwazo katika ujenzi wa utaifa wa jamii kwa kutokuwa waaminifu katika kuzingatia maadili ya jamii zao, na kuwa wabinafsi. Utafiti wa Sang uliufaa utafiti wetu kwa vile ulibainisha baadhi ya changamoto ambazo huikumba jamii katika harakati za ujenzi wa utaifa wa jamii. Hata hivyo, utafiti huu ulitofautiana na wetu kwa vile aliangalia changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Kalenjin kupitia nyimbo pendwa huku wetu ukinuia kuchunguza changamoto zinazokumba ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba kupitia nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Katika utafiti wake kuhusu umahuluti wa utamaduni katika nyimbo za harusi miongoni mwa Wanandi, Koech (2024), anatambua umahuluti wa utamaduni kama mojawapo wa changamoto zinazokumba utaifa wa Wanandi. Anakuli kwamba kuna kundi ambalo linakaribisha mabadiliko hayo ilhali wanaoshikilia utamaduni wa jadi wanahofu kuwa utamaduni wao wa jadi huenda ukatoweka kwa kuiga ule wa Wakoloni. Anafafanua kuwa umahuluti huakisi mwingiliano wa kitamaduni unaotokea pale ambapo jamii huathiriwa na tamaduni za nje kupitia biashara, ukoloni, ndoa za mesto na uhamiaji. Utaifa wa jamii hulenga kuimarisha utambulisho wa kikundi hicho, ukitilia mkazo urithi, lugha, mila na historia yake kama msingi wa mshikamano wa kijamii na kisiasa. Utandawazi huleta vipengele vipya vinavyoweza kuimarisha au kudhoofisha mshikamano huo. Maoni ya Koech (keshatajwa), yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile yalitambua baadhi ya changamoto ambazo hukumba utaifa wa jamii. Kinyume na utafiti wake, utafiti huu ulilenga kupambanua changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba kwa mujibu wa nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

### 2.5 Misingi ya Nadharia

Nadharia ni muhimu katika utafiti wowote kwani huwa ndiyo mwongozo unaotumiwa na mtafiti katika kufanya uchunguzi mahususi (Msokile, 1993). Kuna nadharia nyingi ambazo zinaweza kutumiwa katika utafiti wowote unaohusiana na kazi ya kisanaa. Katika utafiti huu, mtafiti aliongozwa na nadharia mbili kuu ambazo zilitumiwa katika kuchunguza vijenzi vya utaifa wa Akamba katika nyimbo pendwa teule za msanii Ken wa Maria.

### 2.5.1 Nadharia ya Utaifa

Mung'ala, na wengineo (2020), wanasema kwamba nadharia ya utaifa iliasisiwa na Gellner na kuendelezwa na Smith (1991), Shulman (2020). Gellner alihusisha utaifa na fikra na mabadiliko yaliyomkumba mwanadamu. Baadaye, alipanua dhana hii katika misingi miwili mikuu ya taifa na utaifa. Isitoshe, alisema kwamba taifa na siasa zikitumiwa pamoja chini ya utamaduni na itikadi inayofaa huendeleza dhana ya utaifa. Vilevile aliangalia mabadiliko ya kihistoria yaliyohusiana na utaifa kama vile mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kilimo, kiviwanda na kiteknohama ambayo huathiri jamii. Kwa hivyo, nadharia yake ilijikita juu ya mabadiliko haya pamoja na ya kielimu, ya wafanyakazi viwandani na sokoni, ya mawasiliano na usafiri pamoja na ya kuibuka kwa miji.

Kwa mujibu wa Mung'ala (2020), mihimili inayohusishwa na nadharia hii na ambayo ilikuwa muhimu kwa utafiti huu ni kama ifuatavyo;

i. Wananchi katika taifa ni lazima wawe na uhusiano wa utamaduni moja. Mhimili huu ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu ulijaribu kuthibitisha kwamba jamii ya Akamba ina utamaduni moja kupitia nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

ii. Wananchi ambao hujaribu kujenga utaifa kupitia ukombozi ni sharti watoke jamii hiyo na wawe na uhusiano wa kiutamaduni na kutumia lugha moja ili kurahisisha mawasiliano. Mhimili huu ulikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwa vile ulibainisha msanii Ken wa Maria ana utamaduni sawa na jamii ya Akamba kwani huimba kwa lugha ya Kikamba ambayo ndiyo lugha pokezi ya jamii yake.

iii. Wananchi hawa ni lazima wakubali mafundisho au itikadi ya taifa lao bila kuwa na uhusiano wowote na mafundisho ya taifa lingine linaloshindana na taifa lao. Mhimili huu ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwani ulibainisha arki za utaifa katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria katika jamii ya Akmba. Pia, uliweka wazi jukumu la msanii Ken wa Maria katika kutekeleza majukumu ya kuelimisha, kuelekeza na kuadilisha jamii kuhusu masuala yanayodhalilisha utaifa wa jamii ya Akamba.

iv. Mhimili kuhusu uendelezaji wa utaifa katika jamii, kuwezesha kujichumia, kuwa na uwazi, mitazamo iliyo huru, ubinadamu, mizimu na imani ya miungu na unyenyekevu. Mhimili huu ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile ulitumika kubainisha mitazamo huru ya jamii ya Akamba pamoja na imani yao kuhusu miungu na mizimu.

### 2.5.2 Nadharia ya Umitindo

Nadharia ya umitindo hujikita katika kuhakiki kazi ya fasihi kwa kuchanganua na kuhakiki vipengele vya kifani, kimtindo na muundo wa kazi ya fasihi. Nadharia ya umitindo ina historia ndefu iliyofuata mikondo mbalimbali. Wamitila (2008) anasema kuwa nadharia ya umitindo ina misingi yake katika nadharia ya balagha ambayo ilitumiwa katika fasihi ya awali ya Warumi na Wayunani. Nadharia ya balagha ilichunguza jinsi ya kuzungumza na kuwasilisha ujumbe kimaandishi. Aidha, anasema kuwa nadharia ya umitindo ndio huunganisha isimu na fasihi. Anasema kwamba nadharia ya umitindo imejikita katika uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa na hupania kubainisha ubunifu uliopo kwenye lugha.

Njogu na Chimera (2008), Jilala (2016), wanasema kuwa mtindo ni tabia ya utungaji inayombainisha mtunzi mmoja na mwingine. Aidha wanasema kwamba mtindo ndio hutofautisha kazi moja ya sanaa kwa nyingine. Mwangi (2022), Anafafanua mtindo kama kipengele cha fani ambacho huonyesha jinsi kazi ya sanaa ilivyosimuliwa. Maelezo ya wasomi hawa yaliwezesha mtafiti kubainisha mbinu alizotumia Ken wa Maria kuwasilisha utaifa wa Akamba.

Simpson (2004), katika Wamitila (2008), ameshughulikia vipengele ambavyo mtafiti anayeegemea umitindo anastahili kuchunguza kama vile: lugha za kitamathali, sarufi na mtindo, usimulizi na mtindo, uchimuzi na mtindo, uteuzi na mtindo, itikadi, mtazamo na mtindo, mshikamano na mtindo, pamoja na mazungumzo na mtindo wa uwasilishaji.

Utafiti huu uliongozwa na viwango vya nadharia ya umitindo ambavyo vimeorodheshwa na Murumba (2013), Wamitila (2008), Simpson (2004), na Leech (2009). Viwango hivyo vimeweza kugawanya mtindo wa fasihi katika viwango saba ambavyo mtafiti wa umitindo hushughulikia.

i. Kiwango cha uchunguzi wa maandishi au grafolojia. Kipengele hiki huchunguza jinsi maneno katika kazi ya fasihi hutamkwa na kuandikwa. Kipengele hiki kimejikita katika matawi ya isimu ya fonolojia na fonetiki. Hutumiwa kuchunguza mbinu kama vile matumizi ya kipekee ya herufi ndogo, matumizi ya herufi kubwa na matumizi ya italiki ili kujenga maana ya katika fasihi.

ii. Kiwango cha pili ni umbo. Katika kipengele hiki mtafiti huchunguza jinsi mwandishi wa matini ya fasihi amefanya uteuzi wa maneno kiubunifu. Pia, jinsi alivyobuni au kubadili maumbo ya maneno kwa kuzingatia mbinu za inkisari, mazida na tabdila au ritifaa ili kuwezesha matini yake kuwa na upekee wa lugha. Aidha matumizi ya kuchanganya ndimi, utohozi na maneno ya lahaja huchunguzwa katika kiwango cha umbo.

iii. Ngazi ya tatu ni sarufi. Katika kipengele hiki mtafiti huchunguza mtindo wa sentensi na vipengele vya kisintaksia vya matini za fasihi. Mathalani, Matumizi ya sentensi ndefu, fupi na marudio ya maneno katika sentensi. Mtindo wa sajili na lahaja pamoja na upangaji wa neno fulani kutokea katika kila sentensi au mshororo pia huchunguzwa.

iv. Uchunguzi wa semantiki katika fasihi. Mtafiti huchunguza mbinu zilizotumiwa ili kuathiri maana. Kwa mfano, kinaya, chuku, ukweli-kinzani, sitiari, taswira na jazanda.

v. Mtindo wa uwasilishaji wa maelezo. Kwa maoni yao, wahusika ndio huathiriwa na uwasilishaji wa mawazo. Kazi ya mtafiti anayetegemea nadharia ya umitindo ni kuchunguza mbinu ambazo mwandishi ametumia ili kuwezesha mazungumzo na uwasilishaji wa usemi au mawazo ya wahusika. Kwa mfano, lugha ya mhusika inalandana na tabaka lake? Je, mwandishi ametumia monolojia na dayalojia ili kuwezesha uwasilishaji wa mawazo ya wahusika?

vi. Kiwango cha muundo wa masimulizi katika makala za fasihi. Yaani mpangilio au msuko wa masimulizi. Masimulizi yanaweza kuwa na sehemu ya utangulizi, mwendelezo na hitimisho. Mtafiti anastahili kuchunguza mtindo wa mpangilio wa hadithi. Pamoja na hayo, achunguze nafsi ya usimulizi.

vii. Mtazamo, itikadi na mtindo. Katika kipengele hiki mtafiti huchunguza mtazamo wa mwandishi kuhusu yale anayoyashughulikia na itikadi ya mwandishi. Baada ya

kupata itikadi na mtazamo wa mwandishi mtafiti anastahili kuchunguza uteuzi wa maneno yanayojenga mtazamo na itikadi ya mwandishi.

Nadharia hii ilitumiwa katika utafiti huu ili kuchunguza vipengele vya fani katika nyimbo za Ken wa Maria. Nadharia hii ilichaguliwa kwa sababu ina viwango vingi vya fani na hivyo ilimwezesha mtafiti kutafiti vipengele mbalimbali vya kifani vinavyojenga arki za utaifa wa jamii ya Akamba.

## 2.6 Hitimisho

Katika sura hii, kazi zilizoandikwa kuhusu utaifa wa jamii, dhima ya nyimbo pendwa, mbinu za kimtindo na changamoto katika ujenzi wa utaifa zilipitiwa. Kazi hizo zilionyesha kwamba tafiti za ujenzi wa utaifa wa jamii kupitia nyimbo pendwa ni chache barani Afrika. Hata hivyo, mchango wa tafiti hizo ulisaidia kuweka dhahiri pengo la utafiti lililopo katika tafiti zinazohusu utaifa. Sura hii ilijadili pia nadharia ambazo ziliongoza utafiti huu. Mihimili mahususi ya nadharia ya utaifa na nadharia ya umitindo iliyotumiwa katika uchanganuzi wa data ilifafanuliwa na kuonyesha jinsi ilivyotumiwa katika uchanganuzi wa data za arki za utaifa, mbinu za kimtindo na changamoto za ujenzi wa utaifa katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alishughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti pamoja na uteuzi wa sampuli. Mbinu za ukusanyaji wa data ziliteuliwa. Kwa mujibu wa Tromp (2006), mbinu itumikayo katika utafiti wowote ule huamua uzito wa data inayotarajiwa kukusanywa na kuchanganuliwa. Kila utafiti mzuri huwa na hatua ambazo hufuatwa. Hatua hizi humwezesha mtafiti anayehusika kuafikia malengo yake ya utafiti kwa kukusanya data kwa njia ifaayo. Namna data ya utafiti huu ilivyochanganuliwa, uwasilishaji wa data Pamoja na maadili yaliyozingatiwa wakati wa utafiti yaliwekwa wazi.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti ni chombo ambacho huunganisha elementi zote katika utafiti, Ni mkondo kwa jumla wa utafiti (Kombo 2006). Utafiti huu ni wa kifasihi, kwa hivyo kwa kiasi kikubwa ulichukua muundo elezi.Muundo huu unahusu matumizi ya mbinu nyingi katika utaratibu wa ukusanyaji data. Katika hali hii, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake ulifanywa kwa kutumia maneno. Vilevile, matokeo ya utafiti yalielezwa kwa maneno katika sentensi wala si kwa rakamu. Mtafiti alieleza data kuhusu ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba kama alivyoielewa kutokana na nyimbo alizochanganua.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani. Sampuli ya utafiti huu ilipatikana maktabani na mtandaoni. Maktaba yalikuwa mahali mwafaka kwani huhifadhi vitabu na makala mbalimbali ambayo yaliusaidia utafiti huu. Utafiti wa maktaba ulimsaidia mtafiti kupata data aliyohitaji pamoja na kutambua pengo la utafiti. Mtafiti alipata mapitio ya maandishi kuhusiana na suala la utafiti huu. Utafiti wa maktaba ulifanywa ili kupata maelezo ya kimsingi kuhusu nadharia zilizoongoza utafiti huu. Utafiti wa maktaba pia ulimwezesha mtafiti kubainisha tafiti za awali kuhusu nyimbo za jamii ya Akamba. Mtafiti alisakura mtandaoni ili kupakua nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria. Tena utafiti wa mtandao ulimwezesha kupata makala, tasnifu na juzuu zilizochapishwa zinazohusiana na utafiti huu.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Kwa mujibu wa Kothari (1990), walengwa wa utafiti ni watu wote, mtu mmoja au kikundi au elementi zinazokusudiwa kuhusishwa na mtafiti katika utafiti wake. Walengwa wa utafiti ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti (Kothari, 2004; Kombo na Tromp, 2006). Kundi lengwa huhusisha kazi zote ambazo ziko katika mkumbo mmoja na ambazo zina nafasi sawa ya kuweza kuteuliwa kama data ya utafiti. Kazi hizi huwa na sifa moja au zaidi za kimsingi katika utafiti husika. Kwa hivyo walengwa katika utafiti huu zilikuwa ni nyimbo pendwa 24 za msanii Ken wa Maria.

### 3.5 Uteuzi wa Sampuli

Akizungumzia sampuli, Kothari (2004, 1990), anasema kwamba sampuli ya watafitiwa ni kundi ndogo la wasailiwa lililoteuliwa ili liwakilishe hulka za kundi pana ambalo mtafiti anadhamiria kupata data kutoka kwalo. Utafiti huu ulizingatia usampulishaji wa kimakusudi. Usampulishaji wa aina hii huhusisha uteuzi wa sehemu fulani kama eneo la utafiti au watu fulani kama wasailiwa. Creswell (2022), anakuli kwamba usampulishaji wa kimaksudi katika utafiti wa kiuthamano hulenga kuwateua washiriki, maeneo au makala ambayo yatamwongoza mtafiti kikamilifu kuelewa suala lake la utafiti na maswali ya utafiti. Hili halimaanishi usampulishaji wa kishelabela, au kuwateua washiriki wengi na maeneo mengi kama ilivyo katika utafiti wa kiwingidadi. Utafiti huu ulimteua kimaksudi mwanamuziki Ken wa Maria kutoka kwa wasanii kadhaa wa eneo la Ukambani ambao huimba nyimbo pendwa. Hii ni kwa sababu ni msanii mwenye umaarufu mkuu katika eneo la Ukambani. Amefanya mawasilisho mengi katika hafla nyingi kama vile mikutano ya kisiasa, sherehe za harusi pamoja na sherehe za kuadhimisha sikukuu za kitaifa. Ken wa Maria anathamini lugha za kiasili: huimba nyimbo katika lugha ya Kiswahili, Kikamba, Kikuyu na hata Kijaluo. Nyimbo zake huwa zimejaa tamathali za lugha ithibati ya mapenzi yake kwa lugha. Isitoshe, nyimbo zake husheheni maudhui mbalimbali kama vile maudhui ya mapenzi na ndoa, siasa, uzalendo na masuala ya utamaduni na kiuchumi. Mtafiti alitumia sampuli lengwa ambayo ni nyimbo 24 za Ken wa Maria. Idadi hii iliafiki katika kukidhi malengo ya utafiti huu. Mugenda na Mugenda (1999) wanasema kuwa, aina hii ya sampuli hutumika katika utafiti unaolenga kupata habari za kina bila kutoa maamuzi ya kijumla. Kwa hivyo, mtafiti alichagua nyimbo ishirini na nne kimakusudi kwa kuzingatia uzito wa maudhui katika nyimbo pendwa husika kuhusu utaifa wa jamii ya Akamba.

Nyimbo zilizochaguliwa kimakusudi ni zile ambazo Ken wa Maria ametunga na kuimba kati ya mwaka 2004 hadi 2021. Hiki kilikuwa kipindi muhimu nchini Kenya. Kithinji na wengine (2016), wanasema kuwa mwaka wa 1997 hadi 2002 nchini Kenya kilikuwa kipindi muhimu. Ni kipindi ambapo kulikuwa na mfumuko wa kidemokrasia nchini baada ya nchi ya Kenya kukubali mfumo wa vyama vingi. Wananchi walikuwa na nafasi kuu ya kujieleza bila woga na kudai haki zao. Kulikuwa na uhuru wa vyombo vya habari na mfumuko wa utandawazi. Wasanii nao wakachukulia fursa hiyo kuangazia kinaganaga masuala ambayo yalikuwa yanaathiri jamii zao. Kila wimbo ulisimbiwa kwa kodi W kama vile wimbo wa kwanza $W_1$ hadi wimbo wa 24, $W_{24.}$

### 3.6 Ukusanyaji Data

Data ya kimsingi ya utafiti huu ilitokana na nyimbo pendwa 24 za msanii Ken wa Maria. Mtafiti alisakura mtandaoni na kupakua nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria ambazo ameziimba kwa lugha ya Kikamba na kisha kuzihifadhi katika kadi sakima. Kadi sakima zenye nyimbo za msanii Ken wa Maria zilichezwa kwa kutumia tarakilishi. Vilevile, kuna baadhi ya nyimbo ambazo zilisikilizwa kutoka kwa mtandao wa *YouTube* na *Mdundo.com*. Mtafiti alipakua nyimbo zilizokisiwa kuibua mwamko wa utaifa wa jamii ya Akamba, kuzinakili katika daftari na hatimaye kuzitafsiri hadi lugha ya Kiswahili ili mtu asiyeelewa lugha ya Kikamba aweze kuzisoma. Hii ni kwa sababu utafiti huu uko katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti alizichunguza ili kuchanganua arki za utaifa wa jamii ya Akamba, changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba na mbinu za kimtindo ambazo zimetumika katika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria.

### 3.7 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data hutarajia kutimiza malengo ya utafiti na kutoa majibu ya maswali ya majibu (Muriuki, 2013). Mishra (2011), anasema kwamba mtafiti sharti azingatie malengo ya utafiti wake pamoja na mihimili ya nadharia aliyoitumia katika utafiti wake ili kuibuka na uchanganuzi mwafaka wa data ulio na muundo wa kiuthamano. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutegemea malengo ya utafiti huu. Aidha, uchanganuzi wa data uliongozwa na mihimili ya nadharia ya utaifa na ile ya umitindo. Mtafiti alichanganua data kwa hatua tatu. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuchuja nyimbo kulingana na tasinia ya maisha

zinazohusu. Hatua ya pili ni kudondoa vifungu vya maneno vilivyokisiwa kubeba dhana ya utaifa na vile vinavyoonyesha udhalilishaji wa utaifa. Hatua ya tatu ilikuwa kutoa fasili ya kifalsafa kuhusu maana za vifungu vya maneno yanayobeba dhana ya utaifa, mbinu za kimtindo zilizotumika kuwasilisha ujumbe wa utaifa wa jamii ya Akamba na changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba.

### 3.8 Uwasilishaji wa Data

Data iliyokusanywa na kisha kuchanganuliwa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo yaliyotumia sentensi. Mtafiti aliwasilisha matokeo kuhusu utaifa katika jamii ya Akamba kwa kuzingatia nyimbo pendwa ishirini na nne za msanii Ken wa Maria. Katika kufanya hivi, mtafiti aliweka wazi arki za utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria. Pili, alionyesha mbinu alizotumia msanii katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Pia, alibainisha changamoto ambazo zinakumba utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria.

### 3.9 Maadili Wakati wa Utafiti

Maadili wakati wa utafiti ni mambo ambayo huongoza utafiti na huzingatia kufuata kanuni zilizowekwa (Mugenda, 1999). Maadili ya utafiti wowote lazima yazingatie: mtafiti mwenyewe, watafitiwa na mchakato wa utafiti (Kothari,2008). Ili kuhakikisha kaida hizi zimefuatwa mtafiti alizingatia yafuatayo: Kwanza mtafiti aliomba kibali cha kufanya utafiti huu katika Halmashauri ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia (NACOSTI). Mtafiti aliweka wazi matokeo ya utafiti. Pia mtafiti amenukuu kazi zote za kitaaluma zinazohusiana na utafiti huu.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia uwasilishaji pamoja na uchanganuzi wa data ya utafiti. Katika sehemu hii data ilichanganuliwa mintarafu ya madhumuni yaliyokuwa yakishughulikiwa na mtafiti. Utafiti huu ulihusisha madhumuni matatu ambayo ni kuchunguza arki za utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria, kuhakiki mbinu za kimtindo zinazotumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria na kupambanua changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba kwa mujibu wa nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria. Madhumuni haya yalichanganuliwa kwa kurejelea nyimbo pendwa ishirini na nne za msanii Ken wa Maria ambazo ziliteuliwa kimaksudi. Kwa kuzingatia kila madhumuni, vigezo mbalimbali vilichanganuliwa kwa kurejelea misingi ya nadharia mbili ambazo ni nadharia ya utaifa na ya umitindo. Mihimili ya nadharia ya utaifa ambayo iliongoza utafiti huu ni wananchi katika taifa ni lazima wawe na uhusiano wa utamaduni moja, watoke jamii hiyo, wawe na uhusiano wa kiutamaduni na kutumia lugha moja ili kurahisisha mawasiliano vilevile kuwa na imani kuhusu miungu yao na mizimu. Mihimili ya nadharia ya umitindo ambayo ilitumika katika utafiti huu ni uchunguzi wa semantiki katika fasihi na kiwango cha muundo wa masimulizi katika makala ya fasihi.

Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Mtafiti aliainisha data yake kwa kutumia kodi maalum kama vile: W= Wimbo, AR= Arki za utaifa, M= Mshororo, katika kuchunguza arki za utaifa ambayo ni madhumuni ya kwanza. Arki mahususi zilizochunguzwa ziliwakilishwa kwa kodi: U=Utamaduni, UT=Utambulisho, S= Siasa, J=Jiografia na H=Historia. Alama MB ilitumika kuwakilisha mbinu za kimtindo ambazo zimetumika katika ujenzi wa utaifa wa Akamba ambayo ni madhumuni ya pili. Vilevile, mbinu mahususi za kimtindo zilizohakikiwa zilisimbiwa kwa kodi kama vile: SM= usimulizi, T= takriri, Ch = chuku, MS = misemo MT = methali, JZ = jazanda, AF= aforisimu, TS = taswira, UM = ulinganisho na mgotanisho, MJ = majazi na MO = motifu.

Data ya swali la tatu pia iliwasilishwa kimaelezo. Kodi zilizotumika kusimbia changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba ni kama vile: CH kurejelea changamoto katika

ujenzi wa utaifa. Kila changamoto ilipewa kodi yake maalum kama vile UTM = utambulisho mpya, UZ = athari za utandawazi, UH= uhamiaji, UK = ukandamizwaji wa ndani na US = ukosefu wa usemi mkuu kisiasa. Kodi zingine zilizotumika kubainisha changamoto ni UJ =ukosefu wa umoja wa kijamii, SU = siasa za utengano na SL = usaliti wa kisiasa.

## 4.2 Usawiri wa Arki za Utaifa wa Jamii ya Akamba

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza arki za utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria. Kwa mujibu wa Kupchan, (1995), arki za utaifa ni sifa zinazoitambulisha jamii kama taifa kama vile: dini, utamaduni wa jamii, lugha moja asilia na jamii kuwa na asili moja. Uchanganuzi wa usawiri wa arki za utaifa katika jamii ya Akamba uliongozwa na mihimili ya nadharia ya utaifa ya Gellener, (1963), ambayo imezibainisha arki za utaifa wa jamii. Hizi ni pamoja na: jamii kuongozwa na utamaduni mmoja, jamii kuwasiliana kwa lugha moja asilia, kuwa na elimu ya mila zao pamoja na mtazamo wa dini yao asilia kama vile kurejelea mizimu na miungu yao. Katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria, imebainika kwamba kuna arki zinazojenga utaifa katika jamii ya Akamba. Arki za utaifa wa jamii ya Akamba zilizochanganuliwa na kuwasilishwa katika sehemu hii ni utamaduni, utambulisho, siasa na uongozi, jiografia na historia.

### 4.2.1 Arki ya Utamaduni

Utamaduni ni jinsi binadamu anavyoyakabili maisha katika mazingira yake. Inajumuisha ujuzi, imani, sanaa, maadili pamoja na sheria na desturi ambazo mtu anajipata kama mwanajamii (TUKI, 2006,). Utamaduni unahusu mila, asili, jadi na desturi za mavazi, vyakula, tabia na maisha ya jamii kwa jumla (Sengo, 1990). Ngugi (1986), anaona utamaduni kuwa mfumo wa maisha wa binadamu ambao wameuamua wao wenyewe katika harakati za kukabiliana na mazingira yao. Ni jumla ya sanaa zao, sayansi yao na jumla ya vitengo vyote vya kijamii, imani yao pamoja na itikadi. Atieno (2019), anasema kwamba utamaduni unahusu asili na jadi za jamii, mila na desturi zao kimavazi, vyakula, tabia na imani. Hii ina maana kwamba utamaduni ni mtindo wa maisha ya watu wanavyoishi, wanavyokula na wanavyovaa. Kila jamii barani Afrika ina utamaduni wake unaoitambulisha na kuitofautisha na jamii nyingine na kuipa mwelekeo. Kupitia tamaduni hizi jamii inapata mwelekeo thabiti unaostahili kuzingatiwa ili kuzuia mikwaruzano.

Utafiti huu ulibaini kuwa nyimbo pendwa za Ken wa Maria zimesheheni elementi za utamaduni ambazo zinajenga utaifa wa jamii ya Akamba. Hizi ni pamoja na ndoa, imani ya jamii, utamaduni wa vyakula na shughuli za kiuchumi.

**4.2.1.1 Usawiri wa Ndoa**

Ndoa ni asasi inayopatikana katika jamii za ulimwengu. Ndoa halali ni ile iliyounganishwa kwa misingi ya kanuni za kitamaduni na kidini (Atieno, 2019). Ndoa ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii za Kiafrika kwani inapanua jamii na kuendeleza ukoo kupitia watoto. Ken wa Maria anatumia utanzu wa fasihi simulizi hasa kipera cha nyimbo pendwa kuuweka bayana utamaduni wa jamii ya Akamba kupitia shughuli za ndoa. Msanii anatumia nyimbo kuelezea imani, mtazamo na mwelekeo wa jamii hii kuhusu umuhimu wa kuzingatia hatua zote za kufunga ndoa. Asasi ya ndoa ni mojawapo ya elementi za utamaduni ambazo zinajenga utaifa wa jamii ya Akamba. Katika wimbo *$W_{19}AR_U$*, msanii anasema:

| | |
|---|---|
| *Nitwisi kwi miao Song'eni Tawa* M6 | Tunajua kuna sheria Songéni Tawa |
| *Miao ila ituite Ukamba kuhusu syathi* M7 | Sheria zile ziko Ukambani kuhusu hafla |

Kupitia kwa wimbo huu sheria za ndoa ambazo jamii ya Akamba imetunga na kufuata tangu jadi zinabainishwa. Anawajulisha wakazi wa Song'eni eneo la Tawa kuwepo kwa sheria ambazo zinaambatana na sherehe ya kufunga ndoa. Anaposema ya kwamba *Nitwisi* (Tunajua), msanii anazungumza kwa niaba ya jamii yake. Neno *Nitwisi* ni wingi wa neno *Ninisi* (ninajua) ambalo linachukulia kwamba watu wote katika jamii wanatambua mila zao. Hii ina maana kwamba suala la ndoa limo katika utamaduni wa jamii yake kwa hivyo kila mwanajamii katika jamii hii anajua makubaliano yaliyopo kuhusu ndoa. Anaendelea na kusema kuwa *Kwi miao, miao ila ituite Ukamba kuhusu syathi* (kuna sheria, sheria ambazo zimekuwapo Ukambani kuhusu sherehe). Sheria anazozungumzia msanii ni kaida za kuzingatiwa katika sherehe za utamaduni wa ndoa na ambazo kila mwanajamii anapaswa kuzielewa. Kwa mujibu wa msanii, sheria hizi ni za jadi (*ituite*-zimekuwapo). Sheria hizi ni bayana kwa msanii na jamii yake. Anaonekana kuzielewa kisha kuzipitisha kupitia fasihi simulizi. Hizi ni sheria ambazo msanii na wenzake wamejifunza kupitia utangamano na wanajamii wenzake. Suala la ndoa linasawiriwa kama sehemu ya utamaduni wa Akamba. Jamii iliyo na utaifa sawa huwa na kaida ambazo kila mwanajamii

hufuata. Sheria za ndoa zinajenga elementi ya utamaduni ambayo ni sehemu muhimu katika ujenzi wa utaifa. Msanii anaweka wazi utaratibu wa kufunga ndoa ya Kikamba. Katika mshororo $M_{11:}$ *Tukoka na mbui itatu sya ntheo Tawa M11,* msanii anazungumzia kuhusu sherehe mojawapo muhimu ya ndoa inayojulikana kama *ntheo* (kulipa mahari). Utaifa wa jamii unajitokeza kwa vile msanii anatuarifu kwamba hii ni hafla ambayo itahitaji mchango na umoja wa wanajamii. Jamii iliyo na utaifa huwa na ujima wa utamaduni. Katika $M_{2,}$ *Tutwaite Mbasu uthonini Tawa* (Tunapeleka Mbasu kwa shemeji zake Tawa), Mbasu atahitaji mchango wa marafiki zake ambao ni msanii na Nzungu. Wanahitajika waandamane naye kama washenga hadi kwa wakwe zake katika hafla ya kulipa mahari. Katika jamii yenye utaifa huwa kuna kaida na miiko ambayo huiongoza. Jamii hii inaelekea haimtarajii Mbasu kwenda kuwatembelea akiwa pekee. Lazima aandamane na wandani wake katika kutekeleza shughuli hii. Ushirikiano wa wanajamii unasisitizwa hapa. Ingawa ni rahisi kwa mwanajamii kutembea pekee yake, jamii haimtarajii kufanya hivyo kwa vile itakuwa kinyume na sheria zilizowekwa. Ushirikiano wa wanajamii katika sherehe hii utajenga misingi imara ya undugu na utaifa kwa jumla.

Kwa mujibu wa msanii, mchango wa marafiki huanzia katika posa. Msanii anatupa taswira ya namna sherehe hii huwa. Hatua ya kwanza katika sherehe ya ndoa anaibainisha kama posa. Mvulana anapomtambua msichana anayempenda na kutaka kumchumbia, humtuma rafiki yake ili kuwasilisha ujumbe wa posa. Msanii anasema katika $W_2 AR_U$:

| | |
|---|---|
| *Návíká Kibwezi nìèndà úkwíà nyíè nínōníé ngèthé* | Nilipofika Kibwezi niliona msichana |
| *Múkōsí ná Téké yù nínyw'é ándú álá ngútúmá,* | Mukosi ukiwa na Teke nitawatuma |
| *Músémbé Kásàyàní múnéééné mwìná Ngémí* | Mwende Kasayani muongee na Ngemi |

Wajibu wa mwanajamii aliye na azma ya kuoa unafafanuliwa. Msanii amemtambua msichana wa kuposa kwa jina *Ngemi*. Baada ya kumtambua msichana wa kumchumbia, anatuma marafiki wake ili wapeleke ujumbe. Katika wimbo huu msanii anawatambulisha Mukosi na Teke kama wajumbe wake ambao watatembelea familia ya Ngemi kutoa ujumbe kwa niaba yake kuhusu azma yake ya kutoa posa. Msanii anawahusisha marafiki wake wa karibu katika hatua hii muhimu katika maisha yake shabaha ikiwa ni kuchunguza usuli na mienendo ya msichana aliyemtambua iwapo ana maadili mema na iwapo angemfaa kama mke. Ushirikiano huu wa wanajamii ni muhimu katika ujenzi wa utaifa wa

jamii. Msanii anaisawiri jamii ya Akamba kama iliyo na mpangilio maalumu ambapo kila mwanajamii huwa na majukumu yake.

Sheria nyingine katika utamaduni wa ndoa za jamii ya Akamba inajitokeza kupitia hafla ya *Ntheo* (kulipa mahari) ambayo msanii anaisawiri katika $W_{19}AR_{U}$. Atieno (2019), anasema kwamba utamaduni wa Kiafrika unapendekeza ushirikianaji wa familia za pande mbili katika mjadala wa ndoa na sherehe kama ulipwaji wa mahari. Jambo hili huhakikisha kwamba kila familia imehusishwa katika ndoa hiyo kwa njia moja au nyingine. Ndoa ni asasi inayojenga uhusiano mpya baina ya familia za pande mbili husika. Uhusiano huu hujengwa kupitia sherehe za harusi, kutembeleana na kupeana zawadi pamoja na sherehe za posa (Kyalo, 2011). Azma ya hafla ambayo Mbasu ameandaa kwa wakwe zake katika wimbo $W_{19}$ inabainishwa kama kulipa mahari. Anazungumzia kuhusu zawadi ambazo mwanamume anayeoa hutoa kwa wakwe zake. Baadhi ya zawadi muhimu ambazo hutolewa wakati wa sherehe hii ya kwanza katika ndoa zinabainishwa: Mbuzi watatu pamoja na pombe ya kienyeji aina ya *kaluvu*. Msanii anaposema katika mshororo $M_{11,13}$ *Tukoka na mbui itatu sya ntheo Tawa*, *Na kaluvu ko kaitiwa kyathini Tawa (*Tutakuja na mbuzi watatu wa mahari Tawa, na pombe haitawachwa tukija Tawa), anabainisha matarajio ya wanajamii katika hafla hii. Msanii anadhihirisha kwamba ukamilifu wa sherehe ya *ntheo* ni kuwepo kwa pombe aina ya *kaluvu* na mbuzi watatu wanaotolewa kutoka kwa familia ya mwanamume anayeposa. Bila ya haya sherehe haiwezi kukamilika. Utamaduni wa kupokezana zawadi baina ya familia hizi mbili ni ishara kwamba zimekuwa moja.

Utamaduni ambao unakubalika na jamii mbili zinazohusika hapa unakubalia mwanamume anayeoa kutoa zawadi hii kama ishara ya ombi la kutaka posa yake ipokelewe. Msanii anabainisha wazi idadi ya mbuzi ambao wanastahili kukabidhiwa wakwe. Kwa mujibu wa matini hii, mbuzi hawa ni sharti wawe watatu au zaidi ila wasipungue. Utoaji wa mahari kama sehemu ya ndoa ya Akamba unaleta upekee wa utamaduni unaojenga utaifa wao. Musili (2022), anasema kwamba wakwe wanapowakubali na kuwapokea hao mbuzi watatu, hatua inayofuata ni kumchinja mbuzi mmoja ambaye ni beberu ili kuthibitisha kuwa uhusiano kati ya familia hizi mbili umekubalika. Jamii iliyo na utaifa huwa na sherehe za miviga (Maelo, 2014). Katika jamii ya Akamba msanii amewasilisha suala la

miviga kwa kusema kwamba wakipeleka mahari watatoa kafara kwa kumchinja mbuzi mmoja ili kumwaga damu. Hii ni miviga. Haya yanadhihirika katika wimbo $W_{19}AR_{U}$, mshororo $M_{12}$ anaposema: *Na mbui imwe iyita nthakame kyathini Tawa (*Na mbuzi mmoja tuchinje amwage damu katika hafla Tawa).

Hatua inayofuata ni unywaji wa pombe ya kienyeji kwa jina *kaluvu* ambayo msanii anasema ni muhimu katika hafla kama hii. Anasema: *Na kaluvu ko kaitiwa kyathini Tawa, makunde Tawa* (na kaluvu haiwezi achwa katika hafla Tawa, wanywe Tawa). Anaposema kuwa pombe haiwezi kosa kuwepo katika hafla hiyo, anaonyesha umuhimu wa kinywaji hicho katika hafla husika. Mojawapo wa umuhimu wake ni kuwaleta watu pamoja na kushiriki chakula hicho pamoja. Kwa mujibu wa Vatika (2018), pombe ni kiungo muhimu cha kuwaleta watu pamoja katika sherehe mbalimbali za kijamii. Kupitia haya, utaifa wa jamii unajengwa. Ingawa msanii hasemi waziwazi kuhusu bibi harusi, inakuwa bayana kwamba hii ni safari ambayo hufungwa na bwana harusi na aila yake kwenda kuwatembelea wakwe zake. Muktadha ambapo sherehe hii ilifanyika umebainishwa kwamba ni nyumbani kwa bibi harusi katika eneo la Song'eni, Tawa. Sherehe hii haifanyiki kwingine kokote. Umuhimu wa utamaduni huu kuhusu ndoa ni kwamba unajenga misingi thabiti ya utaifa wa wanajamii wa Akamba.

Ndoa ni mojawapo wa hatua muhimu katika maisha ya mwanajamii. Kila mwanajamii hutarajiwa kuoa au kuolewa kwani ndiyo njia pekee ya kuendeleza kizazi. Ndoa za Kiafrika hukamilika watoto wanapozaliwa. Nyamongo (2020), anasema shughuli za ndoa ni kama maigizo ambapo kila mwanajamii ni mwigizaji kwa hivyo kitendo cha kuoa au kuolewa ni jukumu na mpigo ambao kila mwanajamii anapaswa ashiriki. Ikiwa mwanajamii atakosa kuoa au kuolewa katika mazingira ya kawaida, hukataliwa na jamii. Suala la ukapera halikubaliwi katika jamii ya Akamba na hupigwa vita. Katika $W_{14}AR_{U}$ msanii anasema:

| | |
|---|---|
| *Kithio kitu kya Mwafrika no mbaka aume tutwaane M1* | Desturi yetu ya Mwafrika ni sharti wanaume waoe |

Kulingana na matini hii, ni mila na desturi kwa wanaume wa Kiafrika kuoa. Ingawa kauli hii hairejelei jamii ya Akamba kwa ubayana, ni vyema ieleweke kwamba Akamba ni mojawapo wa makabila ya kibantu ambao wanaishi katika bara la Afrika na hasa Afrika Mashariki. Kauli hii ni nzito na huenda isiwe kweli kwa baadhi ya jamii za Kiafrika. Kuna

sababu ambazo zinaweza kumpelekea mwanamume kupendelea maisha ya ukapera. Msanii anaonekana kupuuza haya na kutoa kauli tata kama hii. Msanii anatilia mkazo suala la ndoa za kitamaduni na hatua zinazofuatwa katika utekelezaji wake kwa vile anataka kuonyesha umuhimu unaohusishwa na asasi ya ndoa katika ulimwengu ambao umeathiriwa na utandawazi. Anaposema *no mbaka* (ni sharti) ana maana kwamba ni jambo la lazima na lisiloepukika. Anaona kwamba hakuna mwanajamii ambaye hastahili kuoa au kuolewa. Msanii anazungumzia kuhusu desturi za Kiafrika ambamo jamii ya Akamba imechipuka. Kile msanii anachosema ni kwamba ili jamii kupanuka, lazima wanajamii wakumbatie njia asilia za kuunda jamii kama vile ndoa. Ni katika ndoa ambapo wanajamii wapya huchipuka kupitia watoto wanaozaliwa.

Msanii anaielekeza jamii ya Akamba kurejelea utamaduni wao asilia ambapo asasi ya ndoa ilipewa nafasi kubwa katika jamii ikilinganishwa na sasa ambapo vijana wengi wanaonekana kuenzi maisha ya ukapera kuliko ya ndoa. Jamii inayoundwa ndicho kitovu cha taifa na utaifa. Wazo hili linajenga dhana kwamba ili kuwepo na utaifa wa taifa, lazima kuwe na utaifa wa jamii. Masuala ambayo hujenga utaifa wa taifa kuu huchipuka kutoka kwa utaifa wa jamii. Msanii anaweka wazi imani ya jamii yake kuhusiana na utamaduni wa ndoa. Mwanzo, anasema ni suala la lazima. Hii ni kwa sababu ni kupitia kwa ndoa ambapo kizazi kipya kinaweza kupatikana na kuendeleza jamii husika.

Utamaduni wa jamii ya Akamba unamtarajia mwanamume kuoa nje ya ukoo wake. Ndoa baina ya ndugu wa karibu haziruhusiwi. Msanii anawatuma marafiki wake waende Kasayani mbali na mji wake ambako amepata mchumba ($W_2AR_U$). Anasema:

| | |
|---|---|
| *Múkōsí ná Téké yù nínywíé ándú álá ngútúmá M9* | Mukosi pamoja na Teke nitawatuma |
| *Músémbé Kásàyàní múééné mwìná Ngémí M10* | Muende Kasayani muongee na Ngemi |

Katika mshororo $M_{1,}$ katika wimbo $W_2AR_{U,}$ msanii anasema *Navika Kibwezi* (Nilipofika Kibwezi) alimwona msichana mrembo na alipomwuliza rafikiye, akaelezwa ya kwamba anaitwa Ngemi. Hii inadhihirisha kwamba eneo hilo ni geni kwa msanii kwani alikuwa amelizuru. Kwa hivyo anaoa mbali na asili yake kama ilivyo utamaduni wa Akamba. Kuoa kutoka sehemu za mbali kunachangia kujenga mahusiano ya mbali na hivyo kupanua familia ya jamii. Hili linachangia ujenzi wa utaifa wa jamii.

Msanii katika wimbo $W_{14}$ $AR_U$ anatoa ushauri kuhusu ndoa kwa vijana. Katika mshororo $M_3$, anasema *Kitema Tsunami ena mama yake* (Kitema Tsunami ana mke wake). Anamtambua mwanabendi wa Yatta, Kitema Tsunami kwa kuchukua hatua ya kuingia katika ndoa na msichana Mluhya ambaye wamejaliwa mtoto. Anawahimiza vijana ambao anafanya kazi nao kuingia katika asasi ya ndoa ili wawe wanaume wa kutegemewa duniani. Anachukua nafasi yake kama msanii kuwashauri vijana kuhusu umuhimu wa ndoa kwani itawafanya kuwa kielelezo cha kutegemewa duniani baada ya kuingia katika ndoa. Anasema; *Nienda squad ya Yatta mutwaane ta Kitema* $M_7$ (Nataka kikosi cha Yatta muoe kama vile Kitema). Suala la uongozi katika makundi ya kijamii linabainishwa kwa vile msanii ndiye kiongozi wa bendi ya Yatta. Msanii anaonyesha uongozi kwa kuchukua jukumu la kufanya maamuzi muhimu ya kijamii kuhusiana na masuala muhimu ya kijamii kama vile ndoa. Anawahimiza vijana wa Bendi ya Yatta waoe. Hili linatokea kama agizo kutoka kwa mtu mwenye mamlaka kwa watu wengine ambao wana uwezo mdogo kuliko yeye. Anatarajia agizo hili litekelezwe na wasemewa. Katika muktadha huu, msanii anazungumza kama baba wa vijana ambao wanafanya kazi naye katika Bendi ya Yatta. Anatarajia wafuate agizo lake na kutekeleza wajibu wao wa kijamii. Kupitia fasihi simulizi, msanii anachukua jukumu la mlezi na kuwashauri vijana ambao wanaimba muziki naye katika bendi yake ya Yatta kwamba hata wao waoe kama alivyofanya mwenzao Kitema Tsunami. Suala la ndoa linatiliwa mkazo na ndio maana katika mshororo $M_{10-16,}$ msanii anaradidi maneno *ndutwaane* (oa) huku akiwataja wanabendi wake. Uradidi huu katika matini yafuatayo unaashiria msisitizo wa maudhui ya ndoa:

| | |
|---|---|
| *Kating'anya ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM10* | Kating'anya oa, oa |
| *Kalulu ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM11* | Kalulu oa, oa, oa |
| *Kanyari ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM12* | Kanyari oa, oa, oa |
| *Shughuli ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM13* | Shughuli oa, oa, oa |
| *Savimbi ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM14* | Savimbi oa, oa, oa |
| *Mumina ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM15* | Mumina oa, oa, oa |
| *Kitunusi ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM16* | Kitunusi oa, oa, oa |

Katika matini hii, msanii anaisawiri ndoa kama kitovu cha kuendeleza kizazi. Kuwapata watoto katika jamii ya Akamba linakuwa jambo la fahari. Katika wimbo $W_{14}$ $AR_U$ anasema:

| | |
|---|---|
| *Nina utanu mwana wa Katoko ena kiveti* M2 | Nina furaha mwanawe Katoko ameoa |
| *Mena kana kavisi kailye Kitema copyright Wana*M3 | Mtoto mvulana anayefanana na Kitema |

Msanii anasema ya kwamba familia ya Kitema wana furaha kwa kumpata mwana. Wanashangilia baada ya mke aliyeolewa kupata mtoto. Hii ina maana kwamba jamii hii inatarajia vijana kuoa na kupata watoto ili jamii yao ipanuke. Watoto huenziwa na utasa kukashifiwa (Ngila, 2012). Iwapo jamii inaendelea kukua, basi utaifa wa jamii husika huwa umehakikishiwa kwa vile watumizi wa lugha ya jamii wataendelea kuongezeka. Msanii anafurahia ya kwamba baada ya kijana Kitema kuoa, Wamezaa mtoto mvulana ambaye ataendeleza kizazi chake.

Suala la ndoa linapewa uzito katika jamii hii na linaonekana kama linaloleta furaha kuu kwa wanajamii. Matarajio ya kijamii kwa wanandoa ni kuendeleza kizazi chao na hivyo kuifanya jamii kukua. Utamaduni wa msanii haupendekezi vijana kuzaa nje ya ndoa (Musili, 2022). Msanii anaelekea kuthibitisha haya katika $W_{14}AR_U$ anaposema kuwa *Mena kana kavisi kailye Kitema copyright* (Wana mtoto mvulana anayefanana na Kitema). Linakuwa jambo la aibu iwapo msichana au mvulana atapata mtoto nje ya ndoa. Utamaduni kama tabia ambazo mja hujifunza kupitia wanajamii wenzake unawafunza wanajamii hawa kuwa na maadili mema kabla ya ndoa na pia katika ndoa. Mtoto aliyezaliwa anafanana na babake shilingi kwa ya pili hivyo kuiletea jamii yake fahari kuu. Maadili ndiyo yatadumisha utaifa wa jamii yoyote ile. Isitoshe, msanii anabainisha utamaduni unaoambatanishwa na jamii kupata mtoto wa kiume. Katika wimbo huu, si mtoto tu aliyezaliwa bali ni wa kiume. Suala la jinsia ya mwanajamii mpya aliyejiunga na jamii hii linatiliwa mkazo. Kuzaliwa kwa mtoto wa kiume kunailetea jamii hii furaha kuu. Msanii anasisitiza umuhimu unaohusishwa na kupata mtoto wa kiume katika jamii ya Akamba. Ni kupitia kwa mtoto wa kiume ambapo kizazi kitaendelezwa.

Msanii anaelekea kuunga mkono ndoa mseto katika jamii. Katika jamii ya msanii, ni bayana kwamba suala la mvulana kuoa nje ya ukoo wake au kabila lake linakubaliwa. Katika $W_{14}AR_UM_4$, msanii anasema *Na nuseo nundu ena Mbaluya na ni ndumu* (ni vizuri ameoa Mluhya na mwenye nguvu). Kupitia maelezo haya, tunaelewa kuwa kijana Kitema amepata mke nje ya kabila lake la Akamba. Amepata jiko kutoka jamii ya Abaluhya.

Mahusiano ya kijamii yanajengwa kupitia ndoa hii. Kutokana na ndoa hii mseto, jamii ya Akamba inaendelea kukua kupitia kuongezwa kwa mwanajamii mpya kutoka jamii ya Abaluhya. Musili (2022), anasema kwamba katika jamii ya Akamba, watoto huwa wa baba kwa hivyo watoto watakaopatikana kupitia ndoa hii mseto watakuwa Wakamba. Hivyo basi mvulana anapooa ni hakikisho kwamba familia yake imepanuka. Yule mke na watoto wanapata utambulisho wa familia ya upande wa kuumeni si kuukeni. Kwa vile Kitema ameoa kutoka nje ya jamii yake, mke na watoto wake wanapata utambulisho wa jamii ya Akamba. Hili linakuza utaifa wa jamii ya Akamba. Kwa upande mwingine, matarajio ya jamii ya msanii kuhusu sifa za mke wa kuoa yanafafanuliwa. Katika mshororo huu, tunaelezwa sifa za mke wa Kitema kwamba ni mwenye bidii kazini, mwenye siha njema, mwaminifu, mwenye nguvu na mrembo. Msanii anabainisha baadhi ya sifa ambazo wanajamii wanatarajia mke anayeolewa kuwa nazo. Hizi ni sifa ambazo mvulana anayetaka kuoa atazingatia. Matokeo ya ndoa hii ni kupata watoto ambao watakuwa na sifa zizi hizi na hivyo kuchangia uendelezaji wa jamii ambayo ni imara.

Kwa upande mwingine, taifa la Akamba linatambulishwa kama linalokubalia suala la utala. Utala ni hali ya mwanamume kuoa wake wengi. Anasema: $W_{20}AR_U$

| | |
|---|---|
| *Matwaie mama wetina sweet Bernedetta* M4 | Wampelekee mke wake wa mwisho sweet Bernedetta |

Katika mshororo huu, msanii anamtambua mke wa mwisho kama Benedetta. Hili lina maana kwamba utamaduni wa jamii ya Akamba umewakubalia wanaume katika jamii hii kuoa wake zaidi ya mmoja. Katika mshororo $M_{13\text{-}17,}$ msanii amewataja wakewe wengine kama Mumo na Angela. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Mumo we nduthi, uathime Mbonge(M13)* | Mumo enda ubariki Mbonge |
| *Angela nduthi, uathime Mbonge (M14)* | Angela enda ubariki Mbonge |

Msanii kama mwanajamii wa taifa la Akamba anaendeleza ndoa ya utala. Bernedetta, ambaye ni mkewe wa mwisho, anasifiwa na mume wake kwa kumzalia mtoto mvulana, jambo ambalo linamletea msanii fahari kuu katika jamii. Mtoto wa kiume anapewa hadhi kubwa katika utamaduni wa jamii hii. Katika ndoa za utala inabainika kuwa kuna uke wenza unaoendelezwa na taifa la Akamba. Uke wenza ni uhusiano baina ya wake katika ndoa ya mume mmoja. Katika mfumo wa ndoa za mitala, mwanamume anaweza kuwa na wake wengi na watoto wanaweza kuzaliwa na wake tofauti. Hii inaunda mizizi mingi ya

kijamii ndani ya jamii. Haya ni kupitia kueneza ukoo na kufungamanisha familia nyingi katika mtandao wa mahusiano ya kifamilia. Katika mishororo $M_{13,14}$, msanii anamwambia Mumo vilevile Angela ambao ni mke wake wa kwanza na wa pili waende Mombasa kwa mamake Mbonge (Bernedetta) ili waweze kumbariki mtoto Mbonge ambaye ndiye amezaliwa. Ni bayana kwamba wake wote wana uhusiano mwema. Hili linathibitika wakati msanii anapomtuma mke wake wa kwanza, Mumo na wa pili Angela kwenda kumtembelea mke mwenza mjini Mombasa baada ya kujifungua. Mahusiano haya mazuri ya kijamii yanachangia kujenga familia dhabiti ya msanii na kuchangia utaifa wa jamii pana kwa jumla. Hili linaonyesha uhusiano mwema ambao upo katika jamii hii. Inaelekea wake wake wa kwanza hakuweza kupata mtoto mvulana hivyo basi msanii akamwoa mke wa mwisho ambaye amefanikiwa kujifungua mtoto mvulana. Msanii anaonyesha jinsi ushirikiano kupitia ndoa za mitala na uke wenza zinavyochangia ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

Upekee uliopo kwa taifa la Akamba ni kwamba wake katika ndoa ya utala wamepewa majukumu mbalimbali. Kupitia wimbo $W_{20}AR_U$ msanii anabainisha Jukumu la kwanza kama kuwabariki watoto wa wake wenza. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Mumo we nduthi, uathime Mbonge* | Mumo sasa nenda, ukambariki Mbonge |
| *Angela nduthi, uathime Mbonge* | Angela wewe nenda, umbariki Mbonge |
| *Osa syana syaku, Mum na Susu* | Wachukue wanao, Mum na Susu |
| *Mwitike Mombasa, mwathime Mbonge* | Mfike Mombasa, mkambariki Mbonge |
| *Musyi witu ni munene Twongela Mbonge* | Boma yetu ni kubwa Kuongeza mbonge |

Msanii anawataka wakewe, Mumo na Angela kwenda Mombasa kumbariki mtoto aliyezaliwa na mke wake wa mwisho. Majukumu zaidi ya wake katika ndoa za mitala yanabainishwa katika mishororo $M_{15-21}$ msanii anaposema:

| | |
|---|---|
| *Inyaa Mbonge, wonane na Mumo* | Mama mbonge muonane na mumo |
| *Wonwe kitheka kyaku Matuu* | Muonyeshe shamba yako Matuu |
| *Ve kitheka kyaku wakie Mbonge* | Kuna shamba ujengee Mbonge |

Matini haya yanabainisha majukumu mengine ya wake katika ndoa ambayo ni pamoja na kuzaa watoto, kuwapokea wanajamii wapya katika familia, kuwaonyesha mali ya familia, kuwajengea watoto makazi, kumpokea mke wa pili pamoja na kuwafunza umoja wa

kijamii. Majukumu haya ya wanawake katika ndoa za mitala yanaonyesha utamaduni wa Akamba unaokuza utaifa wao.

Ndoa za mitala zinachangia kupanuka kwa jamii na hivyo kujenga utaifa wa jamii ya Akamba. Msanii katika $W_{20}AR_U$ anasema:

| | |
|---|---|
| *Nundu we Mbonge ni wa nyumba nene* M10 | Kwa sababu Mbonge ni wa nyumba kubwa |
| *Ongela aume nyumba ya wa Maria* M11 | Ameongeza idadi ya wanaume katika nyumba ya wa Maria |
| *Musyi witu yu ni munene twongela Mbonge* M17 | Boma yetu sasa ni kubwa tumemwongeza Mbonge |
| *Musyi witu nienda uneneve twithwae na vinya* M21 | Nataka boma yetu ipanuke tuwe na uwezo. |

Msanii anatumia msemo *nyumba nene* (nyumba kubwa) kuisawiri jamii yake kama iliyo na idadi kubwa ya watu na utajiri. Kuzaliwa kwa mtoto Mbonge kumechangia kupanuka kwa familia ya msanii. Anaionea fahari jamii yake kwa kuongezeka kwa watoto. Wingi wa watu unakuwa rasilimali muhimu kwa jamii ya Akamba. Kisiasa, wingi wa watu inamaanisha uwezo mkubwa kisiasa hasa wakati jamii inapohusishwa katika maamuzi ya kisiasa kama vile upigaji kura. Pili, inaihakikishia jamii ugamvi mkubwa wa rasilimali za kitaifa. Isitoshe, shughuli za kijamii hazitakwama kwa sababu kutakuwa na watekelezaji wa shughuli mbalimbali za kijamii. Jamii inashangilia wakati wanapopata nyongeza ya wanajamii. Idadi ya wanaume katika familia hii imeongezeka na hivyo msanii anaona kwamba watakuwa na nguvu. Katika tamaduni nyingi za Kiafrika ukiwemo utamaduni wa jamii ya Akamba, jinsia ya kiume huhusishwa na uwezo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kijamii, wanaume hujukumika kuilinda jamii kutokana na hatari zinazoikumba jamii kutoka nje na hata ndani kwa ndani. Kuzaliwa kwa mtoto wa kiume kunachangia kudhibiti usalama huu. Uwezo wa kiuchumi pia unathibitika kupitia shughuli za biashara ambazo hutekelezwa na wanaume. Msanii anaposema kwamba boma yao imekuwa kubwa kwa vile wamemwongeza Mbonge, anadhihirisha fahari na umuhimu unaohusishwa na jinsia ya kiume. Msanii anazungumzia kuhusu nafasi ya mwanamume katika jamii hii. Mwanamume anahusishwa na uongozi, ulinzi wa jamii, uchumaji na kuendelezwa kwa ukoo wa mhusika. Msanii anafurahia ya kwamba kitovu chake hakitadidimia kwa vile mtoto wa kiume baadaye ataoa na kupata watoto ambao wataongeza idadi ya wanajamii. Huu ni uwezo wa kijamii. Kutokana na ndoa za mitala, wanajamii wanakuwa na uwezo

mkubwa wa kupata watoto wa kiume ambao watachangia katika kuendeleza kizazi chao ambacho kitaendeleza mila na tamaduni za jamii yao. Kupitia hayo, utamaduni wa jamii ya Akamba utadumishwa.

#### 4.2.1.2 Imani za Kijamii

Kwa mujibu wa Mung'ala (2020), nguzo mojawapo ya nadharia ya utaifa ni imani ya jamii katika miungu na mizimu. Kupitia kwa nyimbo pendwa za Ken wa Maria, ilibainika kuwa utaifa wa jamii ya Akamba unajengwa kupitia imani za kishirikina. Msanii anarejelea imani za kishirikina za Akamba anapokuwa katika harakati za kumtongoza msichana mmoja ambaye ni Mkorea. Ana hofu kuwa huenda akamkosa kutokana na wasifu wa usuli wa msichana huyu. Katika wimbo $W_8$ $AR_U$ msanii anasema:

| | |
|---|---|
| *Ínyiá ni múkóréā nā íthē nī Mùmàsãì* M1 | Mamake ni Mkorea na baba ni Mmasai |
| *Ēendã nìvãndē ítúmô nã āìndēmbēsyā Korea* M2 | Anataka nipande mkuki kisha anitembeze Korea |
| *Nākwã nōtāngùkìā Kãrãtá sya Kikorea* M3 | Na mimi ni kama naogopa karate za Korea |
| V*új*o *syā kìmásãi namina uvanda itumo* M4 | fujo za Kimasai, nikimaliza kupanda mkuki |

Katika kifungu hiki, wasifu wa jamii mbili ambazo zinaishi katika nchi mbili tofauti unasimuliwa. Kwa upande mmoja, kuna wasifu wa jamii moja ya Kiafrika ambayo ni Wamasai na nyingine kutoka bara la Asia, Wakorea. Wakorea wanasifika kutokana na mitindo yao ya kupigana ya *karate*. Wamasai kwa upande mwingine wanasifika katika vita kwa kutumia mikuki. Kwa mujibu wa msanii, jamii hizi mbili zinapenda vita. Anaona kwamba zina uwezo mkubwa wa kivita zikilinganishwa na jamii yake. Utamaduni wa jamii hizi ni tofauti na utamaduni wake na hilo linamtia hofu.

Kwa vile msichana huyu ni zao la ndoa mseto baina ya Mmasai na Mkorea, msanii anahofu kwamba huenda akashindwa kumthibiti msichana huyu. Anamwona kama mwenye uwezo kuliko yeye. Msanii anamsawiri msichana huyu kama mwenye hasira kutokana na usuli wa babake kuwa Mmasai, na aliye na uwezo wa kupigana miereka kama walivyo wakazi wa Korea ambako mamake ana asili. Ana hofu kuwa huenda njama yake ya kumwoa huyu msichana itibuke hivyo basi kukosa fursa ya kutembea Korea. Yeye ana imani katika miungu na mizimu ambao anaona watampa uwezo wa kukabiliana na hali yake ya sasa. Msanii anathibitisha imani yake katika nguvu za mizimu na miungu anapofanya uamuzi

kwamba atasafiri hadi sehemu za Kitui ambako atatafuta hirizi; nguvu za kumwezesha kumpata huyu msichana ndiposa lengo lake litimie. Msanii anasema:

| | |
|---|---|
| *Nìãmbã níthì Kìtūî nãmbē nímánthē ìtítí* $M_9$ | Nataka kuenda Kitui nitafute hirizi |

Anatambulisha eneo la Kitui kama maeneo mojawapo ya Ukambani yanayoendeleza ushirikina. Baada ya kuzipata hirizi, msanii anasema kwamba atamrushia usiku wakati wa kushiriki tendo la ndoa. Imani ya jamii hii katika nguvu za ushirikina inadhihirika. Hizi ni nguvu ambazo si za kawaida na anaamini kwamba zina uwezo wa kumtuliza yule msichana wakati anapotenda tendo la ndoa au kutoa posa. Inabainika kwamba nguvu hizi hazionekani waziwazi lakini zina uwezo wa kumdhibiti binadamu.

*Ititi* (hirizi), ni nguvu anazopewa mja na mganga ili kumwezeshe kutenda mambo ambayo hayawezekani kwa binadamu wa kawaida. Msanii anarejelea watu ambao ni muhimu katika uendeshaji wa shughuli za kiimani za jamii hii. Ndisya (2015), anasema kwamba katika jamii ya Akamba, kulikuwa watu ambao walipewa umuhimu mkubwa katika jamii. Hawa ni pamoja na waganga (Mundu mue [umoja] Andu awe [wingi]), watabiri (Athani), mizimu (Aimu) na wazee wa koo (atumia). Hawa walikuwa na majukumu bainifu kwa wanajamii. Jamii iliwahusisha wakati wa kufanya maamuzi yoyote muhimu. Iwapo jambo fulani lingemwia vigumu mwanajamii, angekimbia kwa mganga ili apate utatuzi na mwelekeo.

Katika wimbo $W_8$ $AR_U$, msanii anaisawiri jamii yake kama iliyopata changamoto geni kutokana na utandawazi. Jamii yake imevamiwa na utamaduni mgeni ambapo mwanamke anatoa posa kwa mwanamume. Katika mishororo $M_{3-4}$ anasema:

| | |
|---|---|
| *Ēendã nìvãndē ítúmô nã āìndēmbēsyā Korea* | Anataka nipande mkuki kisha anitembeze Korea |

Hili ni suala geni ambalo limezuka katika karne ya 21. Mwanamke anaonekana kuchukua usukani katika majukumu ambayo awali yalikuwa ulingo wa mwanamume. Mwanamke anajitokeza kama mwenye uwezo mkubwa wa kijamii na pia kiuchumi. Anaonekana kuchukua majukumu ambayo awali yalionekana kutekelezwa na mwanamume katika jamii. Kitamaduni, wanaume ndio huwa na jukumu la kuwaandama na kuwapa posa wasichana. Wanaume huwa wachumi na hutekeleza majukumu ya kiuchumi kwa familia

zao. Kupanda mkuki ni jazanda ya mwanamume kutenda kitendo cha ndoa. Huwa ni shughuli ya mwanamume wala si ya kike.

Mwanamke katika utamaduni wa Akamba hawezi kupanda mkuki. Ni bayana mwanamke anayezungumziwa hapa amekiuka tamaduni hizi na kuwezeshwa kiuchumi na kijamii ambapo anaonekana kusema anayotaka yafanyike bila woga kama vile kumtaka yule mwanamume kimapenzi na kumwambia hadharani pasi na woga. Huyu ni mwanamke jasiri ambaye hajafungwa na mila na tamaduni za jamii. Ni mwanamke ambaye amepevuka kimawazo na kiuchumi. Anaona ya kwamba baada ya kumpata msanii atamtembeza kwao Korea. Huu ni uwezo wa kiuchumi. Huyu mwanamke wa kisasa ambaye ana asili mseto ana uwezo kiuchumi wa kumpeleka msanii hadi nchi za ughaibuni ili kumtembeza. Hamtegemei mwanamume ili kufanikiwa katika hili. Anaonyesha uhuru wake wa kiuchumi. Katika mshororo $M_{5-7}$, msanii anaona kwamba utamaduni wa jamii umekiukwa na ana hofu kuu kwamba hili ni hatari kwa jamii yake. Anakuli:

| | |
|---|---|
| *Nākwã nōtāngùkìā Kãrãtá sya Kikorea* | Na mimi ni kama naogopa karate za Kikorea |
| *Vújo syā kìmásãi namina uvanda itumo* | Fujo za Kimasai nikimaliza kupanda mkuki |

Msanii anaogopa athari za utamaduni huu mgeni ambao unapenya katika jamii yake. Suala hili linaonekana kuwa tisho kwa utamaduni wa jamii ya Akamba. Ndiposa anaamua aende akatafute nguvu za kukabiliana na suala hili geni. Ndisya (2015), anaona kwamba katika utamaduni wa jamii ya Akamba, wakati jamii ilihisi ya kwamba maisha yao yalikuwa yanapata tisho kutoka kwa makabila jirani, wangeenda kwa waganga na wazee wa kijiji ili kuelekezwa namna ya kukabiliana na tatizo hilo. Wangepata maelekezo na nguvu za kukabiliana na chochote kile ambacho kilikuwa tishio kwao.

Masuala ya imani ya Kiafrika hujumuisha masuala yote ya kimaisha. Hayahusu tu mtu binafsi bali jamii nzima kwa jumla kwani huhusisha masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa hivyo, kuchangia ujenzi wa utaifa wa jamii (Masango, 2006). Msanii anaona kwamba kuna utamaduni wa jamii zingine ambao unavamia na kuathiri utamaduni wa jamii yake. Mwanzo, ni utamaduni wa Kikorea na pili ni utamaduni wa Kimasai. Anaona kwamba huenda hili likafanya jamii yake kukosa nguvu zake katika jamii. Anadhibiti hili kwa kutafuta msaada wa hirizi (*ititi*) ambazo zitafanya wanaotaka kuubadili utamaduni

wake kukosa uwezo na hivyo basi kumfanya yeye kuendeleza utamaduni wa Akamba na kupanua jamii ya Akamba. Katika mshororo $M_{20-21}$ anasema:

| | |
|---|---|
| *Ndumbe alikye mbevo,* | Nimgonge aingiwe na baridi, |
| *Na indi ndivanda itumo* | Kisha nipande mshale |

Msanii atatumia hirizi ili kumtiisha Mkorea na kumfanya kufuata utamaduni wa Akamba. Hivi atakuwa analinda utamaduni wa taifa lake. Kwa vile msanii hana uwezo wa kukabiliana na tatizo lililomkabili, atatumia uwezo ambao si wa kibinadamu ili kukabiliana na changamoto zinazomkumba. Msanii anadhihirisha ya kwamba jamii ya Akamba ina imani katika nguvu za mizimu na miungu, imani ambayo anaiendeleza kupitia simulizi zake za nyimbo pendwa. Hili linachangia ujenzi wa utaifa wa Akamba.

Imani ya ushirikina imejitokeza katika simulizi za msanii ambazo zimechipuka kutokana na utamaduni wa jamii ya Akamba. Suala la imani kwa miungu na mizimu inajitokeza katika wimbo $W_2AR_U$ msanii anaposema *Ná mbésà syáémá níéndá kwà áwé Mwìngí, Ngúní* $M_7$ *(*Na pesa ikishindwa nitaenda kwa waganga Mwingi, Nguni). Kupitia simulizi hii, anataja sehemu za Ukambani, Nguni na Mwingi, ambako anaona ya kwamba atapata msaada huu wa waganga. Hili ni dhihirisho kwamba wanajamii wa sehemu hizo ambazo ni wakilisho la jamii ya Akamba wanaamini katika uwezo wa miungu na mizimu. Kwa vile msanii ni zao la jamii, anasimulia yale ambayo yamo katika utamaduni wake na yanayojenga utaifa wao. Anasawiri nguvu za sihiri kuwa na uwezo zaidi ya pesa. Wakati wa majanga ya kijamii, Mbondo (2006), anasema kwamba wazee hutumwa kwa watu wateule ambao huwa na uwezo wa kuzungumza na mungu na mizimu ili kutoa mwelekeo kwa jamii.

Katika jamii ya Akamba, watu hawa teule huitwa *mundu mue* (mganga) katika umoja, wingi *andu awe*. Kazi yao ni kumpa mja nguvu za kukabiliana na tatizo lolote ambalo limemwia gumu; kupata mali, magonjwa, biashara, uvamizi, kupata ufanisi katika maisha vilevile masuala ya mapenzi (Musembi, 2016). Msanii anakabiliwa na changamoto ya namna yake ya jinsi ya kufanikiwa katika maisha. Hivyo, anaomba msaada wa wazee katika jamii ili wamsaidie katika azma yake kuu. Anasema:

*Múkōsí ná Téké yù nínywíé ándú álá ngútúmá M9*
*Músémbé Kásàyàní múnééné mwìná Ngémí M10*
*Ná mwōná váémá músémbé mwíté Ndíváú Múléí Mákíndú M11*

*Vú vé kätí wé ndé wíà. M12*
*Ngòò yá múndú yò yéndá kíndú vò váítéí M13*
*Kúsémá kwélí yō mbaitu M14*

Mukosi ukiwa na Teke nitawatuma
Mwende Kasayani muongee na Ngemi
Na mkishindwa muite Ndivau Mulei Makindu yeye si mwoga
Roho ya mtu ikipenda kitu hakuna huruma kusema ukweli

Anawatambua Mukosi, Teke na Ndivau Mulei kama wazee ambao atawatuma kuzungumza na Ngemi. Anasema ya kwamba atatumia njia zote ili kumpata msichana huyu. Kwanza atawatuma wazee ili wazungumze na Ngemi ili wamweleze azma ya msanii. Msanii anabainisha utaifa wa jamii ya Akamba katika kutekeleza majukumu muhimu ya kijamii kama vile ndoa.

Kupitia wimbo huu, anaonyesha nafasi ya watu mbalimbali katika jamii. Anabainisha wahusika tofauti tofauti katika shughuli za jamii ya Akamba. Kuna wazee na *awe* (waganga) ambao anawahusisha katika azma yake. Jazanda ya msichana hapa inatumika kuwakilisha ufanisi kiuchumi wa mtu binafsi au jamii. *Ngemi* (furaha), ni jazanda ya ufanisi au kuendelea katika jamii. Msanii ana tamaa ya kufanikiwa kiuchumi na katika nyanja zingine. Anasema ya kwamba amejaribu njia nyingi za kupata kile anachokitamani ila hajafanikiwa. Haonekani kukata tamaa. Atatumia njia zote ili akipate. Anasema ya kwamba atatumia kile alichonacho ili kuufikia ufanisi wake. Ufanisi huu utapatikana kwa kuhusisha wenye hekima (wazee) na iwapo watashindwa basi watatafuta msaada wa *awe* (waganga) ili apate anacholenga.

Msanii anapozungumzia kuhusisha nguvu za hirizi katika utekelezaji wa shughuli muhimu katika maisha yake, anasawiri itikadi za jamii ya Akamba. Anapendekeza matumizi ya itikadi hizi iwapo jamii itajipata katika changamoto fulani. Hirizi hizi huwa si mali ya mtu binafsi bali ni mali ya jamii ambayo hukabidhiwa na mizimu kwa mtu mmoja maalumu ambaye ana uwezo wa kuzungumza na miungu na kuwaeleza wanajamii matakwa ya mungu. Hawa ndio tu wanaoweza kuzifanya nguvu hizi kuwa na uwezo ambao mwanajamii huwa anatafuta (Ndisya, 2015). Hirizi hizi huwa na uwezo wa kuendeleza matakwa ya wanajamii.  Matumizi ya hirizi ni imani muhimu ambayo inautambulisha utamaduni wa Akamba na kuendeleza utaifa wao.

#### 4.2.1.3 Vyakula

Data ya utafiti huu iliyochanganuliwa ilibaini kuwa jamii ya Akamba ina utamaduni wa vyakula. Msanii anaelekea kubainisha umuhimu wa vyakula spesheli katika maisha ya kila siku ya jamii ya Akamba. Anazungumza kuhusu chakula kwa jina *múthokoi* na kinywaji kinachojulikana kama *kalúvú*. Katika wimbo $W_{13}AR_U$ anasema:

> *Mulolongo ni nthi yi raha ūye mundu na muthokoi* M1
> Mulolongo ni nchi ya raha upate mpenzi na muthokoi

Msanii anatambulisha *muthokoi* kama chakula cha kipekee ambacho anakilinganisha na urembo wa wasichana Wakamba. Wimbo huu unasawiri taifa la jamii ya Akamba. Msanii anaposema *ūye mundu na muthokoi* (ule mtu na muthokoi), ana maana kwamba hiki ni chakula ambacho watu hula wakati wa sherehe au raha. Katika wimbo huu, msanii anaonyesha ya kwamba watu wanaokwenda mji wa Mlolongo katika harakati za burudani watakula vyakula na vinywaji mbalimbali vikiwemo *muthokoi*. Kutajwa kwa chakula cha kiasili cha jamii ya Akamba kikiandamana na suala la posa na ndoa kunajenga taswira ya utamaduni wa jamii hii. Msanii anakipa chakula hiki umuhimu sawa na ndoa, ambayo ni mojawapo ya mivigha muhimu ya jamii. Mji wa Mlolongo unakuwa mahali ambapo Wakamba kutoka kaunti zote tatu za Ukambani hukutana na kutangamana huku wakifurahia vyakula na vinywaji vya kiasili. Hili linabainisha utamaduni wa jamii hii. Ingawa mji wa Mlolongo uko karibu na mji mkuu wa Nairobi, msanii anaonyesha kwamba vyakula vya kiasili vinapatikana humo. Japo kuna mengi ambayo yamebadilika katika jamii hii, inaonekana vyakula vya kiasili vimedumishwa. *Muthokoi* ni chakula ambacho huandaliwa aghalabu wakati wa sherehe za ndoa. Ni chakula ambacho huwa hakikosi wakati wa harusi. Kinatambulisha jamii ya Akamba. Mlolongo ni mji ambao una jamii na tamaduni mseto. *Muthokoi* inakuwa kitambulisho cha kitamaduni cha jamii ya Akamba katika sehemu ambayo ina tamaduni mseto na iliyoathiriwa na usasa.

Nafasi ya chakula katika jamii si kuwezesha watu kuishi tu bali chakula ni kipengele cha ujenzi wa utamaduni wa jamii kwani huwaleta watu pamoja, kujumuika katika sherehe za kitamaduni (Vatika, 2018). Katika wimbo $W_{22}AR_{U,}$ msanii anaonyesha jinsi walivyoalikwa sherehe ya harusi na Kyong'oi sehemu ya Kangala Kamutei iliyoko sehemu za Kitui, Kusini. Ken wa Maria anaendeleza utamaduni wa vyakula vya sherehe ya jamii

ya Akamba. Ubeti wa sita na saba katika mishororo ya M $_{26\text{-}30}$ msanii anataja baadhi ya vyakula ambavyo waliandaliwa katika sherehe hiyo ya harusi. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Kínyonyo, Mercy nímwekie naí kyathíni kíu* | Kinyonyo na Mercy mlikosea sana katika hafla hiyo |
| *Neekíiwe líu úte nyama kyathíni kíu* | Nilipewa chakula bila nyama katika hafla hiyo |
| *Na kwaí o nzaú yathínzítwe kyathíní kíu* | Na kulikuwa na fahali aliyechinjwa katika sherehe hiyo |
| *Nasengíe múno ndeúya nyama kyathíní kíu* | Nilishangaa sana nilipokosa kula nyama katika sherehe hiyo |
| *Asyai sorry* | Ombeni msamaha! |

Katika wimbo huu ni bayana kwamba katika sherehe ya harusi wageni huandaliwa nyama ya fahali. Hii ni sherehe ambayo haikuwa ya kawaida kwa vile waandalizi walichagua kumchinja fahali wala si mnyama mwingine yeyote. *Nzau* (fahali) ni ng'ombe dume ambaye amekomaa, ana uzito mkubwa na nyama nyingi. Amelishwa kwa miaka mingi na kutunzwa vyema. Mnyama kama huyu huwa chaguo tosha wakati wa sherehe kubwa kama hii ambayo Kyong'oi amewaalika marafiki wake waje kusherehekea harusi ya wazazi wake. Wageni waalikwa wakiwemo viongozi mbalimbali walikuwa wengi na walitoka maeneo tofauti tofauti nchini. Katika sherehe za Akamba inaelekea ni kosa kwa mgeni kutopewa nyama iliyochinjwa. Hii inadhihirika anapolalamikia chakula alichopewa kwamba hakikuwa na nyama ilhali kulikuwa na fahali aliyekuwa amechinjwa. Katika ubeti huu anawakosoa Kinyonyo na Mercy na kuwataka kuomba msamaha.

Mbali na nyama inabainika kwamba katika sherehe ya harusi wageni huandaliwa pombe. Katika mshororo M $_{12,}$ anaposema *Niwaetie kau na ndoona kwa kyongói M12* (Ulileta fujo na vita kwa Kyong'oi) anazungumzia kuhusu baadhi ya wageni waalikwa ambao walizua vurugu baada ya kulewa. Hili linadhihirika kupitia neno *ndoona* (fujo) ambayo husababishwa tu na mtu aliyelewa pombe chakari. Katika mshororo huu, Teke anakashifiwa kwa kuzua vurugu katika hafla muhimu kama hii. Inasemekana kwamba alipigana vita na dereva wake na hili likawa aibu kwa kila mtu. Teke anasahau nafasi yake na wajibu kama kiongozi kwa kujihusisha na vita na wadogo wake.

Katika wimbo huu msanii anamweleza ya kwamba ni mwiko kwa mja kujihusisha na vita katika sherehe kama hii, anamwambia; *Kyathi ta kiu kuyikawa ou niweekie nai, asya sorry* (sherehe kama hii hufai kufanya hivyo ulikosea omba msamaha). Teke alihusika na vita baada ya kushiriki ulevi wa pombe ya bure ambayo mwenyeji wake Kyong'oi aliwaandalia. Katika ubeti wa 7 mshororo $M_{31-35}$, msanii anashadidia kuwa katika sherehe kama hii, vileo kama vile pombe huandaliwa kwa wingi. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Kanyangi Mbuyu niweekie nai kyathini kiu M31* | Kanyangi Mbuyu ulikosea sana katika sherehe hiyo |
| *Nzovi ya mana yai mbingi tukamilwa muno M32* | Pombe bila malipo ilikuwa nyingi na tukalewa sana |
| *Na tena andu manyusaa o kila mavikila M33* | Pili, watu walikuwa wakilewa vileo vyovyote walivyopata |
| *Ona kau uyu uyingiva nundu wa mbinyu M34* | Hata vita hivi vilichochewa na pombe |
| *Asya sorry M35* | Omba msamaha! |

Katika sherehe hii, tunaelezwa kuwa wageni walitumbuizwa kwa pombe ya aina tofauti. Mshororo $M_{32,33}$ tunaelezwa kuwa wageni walikunywa pombe aina tofauti tofauti hadi wakalewa chakari. Kilichofuata ni kuzuka kwa vita miongoni mwa wageni waalikwa. Hili linadhihirisha kuwa jamii ya Akamba ina vyakula ambavyo huliwa wakati wa hafla za kijamii ambavyo huwaleta wanajamii pamoja na hiyo kujenga utaifa wao wa kijamii.

Katika wimbo $W_{19}AR_U$, msanii anasema kwamba wakati wa sherehe ya kulipa mahari, pombe ya kienyeji aina ya *kaluvu* ni sharti iwepo. Anakuli: *Na kaluvu ko kaitiwa* $M_{13}$ (na kaluvu haiwezi achwa). Msanii kupitia maneno haya anatambulisha kinywaji hiki kama kiungo muhimu katika kuendesha miviga mojawapo ya jamii ya Akamba. Kati ya vitu vyote ambavyo msanii na wenzake wangewapeleka kwa wakwe wa Mbasu, *kaluvu* ilikuwa muhimu. Sherehe ya kulipa mahari na ya harusi zote hutekelezwa katika muktadha wa ndoa ambao msanii anauzungumzia. Hizi ni sherehe ambazo zinadhihirisha utamaduni wa jamii ya Akamba na huchangia katika kuwaleta wanajamii pamoja wakati wanazingatia utaratibu uliowekwa.

Kupitia matini ya wimbo $W_{22}AR_{U,}$ tunapata kuwa ni jukumu la mwenyeji kuwaandalia wageni wake vyakula spesheli wakati wa sherehe. Hili linaweza kuwa tukio la ushirika

ambapo anawahusisha wandani wake katika maandalizi haya ya vyakula na vinywaji. Msanii anamlaumu Kanyangi Mbuyu, mmoja wa wageni waalikwa katika harusi ya wazazi wake Kyong'oi kwa kuleta pombe nyingi na ya aina tofauti tofauti katika hafla hii ya harusi ($M_{31-32}$). Tunaelezwa hivi:

| | |
|---|---|
| *Kanyangi Mbuyu niweekie nai kyathini kiu M31* | Kanyangi Mbuyu ulikosea sana katika sherehe hiyo |
| *Nzovi ya mana yai mbingi tukamilwa muno M32* | Pombe bila malipo ilikuwa nyingi na tukalewa sana |

Inaelekea kwamba Kanyangi Mbuyu alihusishwa katika kupanga sherehe hii kwani alitoa baadhi ya vyakula vilivyotumiwa na wageni. Hili linadhihirisha umoja wa kijamii na hata ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

Aina nyingine ya chakula cha kiasili cha jamii ya Akamba inajitokeza katika wimbo $W_{21}AR_U$. Katika simulizi hii maisha ya awali ya msanii yanabainishwa. Anatusimulia kuhusu maisha yake alipokuwa akifanya kazi kijijini kabla ya kuhamia jiji la Nairobi. Analinganisha maisha ya vijijini na mjini na kusawiri ugumu wa hali ya juu wanaopitia walioko vijijini. Kule vijijini, anasema kuwa alipata taabu sana. Anasema;

| | |
|---|---|
| *Tina, Tina Tina, twaisaa malenge (M1)* | Tina, Tina, Tina, tulikuwa tukila malenge |
| *Twi kundu kuasa, Kitui Kanyangi (M2)* | Tukiwa mahali mbali, Kitui Kanyangi |
| *Ngithinia musyi kuu kwa mwendwa(M3)* | Nikitesekea huko nyumbani, kwa mpenzi wangu |
| *Ngiithya musyi kuu kwa mwendwa (M4)* | Nikilisha mifugo, nyumbani kwa mpenzi wangu |
| *Ngisuvia indo kuu kwa mwendwa(M5)* | Nikichunga mifugo, nyumbani kwa mpenzi wangu |
| *(Wa Maluki)* | (Wa Maluki) |

Msanii anaposema *ngithinia musyi kuu kwa mwendwa* $M_3$ (nikitesekea nyumbani kule kwa mpenzi wangu) anaelezea kuhusu hali gumu ya maisha aliyoipitia alipokuwa akifanya kazi za sulubu pamoja na kulisha mifugo. Chakula alichokila kilikuwa tu *malenge* (boga). Aina hii ya chakula hukuzwa tu katika sehemu kame. Ukame hutokana na ukosefu wa maji. Maisha kijijini huenda yakawa magumu kweli kweli. Anasema kuwa Kitui ni mbali. Umbali anaouzungumzia ni ule wa kuwa mbali na miji ambako anaona kuwa maisha ni mepesi kwani kuna mengi mazuri (mataani). Baada ya kufika mjini, maisha ya msanii

yametengenea ndiposa anamwambia mpenziwe kwamba atafika kijijini kumchukua ili akamwonyeshe maisha mazuri ya mjini ambayo angeyafurahia.

Kabla ya majilio ya wakoloni, jamii ya Akamba ilijihusisha na uwindaji na ukusanyaji wa matunda na mazao mengine ya mwituni. Baadaye, wakawa wafugaji wa kuhama hama kutokana na uvamizi wa jamii jirani ambao wangenyakua mifugo wao. Kadri maisha yalivyobadilika ndivyo jamii hii iliendelea kubadilika. Wakaanza shughuli za ukulima kama njia mojawapo ya kuongeza mapato na hata chakula (Nzioki, 1982). Mazao ya shambani ndiyo msingi wa vyakula walavyo jamii ya Akamba. Wao hupenda kula nyama na maziwa pia. Maziwa hunywewa na watoto na wanawake (Mbondo, 2006). Wakati wa sherehe maalum za kitamaduni kama vile ndoa, kuzaliwa kwa mtoto, ujinaishaji, mazishi na hata tohara, vyakula maalum huandaliwa.

Wakati wa ndoa, vyakula spesheli huandaliwa. Tunaelezwa kuwa baada ya kuoa, bwana harusi angetuzwa na dada za mke wake kwa kazi nzuri ya kuvunja ubikira wa dada yao. Angeandaliwa *muthokoi*, chakula cha kiasili cha Akamba ambacho hutengenezwa kwa kuchanganya maharagwe na mahindi yaliyotwangwa kwa kinu (Mwikali, 1990). Kulingana na mila za Akamba, *kaluvu* (pombe ya kienyeji) ilinywewa tu na wanaume wazee. Wanawake na vijana barobaro hawakuruhusiwa kunywa pombe. Si kila wakati ambapo pombe ilinywewa. Ilitumiwa tu wakati wa sherehe muhimu kama vile wakati wa kulipa mahari, kusherehekea kuzaliwa kwa mtoto, wakati mtu mashuhuri aliaga dunia na wakati wa kutoa kafara kwa mungu. Pombe hii kwa jina *kaluvu* ilitengenezwa kwa kutumia asali na wakati mwingine miwa. Vijana wanaume walipata ruhusa ya kushiriki pombe kutoka kwa baba zao baada ya kuoa na kuwa na familia (Mbondo, 2006). Kupitia maelezo haya, vyakula vya kiasili vya jamii ya Akamba vinabainishwa kama muthokoi, boga, nyama na pombe ya kiasili kwa jina kaluvu. Hivi ni vyakula ambavyo huliwa takriban wakati wa sherehe au wakati miviga muhimu katika jamii ya Akamba inapotekelezwa na hivyo kuchangia ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

#### 4.2.1.4 Shughuli za Kiuchumi

Jamii ya Akamba ni mojawapo wa makundi yanayounda kundi kuu la Wabantu. Wao ni Wabantu wa Mashariki ambao wanasemekana kwamba walihamia nchini Kenya na kwingineko kutoka Shungwaya. Shughuli zao muhimu za kiuchumi ni ukulima, ufugaji,

biashara pamoja na ufundi wa kitamaduni kama vile uchongaji vinyago na ufumaji wa vikapu (Mutisya, 2022). Utaifa wa jamii hujengwa kupitia shughuli za kiuchumi. Kupitia kwa nyimbo pendwa za Ken wa Maria, shughuli za kiuchumi za wanajamii zinabainika. Wananchi wanajihusisha na shughuli mbalimbali zikiwemo usanii, biashara, uchongaji wa vinyago na ufugaji. Wanajamii hupata ajira katika taasisi za kiserikali, biashara za watu na pia nyumbani kama vile kazi ya kuchunga mifugo.

Wimbo $W_3AR_U$ unabainisha shughuli mojawapo za kiuchumi za jamii ya Akamba. Msanii ni mwimbaji wa nyimbo za kutumbuiza. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Tuikuna ndanzi Makutano nina aa Mbasu M1* | Tukipiga muziki Makutano pamoja na akina Mbasu |

Kupitia wimbo huu, tunaelezwa kuwa msanii anafanya kazi ya kuwatumbuiza watu katika maeneo tofauti tofauti. Anafanya hivi pamoja na wanabendi wenzake ambao ni Mbasu. Kazi ya usanii inakuwa kitega uchumi kwake yeye na wenzake. Haya yanajitokeza pia katika wimbo $W_{11}AR_U$ msanii anaposema kwamba anakusudia kuacha kazi ya usanii ili ajiunge na Mutua na aweze kufundishwa namna ya kufanya biashara. Anasema: *Nienda ukola wathi, ambundisye viasala* $M_{32}$ (Nataka kuacha usanii, anifunze biashara). Msanii anaisawiri jamii ya Akamba kama inayoshiriki katika biashara mbali na shughuli ya usanii ndiposa angependa kuacha usanii na kuingilia biashara. Katika wimbo ($W_{11}AR_U$), msanii anazungumzia biashara ya kuuza vyuma vikuukuu. Haya yanabainika katika mshororo $M_{34-36}$, anapoeleza kwamba angependa Mutua Katuku amfunze biashara ya vyuma vikuukuu na vya ujenzi. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Nienda ukola wathi, M32* | Nataka kuacha kuimba wimbo |
| *Ambundisye viasala, M33* | Anifunze biashara |
| *Viasala wa syuma, M34* | Biashara za vyuma |
| *Ila sya sikilevu M35* | zile vyuma za mabaki |
| *Na syuma sya myako, M36* | Na vyuma vya mjengo |

Hii ni biashara ambayo mfanyibiashara huyu anaiendeleza mjini Mombasa. Biashara ya vyuma vikuukuu huwafanya Wakamba kuzuru sehemu mbalimbali za Ukambani wakinunua vyuma hivi. Katika shughuli hiyo, wao hutangamana na kujenga utaifa wao. Wafanyibiashara kutoka jamii hii wamesawiriwa kama wajenzi wa utaifa, wanawaalika watu kutoka jamii yao katika sherehe zao. Katika wimbo $W_{11}AR_U$, msanii anatueleza

kuhusu ukarimu wa mfanyibiashara wa vyuma vikuukuu kwa jina Mutua Katuku. Anamwalika msanii pamoja na wanabendi wenzake walipokuwa wametembea mji wa Mombasa. Biashara hii inachangia katika ujenzi na udumishaji wa utaifa wa jamii ya Akamba kupitia maendeleo ya kiuchumi ambayo msanii na Mutua Katuku wanaleta katika maeneo yao. Msanii anaona kuwa kwa upande wake, vijana kutoka eneo la Matuu, Kasolongo na wa Kwa Kipevu watapata ajira kupitia biashara yake. Msanii atakuwa ameingia kiwango cha *kusuvia mbai* (kuisadia jamii) kama anavyofanya mwanabiashara Mutua Katuku. Hili litadumisha umoja na utangamano wa jamii yake.

Jamii ya Akamba inajihusisha na biashara ya ufumaji wa vikapu. Akishadidia kauli hii, Mutinda (2005), anasema kwamba ufumaji wa vikapu ni kazi inayofanywa na akina mama katika eneo la Machakos. Anaona kuwa umuhimu wake umebadilika kutoka matumizi ya kinyumbani hadi kuwa biashara ya soko la ndani na hata nje. Ufundi huu huhusisha kuvuna nyuzi za mkonge, kuzipa rangi na kuzisokota. Anaendelea kusema kwamba akina mama hushiriki katika ufumaji wa vikapu (kyondo) kwa sababu ya mapato, urithi wa kitamaduni na kama njia ya kuwaleta wanajamii pamoja.

Katika wimbo $W_{23}AR_U$, msanii anamsifia mwaniaji wa kiti cha ubunge cha Kitui ya Kati ambaye ameahidi kutafuta soko la kuuza vikapu bara la Ulaya na sehemu nyinginezo.

| | |
|---|---|
| Kyalo wa maendeeyo M5 | Kyalo wa maendeleo |
| Mivango ena myailu M9 | Ana mipango mizuri |
| Syondo syina soko M12 | Vikapu vinapata soko |

Mishororo hii inabainisha kwamba jamii ya Akamba imewekeza katika viwanda vya ufumaji wa vikapu. Ufumaji wa vikapu maarufu *Kyondo* umekuwa sehemu ya uchumi na utamaduni wa Akamba tangu zamani (Daniel, 2020). Kwa mujibu wa Mutinda na Kiumbuku (2014), kazi ya ufumaji wa vikapu ilifanywa na jinsia zote. Ufumaji wa vikapu huwaleta watu pamoja wakati wa ufumaji na uuzaji. Shughuli hizi zinajenga utaifa wa jamii.

Ufugaji unatambulishwa kama shughuli ya kiuchumi inayoendelezwa na jamii ya Akamba kupitia wimbo $W_{22}AR_U$, mshororo M4: *Ngiithya musyi kuu kwa mwendwa* (Nikilisha mifugo, nyumbani kwa mpenzi wangu). Msanii anamkumbusha Tina mpenzi wake kwamba wakiwa sehemu ya Kanyangi, Kitui alifanya kazi ya kuwalisha na kuwachunga

mifugo wa mwajiri wake. Kazi ya kuchunga mifugo ilimpa msanii ajira. Ufugaji kama shughuli ya kiuchumi pia inajitokeza katika nyimbo $W_{19}AR_U$ na $W_{14}AR_U$ ambapo anaahidi kuwapeleka mbuzi watatu kwa sherehe ya kutoa posa. Hii ni dhihirisho kwamba Akamba hufuga mbuzi kama shughuli ya kiuchumi. Mbuzi hawa ndio hutumiwa katika sherehe za kitamaduni kama vile ndoa ambazo huwaleta Wakamba pamoja. Mbali na ufugaji wa mbuzi msanii ametaja ufugaji wa ng'ombe kama shughuli ya kiuchumi ya Akamba. Katika wimbo $W_{21}AR_U$, msanii anasimulia mwaliko wa sherehe ya harusi ya wazazi wake Kyong'oi ambako wageni waliandaliwa nyama ya ng'ombe ingawa haikutosha. Ufugaji kama shughuli ya kiuchumi huwapa vyakula vya sherehe vinavyowaleta watu pamoja na kuendeleza utaifa wa jamii yao.

Ajira kama shughuli ya kiuchumi inadhihirika kupitia nyimbo $W_{11}$, $W_{12}$ na $W_{22}$ . Msanii anasema kwamba baada ya kupata ujuzi wa kufanya biashara ya kuuza vyuma vikuukuu, ataanzisha biashara yake kama hiyo ya Mutua Katuku na kuwaajiri vijana kutoka maeneo ya Matuu, Kasolongo na Kwa Kipevu ili waendeshe biashara yake ya kuuza vyuma vikuukuu ($M_{48-53}$). Biashara yake inawapa ajira vijana kutoka maeneo mbali mbali ya ukambani. Katika $W_{12}$, Dr. Mueni ana ajira ya kutibu watu kwani yeye ni daktari. Wanajamii wanamwita wakati wanapopata magonjwa naye huwahudumia haraka na kwa njia nzuri hadi wanapata afueni ya haraka. Katika wimbo $W_{22}$, tunaelezwa kuwa Teke, ambaye ni mmoja wa waalikwa katika sherehe ya arusi ya wazazi wake Kyong'oi alipigana na dereva wake na kuleta aibu kubwa katika sherehe hiyo. Mhusika Dereva amepata ajira ya kuwa dereva wa mwajiri wake ambaye ni Teke.

### 4.2.2 Arki ya Utambulisho

Utambulisho ni jumla ya vigezo maalum vinavyotumiwa kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii moja au taifa fulani (Msanjila na wenzake, 2009). Vigezo hivi hubainisha kuwa kundi fulani ni tofauti na lingine, jamii moja ni tofauti na nyingine, mtu mmoja ni tofauti na mwingine au taifa moja ni tofauti na lingine (Ndung'u, 2022). Utambulisho wa kijamii ni dhana ambayo hutokana na maarifa aliyonayo mwanajamii kuhusu kikundi cha kijamii anachohusiana nacho na kujiona kama mmoja wa kikundi au jamii hiyo pamoja na hisia ambazo zimefungamanishwa na uanachama wa kundi husika. (Tajfel, 1981, 1982). Utambulisho wa kijamii umefungamanishwa na utamaduni ambao huashiriwa kupitia lugha. Utambulisho wa kijamii kulingana na Msanjila (2011), ni ule upekee wa jamii

ambao unabainishwa kwa misingi ya kitamaduni ambayo iko tofauti na misingi ya tamaduni zingine.  Kwa jumla utambulisho ni kiungo cha kupambanua jamii moja na nyingine. Nyimbo na ngoma za kitamaduni zilileta muumano katika jamii huku zikiwashajiisha wanajamii kutafakari maisha yao ya awali pamoja na kutathmini hali ya sasa (Mwikali, 1990). Msanii anaelekea kuwa na azma iyo hiyo anapoimba nyimbo zake.

Kupitia nyimbo pendwa tulizozichanganua utambulisho wa utamaduni wa jamii ya Akamba unajitokeza. Msanii ametumia nyimbo zake kujenga taadhima ya jamii ya Akamba, umoja miongoni mwao na kutambulisha kundi hilo huku akichangia ujenzi wa utaifa wa kitamaduni wa jamii ya Akamba. Msanii anaitambulisha lugha ya jamii yake kama Kikamba. Lugha ya Kikamba ndiyo aliyoitumia kutungia nyimbo zake na kuziwasilisha. Lugha ni kipengele cha kutambulisha utaifa wa jamii fulani. Katika ulimwengu ambao unaelekea kuzifanya jamii kupoteza utambulisho wao wa kitamaduni, utaifa wa kitamaduni huwa na jukumu la kuwawezesha wanajamii kuishi pamoja huku wakionea fahari lugha yao, mitindo yao ya mavazi pamoja na vyakula.  Wanajamii huweza kujionea fahari jinsi walivyo bila kuhisi kwamba utambulisho wao wa kitamaduni unadunishwa (Ndung’u, 2022).

Katika wimbo $W_{19}AR_{UT}$ *Kyathi Tawa* (Hafla ya Tawa), msanii anaisawiri jamii ya Akamba kama iliyo na utambulisho wa kitamaduni. Kuna sheria ambazo hufuatwa wakati wa kuendesha shughuli za kijamii. Sheria hizi hazijaandikwa bali hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia fasihi simulizi. Msanii anaisawiri jamii ya Akamba kama iliyo na utaratibu katika sherehe zake.  Sheria hizi ndizo zinazoongoza miviga ya kijamii kama vile ndoa, mazishi, ujinaishaji, kutoa kafara na shughuli za jandoni. Wakati wa kutoa posa na mahari, kuna idadi mahususi ya zawadi ambazo familia ya bwana harusi ni sharti itoe. Zawadi zenyewe zimebainishwa: mbuzi watatu na aina ya kinywaji cha kitamaduni kwa jina *kaluvu* ambavyo ni viungo vya lazima wakati wa kutekeleza miviga hii. Kaida hizi zimetajwa vilevile katika nyimbo $W_{19}AR_{UT}$ na $W_{14}AR_{UT}$.

Ken wa Maria pia anaitambulisha jamii yake kupitia vyakula vya kitamaduni. Katika wimbo $W_{13}AR_{UT}$, msanii anabainisha kuwa wanajamii wanapokutana katika mji wa Mlolongo kuburudika huwa wanashiriki chakula cha kitamaduni *Muthokoi.* Chakula hiki cha kitamaduni kinakuwa kiungo muhimu cha kuwaleta pamoja Wakamba kutoka sehemu

zote za Ukambani katika mji huu. Msanii vilevile ametambulisha sehemu mbalimbali ambako jamii ya Akamba huselea. Katika wimbo $W_{13}$, msanii anatambulisha mji wa Mlolongo kama mji ambao unamilikiwa na jamii ya Akamba kwa kurejelea vitambulisho vitatu: chakula (Muthokoi), wanawake warembo na muziki wa Kikamba. Mji huu unapewa umuhimu wa burudani kwa jamii ya Akamba ambao wanautambua kama 'Mombasa' yao ambayo inahusishwa na burudani. Maeneo mengine ambayo ametambulisha ni pamoja na Tawa, Wote, Kibwezi, Matuu na Makutano.

Utambulisho wa taifa pia umebainika kiuana. Msanii anaonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii ya Akamba. Anampa mwanamke utambulisho katika jamii ambayo imekolea ubabedume. Anamsawiri mwanamke kama mwenye bidii, mlezi, msomi na mwaminifu. Wanawake wanashiriki katika ujenzi wa taifa. Wao hutunza jamii zao, hushiriki katika shughuli za uzalishaji mali pamoja na kuwaelekeza wana wao ili kuleta mshikamano katika jamii. Mung'ala (2020), anaeleza kwamba wanawake hutumiwa kama ishara ya kuendeleza kitambulisho cha utaifa kwani huwa kama ishara ya kustawisha ushirikiano katika tamaduni nyingi za Kiafrika. Mwanamke katika jamii amechorwa na kupewa umuhimu mkubwa kwa kupewa sifa tano. Kwanza, mwanamke ni ishara ya kitambulisho na heshima. Pili, ni kitambulisho cha urithi na thamani ya maadili ya kitaifa. Tatu, ni ishara ya utangamano, nne, kupitia kwake uhusiano na utawala pamoja na upinzani huendelezwa na mwisho, mwanamke ni ishara ya usuli wa mwanadamu. Mwanamke si tu kiwakilishi cha taifa bali pia huendeleza hisia za utangamano miongoni mwa wanajamii tofauti. Mawazo haya yanadhihirika kupitia nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria. Katika wimbo $W_4AR_{UT,}$ msanii anasema kwamba alimpata msichana mrembo mjini Wote kwa jina Winnie. Msanii alimpenda na akajaribu kumtongoza. Hata hivyo, Winnie alimtahadharisha kwamba tayari alikuwa na mpenzi. Winnie alikataa penzi lake, jambo ambalo linamstaajabisha msanii. Winnie anashikilia msimamo wake licha ya msanii kumshinikiza akubali ombi lake. Msanii anatumia uwezo wa kiuana ili apate urafiki wa huyu mwanamke lakini anashindwa. Mwanamke anatambulishwa kama anayeheshimu asasi ya ndoa. Winnie anakataa ombi la msanii kwa sababu ameolewa (… *ni mali yeene* $M_{14}$). Msemo ni *mali yeene* (mali ya wenyewe) una maana kwamba Winnie ameolewa hivyo basi ana mume na hangetaka kuvunja ndoa yake kutokana na urafiki ambao msanii

anauomba. Mwanamke anakuwa chanzo cha mshikamano wa kijamii na kuchangia ujenzi wa utaifa wa jamii yake.

Katika wimbo $W_{12}AR_{UT}$, msanii anamtambulisha mwanamke kama msomi na ambaye amejikomboa. Wanawake wamesawiriwa kama wanaoshiriki katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Smith (1998), anazungumzia nafasi ya mwanamke katika ujenzi wa utaifa wa jamii. Anawaona wanawake kama kiini cha uundaji na uzalishaji wa miradi ya kikabila na kitaifa na wanataja vipengele vitano vikuu vya shughuli na uwepo wao. Wanawake, wanahoji, wanapaswa kuonekana kama wazazi wa kibayolojia wa wanachama wa makundi ya kikabila, wazazi wa mipaka ya makundi ya kikabila au kitaifa, washiriki wa kati katika uzalishaji wa kiitikadi wa jamii na kama wasambazaji wa utamaduni wake. Pia, wanawake ni viashiria vya tofauti za kikabila au kitaifa; kama kitovu na ishara katika mijadala ya kiitikadi inayotumika katika uundaji, uzalishaji na mabadiliko ya makundi ya kikabila na kitaifa na washiriki katika harakati za kitaifa, kiuchumi, kisiasa na kijeshi. Haya yanasawiriwa katika wimbo $W_{12}$.

Msemewa katika wimbo huu kwa jina 'Daktari Mueni' ni msomi. Amesoma hadi akahitimu kuwa daktari. Wanawake hawajapata fursa za kutosha za kujumuishwa katika taaluma zenye hadhi kama vile udaktari katika jamii zilizokolea ubabedume. Daniel (2020), anasema kwamba wanawake waliachiwa taaluma kama vile ualimu, uuguzi au kuwa mke nyumbani. Katika wimbo huu Mueni amepata hadhi kuu katika jamii ya kuwa daktari. Msanii anaonyesha jinsi wanawake katika jamii ya Akamba waliosomea taaluma ya udaktari wanakuwa tegemeo la jamii. Katika $W_{12}AR_{UT}$ mshororo *Neew'a nai ndumanaa ndakitali umwe* (Nikiwa mgonjwa natafuta daktari mmoja) unaonyesha jinsi msanii wakati anaugua huwa anategemea Daktari Mueni kumtibu. Daktari ni kiungo muhimu katika uhifadhi wa uhai kwa kuhakikisha siha njema. Kupitia kwa taaluma hii, jamii inamtegemea mwanamke. Msanii anakuli kwamba daktari anapowasili kwake, anapona magonjwa yake yote. Kupitia kwa mwanamke, jamii inapata afueni. Mwanamke anachangia katika utatuzi wa masuala yanayoikabili jamii yake.

Mwanamke anatambulishwa kama mlezi bora katika jamii. Katika wimbo $W_{20}AR_{UT}$, msanii amemtaja mkewe wa kwanza Mumo kama mlezi wa wanawe wawili Mumbu na

Susu ambao anatarajia wataandamana na Mumo kwenda kumsalimia Mbonge. Msanii amemtambulisha mkewe wa mwisho *Inyaa Mbonge* ambaye amemzalia mtoto wa kiume. Anamshukuru Mama Mbonge kwa kumzalia mtoto mvulana. Anamshauri amtunze huyu mtoto Mbonge kwani ni wa nyumba kubwa. Mumo, ambaye ni mke wake wa kwanza anatwikwa jukumu la kuhakikisha kwamba mtoto aliyezaliwa atapata mahitaji yake yote. Ni bayana kwamba jukumu la kulea mtoto ni la mwanamke. Mwanamke ndiye kitovu cha jamii ya Akamba na kupitia kwake jamii inapanuka kutokana na kuongeza wanajamii wapya. Msanii anafurahia mkewe kwa kumzalia mtoto ambaye ameongeza idadi ya watoto wake. Anasema ya kwamba nyumba yake sasa imekuwa kubwa kwa kuongeza mtoto Mbonge. Kuzaa na kulea yanasawiriwa kama majukumu muhimu ya wanawake ambayo yanachangia kupanuka kwa jamii ya Akamba. Kuzaliwa kwa mtoto katika jamii kunaileta jamii pamoja. Wanajamii wanajumuika na kusherehekea tukio hili la kijamii ambalo linachangia ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Shughuli ya ulezi katika jamii inatekelezwa na wanajamii wote ila si mama mtoto pekee. Hili linachangia utaifa wa jamii yao.

### 4.2.3 Arki ya Siasa na Uongozi

Suala la siasa na uongozi katika jamii ya Akamba linajitokeza katika data ya utafiti huu. Ngugi (1986) anasema kwamba wasanii wote huwa wanasiasa. Kupitia kwa kazi yake, msanii atasawiri michakato yote ya kisiasa katika jamii yake. Kupitia kwa msanii, vipindi vya kisiasa ambavyo jamii yake imepitia hubainika. Mwanzo, ametambulisha baadhi ya viongozi maarufu wa jamii ya Akamba. Katika wimbo $W_{15}AR_{S,}$ anamtambulisha mwanasiasa Kalonzo Musyoka kama mwangaza wa jamii ya Akamba. Mwangaza ni neno la kijazanda la siasa ambalo linarejelea uwezo wa kiongozi kuonyesha jamii yake mwelekeo kutoka kwa giza au changamoto mbalimbali. Anasherehekea kuteuliwa kwa mwanasiasa Kalonzo Musyoka kama makamu wa rais wa 10 nchini Kenya mwaka wa 2008 na kueleza kwamba ni wakati wa jamii yake 'kujisalimu'. Kujisalimu ni jazanda yenye maana kwamba jamii ya Akamba imepata nafasi ya maendeleo mengi kwani Kalonzo amepewa nafasi ya juu katika serikali. Msanii anaizindua hadhira yake ya taifa la Akamba kwamba ni wakati wao wa kujiendeleza. Hadhira ni muhimu kwa sababu huchangia ujenzi wa utaifa wa jamii yao kwa mawazo yao ya kisiasa kupitia uelewa wao wa nyimbo husika.

Utaifa haujikiti tu katika maneno bali pia katika utendaji wa msanii na namna hadhira inavyozifasiri nyimbo husika. Ngugi (1986) anakuli:

> Wasanii na wanasiasa wanashabihiana katika mambo mengi; wote hutumia maneno. Wote ni zao la uhalisia wa ulimwengu unaowazunguka. Matakwa yao na shughuli zao huhusu suala moja: binadamu na mahusiano ya kibinadamu. Fasihi bunifu huathiri mahusiano ya kijamii pamoja na uelewa wao na siasa. Inahusu matumizi ya uwezo wa siasa na mahusiano ya kisiasa katika jamii. Siasa na sanaa huweza kubainika ndani ya kila moja.

Msanii amebainisha eneo la kisiasa la jamii yake kama *Ukamba*. Katika mshororo $M_{18,}$ msanii ametumia maneno W*isi nesa Kalonzo* (unajua vizuri Kalonzo), kuonyesha kwamba Kalonzo kama kiongozi wa kisiasa ni mmoja wao kwani anaelewa eneo lake na shida zao. Kwa hivyo, jamii ya Akamba inatarajia kwamba uteuzi wa kiongozi wao utaleta utajiri. Katika mshororo $M_{17,18,19}$, Kalonzo anakumbushwa kwamba kama kiongozi wa Akamba ana jukumu la kutatua tatizo la maji na barabara katika taifa la Akamba. Haya yanashadidiwa na Ngugi (1986), anaposema kwamba siasa huweza kuelezwa kupitia mahusiano ya kiuwezo. Anaendelea kusema kuwa linalomwongoza msanii ni hali ya mabadiliko ya kijamii ambayo hutokea kila mara katika jamii ambamo yeye ni mhusika. Mahusiano ya kiuwezo katika jamii huathiri msanii pamoja na tungo zake. Mwanzo, msanii mwenyewe ni zao la historia, wakati na mahali. Pili, mada kuu ya msanii huwa historia isitoshe, zao la ubunifu wa msanii huwa kioo cha jamii husika: mifumo yao ya kiuchumi, ujenzi wa matabaka, ujenzi wa utaifa, mapambano yao kiuchumi na kisiasa na miundo yao ya kimaadili.

Kupitia nyimbo pendwa, inabainika kwamba jamii ya Akamba ni taifa lenye utaifa wake. Alter (1994), anasema kuna aina mbili za taifa. Kwanza kuna taifa la kisiasa ambalo linajengwa kupitia kwa nia au maamuzi huru na unyenyekevu wa raia kwa taifa yaani demokrasia. Kwa mfano Ufaransa, Marekani na Uingereza ambapo raia hujitambulisha kwa chama cha siasa. Pili ni taifa kupitia urathi wa utamaduni kama vile: lugha, dini, mila na desturi. Kwa kuzingatia aina ya pili ya taifa, jamii ya Akamba wana taifa. Hii ni kwa sababu wanaishi sehemu moja ya Ukambani (Ndeti, 1972). Wanazungumza lugha moja ya Kikamba (King'ei, 1982; Musyimi, 2011), Aidha wana mpangilio wa koo kumi na mbili ambazo zinashirikiana kujenga jamii pana (King'ei, keshatajwa). Pamoja na hayo Wakamba wana dini na mfumo wa fasihi simulizi wa kuelimisha watoto wao (Mbiti, 1991).

Katika wimbo $W_{15}AR_S$, msanii anaonyesha utaifa wa Akamba katika siasa anaposema:

| | |
|---|---|
| *Kula syitu sya Ukamba* M4 | Kura zetu za Ukambani |
| *Sya kivila kiu kyailu* M5 | Za kiti hicho kinachostahili |
| *Kya usumbi twanengie Kalonzo* M6 | Cha urais tulimpatia Kalonzo |

Katika maelezo haya jamii ya Akamba kama taifa wameamua kumpa Kalonzo Musyoka kura zao zote ili awawakilishe kisiasa. Haya ni makubaliano ya kijamii yanayotokea baada ya kumtambua kiongozi wa taifa lao. Jamii yenye utaifa huwa na makubaliano ya mwelekeo wa kisiasa. Katika $M_{13}$, msanii ametaja neno *mbaitu* (watu wetu). Hapa anarejelea watu wa taifa la Akamba. Huu ni wito wa msanii kwa watu wa taifa la Akamba kushirikiana katika maamuzi ya kisiasa. Msanii katika mshororo $M_{16}$ anamwambia Kalonzo *Withiwe kyeni kwitu* (uwe mwangaza kwetu) kumaanisha kwamba jamii imemwidhinisha Kalonzo Musyoka kama kiongozi wao. Wanajamii wanatarajia kwamba kupitia mwanasiasa huyu, utaifa wao utaimarishwa na kuwaletea mafanikio ya kijamii. Kiongozi huyu atakuwa msemaji wao wa kijamii na kitaifa. Utaifa wa jamii ya Akamba unajitokeza kutokana na jinsi wanajamii ya Akamba walivyojitokeza kumpigia kura mmoja wao wakati alipokuwa akiwania kiti cha urais.

Taifa lenye utaifa huwa linawatambua mashujaa wake. Hili linadhihirika katika mshororo $M_{11}$ msanii anapomrejelea Kalonzo kama *Nzamba* (shujaa). Wamemtambua kama shujaa kwa sababu ya uteuzi wake kama makamu wa rais kupitia chama cha Wiper. Kama shujaa, anaonyesha ujasiri wa kujiunga na serikali ya mseto ili kuondoa hofu katika taifa la Kenya. Jamii yenye utaifa huwa na changamoto zinazowakabili pamoja kama vile magonjwa na njaa. Katika mshororo $M_{17}$, matatizo ya kijumla ya jamii ya Akamba yametajwa kuwa maji na barabara. Matatizo haya huwa yanatatuliwa na jamii kwa pamoja huku wakielekezwa na kiongozi wa taifa lao. Katika mshororo $M_{20}$. Msanii anamweleza Kalonzo kwamba jamii ya Akamba ina matarajio kwamba atasuluhisha matatizo haya.

Msanii vile vile ameonyesha jinsi siasa na uongozi katika jamii mahususi huathiri siasa ya taifa kuu. Baada ya jamii ya Akamba kumtambua Kalonzo Musyoka kama kiongozi wao wa kijamii wanampigia kura za kuwania uongozi wa taifa la Kenya kupitia chama chake cha Wiper. Kupitia wimbo $W_{15}AR_S$, msanii anasimulia matukio ya vita vya baada ya uchaguzi nchini Kenya na namna mwanasiasa Kalonzo Musyoka kutoka jamii ya Akamba alivyochangia kuleta amani nchini wakati ambapo joto la kisiasa lilikuwa limepanda.

Anapokubali kuteuliwa na aliyekuwa rais wa Jamhuri ya Kenya wakati huo, hayati rais Mwai Kibaki, anachangia umoja wa kijamii na utaifa kwani Kalonzo alikuwa tayari kwenye mrengo uliopinga serikali. Kalonzo anakuwa ishara ya umoja wa wanajamii. Hatua hii inachangia utaifa wa taifa la Kenya. Mwanasiasa huyu anaweka kando masilahi yake ya kibinafsi kama mwanasiasa wa upinzani na kuthamini masilahi ya nchi nzima ambayo ni umoja, amani na upendo. Hatua ya Kalonzo ilichangia kutuliza joto la kisiasa la wakati huo. Utaifa wa jamii katika muktadha huu unachangia ujenzi wa utaifa wa taifa kuu.

Katika mshororo $M_4$ msanii anaposema *Aswaili mo maisye mbatili ya Musa ni Huseni yuyu twina munini wa musumbi (*Waswahili walisema batili ya Musa ni Hussein, sasa tuko na naibu wa rais), anasawiri utaifa katika siasa za jamii ya Akamba kwamba walimchagua Kalonzo kuwa rais wa Kenya na ingawa hakufanikiwa kutwaa kiti cha urais wameridhika kwamba ameteuliwa kama makamu wa rais nchini Kenya. Maneno Musa na Hussein ni ya kijazanda. Walitarajia kupata *Musa* (urais) lakini wakapata *Hussein* (makamu wa rais). Mwelekeo huu wa kukubali kwamba Kalonzo awe makamu wa rais unadhihirisha umoja wa taifa la Akamba katika kukubali matokeo ya maamuzi ya kisiasa.

Msanii anamkumbusha Kalonzo kuwa amefika huko kileleni kutokana na utaifa wa jamii ya Akamba kwa hivyo ashughulikie matatizo yanayoikumba jamii yake. Msanii anamwomba mwanasiasa huyu ahakikishe kwamba ameleta maendeleo katika eneo la Ukambani. Anamkumbusha kuhusu baadhi ya changamoto ambazo zinaikumba jamii. Msanii anazibainisha kama ukosefu wa maji na barabara nzuri au miundo misingi. Katika wimbo huu, msanii anakuwa kipaza sauti cha jamii ya Akamba. Anabainisha wazi matarajio ya jamii hii kwa viongozi ambao wamewachagua. Jamii inataka suala la miundo misingi lishughulikiwe kwani ndicho kitovu cha maendeleo ya jamii yoyote ile. Jamii ambayo itakosa miundo misingi bora inabaki nyuma kimaendeleo.

Msanii anamsawiri Kalonzo Musyoka kama mwanasiasa ambaye amechangia pakubwa kubadilisha historia ya jamii yake. Jamii iliyo na utaifa huwa inajivunia historia moja kisiasa. Kalonzo Musyoka anakuwa naibu wa rais wa kwanza kutoka jamii ya Akamba. Pia, anakuwa mwanasiasa wa kwanza kutoka mrengo wa upinzani kuteuliwa katika wadhifa wa serikali. Hatua hii inachangia pakubwa katika kuleta mshikamano wa kijamii na taifa kwa jumla. Ni hatua ambayo ilichangia katika kurejesha amani nchini Kenya

wakati wa baada ya vita vya baada ya uchaguzi wa mwaka 2007/2008. Linakuwa jambo la kihistoria ambapo msanii anachukua fursa hiyo kuwarai viongozi wengine wa kisiasa kuiiga. Isitoshe, msanii anajenga hali ya fahari kwa kurejelea ushindi huu wa Kalonzo Musyoka.

Katika wimbo $W_{17}AR_S$, suala la wajibu wa vyombo vya utawala linaibuka kupitia anwani *Katiba Myau?* (Katiba gani?). Msanii anasaili umuhimu wa katiba mpya ambayo wanasiasa wanataka ipitishwe. Shughuli ya uundaji wa katiba mpya inasawiriwa kama iliyo na umuhimu kisiasa na kihistoria. Msanii anaona kwamba katiba hii itaathiri jamii ya Akamba kiuchumi na kijamii. Haoni haja ya wanajamii kuipigia kura katiba mpya ili kuipitisha kwani imegubikwa na masuala mengi ambayo hayaeleweki. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Sya katiba mwamina M1* | Za katiba mkamaliza |
| *Mweka nesa mwamina M2* | Mmefanya vizuri kumaliza |
| *Yes - No unai thina M3* | Ndio - La ilikuwa shida |
| *Siasa mbingi sya thina M4* | Siasa mingi za shida |
| *Katiba myau?M5* | Siasa mingi za shida |

Kupitia kwa msanii, tunapata kuelewa kwamba kampeni za Ndio – La za kuunga au kutounga mkono katiba mpya zimechangia ukosefu wa umoja wa kijamii. Ni shughuli ambayo imeleta migawanyiko ya kijamii kisiasa, kidini, kiuchumi na katika vyombo vya habari. Kutokana na siasa hizi za katiba mpya, jamii inaathirika pakubwa kwani bei ya bidhaa muhimu inapanda. Msanii anaona kwamba wananchi ndio wanaumia pakubwa.

Kutamatika kwa kampeni hizi za Ndio – La kunaleta afueni kwa jamii. Katika mshororo $M_{14-17}$, msanii anawarai wanajamii wajumuike pamoja washerehekee kwani jambo lililokuwa linawatenganisha limewaondokea. Anaona kuwa kupitia kwa nyimbo ataweza kuwaleta wanajamii pamoja. Anairai jamii kurejelea mshikamano wao wa awali wa kijamii suala ambalo linajenga utaifa wa jamii ya Akamba.

Msanii anazungumza kwa niaba ya wanajamii wenzake. Anaona kwamba katiba kielelezo haijaleta manufaa kwa jamii ya Akamba ila imeishia kuleta migawanyiko kwa misingi mbalimbali. Anaona kwamba wanasiasa kutoka jamii hii wanachangia katika kufumuka kwa mshikamano wa kijamii hivyo, anajitokeza kutoa mwelekeo mbadala kwa jamii ya Akamba. Maoni ya msanii ni kwamba serikali, kanisa, wanasiasa, vyombo vya habari na

katiba husika imefeli katika kuwaunganisha wananchi. Kutokana na changamoto hizi anasema katika mshororo $M_4$ kwamba kumetokea utengano wa wanajamii jambo ambalo limesababisha bei ya bidhaa muhimu kupanda. Haya yote yametokea kwa sababu viongozi wa kisiasa na kidini wamefeli katika kutoa mwelekeo kwa jamii. Anachukua jukumu la kutoa uongozi kwa Wakamba wakati ambapo viongozi waliochaguliwa wamegawanyika kwa misingi ya Yes–No. Ni bayana kwamba yeye mwenyewe haungi mkono katiba hii kwa vile haina manufaa kwa jamii ndiposa anauliza kwa kejeli *Katiba Myau?* (Katiba ya aina gani?). Jamii ya Akamba haijasazwa na changamoto zililizotokana na upigiaji kura katiba kielelezo. Kupitia nyimbo pendwa, msanii anapendekeza utaifa wa jamii ya Akamba ili waweze kutatua matatizo yanayowakabili. Kupitia maneno *Twine wathi vai thina* $M_{16}$ (Tuimbe wimbo kama hakuna shida) msanii anawahimiza wanajamii kuja pamoja na kusherehekea kwa vile matatizo yao yamekwisha. Jamii yenye utaifa huungana katika hafla mbalimbali za kijamii na kusherehekea mafanikio yao.

Msanii anaonyesha umakini wake katika kuyachunguza na kuyaweka wazi baadhi ya matukio ya kisiasa yanayotokea nchini Kenya baada ya kipindi cha kupata uhuru. Anateka nathari za hadhira yake anapoimba kuhusu kifo cha mwanasiasa maarufu Tony Ndilinge, ambaye alikuwa mbunge wa Kilome. Anapoimba wimbo $W_{16}AR_S$, msanii anabadilisha lugha ya mawasiliano na kuamua kutumia lugha ya Kiswahili. Anafanya hivi kimakusudi kwa vile anamsawiri kiongozi huyu kama wa kitaifa. Umaarufu wa Tony Ndilinge ulipiku ule wa kijamii. Katika mshororo $M_1$, msanii anasema kwamba kila mwananchi anaomboleza kifo cha kiongozi huyu wa kisiasa ambaye alikuwa mbunge wa Kilome. Msanii anazungumza na nchi nzima kwa vile nchi nzima inaomboleza. Tony Ndilinge anapewa utambulisho wa kiongozi wa kitaifa. Kupitia mishororo $M_{2,4}$, anamtambulisha Tony Ndilinge kama Kiongozi wa eneo bunge la Kilome na Ukambani kwa jumla. Kisha anaelezea hadhira ya kwamba waliopoteza zaidi ni wananchi wa Kilome na familia yake. Wananchi wa eneo la Ukambani wanaletwa pamoja na habari hizi za tanzia katika kumwomboleza mmoja wao ambaye alikuwa kiongozi wa kisiasa. Hili linachangia ujenzi wa utaifa wa jamii na hata wa kitaifa. Katika jamii yenye utaifa huwa na simulizi za tanzia ambazo wamepitia kama vile kuwapoteza mashujaa wao. Nyimbo pendwa zimetumiwa kuendeleza simulizi ya tanzia ya kisiasa kwa jamii ya Akamba. Inaelekea uongozi wa Tony

Ndilinge haukuathiri tu wananchi wa eneo lake la uwakilishi bunge bali taifa nzima ndiposa anaombolezwa kitaifa.

Msanii anaweka wazi kwamba kifo cha mbunge huyu hakikuwa cha kawaida kwa kudokeza kwamba Tony Ndilinge aliuawa. Mauaji haya yanaipokonya jamii ya Akamba kiongozi wao ambaye ni dhahiri jamii ya Akamba ilikuwa ikimtegemea. Suala kama hili linawaleta wanajamii pamoja katika harakati za kupinga mauaji ya wanajamii wao kiholela. Mauaji kama haya ya kisiasa hufanya jamii kuhofia usalama wao na wa viongozi wao. Msanii hataki kutokee vurugu kuhusu mauaji haya. Anawaongoza wanajamii kuomboleza kifo cha kiongozi wao kwa njia ya amani. Kwa njia hii, msanii anajenga utaifa wa jamii yake kupitia suala la kisiasa.

Uongozi na siasa pia umewasilishwa katika wimbo $W_{23}AR_S$ kupitia mishororo ifuatayo:

| | |
|---|---|
| Andu a Kitui tanai M1 | Wakazi wa Kitui |
| Kitui Central sililai M2 | Kitui ya Kati shangilieni |
| Kyalo wa Muli tyuuyu M3 | Kyalo wa Muli ndiye huyu |
| Kyalo wa Dubai tyuuyu M4 | Kyalo wa Dubai ndiye huyu |
| Kyalo wa maendeeyo M5 | Kyalo wa maendeleo |

Msanii katika mishororo $M_{1,2}$ anatanguliza kuelezea siasa za eneo la Kitui ya Kati. Katika eneo hili kuna kampeni za uchaguzi wa wabunge zinazoendelea. Katika mshororo $M_{3-5}$, anatuonyesha jinsi wanasiasa wa jamii ya Akamba hujibandika majina ya kuwarai wanajamii wenzao kuwapigia kura. Msanii anawaelimisha wanajamii yake kuhusu wasifu wa viongozi bora wa kisiasa ambao wanafaa kuzingatia. Kiongozi mtarajiwa ni sharti awe amesoma, alete maendeleo na aweze kusaidia jamii ya Akamba. Mwanasiasa Kyalo wa Muli anapendekezwa kwa wakaazi wa eneo la Kitui ya Kati kwani ni mtoto wao, amesoma, ameonyesha nia ya kuleta maendeleo katika eneo hili na atasaidia taifa la Akamba. Mwanasiasa Kyalo wa Muli anaonyesha ufahamu wake wa changamoto inayokabili jamii yake kuhusu soko la uuzaji wa vikapu. Ameanzisha wakfu ambao una mipango ya kupata soko la kuuza vikapu Ulaya na kwingineko ambavyo vinafumwa na wanajamii wa taifa la Akamba. Mpango huu utakuwa kitega uchumi kwa akina mama wa taifa la Akamba. Kwa jumla, msanii anahimiza umuhimu wa kuchagua kiongozi wa kisiasa anayechangia ujenzi wa utaifa wa jamii yao.

### 4.2.4 Arki ya Jiografia

Wakamba wanaishi katika kaunti za Kitui, Machakos na Makueni nchini Kenya. Eneo hilo lote hujulikana kama Ukambani (Musembi, 2016). Hata hivyo, Kieti na Coughlin (1990), wanasema kwamba, kuna Wakamba ambao wanapatikana katika sehemu zingine kama Mwea katika Kaunti ya Embu, sehemu za pwani hasa Shimba Hills katika wilaya ya Kwale, sehemu za Taita Taveta na Mombasa kisiwani.

Msanii anasimulia Jiografia ya taifa la Akamba na namna inavyofungamana na sehemu zingine katika enzi hizi za utandawazi. Katika wimbo $W_8AR_J$ msanii anabainisha utambulisho mpya ambao ni zao la nguvu za kiutandawazi ambazo zinafanya mwingiliano wa utambulisho kati ya Mkamba, Mmasai na Mkorea. Hii ni katika harakati za Mkamba kutaka kupanua himaya yake ndani na nje ya nchi. Haya yanabainika katika maneno ya msanii anaposema:

| | |
|---|---|
| *Ēndã nìvãndē ítúmô M3* | Anataka nipande mkuki |
| *Nã āìndēmbēsyā Korea M4* | Na anitembeze Korea |
| *Tena nivyulye ngati M24* | Lazima nijikaze, kama fahali |
| *Mumiwe Kikorea M25* | Na nitie bidii, mnisikie Korea |

*Kuvanda itumo* (Kupanda mkuki) katika jamii ya Akamba ni msemo wenye maana kwamba umenyakua sehemu ambayo umeshindilia huo mshale. Katika muktadha huu, msanii anapata himaya mpya kupitia uhusiano wake na msichana Mkorea. Uhusiano huu utamwezesha kuzuru nchi ya Korea ambako atapata fursa ya kuendesha na kupanua biashara yake ya usanii. Msanii anatarajia kujifunza lugha ya Kikorea itakayomwezesha kutunga na kuimba kwa Kikorea. Msanii anaielezea jamii ya Akamba kuhusu umuhimu wa kuwa na mahusiano kama haya ya kitaifa. Msanii hazungumzii tu utaifa wa Akamba pekee. Anaona kuwa jamii ya Akamba itakuwa na nguvu na kupanuka zaidi iwapo itakubali kutangamana na jamii zingine kama vile Wamasai na Wakorea. Anaona kuwa hali ya utandawazi ina manufaa makubwa kwa jamii yake kwa vile itapanuka na kupata nguvu zaidi. Hii ni mbinu ya kupanua utaifa wa jamii ya Akamba.

Msanii anataja sehemu na miji mbalimbali nchini ambayo anaamini inaunda eneo linalojulikana kama Ukambani. Mipaka anayoweka ya kieneo ni tofauti na ile iliyowekwa na wakoloni. Msanii anakosoa hatua hii ya wakoloni ya kubadilisha mipaka ya kijamii. Analalamika kuwa waliochora ramani ya nchi ya Kenya

waliuweka mji wa Mlolongo katika eneo la Nairobi jambo ambalo yeye na wanajamii wenzake wanapinga. Anasema kuwa wao wanajua kuwa Mlolongo ni sehemu ya Ukambani. Wimbo $W_{13}AR_J$ unatupa taswira hiyo anaposema:

| | |
|---|---|
| *Mulolongo maisye yi IloviM1* | Mlolongo walisema iko Nairobi |
| *Lakini ithye twisyi yi Ukamba M2* | Lakini sisi tunajua ni Ukambani |
| *Mulolongo ni nthi yi vata M3* | Mlolongo ni nchi ya maana |
| *Ni Mombasa witu Ukamba M4* | Ni Mombasa ya Ukambani |

Katika mshororo wa Kwanza, msanii anachora ramani mpya ambapo anabainisha eneo linaloitwa Ukambani anaposema kuwa mji wa Mlolongo upo katika eneo la Ukambani wala si Nairobi. Anabainisha mji huu kama mji mkuu wa Akamba ambapo wanajamii hii hujumuika pamoja na kushiriki shughuli muhimu za kijamii kama vile posa na ndoa, biashara, siasa, shughuli za kitamaduni pamoja na kufurahia muziki kutoka kwa bendi anuwai za Ukambani. Vyakula vya kitamaduni vya jamii ya Akamba ambavyo vinapatikana katika mji huu vinatoa utambulisho wa jamii ya Akamba. Msanii anasema ya kwamba ukifika mlolongo utaweza kupata chakula maarufu cha Wakamba, *muthokoi*. Hiki ni chakula ambacho hupikwa wakati wa sherehe muhimu katika jamii hasa sherehe za posa na ndoa. Msanii anawajulisha wanajamii wenzake kwamba katika mji huu wao, chochote ambacho watahitaji watakipata humo kwa hivyo hakuna haja ya kwenda miji mingine. Mlolongo ni mji wao mkuu kwa hivyo waukuze. Anaongoza jamii yake kuonea fahari Mlolongo kama mji wa Akamba ambao raha zake ni sawa na zile zinazopatikana mjini Mombasa.

Miji mingine ambayo Wakamba wanamiliki imetajwa. Katika wimbo $W_2AR_J$, msanii ametaja mji wa Kibwezi, $W_3AR_J$ akataja mji Makutano, $W_4AR_J$ akautambua mji wa Wote, na mji wa Mombasa ukatambulisha katika $W_{11}AR_J$ kama eneo muhimu la biashara kwa wanajamii wa Akamba. Mutua Katuku ni mfanyibiashara katika mji wa Mombasa, mji ambao msanii anaona kuwa ni himaya ya jamii ya Akamba. Msanii anadokeza kwamba mji wa Mombasa unapatikana katika ikolojia ya jamii ya Akamba. Katika wimbo $W_{18}AR_J$ msanii anawarai wananchi katika kaunti saba wazae kwa wingi ili idadi ya Wakamba iongezeke. Kupitia haya, anabainisha ya kwamba eneo la Ukambani linahusisha Kaunti za Makueni, Kitui, Machakos, Nairobi, Mombasa, Taveta na Embu. Haya yanafuatia fedheha aliyopata mwaniaji wa kiti cha urais na ambaye ni kinara wa siasa wa jamii ya Akamba

Kalonzo Musyoka, baada ya kupata idadi ndogo ya kura za kitaifa katika uchanguzi wa urais wa mwaka 2007 nchini Kenya. Msanii anasema ya kwamba kigogo huyu wa kisiasa alishindwa uchaguzi kwa vile idadi ya Wakamba ni ndogo. Anasema kuwa kaunti hizo saba watii mwito wa viongozi wao wa kisiasa na kuzaana ili wajaze kikapu cha kura. Hii ni jazanda ya kuwasimanga wanajamii ya Akamba kwamba hawana uwezo kisiasa kwa vile maamuzi ya kisiasa hufanywa kwa njia ya kura. Msanii anaomba utaifa wa jamii ya Akamba ili kuhakikisha kwamba kiongozi wao atapata kura za kutosha kutoka kwa jamii yake za kumfanya kiongozi wa kitaifa.

### 4.2.5 Arki ya Historia

Dhima mojawapo ya nyimbo ni kupitisha na kuhifadhi historia ya jamii. Wasanii kama wanajamii wengine hupitia katika vipindi mbalimbali vya historia. Wao huelezea tajiriba zao za historia ya jamii yao kupitia tanzu mbalimbali za fasihi. Kutokana na data ya utafiti huu, ilibainika kuwa msanii amewasilisha baadhi ya matukio ya kihistoria ya jamii ya Akamba kupitia nyimbo pendwa. Kupitia kwa nyimbo pendwa, wanajamiii hasa vijana hupata fursa ya kusoma kuhusu historia ya jamii yao na hivyo kuchangia utaifa wa jamii. Msanii huongozwa na uhalisia wa kijamii na huwa na maarifa muhimu kuhusu historia na utamaduni wa jamii yake ambao huupitisha kwa wanajamii. Wanajamii wanapojumuika pamoja na kumsikiliza, wanapata kuelewa usuli wa jamii yao.

Wimbo $W_{11}AR_H$ unajenga upya taswira ya kipindi cha kabla ya ukoloni nchini Kenya. Msanii anaisawiri jamii ya Akamba kiuchumi na kisosholojia. Anarejelea utaifa ambao wanajamii walikuwa nao kabla ya wakoloni. Wanajamii waliishi kwa umoja kwa kushirikiana wakati wa heri na shari. Iwapo mmoja wao angepata shida, basi wenzake wangekuja pamoja ili kumsaidia. Hali hii ndiyo wanajamii wanayoiita *kusuvia mbai* (Kuichunga jamii). Katika mshororo $M_1$, msanii anamwambia Mutua Katuku *Suvia mbai mani* (chunga jamii ndugu), maana yake ni kuwa ashughulikie jamii ya Akamba kwa vile ana uwezo wa kiuchumi. Msanii anamtarajia Mutua Katuku kusaidia jamii yake kama ilivyo katika utamaduni wa Akamba kwamba wale wenye uwezo walitarajiwa kuilinda jamii yao. Maneno hayo *suvia mbai* yametumiwa kama kibwagizo katika wimbo huu. Haya yanadhihirisha umuhimu wa wale wenye uwezo kuilinda jamii ya Akamba. Katika mshororo $M_5$, msanii anasema *mbai yumbanite* (jamii umekusanyika). Hii ina maana ya

watu wa jamii ya Akamba kuja pamoja wakati wa tukio fulani. Msanii anaturejesha katika kipindi cha ujima wakati watu wa jamii ya Akamba walishirikiana na ambapo kila mwanajamii alitarajiwa kuhusika katika shughuli za kijamii. Msanii anarejelea biashara ya vyuma inayoendeshwa na Mutua Katuku mjini Mombasa. Msanii anabainisha shughuli za kiuchumi ambazo wanajamii walishiriki; biashara kati ya bara na pwani hadi sehemu za bonde la ufa wakipitia Nairobi (Mbiti, 1991). Biashara yao ilihusisha uuzaji wa chuma miongoni mwa bidhaa nyingine. King'ei (1999), anasema kuwa Wakamba walipata vyuma vilivyoingizwa ndani ya nchi na pia kutoka kwa mashamba yao. Wakamba waliwauzia majirani wao chuma kwa mfano, jamii ya Wanyika ambao pia walipata bidhaa hii kutoka kwa Waarabu.

Kutokana na kauli hii, ni bayana kwamba Wakamba walishiriki biashara ya kuuza chuma kabla ya majilio ya wakoloni hadi sasa. Hii inadhihirisha historia ya jamii ya Akamba kupitia usimulizi wa msanii. Hapo awali, biashara iliongozwa na watu mashuhuri kama vile chifu na wengineo. Katika wimbo $W_{11}AR_{H}$, mhusika huyu anasawiriwa kama chifu ambaye anasimamia na kuendesha biashara ya kuuza chuma kati ya miji miwili mikuu; Nairobi na Mombasa. Mwikali (2021), anasema kwamba jamii ya Akamba ina ujuzi wa juu kama wafua chuma. Jamii hii ilikuwa miongoni mwa makundi ya Kibantu ambayo yalitambulisha teknolojia ya madini ya chuma katika eneo la Afrika Mashariki. Anaendelea kusema kuwa ingawa madini yale ya thamani ya juu hayajapatikana bado katika eneo hili, kuna kiwango kikubwa cha madini ya chuma yenye thamani kuu ambayo yanapendwa na watu wa Mombasa na wengine kutoka nchi ya India. Lindbloom (1920) anasema kuwa wakaazi wa eneo hili la Ukambani walikuwa na ufahamu wa uwepo wa madini haya ya chuma katika eneo hili ndiposa wakachukua eneo hilo kuwa makazi yao na kuliita Kitui; mahali pa kufua chuma yenye thamani ya juu. Msanii anaona kwamba biashara ya chuma inawaleta pamoja wanajamii ya Akamba na kujenga utaifa wao wakati mfanyibiashara Mutua Katuku anapoamua kushughulikia masilahi ya msanii pamoja na wanabendi wenzake.

Historia ya Akamba pia imewasilishwa kupitia wimbo $W_{15}AR_{H}M_{9}$, anapoelezea kuteuliwa kwa makamu wa rais wa kwanza kutoka kwa jamii ya Akamba. Anasema *Yuyu twina munini wa musumbi* M9 (Sasa tuko na makamu wa rais). Hiki ni kipindi maalum cha

kihistoria kwa jamii hii ya Akamba kwa vile ni mara yao ya kwanza kupata nafasi kuu ya uongozi serikalini. Msanii anarejelea tarehe 8/01/2008 wakati Kalonzo Musyoka aliteuliwa na rais Mwai Kibaki kuwa naibu wa rais wa kumi wa Kenya. Uteuzi huu wa kihistoria unaleta jamii ya Akamba pamoja kusherehekea ushindi wao. Hatua hii inachangia kurejesha amani nchini baada ya vita vya kikabila vya baada ya uchaguzi wa mwaka 2007 kulipuka. Wimbo huu unakuwa muhimu kwa jamii katika kusawiri hisia halisi zilizoambatana na kipindi hiki kwa taifa la Akamba na taifa la Kenya. Akishadidia umuhimu wa nyimbo pendwa, Maelo (2014), anasema:

> Watu ambao huwepo wakati matukio muhimu ya kihistoria yanapochipuka mara nyingi huyaelezea kupitia mashairi hasa nyimbo. Ingawa baadhi ya nyimbo huonekana sahili, huwa ni chemchemi ya habari kwa mwanahistoria kwa vile huwa ni kumbukumbu halisi ya vile watu walihisi wakati huo. Pia huonyesha namna walivyohifadhi hisia na mawazo yao.

Jamii ya Akamba inahisi kwamba wamepata ushindi na pia fursa ya kushiriki katika ulaji wa keki ya taifa. Hali hii inachangia utaifa wa jamii ya Akamba ambapo wanajamii wanamkumbusha kiongozi wao wa kisiasa kwamba walimpigia kura kwa hivyo ushindi wake ni wa jamii nzima. Maneno yafuatayo yanashadidia kauli hii:

| | |
|---|---|
| *Kula syitu sya Ukamba* M4 | Kura zetu Ukambani |
| *Sya kivila kiu kyailu* M5 | Za kiti hicho kinachostahiki |
| *Kya usumbi twanengie Kalonzo* M6 | Cha urais tulimpa Kalonzo |
| *Nundu nuvikie* kuuM14 | Sababu ulifika huko |
| *Yu maundu maitu usisye* M15 | Mambo yetu ungalie |
| *Withiwe kyeni kwitu* M16 | Uwe mwangaza wetu |

Wanajamii wa Akamba wanabainisha kwamba wana umoja wa maamuzi pia, wa azma yao. Wanaona kwamba wote ni washika dau katika ushindi wa kiongozi wao kwa hivyo wana haki ya kunufaika na matunda ya nafasi ile. Wanadhihirisha kwamba ushindi wa kiongozi yule kisiasa si wake pekee bali wa jamii zima. Kama washika dau, wanatoa ushauri kwa kiongozi huyu kuhusu namna atakavyotenda kazi kule serikalini. Anakumbushwa kwamba afanye kazi kwa bidii bila kusikiliza sauti za kumpinga na alete maendeleo kwa jamii yake. Haya yanadhihirisha utaifa wa jamii ambapo wanajamii wanajiona kama sehemu ya ushindi wa kiongozi wao na kutarajia manufaa.

Kipindi kingine cha kihistoria ambacho kimerejelewa ni wakati wa kupiga kura ya maoni ya katiba kielelezo mwaka wa 2005. Katika wimbo $W_{17}AR_{H}$, Msanii anaona ya kwamba

wanasiasa na viongozi wengine wa kijamii kama vile viongozi wa kidini wamefeli katika kuiongoza jamii na kudumisha mshikamano wa kijamii. Haya yanabainika kupitia mishororo $M_{6-11}$ ambapo anaweka wazi taasisi mbalimbali ambazo ziliathiriwa na tukio hili la kihistoria.

| | |
|---|---|
| *Makanisa unai thina M6* | Redio zilikuwa shida |
| *Selikali inai thina M7* | Magazeti ilikuwa shida |
| *Siasa mbingi no thina M8* | Siasa mingi za shida |
| *Katiba myau M9* | Katiba gani |
| *Redio inai thina M10* | Redio zilikuwa shida |
| *Magazeti unai thina M11* | Magazeti ilikuwa shida |

Kwa mujibu wa matini hii, taasisi muhimu za kijamii kama vile serikali, makanisa na vyombo vya mawasiliano vimeathiriwa na shughuli hii muhimu ya kitaifa. Umoja wa kijamii pia kitaifa umesambaratishwa na mojawapo wa shughuli ambayo inastahili kuwaunganisha. Wanajamii katika taifa lolote lile huunganishwa na vyombo vya uongozi kama vile serikali, dini, katiba na vyombo vya habari. Katika muktadha huu, hali inakuwa kinyume. Kwa mujibu wa msanii kuna wale wanaounga mkono katiba kielelezo na wengine wanaoipinga, hali inayosababisha kusambaratika kwa umoja wa taifa la Akamba. Katika mishororo $M_{19-21}$, msanii anasimulia madhara ya hali hii ambayo ni pamoja na siasa nyingi, chuki na mfumuko wa bei za bidhaa muhimu.

Msanii anasaili umuhimu wa katiba hii kielelezo. Madhara haya yanaathiri mshikamano na uchumi wa wanajamii ya Akamba. Msanii anajitenga na mchakato mzima wa kura ya maoni anaposema katika mshororo $M_{1,}$ *Sya katiba mwamina, mweka nesa mwamina* (Ya katiba mmemaliza, mmefanya vizuri kumaliza) kuonyesha kwamba hakuridhika na katiba kielelezo kwa hivyo hakushiriki katika shughuli yenyewe. Vile vile, anachukua fursa hiyo kutoa mwelekeo kwa jamii ambayo anaiona kama iliyoachwa bila mwelekeo. Anwani *Katiba Myau?* (katiba gani?) inakejeli katiba kielelezo kwa kutowahusisha wananchi wote ndiposa anakejeli umuhimu wake. Anaiomba jamii kuipinga katiba hii kielelezo kwa vile imesababisha utengano baina ya wanajamii.

Msanii anarejelea uhasama wa kijamii ambao ulikuwa ukitendeka katika miaka ya kabla ya wakoloni kuingia nchini. Kulikuwa na uhasama kati ya kabila la Kimasai na Wakamba ambapo Wamasai walikuwa wakinyakua mifugo kutoka kwa jamii ya Akamba. Vivyo hivyo, jamii ya Akamba ingeivamia jamii ya Wamasai na kuiba mifugo wao, wanawake

pamoja na bidhaa nyingine muhimu (Mwikali, 2021). Katika wimbo $W_8AR_H$ msanii anarejelea zana za kihistoria za vita kama vile *itumo* (mkuki) na fujo za Kimasai. Mkuki ni zana ya kivita ya jamii ya Kimasai. Pili, Wamasai wana wasifu wa kuwa na fujo. Msanii ana woga kwa sababu anaelewa fika wasifu wa jamii ya Wamasai. Wana hasira nyingi sana. Anasema: *Nākwã nōtā ngùkìā… vújo syā kìmásãi* (Na mimi ni kama naogopa… fujo za Kimasai). Katika mshororo huu msanii anaturejesha katika historia ya Wamaasai ambapo jamii zingine ziliwaogopa kutokana na mashambulizi yao ya mara kwa mara yaliyoambatana na fujo. Jamii ya Wamaasai walitegemea zana ya mkuki katika uvamizi wao kwa makabila mengine. Kupanda mkuki ni msemo ambao unamaanisha kunyakua, pia kuilinda jamii. Msanii anarejelea historia ya jamii yake kwa njia ambayo inaiunganisha jamii ya sasa na kuchangia utaifa wa jamii. Jamii ya Akamba ilikuwa na uhasama na jamii ya Wamasai na wakati mwingine vita vingetokea baina ya makabila haya.

Matukio mengine ya kihistoria ambayo yamesimuliwa kupitia nyimbo pendwa na kuchangia utaifa wa jamii ya Akamba yanapatikana katika wimbo $W_{16}AR_H$. Msanii anasimulia tanzia ya mwanasiasa Tony Ndilinge, mbunge wa eneo mbunge la Kilome na ambaye alikuwa pia kiongozi wa kitaifa aliyeuliwa. Tukio hili ambalo ni la kihistoria kwa jamii ya Akamba linabainika katika mshororo $M_3$ msanii anaposema: *Aliuwawa akiwa kwa gari mwaka elfu mbili na moja Agosti mbili.* Katika mshororo huu, msanii anataja mahali na wakati bainifu wa mauaji haya kama Agosti 2, 2001 anaposema aliuliwa akiwa kwa gari mwaka elfu mbili na moja. Hii ni tarehe ambayo imehifadhiwa kihistoria. Kwa mujibu wa msanii, haya ni mauaji ya kisiasa ambayo yanawaleta pamoja wanajamii wa jamii ya Akamba katika kumwomboleza shujaa wao. Hili linachangia ujenzi wa utaifa wa jamii.

Kupitia nyimbo pendwa msanii anajenga taswira ya uhusiano kati ya jamii za Kiafrika na zile za Kimagharibi kupitia wimbo wa kimapenzi, $W_1AR_H$. Wimbo huu unahusu mwanamume ambaye anawazia namna ya kumtembelea mpenzi wake, Mwende ambaye anaishi Ujerumani. Wimbo huu unaonyesha ukoloni ambapo jamii ya Akamba imeshindwa kukata minyororo ya kikoloni na kujikomboa kijamii, kisiasa na kiuchumi kupitia kwa mhusika huyu ambaye ametekwa nadhari na suala la kuzuru Ujerumani. Wimbo huu unakuwa uhakiki wa namna jamii ya Akamba haijaweza kujikomboa kutoka kwa minyororo ya kikoloni kwa vile mawazo yao yanaathiriwa na masuala ya kimagharibi.

Mhusika mwanamume katika wimbo huu ana tamaa ya kumtembelea mpenzi wake, Mwende, anayeishi Ujerumani. Anajaribu usafiri wa ndege na meli bila mafanikio kwa sababu ya ukosefu wa pesa. Anaonyesha kasumba ya kuthamini nchi za wakoloni kwa kuamua kutembea hadi Ujerumani. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Ngilasya niilye ngethia ngiota na Mwende M1* | Nikiwa nimelala naota na Mwende |
| *Ngethe yi muingo Germany kweli ngewa kuia M2* | Msichana aliyeenda Ujerumani nasikia kulia |
| *Ngakwatwa ni mutwe wa kwenda kuka naku ngwone M4* | Napatwa na mawazo ya kukuja nikuone |
| *Niendaa airport mbangite nyie ulisa ndeke M5* | Napanga kwenda uwanja wa ndege kusafiri |
| *Ngewa vai sare ya ndeke nombaka ngaiva M6* | Naambiwa hakuna cha bure sharti nilipe |

Ingawa mkoloni aliondoka barani Afrika, bado mapenzi yapo kwa yule mkoloni. Nchi za Kiafrika bado zinategemea nchi za magharibi katika kuendesha shughuli zao nyingi miongo mingi baada ya mkoloni kuondoka barani Afrika. Nchi hizi za Kiafrika hazijaweza kukata minyororo ya kikoloni na kuondoa kasumba zao. Msanii anarejelea hali hii ya utegemezi katika wimbo $W_1AR_H$. Ingawa msanii angependa kumtembelea mpenziwe, anakosa uwezo wa kifedha. Anajaribu mbinu kadhaa lakini anashindwa. Anaelezwa ya kwamba hakuna cha bure; lazima alipe. Hili linabainisha kwamba mataifa haya machanga ya Kiafrika bado yana uwezo mdogo ikilinganishwa na mataifa ya kimagharibi hali ambayo inayafanya yashindwe kuondoa utegemezi wao. Huu ni ukoloni mamboleo. Kwa njia hii, msanii anasawiri jinsi mataifa ya kimagharibi yanavyoathiri uendeshaji wa nchi changa barani Afrika. Jamii ya Akamba imeathiriwa na ukengeushi huu. Msanii anaiomba jamii isikubali kukengeushwa na mawazo ya kikoloni kwamba ufanisi wao utatokana na maingiliano yao na jamii za kimagharibi. Msanii ameshindwa kuuvunja uhusiano huu ingawa hafaidiki nao. Hii ni hali ambapo jamii ya Akamba imeshindwa kuvunja uhusiano na nchi za kigeni; uhusiano ambao hauna manufaa yoyote kwa wanajamii.

Msanii anasimulia historia ya jamii ya Akamba katika kipindi cha utandawazi. Kipindi cha utandawazi ni kipindi cha historia ambacho kimewezesha watu wa mabara na nchi mbalimbali kutagusana katika shughuli mbalimbali na kukopa tamaduni. Katika $W_8AR_H$, kuna mwingiliano wa jamii ya Akamba na jamii nyingine kama vile Wamaasai na

Wakorea. Mwingiliano huu unatarajiwa kuathiri uchumi na utamaduni wa jamii ya Akamba kwa mfano, katika mshororo $M_{25}$ msanii anatarajia kujifunza Kikorea ili atunge nyimbo kwa Kikorea (*Mumiwé Kikorea* - mnisikie Kikorea). Hivyo, atajifunza utamaduni wa Kikorea ili aweze kukuza usanii wake. Kupitia mahusiano haya, uchumi wa jamii ya Akamba utaimarika.

Katika wimbo $W_{23}AR_{H,}$ msanii amemtaja Kyalo wa Muli kama mwanabiashara anayeshiriki biashara za kimataifa. Katika mshororo $M_4$, anatueleza kwamba Kyalo hushiriki biashara Dubai. Biashara ya kimataifa ni sehemu ya utandawazi. Kyalo wa Muli ana mpango wa kuuza vikapu Ulaya na sehemu nyinginezo. Hii inaonyesha kuwa jamii ya Akamba inaendeleza utandawazi kupitia biashara. Mwanasiasa kwa jina Kyalo wa Maendeeyo (Kyalo wa Maendeleo) ameanzisha wakfu ambao kupitia kwake wanajamii watashirikiana kufuma vikapu ambavyo vitauzwa Ulaya na kwingineko. Ushirikiano huu kupitia wakfu na ufumaji wa vikapu unawaleta pamoja wanawake wa Akamba na kujenga utaifa wao.

### 4.3 Uhakiki wa Mbinu za Kimtindo Zinazojenga Utaifa wa Jamii ya Akamba

Madhumuni ya pili ya utafiti huu yalijihusisha katika uhakiki wa mbinu za kimtindo zinazojitokeza katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria ambazo zinajenga utaifa wa jamii ya Akamba. Uhakiki wa maumbo katika fasihi ni muhimu kwa vile huchunguza vipengele anuwai vya kimtindo na kifani na kutathmini umuhimu wake katika ujenzi wa utaifa wa jamii. Ndung'u (2022), akirejelea nadharia ya umitindo alidai kuwa vipengele vya kimtindo kama vile ploti, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha ni muhimu kwani husaidia katika kuchanganua mtindo katika tanzu za fasihi. Mihimili ya nadharia hii ambayo ilimwongoza mtafiti katika kuhakiki dhana ya maumbo katika utafiti huu ni uchunguzi wa semantiki katika fasihi na pili ni kiwango cha muundo wa masimulizi katika makala ya fasihi. Mtafiti alibaini kuwa msanii ametumia mbinu za kimtindo anuwai kupitia lugha ambazo zinajenga utaifa wa jamii ya Akamba.

Lugha huwa na mchango muhimu katika kazi yoyote ile ya fasihi. Lugha ndiyo hutofautisha fasihi na sanaa nyingine kama vile uchoraji, uchongaji na ufinyanzi. Senkoro (1982), anasema kuwa lugha katika fasihi ndiyo malighafi ya kuundia sanaa hiyo. Lugha hutumiwa kuelezea kuhusu yanayotendeka katika jamii fulani kwa njia ya kibunifu. Katika

sehemu hii, mtafiti alichunguza vipengele mbalimbali vya lugha vilivyotumiwa katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria. Dhana za lugha zilizohakikiwa ni kama vile usimulizi na misemo. Vigezo vingine vya lugha ambavyo vilichanganuliwa ni pamoja na matumizi ya taswira, methali, chuku, majazi, jazanda pamoja na aforisimu. Hizi zilijumuishwa katika tamathali za usemi. Wamitila (2008) anakuli kwamba tamathali za usemi ni lugha ya kitamathali zinazojumuisha sifa nyingi za kimtindo. Dhana hii huelezea aina ya ukiushi wa kimaksudi katika matumizi ya lugha. Ukiushi huu unaweza kuwa wa kimaana au kimuundo. Katika ukiushi huu, neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi.

Mbatiah (2001) anaona kwamba tamathali za usemi ni ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha katika kiwango cha maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Tamathali ya usemi ni fungu la maneno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine. Lugha ya tamathali huwa na umuhimu mkubwa katika utunzi wa kazi za kifasihi. Kwanza ni urembeshaji wa kinachozungumziwa au kurejelewa na lugha hiyo na kukifanya kiwe na mvuto mkubwa wa kisanaa au kiumbuji. Pili, ni jukumu la ufafanuzi wa kinachohusishwa na tamathali maalum na tatu ni jukumu la uthabitishaji yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani (Wamitila, 2008). Majukumu haya huwa na lengo la kuzua lugha au usemi wenye uwezo wa kushawishi.

Mbinu za kitamathali huifanya kazi ivutie, iwe na msisitizo na mnato mkubwa. Huvutia nadhari ya hadhira na kuziathiri hisia zao. Ni kigezo mojawapo cha kupimia ubunifu na umbuji katika kazi fulani. Utafiti wetu ulibaini kuwa msanii Ken wa Maria hutumia mbinu mwingiliano katika kupitisha ujumbe wake wa ujenzi wa utaifa wa jamii. Kuna mwingiliano wa maudhui ya ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo zake kwa mfano, $W_8$, $W_3$. Hali ya mikorogo katika jamii inazaa suala la Mkorea ambapo wanajamii wanakiuka majukumu yao ya kijamii. Uhusiano wa msanii na Mkorea unaleta hali ya mkorogo katika jamii. Mwanamke anachukua jukumu la kumtongoza mwanamume, suala ambalo halikubaliwi katika jamii nyingi za Kiafrika ikiwemo jamii ya Akamba. Huu ndio mkorogo ambao msanii anaurejelea. Katika utafiti wetu, tuliangalia tu zile mbinu ambazo

zilibainisha ujenzi wa utaifa miongoni mwa jamii ya Akamba kupitia nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

### 4.3.1 Usimulizi

Dhana hii imefasiliwa na wataalamu wengi kwa njia tofauti. Wales (1990), anasema kuwa usimulizi ni kipengele cha mchakato mzima wa mawasiliano au diskosi baina ya mwandishi na msomaji, na kati ya msimulizi na msimuliwa. Njogu na Chimerah (1999), wanasema kuwa usimulizi ni sauti ya uwasilishaji wa hadithi. Naye Wamitila (2003), anaeleza usimulizi kama uelezaji wa matukio katika hadithi. Mutembei, (2012) anasema kwamba usimulizi ni namna mtunzi anavyotoa visa vyake kupitia kwa wahusika ambao anawapa lugha, matendo na kuwavisha uhalisia. Wambui (2018), amebainisha aina saba za usimulizi; usimulizi ndani, usimulizi nje, usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya pili, usimulizi wa nafsi ya tatu, usimulizi sawia na usimulizi sogomezi. Mwangi, (2021), anasema kuwa kuna aina mbalimbali za usimulizi. Kwanza kuna usimulizi unaoendelezwa na msanii mwenyewe kuelezea matukio fulani yanayofungamana na jamii husika. Aina ya pili ni masimulizi yanayosimuliwa na wahusika wengine. Aina nyingine ni masimulizi yanayojitokeza katika nafsi ya mhusika. Katika kuchanganua mbinu hii, mtafiti alibaini kuwa mbinu ya usimulizi ilijitokeza katika nyimbo teule za msanii Ken wa Maria na kukuza utaifa wa jamii ya Akamba.

Katika kuchanganua mbinu hii, mtafiti aliongozwa na nguzo ya usimulizi na mtindo iliyohakikiwa na Simpson (2004), katika nadharia ya umitindo. Simpson alidokeza kuwa usimulizi katika utanzu wowote wa fasihi ni muhimu katika kuelezea matukio yanayoshughulikiwa na mtunzi. Katika wimbo $W_{11}MB_S$, msanii ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza. Usimulizi wa nafsi ya kwanza huhusisha matumizi ya kiambishi ‘ni’ katika kauli kudhihirisha uwepo wa msimulizi katika matukio anayosimulia. Msanii hutumia nafsi ya kwanza kupitia viwakilishi ‘mimi’ na ‘ni’ ili kujitambulisha kwa wasomaji. Vile vile, viwakilishi ‘mimi’ na ‘ni’ humfanya msomaji anaposoma hadithi amfuatilie msimulizi na kukubaliana na mtazamo wake katika simulizi.

Msimulizi hutawala matukio ya hadithi (Wambui, 2018). Kiambishi ‘ni’cha usimulizi wa nafsi ya kwanza hujitokeza kama kiambishi ‘na’, ‘ne’ pamoja na ‘ni’ kwa lugha ya Kikamba. Katika mshororo $M_{11}$, msanii anasema *naumite* (nilikuwa nikitoka), kiambishi

'na' kimetumika kumtambulisha msanii kama msimulizi na pia mhusika katika usimulizi huu. Msanii amesimulia kuhusu ziara yake mjini Mombasa ambapo alikuwa ameenda kuchukua picha za video za wimbo wake Freddie. Anasimulia kuhusu ukarimu wa Mutua Katuku ambaye anashughulikia masilahi ya msanii pamoja na wanabendi wenzake. Kupitia wimbo huu, masuala kadhaa kama vile suala la utaifa wa jamii ya Akamba yanajitokeza. Kwanza, wimbo huu unasimulia shughuli za kijamii za jamii ya Akamba kabla ya ukoloni hadi sasa. Jamii ya Akamba ilijulikana kwa kushiriki katika biashara ya masafa marefu baina ya jamii tofauti nchini na nje ya nchi. Walifanya biashara kati ya mji wa Nairobi hadi Mombasa. Katika mishororo $M_{12-14}$, msanii anasema ya kwamba alikuwa ametoka Nairobi kwenda Mombasa na shughuli iliyompeleka kule ilikuwa ya kibiashara; kuchukua picha za video katika uundaji wa video mpya aliyoimba kwa jina Freddie. Anasimulia namna alivyotoka Nairobi kwenda Mombasa na yaliyojiri kule. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Naumite Ilovi, M11* | Nilitoka Nairobi |
| *Ngavika Mombasa, M12* | Kuelekea Mombasa |
| *Kwosa tumavisa, M13* | Kuchukua video |
| *Wathi ula wa Freddie, M14* | Wimbo wa Freddie |

Wimbo huu unasimulia kuhusu biashara anayofanya Mutua Katuku ambayo ni ya kuuza vyuma vikuukuu. Ni biashara ambayo msanii angependa kufunzwa na kujihusisha nayo kwa vile anaona kuwa itakuwa na manufaa mengi, si kwa msanii pekee bali kwa jamii nzima kwa jumla. Tangu jadi jamii ya Akamba imehusika na ufuaji wa vyuma na uuzaji wake baina yao na jamii zingine humu nchini na nje. Wakamba walifanya biashara na Waarabu na jamii za kutoka bonde la ufa (Mbiti (1991), King'ei (1999)). *Viasala wa syuma* (biashara ya kuuza chuma) imekuwa shughuli muhimu ya kiuchumi ya jamii hii na ilikuwa utambulisho wa jamii ya Akamba. Msanii pia anaelekea kusimulia kuhusu baadhi ya miji ambayo biashara hii ilikuwa ikitendeka: kati ya mji wa Nairobi na Mombasa. Haya yalikuwa maeneo ya biashara ya jamii ya Akamba. Kupitia kwa usimulizi huu wa kihistoria, msanii anabainisha hali ya bidii kazini waliyo nayo wanajamii ya Akamba.

Mbinu hii ya usimulizi kupitia nafsi ya kwanza pia inajitokeza katika wimbo $W_1MB_S$, ambao ni usimulizi wa msanii mwenyewe. Anasimulia kuhusu namna anavyompeza Mwende pamoja na juhudi zake za kwenda kumtembelea mpenzi wake ambaye yuko ng'ambo. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Ngilasya niilye ngethia ngiota na Mwende M1* | Nikiwa nimelala naota na Mwende |
| *Ngethe yi muingo Germany kweli ngewa kuia M2* | Msichana aliyeenda Ujerumani nasikia kulia |
| *Wiku muingo ngumisia muno we Mwende M3* | Ukiwa kule ughaibuni nakupeza sana Mwende |

Msanii anasimulia kuhusu upweke anaoupitia kutokana na utengano wa kimasafa kati yake na mpenzi wake, Mwende. Anakumbwa na changamoto nyingi katika azma yake ya kutaka kumtembelea mpenziwe. Uhusiano wa msanii na mpenzi wake umekumbwa na tatizo kwa sababu wawili hawa wametenganishwa na umbali wa nchi hizi mbili. Utaifa wa jamii ya Akamba unaathirika wakati ambapo wanajamii wake wanatengana na kuishi katika maeneo tofauti tofauti ya ulimwengu. Mojawapo wa arki zinazojenga utaifa wa jamii ni jiografia ambapo watu ambao wana utaifa wao ni sharti wawe katika eneo moja la kijiografia.

Licha ya changamoto anazopitia, msanii haelekei kukata tamaa. Anaamua kwamba atatembea hadi nchi ya Ujerumani ili angalau awe na Mwende, mpenzi wake. Msanii ameturejesha nyuma katika nyakati za kabla ya ukoloni wakati mbinu za usafiri zilikuwa chache na za kitamaduni kama vile kutembea. Msanii anasema kwamba amejaribu mbinu za kisasa zilizoletwa na mkoloni kama vile kuabiri ndege na kuabiri meli lakini juhudi zake zote zimegonga mwamba kutokana na ukosefu wa pesa. Hivyo, anaamua kutembea hadi mji wa Munich nchini Ujerumani ambako mpenzi wake Mwende yuko. Katika mshororo $M_9$, msanii anaposema *Niuka na maau Germany- Munich switie* (Nitakuja Ujerumani kwa miguu mpenzi), msanii anaonekana kupingana na ukoloni ambao ndio chanzo cha masaibu yake. Ni kana kwamba msanii anairejesha jamii kwenye kipindi cha majilio ya wakoloni lakini wakati huu Waafrika wanafanya mambo kinyume. Hataki kutumia miundo misingi iliyoletwa na mkoloni bali anataka atumie mbinu za usafiri za awali za jamii yake; kutembea kwa miguu. Anaona kwamba changamoto ambazo zimeletwa na mkoloni na ambazo zimechangia kudidimia kwa utaifa wa jamii yake zinaweza kuepukwa iwapo Waafrika watatumia mbinu zao za kiasili.

Usimulizi wa nafsi ya kwanza pia umetumika katika $W_3MB_S$ msanii anaposimulia kuhusu namna wasichana kutoka jamii ya Akamba walivyokengeuka. Kupitia mbinu hii ya usimulizi, msanii anatuchorea picha halisi ya namna msichana waliyemwona mjini

Makutano alivyolimatia mienendo ya kizungu hadi kudharau rangi ya ngozi yake. Msichana huyu amekengeuka kiasi kwamba anaona rangi ya ngozi yake ni duni hivyo basi anajipaka vipodozi ili ngozi yake ifanane na ile ya wazungu. Katika mshororo $M_{2-6}$ Anasema *nonie ngethe yathandika yiilye Musungu* (niliona msichana aliyekaa mzungu). Msemewa katika mshororo huu amebadili sura yake ikafanana na ya mtu mweupe. Msanii anaona kwamba utaifa wa awali wa jamii yake umeanza kusambaratishwa na mienendo hii ya kigeni.

Llobera (1999), anasema kwamba kila jamii huwa na utaifa wa awali. Utaifa wa awali huchukulia kwamba kila kikundi lazima kijitambulishe. Aidha, katika jamii mbalimbali, kuna mahusiano ya kiukoo au damu, rangi, lugha, dini na mahusiano ya kimaeneo ambayo japo hayaelezeki ni ya lazima. Kwa kuzingatia maneno ya msomi huyu, msanii anaona kuwa utaifa wa jamii ya Akamba umo hatarini. Anataka wanajamii wenzake wajivunie ngozi yao, lugha yao, eneo lao na usuli wao. Katika mshororo $M_{12}$, Msanii ana mawazo kwamba ngozi yake ni nzuri kwani yeye ni *Mukamba kivindyo* (Mkamba halisi). 'Mukamba kivindyo' ni yule mkamba ambaye anajua na kuzielewa mila na desturi za jamii yake ya Akamba. Amezaliwa Ukambani, akakulia kule na hajaathiriwa na usasa. Huyu ni yule ambaye anajivunia rangi yake ambayo ndicho kitambulisho cha asili yake.

Kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza msanii anaelekea kuitahadharisha jamii yake kuhusu kupapia mitindo ya kigeni ambayo anaona itakuwa hatari kwa utaifa wa jamii ya Akamba. Katika mshororo wa saba $M_{7,}$ Msanii anasema kwamba vipodozi wanavyojipodoa ni kemikali hatari. Wasichana wanaotumia mikorogo hii ni wale ambao wana nia ya kuwavutia wanaume na kuwanasa katika madanguro mjini Makutano. Makutano unakuwa mji ambapo utamaduni wa jamii ya Akamba unakutana na utamaduni wa kigeni (Kiio, 2023). Kupitia mkutano huu, kuna tishio kwamba utaifa wa jamii ya Akamba umo hatarini ya kuathiriwa na utamaduni huu mgeni ambao una nguvu zaidi. Tabia hii ya wasichana mjini Makutano ni kinyume cha utamaduni wa jamii ya Akamba ambapo mahusiano kama haya hayakurusiwa.

Mwikali (1990), anasema kwamba wakati Wazungu walivamia eneo la Ukambani, walipata jamii ambayo ilikuwa imeunganishwa pamoja. Maisha ya jamii hii yaliendeshwa kwa sheria, mila na tamaduni za kijamii ambazo zilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi

kingine. Masilahi ya jamii hii yalitegemea uzingativu wa haki na miiko ya kijamii. Kupitia mbinu ya usimulizi msanii anabainisha kuwa wapo wanajamii ambao wameasi utamaduni wa jamii ya Akamba na kulimatia utamaduni wa kigeni kama vile mhusika Mwikali wa Kaumbulu katika wimbo huu. Kupitia mbinu ya usimulizi, msanii anaitahadharisha jamii yake kuhusu kukumbatia utamaduni ambao utavunja utaifa wa jamii ya Akamba. Anaitaka jamii ilimatie utamaduni wao na kuenzi hali yao ya kimaisha kwani inahalisi namna ilivyo.

Usimulizi wa nafsi ya pili umejitokeza katika $W_7MB_{S.}$ Katika usimulizi wa nafsi ya pili kiambishi kiwakilishi ‘u’ katika umoja na ‘m’ katika wingi ndicho hutumiwa katika kujenga uhusiano wa karibu baina ya msimulizi, wahusika na msomaji. Viambishi hivi hujidhihirisha kama ‘u’, ‘wa’ na ‘mwa’ kwa lugha ya Kikamba. Katika mshororo $M_{1,3,}$ ametumia viambishi ‘wa’ katika neno ***wa**-mbíie* (uliniambia) na ‘u’ katika ***u**-kanzuvia* (utanitunza) kurejelea mhusika mwanasiasa ambaye alitoa ahadi wakati wa kampeni. Viambishi hivi vimetumika na msanii kubainisha mchango wa viongozi katika ujenzi wa utaifa. Kiongozi anayerejelewa ameisaliti jamii ya Akamba na kuwa kikwazo katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Wakati wa kampeni viongozi wa Akamba hujitokeza na ahadi kwa taifa la Akamba ambazo huwa ni za kutatua matatizo yao kama jamii. Hata hivyo, baadhi ya ahadi hizo huwa hazitimizwi. Hivyo nafsi ya pili inakuwa muhimu katika kuwakumbusha viongozi ahadi walizotoa.

Aina nyingine ya usimulizi ambao umetumiwa na msanii ni usimulizi wa nafsi ya tatu. Mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu kama alivyodokeza Wambui (2018), akimnukuu Stanzel (1984), hutambulishwa kwa kiambishi cha mofu ‘a’ na ‘wa’ katika umoja na wingi mtawalia kumrejelea mhusika mkuu katika simulizi yake. Usimulizi huu huonyesha kuwa msimulizi amejitenga na matukio anayosimulia katika hadithi. Msimulizi husimulia kuhusu mtu mwingine wala si yeye mwenyewe. Usimulizi wa nafsi ya tatu katika lugha ya Kikamba huchukua viambishi ‘a’, ‘ma’ pamoja na ‘e’ katika umoja na wingi. Usimulizi huu unajitokeza katika wimbo $W_6MB_S$ ambapo msanii anasimulia kisa cha sungura na ndovu, ambao umechotwa kutoka simulizi za jamii ya Akamba.

| | |
|---|---|
| *Kavaluku keiwe ni Nzou* M1 | Sungura aliambiwa na ndovu |
| *Uyu ni usi muliku* M2 | Huu mto ni una kina kirefu |
| *Ndukatate kuinga ta Nzou* M3 | Usijaribu kuvuka kama ndovu |
| *Ndukatwawe ni kiw’u* M4 | Usisombwe na maji |

| | |
|---|---|
| *Kavaluku keie nzou* M5 | Sungura akamwambia ndovu |
| *Ndukatate undia* M6 | Usije ukaniacha |
| *Kitaeka nyie ngulise muongo* M7 | Wacha nipande mgongo wako |
| *Ndikatwawe ni kiw'u* M8 | Nisisombwe na maji |

Katika mshororo $M_{1-11}$, msanii ametumia viambishi 'ka' na 'ke' badala ya 'a'na 'e' kama viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya KA –TU ambayo ni ya udunishaji kwa vile sungura ni mnyama mdogo akiliganishwa na ndovu. Katika lugha ya Kiswahili, viambishi vya udogo ambavyo hutumika pia katika udunishaji ni KI (ji)- katika umoja na VI (ji)- katika hali ya wingi. Msanii amevitumia viambishi hivi ili kusimulia matendo ya wahusika Ndovu na Sungura. Viambishi hivi vinampa nafasi msanii kusimulia uhusiano kati ya viongozi na wananchi wa taifa la Akamba katika ujenzi wa utaifa bila kumhusisha msanii moja kwa moja. Msanii anasema kuwa siku moja Sungura na Ndovu wakiwa katika harakati za kuvuka mto ambao ulikuwa umefurika Ndovu alimshauri Sungura kwamba asithubutu kuuvuka ule mto kama Ndovu kwa kuwa angesombwa na maji. Sungura naye akamwomba Ndovu asije akamwacha heri ambebe mgongoni ili amvushe mto. Ndovu akakubali na kumvusha ule mto. Sungura alipotua salama upande wa pili wa mto hakumshukuru Ndovu kwa wema wake ila alimsimanga kuwa hakuna jambo kubwa ambalo alikuwa ametenda. Ndovu hakukasirika ila aliendelea na shughuli zake lakini akamwonya Sungura ya kwamba iwapo angetaka kurejea alikotoka, ingebidi atafute namna nyingine. Usimulizi huu unabainisha baadhi ya changamoto zinazokumba ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba kama vile ubinafsi na ukosefu wa fadhila miongoni mwa wanajamii. Unakuwa funzo kwa jamii ya Akamba kuhusu wanajamii ambao huomba msaada kwa wanajamii wenzao lakini baada ya kupata ule msaada wanakosa shukrani. Wao huwaona wale waliowaauni wakati wa dhiki kwamba hawakutenda lolote kubwa na kudhani kwamba wangefanikiwa bila usaidizi wao.

Kupitia usimulizi katika wimbo huu, mpangilio wa kijamii wa jamii ya Akamba unajitokeza. Msanii anabainisha kwamba jamii ya Akamba haienzi ubinafsi miongoni mwao. Mambo hufanywa kwa umoja na ushirikiano wa wanajamii wote. Shida ya mwanajamii mmoja huwa mzigo kwa wote na wanajamii huungana katika kutatua matatizo yao. Katika mshororo $M_1$, msanii anadokeza kwamba kuna wale ambao wanashikilia nyenzo za uongozi. Hawa ndio huiongoza jamii yao hadi ifikie ufanisi. Hawa ndio

wanaowakilishwa na ndovu. Hutoa tahadhari kwa wanajamii wenzao na mwelekeo wakati wa hatari na kuhakikisha kwamba jamii inafanya maamuzi ya busara wakati wowote ule. Wao huiongoza jamii kisiasa, kiuchumi na kijamii. Matarajio yao ni kwamba wanajamii watafuata maelekezo wanayotoa ili kufikia ufanisi. Viongozi hawa ndio huhakikisha utaifa wa jamii umedumishwa. Wanaposimangwa au kudharauliwa na wanajamii wanaojiona kama wajanja huwa hawachukulii kama jambo kubwa. Haya yanajitokeza katika mshororo wa $M_{13}$ msanii anaposimulia kuhusu hatua alizochukua Ndovu; *Nawe Nzou ndaosa tondu* $M_{13}$ (Ndovu hakuchukulia hilo kwa uzito). Msanii anadhihirisha kuwa utaifa wa jamii utajengwa na kudumishwa na viongozi ambao hawaathiriwi vibaya na vitendo vya kibinafsi vya wanajamii wenzao. Jukumu la viongozi wa kijamii ni kuona kwamba changamoto zinazoikumba jamii zimetatuliwa na mshikamano wa jamii yao umedumishwa. Kunao wafuasi ambao huwa kama Sungura. Hawana nguvu ila wanategemea uwezo wa wanajamii wenzao hasa viongozi. Wakati wanapopata msaada walioutaka basi wanajitenga na jamii yao na kuanza maisha yao upya. Msanii anaionya jamii ya Akamba kuhusu wanajamii kama hawa ambao huenda wakavunja mshikamano wa kijamii.

Wimbo $W_6MB_S$ umesilimishwa kutoka fasihi simulizi ya jamii ya Akamba. Kupitia kwa wahusika wanyama katika wimbo huu, utaifa wa jamii ya Akamba unajitokeza kupitia usuli wa jamii hii. Baada ya jamii ya Akamba kuhama kutoka msitu wa Kongo, walipiga kambi katika maeneo ya Kilimanjaro ambayo yalikuwa makao ya wanyama mwitu kama vile ndovu na sungura. Wimbo huu unasimulia namna jamii hii ilivyohama kutoka makao yao ya kiasili hadi kufika waliko kwa sasa. Wimbo huu pia unaweka mwanga imani ya jamii ya Akamba kuhusu uongozi na ushirikiano wa kijamii. Ndovu anaashiria viongozi ilhali Sungura anawakilisha wanaoongozwa katika jamii. Wimbo huu unaonya wanajamii kuhusu hali ya kutotosheka katika jamii, jambo ambalo linaweza kuvunja utaifa wa jamii ya Akamba.

Usimulizi wa nafsi ya tatu umetumika katika $W_{11}MB_S$ kutoa wasifu wa mhusika Mutua Katuku ambaye anasawiriwa kama kielelezo cha wanajamii ambao huchangia katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Katika mishororo $M_{25\text{-}30}$, msanii anasema:

*Mbaitu mukamwona, M25* Watu wangu mkimwona

| | |
|---|---|
| *Mundu mutheke vyu, M26* | Mtu mwembamba sana |
| *Lakini akili, M27* | Lakini akili |
| *Ya kumantha mbesa, M28* | Ya kutafuta pesa |
| *Na kutongoesya mbai, M29* | Na kuongoza jamii |
| *Mutua Katuku ii, M30* | Mutua katuku |
| *Mundu ute mathinaa M31* | Mtu asiye na shida |

Katika mshororo $M_{31}$, kiambishi ‘u’ ambacho kinawakilisha nafsi ya tatu umoja katika lugha ya Kikamba kimetumiwa kumrejelea mhusika Mutua Katuku. Kwa mujibu wa msanii, Mutua ana bidii kazini na pia ni kiongozi shupavu wa jamii. Kupitia kwa mhusika Mutua Katuku, msanii anamsawiri kiongozi wa kijamii au chifu (*kutongoesya mbai* – kuongoza jamii), ambaye anachunga masilahi ya jamii yake (*Kusuvia mbai*). Pia anawafunza wengine biashara hii ya kuuza chuma ili waweze kujikimu maishani. Haya yanajitokeza katika mshororo wa $M_{32}$ msanii anaposema:

| | |
|---|---|
| *Nienda ukola wathi, M32* | Nataka kuacha kuimba wimbo |
| *Ambundisye viasala, M33* | Anifunze biashara |

Mshikamano wa kijamii unajitokeza kupitia matendo ya mhusika Mutua Katuku. Anahakikisha kuwa wanajamii wenzake hawapati shida wanapokuwa katika ziara yao mjini Mombasa. Inaelekea mhusika huyu ndiye anayeongoza biashara hii mjini Mombasa ndiposa msanii anadokeza kwamba ataacha usanii kwa muda ili akafundishwe biashara na Mutua Katuku. Katika jamii nyingi za Kiafrika kabla ya majilio ya elimu rasmi, wanajamii walipata mafundisho kuhusu taaluma mbalimbali kupitia kwa magwiji waliobobea katika taaluma hiyo. Wao ndio waliokuwa walimu wa taaluma husika. Walihakikisha kuwa ufundi waliokuwa nao ungepitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine ili kuendelea kuifaidi jamii yao. Taaluma na ufundi mbalimbali katika jamii ya Akamba ilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia mbinu hii. Akishadidia kauli hii, Mwikali (2021), anasema kuwa maarifa yalipitishwa kwa njia ya mdomo kutoka kwa mwenye ujuzi hadi kwa anayesoma kupitia mbinu ya uanagenzi. Msanii anathibitisha haya kupitia mishororo $M_{32\text{-}38}$, anaposema kuwa ataacha usanii kwa muda mfupi ili aende kwa Mutua Katuku ili aweze kufundishwa namna ya kuiendesha biashara hii ya kuuza vyuma kuu kuu. Kupitia usimulizi huu msanii anaisawiri jamii ambayo ina mshikamano ambao unachangia ujenzi wa utaifa wao.

Katika mshororo $M_{40-53}$, msanii anasimulia kuwa baada ya kujua namna ya kuiendesha ile biashara atarudi mjini Nairobi, aanzishe biashara yake ya kuuza chuma ili atengeneze pesa kama Mutua Katuku na aanze kushughulikia masilahi ya jamii yake. Kupitia kwa biashara hii, msanii anaona kwamba jamii yake itafaidika pakubwa kwani itatoa ajira kwa vijana wengi ambao hawana kazi katika eneo la Ukambani la Matuu, Kasolongo na Kwa Kipevu. Kupitia usimulizi wa msanii, umoja na mshikamano wa kijamii unajidhihirisha. Jamii inayosawiriwa na msanii ni ile inayojaliana, kupendana na kusaidiana wakati wa dhiki. Msanii anapendekeza wanajamii kuwa kama Mutua Katuku ambaye anaiunganisha jamii ambapo kila mwanajamii anajali masilahi ya mwanajamii mwenzake hali ambayo inakuza utaifa wa jamii ya Akamba.

### 4.3.2 Takriri

Wandera (2022), anasema kuwa takriri katika kazi ya fasihi ni urudiaji wa silabi, maneno au sentensi kwa nia ya kusisitiza jambo linalozungumziwa na mtunzi. Takriri ni marudio ya maneno fulani katika tungo ili kuleta hisia na athari fulani katika akili ya msomaji au kwa masikio ya msikilizaji. Lengo kuu la kutumia mbinu hii ni kuteka nathari ya hadhira. Senkoro (2011), akifafanua dhana ya takriri anadokeza kuwa takriri ni mbinu ya utunzi inayohusu urudiaji wa sauti, silabi, mistari, maneno, vifungu na hata sentensi na mistari fulani katika kazi ya fasihi kwa madhumuni maalum. Kwa upande mwingine, Ngure (2003), anakuli kwamba takriri ni urudiaji wa silabi au sauti zinazowiana au kukaribiana kimatamshi kwa kusudi la kutilia mkazo au kusisitiza jambo fulani. Katika mbinu hii, msanii katika utunzi wake ana uwezo wa kurudia maneno, sauti, kishazi, kirai na hata sentensi katika kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa utafiti huu, uradidi ni ile hali ya kurudiarudia maneno au sentensi katika maandishi ukiwa na lengo fulani. Mbinu hii imetumiwa na msanii kuleta msisitizo ambao unadhamiria kujenga utaifa wa jamii ya Akamba.

Katika wimbo $W_{12}MB_{T}$, msanii ametumia mbinu ya takriri mshororo ili kuleta dhana ya msisitizo. Maneno *ngwendeaa kuka oyu kwa mituki mituki mituki* (nakupenda kwa kuja sasa haraka haraka haraka) yamerudiwa rudiwa. Kupitia kwa mbinu ya takriri msanii anaweka wazi majukumu muhimu yanayotekelezwa na mwanamke katika jamii ya Akamba. Katika mishororo $M_{1-6}$, mwanamke amesawiriwa kama mwenye bidii na wa

kutegemewa katika jamii. Msanii anasema ya kwamba anapomwita daktari, yeye huja kumhudumia kwa haraka na kuhakikisha kuwa amepata siha njema. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Ngwéndéá kuká oyu kwa mituki mituki mituki M1* | Nakupenda kwa kuja haraka haraka haraka |
| *Ngwéndéá kuká oyu kwa mituki mituki mituki M2* | Nakupenda kwa kuja haraka haraka haraka |
| *Ngwéndéá kuká oyu kwa mituki mituki mituki M3* | Nakupenda kwa kuja haraka haraka haraka |
| *Ngwéndéá kuká oyu kwa mituki mituki mituki M4* | Nakupenda kwa kuja haraka haraka haraka |
| *Ngwéndéá kuká oyu kwa mituki mituki mituki M5* | Nakupenda kwa kuja haraka haraka haraka |
| *Ngwéndéá kuká oyu kwa mituki mituki mituki M6* | Nakupenda kwa kuja haraka haraka haraka |

Uradidi ambao unajitokeza katika mishororo hii unaonyesha vile mwanamke alivyo wa kutegemewa katika jamii. Mwanamke amesawiriwa kuwa mwenye bidii kazini. Daktari Mueni anatekeleza kazi yake kwa bidii kwa kuwatibu wagonjwa katika jamii. Pia, kupitia mbinu hii ya takriri, uaminifu wa mwanamke katika jamii unajitokeza. Daktari Mueni anapoitwa na wanajamii kuwahudumia, anatekeleza jukumu hilo kwa uaminifu. Msanii anaweka wazi thamani ya mwanamke katika jamii ya Akamba.

Msanii ametumia mbinu ya takriri kirai katika ujenzi wa utaifa wa Akamba katika wimbo $W_{11}MB_T$ kupitia matumizi ya kirai *kusuvia mbai* (kulinda jamii). Kirai *kusuvia mbai* kimerudiwa kama wito wa msanii kwa viongozi wa jamii yake kukuza utamaduni wa kuwasaidia watu wa taifa la Akamba. Kupitia wimbo huu, msanii anaonyesha vile wanajamii katika jamii ya Akamba huzingatia umoja wao katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii. Umoja wa jamii unadhihirika wakati mwanabiashara Mutua Katuku anapowasaidia msanii na wanajamii wengine ambao walikuwa wamekusanyika mjini Mombasa kwa kuyashughulikia masilahi yao. Vivyo hivyo, msanii anaona kuwa akishafunzwa na kuijua kazi hii ya kuuza chuma kuu kuu atawapa ajira vijana kutoka Ukambani. Kitendo hiki kinakuza uchumi wa jamii yake na hivyo kuchangia ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

Mbinu ya takriri kirai inajitokeza katika wimbo $W_8MB_T$ ambapo msemo *kuvanda itumo* (kupanda mkuki) umeradidiwa. Msemo huu unatoa maana ya kunyakua himaya mpya na

kupata utajiri mpya. Msanii anaona kwamba baada ya kumwoa Mkorea, jamii yake itapanuka kwa vile watakuwa wamemwongeza mwanajamii mpya. Utajiri wake utaongezeka kwa vile ataweza kuwekeza katika nchi za kigeni. Msanii anazungumzia kuhusu fursa ambazo wanajamii kutoka jamii ya Akamba wanapata za kupanua uwezo wao wa kiuchumi kwa kuwekeza katika nchi za kigeni. Kwa njia hii, jamii itakuwa na utajiri mwingi na maisha ya wanajamii wao yataimarika, jambo ambalo litakuza utaifa wao.

Katika wimbo $W_{18}MB_T$ mishororo $M_{11-20,}$ msanii ametumia takriri ya kirai *kusyaa vyu* (kuzaa kabisa) katika beti zake tatu za mwisho. Amefanya hivi ili kuirai jamii ya Akamba wazingatie kuongeza idadi yao ya watu kutokana na tukio la kisiasa ambapo kiongozi wao wa kisiasa Kalonzo Musyoka, ambaye alikuwa anawania kiti cha urais mwaka wa 2007 katika uchaguzi mkuu wa urais nchini Kenya kwa tiketi ya chama cha ODM Kenya alikejeliwa na wapinzani wake kwa vile hakuweza kuleta kura nyingi za kitaifa. Haya yanadokezwa katika ubeti wa kwanza wa wimbo $W_{18}MB_T$ msanii anapotanguliza hivi:

| | |
|---|---|
| *Akamba twiiwe tuina andu M1* | Akamba walisema hatuna watu |
| *Mwiwie muvisi ayiumwa M2* | Mlisikia kijana wetu akitusiwa |
| *Kikavu kya siasa ndaususya M3* | Kikapu cha siasa hatuwezi jaza |
| *Na nyie ngewa woo mwingi M4* | Na nikasikia uchungu sana |

Hili lilimaanisha kwamba jamii ya Akamba ilikuwa na idadi ndogo ya wapiga kura hivyo kuzifanya jamii zingine zenye idadi kubwa ya wapiga kura nchini Kenya kususia kuungana nao katika kuunda muungano wa kisiasa ambao ungewasaidia kushinda kiti cha urais katika uchaguzi huo. Msanii katika mshororo $M_4$ anasema kwamba amegadhabishwa na hali hii ndiposa anachukua hatua ya kuwarai wanajamii wenzake wazae kwa wingi ili jamii zingine ziweze kuwatambua na kuungana nao kisiasa. Oduor, (2022), anazungumzia hali hii anapokuli:

> Kwa hivyo ni karibu hali isiyowezekana kwa makundi madogo sana ya kikabila kama vile Ogiek, El- Molo au Pokomo kushinda uchaguzi wa urais nchini Kenya kwani makundi ya kikabila yenye idadi kubwa kama vile Waluya, Wakalenjin, Wakikuyu na Wajaluo yanaweza kuunda miungano yenye ushindi bila wao (Tafsiri yangu mwenyewe).

Msomi Oduor (2022), anaona kwamba iwapo kabila fulani nchini Kenya lina idadi ndogo ya wapiga kura, basi watatengwa na makabila yenye wapiga kura wengi na ambao wamemteua mwaniaji kiti cha urais kwani azma yao ni kupata uungwaji mkono na kabila au makabila mengine yenye idadi kubwa ya wapiga kura. Kutokana na hali hii, msanii anaamua kupitisha ujumbe huu muhimu kwa wanajamii wenzake kwa kuwataja viongozi mashuhuri wa kisiasa kutoka jamii ya Akamba. Msanii anasema kwamba wamewaambia Wakamba wazae kwa wingi ili kuongeza idadi yao ya wapiga kura katika chaguzi za baadaye. Katika mshororo $M_{9-12}$ anasema:

| | |
|---|---|
| *Muvisi aisye tusyae vyu M9* | Kijana wetu alisema tuzae kabisa |
| *Maanzo aisye tusyae vyu M10* | Maanzo alisema tuzaane kabisa |
| *Muthama aisye tusyae vyu M11* | Muthama alisema tuzaane kabisa |
| *Mutula aisye tusyae vyu M12* | Mutula alisema pia tuzaane kabisa |

Kupitia mbinu ya takriri msanii anawatumia viongozi tajika kutoka jamii ya Akamba ili kuleta wananchi pamoja na kuwatanabaisha kuhusu umuhimu wa kuwa na idadi kubwa ya wapiga kura. Katika wimbo huu msanii amewataja Muvisi, ambalo ni jina la utani la Kalonzo Musyoka, Maanzo ambaye amekuwa mbunge wa eneo bunge la Makueni kwa awamu mbili na kwa sasa ni seneta wa Kaunti ya Makueni, Muthama ambaye amewahi kuwa seneta wa Kaunti ya Machakos na ni kiongozi katika chama cha Wiper ambacho mwanzilishi wake na kinara ni Kalonzo Musyoka na pia Mutula Kilonzo ambaye alikuwa seneta tajika kutoka Kaunti ya Makueni na pia mwanachama wa chama cha Wiper (Hornsby, 2022). Msanii anafanya hivi ili kutilia mkazo umuhimu wa kuwa na umoja wa kijamii iwapo jamii ya Akamba inatarajia kupata ufanisi wa kisiasa. Viongozi hawa wamechaguliwa kimaksudi na msanii kwa vile wanawakilisha kaunti tatu za Ukambani ambamo jamii ya Akamba inapatikana: Machakos, Kitui na Makueni. Msanii anachangia ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba kwa kuwaelekeza wanajamii wenzake kuungana ili kutatua tatizo la kisiasa ambalo limekumba jamii yake. Kupitia wimbo huu, utaifa wa jamii hii unakuzwa katika kutekeleza jambo ambalo linaathiri mustakabali wa jamii ya Akamba.

Suala hili la kuongeza idadi ya wanajamii ya Akamba pia limerejelewa katika wimbo $W_{19}MB_T$. Msanii ametumia mbinu ya takriri katika kuwarai wanajamii wenzake hasa vijana kuoa ili wapate watoto ambao ni wanajamii wapya. Neno *ndutwaane* (oa) limeradidiwa katika wimbo huu katika mishororo ifuatayo:

| | |
|---|---|
| *Katingánya ndutwaane ndutwaane ndutwaane M10* | Kating'anya oa oa oa |
| *Kalulu ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM11* | Kalulu oa oa oa |
| *Kanyari ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM12* | Kanyari oa oa oa |
| *Shughuli ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM13* | Shughuli oa oa oa |
| *Savimbi ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM14* | Savimbi oa oa oa |
| *Mumina ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM15* | Mumina oa oa oa |
| *Kitunusi ndutwaane ndutwaane ndutwaaneM16* | Kitunusi oa oa oa |

Mbinu ya takriri imetumiwa ili kusisitiza ujumbe kuhusu umuhimu wa ndoa kama chanzo cha jamii. Msanii anawarai vijana katika jamii yake kuingia katika asasi ya ndoa kwa vile anaona kwamba ukoo wa jamii yake utaendelezwa kupitia ndoa. Pia, kupitia kwa ndoa, wazungumzaji wapya wa lugha ya Kikamba watapatikana hivyo kuchangia ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

Mtindo mwingine wa takriri ni ule wa takriri neno. Mtindo huu umejitokeza katika wimbo $W_3MB_T$ ambapo maneno *asungu* (wazungu), Makutano na *mikorogo* yameradidiwa. Msanii anarudia rudia neno *mikorogo* kurejelea changamoto ambazo zinakumba utaifa wa jamii ya Akamba. Anazungumzia kuhusu utamaduni mpya ambao umevamia jamii yake na kutishia kuuvunja utaifa wa jamii ya Akamba unaotokana na wao kujivunia rangi ya ngozi yao, lugha yao, eneo lao na utamaduni wao. Katika mshororo $M_7$, msanii anasema *misamu yiitwa mikorogo* (vitu vinaitwa mikorogo) na mshororo $M_{13}$, anaiita *minyamu* (mavitu). Msanii anadunisha vipodozi hivi na kutumia maneno ya kuvidharau ili kuonyesha kwamba ni hatari kwa wanajamii. Hili linadokeza kwamba iwapo utaifa wa jamii utadumu ni sharti wanajamii wakubaliane kudumisha utamaduni wao na kuutupilia mbali ule wa kigeni ambao ni hatari kwao. Neno *asungu* (wazungu) limeradidiwa ili kurejelea wageni wenye utamaduni wa kigeni unaoathiri utaifa wa Akamba. Msanii ameradidi neno makutano ili kuwakilisha sehemu ambapo watu kutoka jamii ya Akamba hukutana na kufanya makubaliano kuhusu namna ya kujenga na kudumisha utaifa wao wa kijamii.

Msanii ametumia mbinu ya takriri aya katika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba kupitia wimbo $W_9MB_T$ anaposema hizi ni vitu, hizi ni zangu, hizi ni zako na hizi ni *fundamentals* katika lugha nne ili kusisitiza hali ya ushirikiano baina ya wanajamii. Kupitia wimbo huu, msanii anaeleza kwamba vitu ambavyo ni muhimu katika jamii havimilikiwi na mtu mmoja. Ni dhahiri kwamba katika jamii ya Akamba kuna ujamaa. Wanajamii ya Akamba

wana umoja wao ambao huwawezesha kuendeleza umiliki wa pamoja na kudhihirisha kwamba katika jamii ya Akamba ukarimu unaenziwa na ubinafsi kukashifiwa.

Katika wimbo $W_{17}MB_T$, kibwagizo cha wimbo huu kimeradidiwa. Maneno *katiba myau*? (katiba gani?) yamekaririwa kama swali balagha linalotarajiwa kuwazindua jamii ya Akamba kuhusu athari za katiba kielelezo ambayo msanii anaona haichangii utaifa wa jamii yake. Shughuli nzima ya kuunda na kupitisha katiba kielelezo inakejeliwa kwa kuonyesha kwamba haitawafaa wananchi katu. Inahofiwa kwamba katiba hii kielelezo imechangia utengano wa jamii ya Akamba katika misingi ya kidini, kiuchumi, kijamii na kisiasa. Wanajamii wenzake wana misimamo tofauti kuhusu katiba hii kwa hivyo anahofia mshikamano wa kijamii utavunjika iwapo itapita. Msanii anatafuta uungwaji mkono kutoka kwa wanajamii wa taifa la Akamba katika kupinga katiba kielelezo ambayo anaona haitakuwa na manufaa kwa taifa la Akamba.

### 4.3.3 Chuku

Chuku ni mbinu ya kisanaa ambayo hukuza mtu, kitu au jambo fulani zaidi ya uwezo wake wa kawaida (Ismail, 2019). Mbuvi (2014), anadokeza kuwa chuku ni mbinu ambayo kwayo waandishi hutilia chumvi kauli au habari zisizo za kweli katika maelezo ili kuyafanya yavutie. Mbinu hii humchochea msomaji na kumfanya afikirie zaidi kuhusu dhana iliyotiliwa chumvi na kuihusisha na hali ya kawaida.

Mbinu ya chuku inajitokeza katika nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria. Wimbo $W_1MB_{Ch}$ ni mfano wa namna msanii anavyotumia mbinu ya chuku katika kuendeleza maudhui ya ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Katika wimbo huu, msanii anasimulia kisa ambapo anatafuta namna ya kumfikia mpenzi wake, Mwende ambaye yuko ughaibuni. Msanii anasema ya kwamba amejaribu kila mbinu ya kusafiri lakini juhudi zake zimegonga mwamba kwani hamudu nauli ya usafiri. Anaishia kukata kauli kwamba atatembea hadi mji wa Munich Ujerumani ili akaungane na mpenzi wake ambaye amekawia kurudi nyumbani. Anasema: *Niuka na maau Germany- Munich switie M9* (Nitakuja Ujerumani kwa miguu mpenzi). Litakuwa jambo lisilowezekana kwa msanii kutembea kwa miguu hadi nchi ya Ujerumani. Kupitia kwa mbinu hii ya chuku, msanii anaweka wazi athari za ukoloni na ukoloni mambo leo ambao ni pamoja na uporaji wa rasilimali za jamii na mataifa ya kimagharibi, kutoweka kwa utambulisho wa kijamii na uchakachuaji wa akili.

Mwende ni mfano wa watu waliosoma ambao wanaishia kwenda kuyatumikia mataifa ya kigeni huku jamii zao zikiendelea kuzongwa na umaskini. Msanii, ambaye ni mpenziwe Mwende ni maskini. Hawezi kumudu nauli ya ndege au meli ili ajiunge na mpenzi wake. Anaona ya kwamba jamii inastahili kufanya kila juhudi ili kuzilinda rasilimali zake ili ziache kuporwa na mataifa ya kigeni. Msanii anawakilisha mataifa mengi ya Kiafrika ambayo yanafanya kila juhudi kurejesha nchini rasilimali zao zilizoporwa na mataifa ya kigeni.

### 4.3.4 Misemo

Misemo ni kifungu cha maneno kinachotumiwa na jamii ya watu wenye lugha kwa namna maalum ili kutoa funzo, maadili na kutahadharisha jamii (Mwangi, 2021). Tuki (2014), wanabainisha misemo kama kauli fupi fupi zinazotumiwa na jamii ili kusisitiza ukweli wa jambo au kutoa msisitizo wa maadili fulani. Nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria zimetumia mbinu hii kwa kiasi kikubwa katika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba. Katika wimbo $W_8MB_{Ms}$, misemo kadhaa inajitokeza:

| | |
|---|---|
| *Kuvanda itumo* M3 | Kupanda mkuki |
| *Nikase ngai, M22* | Lazima nijikaze |
| *Nthukume ki nzau ngume M23* | Nitie bidii kama fahali |

Msemo *kuvanda itumo* (kupanda mkuki) katika wimbo huu una maana ya kubainisha kile kilicho chako na kukimiliki. Ni hali ya jamii ya Akamba ya kutalii anga mpya na kuzinyakua kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika harakati hizi, jamii itahitaji kutumia mbinu anuwai na kutia bidii iwapo inatarajia kufanikiwa. Ndiposa msanii anatumia msemo *níkase ngaí* (kujikaza) na *nthúkúme kí nzaú ngúme* (nitie bidii kama fahali). Misemo hii inaihimiza jamii ya Akamba kutia bidii katika shughuli zote wanazofanya iwapo wanatarajia maendeleo katika eneo lao. Hili linathibitisha kwamba uchumaji wa mali na bidii kazini ni sehemu ya utamaduni wa Akamba na kiungo muhimu cha ujenzi wa utaifa wa Akamba.

Misemo pia imetumiwa katika wimbo $W_{15}MB_{Ms}$ pamoja na anwani ya wimbo huu. Mifano ni kama vile:

| | |
|---|---|
| *Kalonzo ika nesa* | Kalonzo tenda mema |
| *Twambe twikethye* M12 | Kwanza tujisalimu |
| *Withiwe kyeni kwitu M16* | Uwe mwangaza kwetu |

*Ve tumundu twa kilomo M21* Kuna vijitu vya mdomo

*Tilai tulomo* M27 Punguzeni midomo

Msanii anapotumia msemo *Akamba twambe twikethye* (Akamba kwanza tujisalimu) ana maana kuwa jamii ya Akamba ijipongeze kwa kazi nzuri waliyoifanya. Hii ni kutokana na kitendo chao cha kupiga kura kwa amani na kwa umoja wa kijamii ili kuhakikisha kwamba mmoja wao ambaye alikuwa akiwania kiti cha urais amepata kura nyingi. Msanii anasema kuwa kura zote za Ukambani zilimwendea kiongozi wa kisiasa wa jamii ya Akamba, Kalonzo Musyoka. Hili lilibainisha umoja wa kijamii katika kufanya maamuzi ya kisiasa. Anasema:

*Kula syitu sya ukamba sya kivila kiu kyailu kya usumbi twanengie Kalonzo M2*
Kura zetu Ukambani za kiti cha urais tulimpa Kalonzo

Jamii ya Akamba ilijitokeza kwa wingi na kumpigia kiongozi wao wa kisiasa kura. Kutokana na umoja huu, jamii ya Akamba inapata kuwa na makamu wa rais wa kumi katika historia ya siasa za nchi ya Kenya. Msanii anaona kwamba utaifa wao katika kufanya maamuzi ya kisiasa umewaletea ufanisi mkubwa kwa vile anaona kwamba shida ambazo zimeizonga jamii kwa muda zitatatuliwa. Jamii hii imepata nafasi ya kuwa mamlakani kwa mara ya kwanza. Kwa vile kiongozi wao wa kisiasa Kalonzo Musyoka atakuwa katika meza ya kugawa rasilimali, matarajio ya msanii ni kwamba jamii ya Akamba itanufaika. Oduor (2022), anadokeza haya anaposema kuwa kupatikana kwa madaraka ya kisiasa kwa jamii mara nyingi yanahusiana na upatikanaji wa rasilimali kama vile ardhi, ajira za umma na fursa za kibiashara. Anaongeza kuwa ukosefu wa moja mara nyingi huashiria ukosefu wa nyingine. Ni kutokana na mawazo kama haya ambapo viongozi wa kisiasa nchini Kenya hutamka maneno kama vile ‘Ni wakati wetu kula’ pindi wanapopata fursa ya kuziwakilisha jamii zao serikalini. Wanajamii wenzao huwa na matumaini kwamba watazawadiwa kwa kuiunga serikali mkono. Umoja wa jamii husika katika kupiga kura unakuwa wa manufaa makubwa na hivyo kuchangia ujenzi wa utaifa wao.

Msanii anatumia msemo *Withiwe kyeni kwitu* (uwe mwangaza kwetu), anapomshauri Kalonzo kama kiongozi wa kisiasa wa jamii ya Akamba. Anamwona Kalonzo kama kiongozi ambaye ataikomboa jamii yake kutoka kwa changamoto wanazopitia. Changamoto hizi ni pamoja na ukosefu wa maji, ukosefu wa miundo msingi bora na hata kutengwa kisiasa. Msanii anamwambia Kalonzo kuwa anazielewa shida zao kama jamii

hivyo anapochukua wadhifa mpya wa kuwa makamu wa rais,’ akumbuke kutatua changamoto zinazowakumba. Neno *kwitú* lenye maana ya kwetu linawakilisha eneo la kijiografia ambapo utaifa wa Akamba unaendelea na pia sehemu inayomtarajia Kalonzo kusuluhisha matatizo yao. Katika mishororo $M_{14-20}$ anasema:

| | |
|---|---|
| *Nundu nuvikie kúu M14* | Sababu ulifika huko |
| *Yu maundu maitu usisye M15* | Mambo yetu uangalie |
| *Withiwe kyeni kwitu M16* | Uwe mwangaza kwetu |
| *Thina munene ukamba M17* | Shida kubwa Ukambani |
| *Wisi nesa Kalonzo M18* | Unajua vizuri Kalonzo |
| *No malelu na kiw’u M19* | Ni barabara na maji |
| *Ndusiisye, sisya M20* | Uangalie, angalia |

Msanii anaona ya kwamba wajibu wao kama wanajamii kutoka jamii ya Akamba haukomei katika kupiga kura. Wanastahili kuhakikisha kwamba waliyemchagua kama mwakilishi wao katika serikali kuu anatimiza ahadi zake za kuleta miradi ya maendeleo katika eneo lake. Hili litawezekana iwapo wanajamii wataungana na kuzungumza kwa sauti moja na hivyo kujenga utaifa wa jamii yao.

Msemo *ve tumundu twa kilomo* (kuna vijitu vya mdomo) katika mshororo wa $M_{27}$ una maana kuwa katika wadhifa mpya ambao kiongozi huyu wa kisiasa wa jamii ya Akamba amepata, hakutakosa pingamizi kutoka kwa wapinzani wake. Msanii anaona kuwa baadhi ya wapinzani hawa huenda wanatoka katika jamii yake na wengine kwingineko. Msanii anamshauri mwanasiasa huyu kuwa aitumikie jamii yake vilivyo licha ya upinzani kutoka kwa mwanasiasa wa jamii yake na wengine kutoka jamii nyingine. Wapinzani hawa wanashauriwa waache kupiga kelele ili wampe Kalonzo nafasi ya kufanya kazi ndiposa anawashauri *tilai tulomo* yaani punguzeni upinzani. Wakati kuna upinzani katika kikundi chochote ina maana kwamba utaifa wa jamii hiyo umo hatarini hivyo kuathiri maendeleo yao.

Anwani ya wimbo huu, *Kalonzo ika nesa* (Kalonzo tenda makuu) ni msemo. Msanii anamshauri Kalonzo atende mema. Wakati kiongozi anapopata fursa ya uongozi serikalini, jamii yake huwa na matarajio kwamba kiongozi huyu wa kisiasa atahakikisha jamii yake imenufaika kutokana na wadhifa ule. Aghalabu utawasikia wakisema kwa sauti za chini kwamba *twambe twikethye* (kwanza tujisalimie) msemo wenye maana kwamba ‘ni wakati wetu wa kula’. Hii ina maana kuwa jamii nyingi huona kuwa hawapati rasilmali za kutosha

ili kufanya maendeleo katika maeneo yao iwapo hawana uwakilishi mzuri serikalini. Ushauri huu unaelekea kumkumbusha Kalonzo kwamba ana jukumu katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba kwa kuleta miradi mbalimbali kwa hivyo atie bidii kwa kuleta rasilimali kwa wananchi.

Katika wimbo $W_{11}MB_{Ms}$, msanii ametumia msemo *kusuvia mbai* (kuchunga ukoo). Msemo huu una maana ya mtu kujali masilahi ya watu wake au ukoo wake. Msemo huu umeelekezwa kwa wanasiasa kutoka jamii ya Akamba ambao wanaonekana kuwa wameshindwa na wajibu wa kuangalia masilahi ya jamii yao. Msanii anatumia mhusika ambaye katu hajulikani na wanajamii na kummiminia sifa namna alivyowasaidia wakiwa mjini Mombasa. Katika simulizi hii, msanii anaonyesha kuwa pana pengo la uongozi wa kisiasa katika jamii ya Akamba na pengo hili linahitaji kujazwa. Anamteua mhusika ambaye hadi hapo wanajamii hawamjui, hawajamwona na si kiongozi wa kisiasa na kusema kuwa ana uwezo wa kuiongoza jamii ya Akamba. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Mbaitu mukamwona, M25* | Watu wangu mkimuona |
| *Mundu mutheke vyu, M26* | Mtu mwembamba sana |
| *Lakini akili, M27* | Lakini akili |
| *Ya kumantha mbesa, M28* | Ya kutafuta pesa |
| *Na kutongoesya mbai, M29* | Na kuongoza jamii |
| *Mutua Katuku ii, M30* | Mutua katuku |
| *Mundu utemathinaa M31* | Mtu asiye na shida |

Kupitia msemo *kusuvia mbai*, msanii anawatahadharisha wanasiasa kutoka jamii ya Akamba kwamba jamii imo katika juhudi za kutafuta wawakilishi wao ambao wataangalia masilahi ya jamii kwa jumla wala si masilahi yao kama viongozi. Sifa za kiongozi bora ambaye jamii ya Akamba inazingatia ni pamoja na kiongozi kuwa na uwezo wa kuiongoza jamii, awe na uwezo wa kujenga na kudumisha utaifa wa jamii hii pamoja na kuwa na ujanja wa kuhakikisha rasilimali zilizotengwa kisiasa kwa jamii ya Akamba zimewafikia na kuchangia maendeleo katika eneo la Ukambani. Msanii anawaonya viongozi wasiowajibika kuwa hawataendelea kupata dhiki chini ya viongozi ambao hawajali masilahi yao.

Msemo *mukamba kivindyo* (Mkamba halisi) katika wimbo $W_3MB_{Ms}$ unatumiwa kumtambulisha mwanajamii halisi wa taifa la Akamba. Msanii ametumia msemo huu kubainisha utambulisho halisi wa mwanamke mwenye asili ya Kikamba. Anafanya hivi

kwa kulinganisha utambulisho wa msichana anayeitwa Mwikali Kaumbulu anayejulikana kijijini kwao na Mwikali, ambaye msanii anakutana naye katika mji wa Makutano, ambaye amebadili sura na kukaa kama mzungu. Mkamba halisi ni yule ambaye anaionea fahari lugha yake, ngozi yake, utamaduni wake na hata historia yake. Ni bayana kwamba mhusika Mwikali ambaye amebadili ngozi yake anaukana utambulisho wake wa Kikamba wa rangi kwa kujipaka *mikorogo*. Mwikali ameuasi utamaduni wake na kukubali kukengeushwa na mienendo ya kimagharibi. Msanii anaikashifu tabia hii ambayo anaona inatishia utaifa wa jamii ya Akamba na kuwaomba wanajamii kuuonea fahari utamaduni wao, lugha yao, ngozi yao na jiografia yao ambavyo ndivyo vipengele vinavyojenga utaifa wao.

### 4.3.5 Methali

Mieder (2016) anaona kuwa methali huwa sentensi fupi inayojulikana na yenye maarifa, ukweli, tabia, na maoni ya kiutamaduni yanayojitokeza kistiari ambayo inarithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mujibu wa TUKI (2014), methali ni usemi wa kisanii wa kimapokezi unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Wandera (2022), anasema kuwa methali ni mojawapo ya bunilizi za kisimulizi ambazo hutungwa na wanajamii kutokana na mazingira yao. Kila jamii ulimwenguni ina methali zake zilizoundwa kutokana na mazingira yao. Katika mazungumzo ya kawaida baina ya wanajamii, methali hutumiwa kuadilisha, kushauri, kuonya na wakati mwingine kukashifu tabia isiyokubalika na jamii husika.

Mbinu hii imetumika katika nyimbo pendwa ambazo utafiti huu ulichanganua. Msanii ametumia methali ambazo zinapitisha ujumbe tofauti tofauti kwa wananchi. Katika wimbo $W_{15}MB_{Mt}$ kuna matumizi ya methali ambazo zinaendeleza ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Msanii katika mishororo $M_{1\text{-}3}$, anaanzia wimbo wake kwa maneno *Wesa kwíw'a mwa kaúndú, keíkalanga kaiwetwa ní dalili sya maúndú* (ukisikia jambo likisemwa semwa ujue ni dalili ya mambo) ambayo yanaweza kutafsiriwa na kuwa lisemwalo lipo na kama halipo liko njiani laja. Anatumia methali hii ili kuijulisha jamii yake kuwa kulikuwa na habari njema kwani mmoja wao alikuwa amepata wadhifa mkuu serikalini. Ilikuwa njia ya kuishukuru jamii ya Akamba kwa vile walikuwa wamempigia mwanasiasa Kalonzo Musyoka kura nyingi za urais. Kiongozi huyu wa kisiasa ambaye anatoka jamii ya Akamba

alikuwa akiwania kiti cha urais ingawa hakupata kura za kutosha. Baada ya sintofahamu kutokea baina ya aliyekuwa rais wakati huo hayati Mwai Kibaki na kiongozi wa upinzani Raila Odinga ambao walikuwa wawaniaji wenza wa wadhifa wa urais, hali ya vurugu ilishuhudiwa nchini. Hali hii ilizaa vita vikali vya kikabila ambavyo vilitishia amani na umoja wa wanajamii. Wakati huu ndipo hayati rais Mwai Kibaki alipomteua mwanasiasa kinara wa jamii ya Akamba Kalonzo Musyoka kuwa makamu wake wa rais. Uteuzi huu uliipa nchi afueni kwani sasa rais alikuwa akifanya kazi na mmoja wa wapinzani wake.

Msanii anatumia methali 'Batili ya Musa ni Hussein' kurejelea hali hii ambapo ingawa Kalonzo Musyoka hakuweza kupata kura za kutosha ili kuwa rais wa Jamhuri ya Kenya, alifanikiwa kuteuliwa katika wadhifa ambao ulikuwa karibu na huo; makamu wa rais. Methali hii ina maana kuwa unapokosa kile ulichokuwa unalelenga kukipata na kupata kingine ambacho kina manufaa karibu sawa, basi inakuwa jambo la manufaa kwako kwa vile hujapoteza. Ingawa jamii ya Akamba ilikuwa imempigia kura kwa wingi Kalonzo Musyoka wakiwa na matumaini kwamba angenyakua kiti cha urais, hawakufanikiwa kwa sababu ya uchache wa kura zao. Badala yake, alipata kiti cha makamu wa rais ambacho msanii anaona kwamba hata hivyo kitakuwa na manufaa kwa wanajamii ya Akamba. Wanashukuru kwa kupata wadhifa huo. Anawapongeza wanajamii wenzake kwa kuhakikisha kuwa walimpa Kalonzo kura zote za ukambani kupitia umoja wao wa kisiasa. Msanii anaonyesha utaifa wa jamii ya Akamba kupitia methali hii kwa kuwa wanajamii wanakubaliana kuwa wadhifa walioupata wa makamu wa rais wa nchi ya Kenya utawafaa pia.

Katika wimbo $W_{10}MB_{Mt}$, msanii anamwambia mpenziwe kuwa *ndúú ti ndúúka* (urafiki si wenda wazimu) kusisitiza umuhimu wa kudumisha heshima, urafiki na ushirikiano baina ya wanajamii. Ushirikiano ni kiungo muhimu cha mshikamano baina ya wanajamii wanaojivunia utaifa mmoja. Mshikamano na heshima baina ya wanajamii ni muhimu katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

### 4.3.6 Jazanda

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), jazanda ni mafumbo ambamo ndanimwe maana ya kitu imefichamana. Ni sawa na sitiara yaani kilichositiriwa. Sitiara ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea aina fulani ya sitiari iliyopanuliwa. Hutumiwa kuelezea hali

ambapo wimbo fulani unaweza kufasiriwa kwa namna tofauti. Kazi fulani ya sanaa huwa na maana nyingine zaidi ya ile ya kijuu juu. Hulinganishwa na watu au matukio yaliyo nje ya ulimwengu wake (Wamitila, 2008).

Mbinu ya jazanda inajitokeza katika nyimbo za msanii Ken wa Maria. Katika wimbo $W_2MB_{Jz,}$ msanii anatumia lugha kuelezea kuhusu uana wa msichana ambaye amekutana naye. Anasema:

*Návíká Kibwezi níèndà úkwíà nyíè ní nōníé ngèthé M1*
*Nákúlyà Múng'éng'è àmbííè yítàwā* _Ngémì_ *M2*

Nilipofika Kibwezi niliona msichana mrembo
Nilipouliza Mung'eng'e aliniambia msichana anaitwa Ngemi

Jina *Ngemi* katika mshororo $M_2$ ni la kijazanda lenye maana ya kumetameta. Kinachometameta hupendeza macho na huwa ni kitu cha thamani. Msanii amechagua jina hili kuwakilisha uana au jinsia ya kike ambayo kwake anaona kuwa ni tunu. Mwanamke katika muktadha huu amesawiriwa kama aliye na nafasi muhimu katika jamii kwani ni nguzo ya jamii. Ana thamani kubwa kwa wanajamii hivyo basi, anahitaji kutunzwa. Mwanamke anakuwa chanzo cha kuendeleza kizazi kwani yeye ndiye hupata watoto, kuwalea na kuwatunza. Mwanamke anapewa jukumu la uongozi katika siasa za jamii ya Akamba. Katika mshororo $M_{15-16}$, msanii anasema kwamba wanajamii ya Akamba wameamua kumchagua mwanamke kama kiongozi wao katika uwakilishi wodi wa kaunti yao. Anasema kuwa watampa fursa ya kuwa mwakilishi wadi katika eneo la Kisaayani. Haya ni kwa mujibu wa mishororo ifuatayo:

| | |
|---|---|
| *Na niwe tuusakua kansala kuuya Kisaayani M15* | Ni yeye tutachagua kama Kansala kule eneo la Kisaayani |
| *Ni ngethe mbailu M16* | Ni mwanamke ambaye anafaa. |

Katika muktadha huu, nafasi ya mwanamke inabainishwa kama ya kuwaunganisha wanajamii na pia mwenye uwezo wa kuiongoza jamii yake kisiasa na kijamii licha ya urembo wake. Msanii hamwoni mwanamke kama kiumbe mwenye urembo wa sura pekee bali ana akili za kuiongoza jamii yake. Kupitia kwa mwanamke, utaifa wa jamii ya Akamba unajengwa kupitia makubaliano ya wanajamii ya kumchagua mwanamke kama mwakilishi wodi katika eneo moja la Ukambani.

Jina *Mwende* katika wimbo $W_1MB_{Jz}$ limetumika kijazanda kuashiria athari za ukoloni katika nchi. Jina hili lina maana ya mwanajamii ambaye anapendwa. Katika jamii ya Akamba, jina hili hupewa mtoto wa jinsia ya kike. Katika muktadha wa wimbo huu *Mwende* kuwa ughaibuni anawakilisha rasilimali ambazo zimetolewa nchini na ambazo haziwafaidi wananchi ambao wanazihitaji. Bara la Afrika limepoteza rasilimali nyingi kupitia ukoloni na ukoloni mamboleo. *Mwende* ni jazanda ya uchakachuaji wa akili kutoka bara la Afrika. Uchakachuaji wa akili ni mchakato wa watu wenye ujuzi au wenye vipaji kuondoka nchi yao ya asili na kwenda kufanya kazi au kuishi katika nchi nyingine. Hili huwa kutokana na fursa bora za kazi, mishahara mikubwa na mazingira bora ya maisha ambayo yanapatikana ughaibuni na kukosekana katika nchi nyingi barani Afrika. Msanii analalamikia masaibu anayopitia katika azma yake ya kwenda ughaibuni hivyo, kuishia kukata kauli ya kutembea hadi huko. Anasema kuwa ameamua kutembea hadi Ujerumani ili kumrejesha mpenzi wake. Rasilimali zilizoibiwa zinawakilishwa na fumbo la mwanamke kwa jina *Mwende*, mwanamke anayependwa. Mwanamke ana jukumu kubwa katika jamii; ni kitovu cha uhai, ni nguzo ya familia, mlezi, mwalimu na mengineyo. Mwanamke anapoondoka katika jamii basi jamii husika hupata shida. Kupitia kwa jazanda ya *Mwende,* tunapata uelewa wa namna maisha ya Waafrika yalivyosambaratishwa na ukoloni kupitia uporaji wa rasilimali muhimu za jamii. Haya ni kupitia usimulizi wa wimbo huu wa mapenzi ambapo mpenzi wa msimulizi amesafiri hadi nga'mbo na msimulizi hana namna ya kumfikia.

Wimbo $W_{10}MB_{Jz}$ ni jazanda. Msanii anasema:

| | |
|---|---|
| *Ndánú líkā ngālínì ōíno yã mútōngōî* | Ndanu ingia gari ya kiongozi |
| *Wīāmbã ùvōndéthwã rãhã īwē ní mūtōngōí* | Utaonyeshwa raha ni kiongozi |
| *Mbēsã îtwìngwã shîdã îwê kwã mútõngõì* | Pesa sio shida kwa kiongozi |
| *Kãrībū kwã mūtõngõî tyū* | Karibu kwa kiongozi huyu hapa. |

Katika wimbo huu, msimulizi ambaye anajitambulisha kwa jina Kiongozi anambembeleza msichana anayeitwa Ndanu aingie ndani ya gari lake. Anamhakikishia kuwa akishaingia mle atapata faida nyingi. Atapata maisha mazuri ya raha, hatapata shida zozote na pia atapata pesa za kutosha za kukidhi mahitaji yake. Ni bayana kwamba msimulizi anamkaribisha Ndanu katika gari lake kwa moyo mkunjufu. Katika wimbo huu, mali ya kiongozi inawakilisha rasilimali za jamii ya Akamba. Hizi ni pamoja na ardhi au

mashamba, lugha, siasa, utamaduni wa jamii pamoja na vibainishi vingine vya utambulisho wa kijamii. Ndanu ni metonimu ya kitaifa ya utambulisho wa jamii ya Akamba. Ni kiwakilishi cha jamii nzima ya Akamba.

Neno *Mutongoi* (kiongozi) limetumiwa kama jazanda ya viongozi wa kijamii. Gari nalo ni jazanda ya mbinu za uongozi wa kisiasa wa jamii ya Akamba. Katika muktadha huu, viongozi wa kijamii wanawaelekeza wanajamii kuungana pamoja kwa kufanya kazi pamoja ili waweze kufikia ufanisi wa kijamii. Viongozi wanawaalika wananchi kuingia katika mipangilio waliyoweka kwani wanaona kuwa maendeleo ya kijamii yatapatikana iwapo tu wananchi wote watakubali kusikiza maelekezo ya viongozi wao (kuingia katika gari lao), kukubali kufanya kazi pamoja (kuwa katika gari moja) ili nao viongozi waweze kuwaletea maendeleo ya kijamii (kupondeshwa raha). Ili kujenga utaifa wa jamii ya Akamba, msanii anasisitiza kuwepo kwa umoja na mshikamano wa kijamii iwapo jamii ya Akamba inapania kupata ufanisi wowote.

Wimbo $W_6MB_{Jz}$ ni jazanda ya kisiasa. Wanyama waliotumiwa katika wimbo huu wanawakilisha utaifa wa jamii kupitia utambulisho wa uongozi wa kisiasa. Kupitia kwa motifu ya safari, msanii anasawiri suala la siasa ambalo analifananisha na safari ndefu. Ni safari ambayo wasafiri wake hukumbwa na changamoto nyingi. Katika wimbo huu, jina ndovu limetumika kama jazanda ya viongozi katika jamii ya Akamba. Katika wimbo huu Ndovu anachukua jukumu la kumwongoza Sungura katika safari ya kuvuka mto. Yeye anatoa mwongozo na tahadhari kwa Sungura kuhusu kina cha mto ambao wanataka kuuvuka. Isitoshe, wanapokabiliwa na tatizo la kina kirefu cha mto, Ndovu anatoa suluhu kwa tatizo hili kwa kumwambia Sungura ampande mgongoni ili amvushe mto wenye kina kirefu. Kiongozi wa kisiasa wa jamii ya Akamba Kalonzo Musyoka analinganishwa na mnyama ndovu ambaye ana nguvu na hekima ya kuiongoza jamii. Kutokana na matini hii, kuna dokezo kwamba kiongozi wa kijamii anastahili kuwa na nguvu, uwezo na anayeweza kuyakimu mahitaji ya jamii yake. Kiongozi wa kijamii ndiye hutoa mwongozo wa mwelekeo wa kisiasa ambao jamii yake huchukua. Kwa upande mwingine, mhusika Sungura ni jazanda ya viongozi chipukizi wa kisiasa. Msanii amemsawiri Sungura kama mnyama dhaifu asiye na uwezo wa kuiendesha jamii, mwepesi wa kuomba msaada kutoka kwa viongozi mashuhuri wa kijamii na asiye na shukrani hata baada ya kupokea

msaadakutoka kwa viongozi wenye nguvu katika jamii. Viongozi hawa chipukizi wanahitaji mafundisho na uelekezi wa viongozi wakongwe (Ndovu) na wanahitaji kusaidiwa mara nyingi. Jamii ya Akamba inahitaji kiongozi mkuu mmoja wa kisiasa ambaye atachukua jukumu la kuwaelekeza na kuwafundisha wanasiasa chipukizi namna ya kuiongoza jamii iwapo jamii itapiga hatua za kimaendeleo. Katika wimbo huu, Ndovu anamshauri Sungura kwamba mto walioufikia una kina kirefu hivyo basi Sungura asithubutu kuuvuka kama Ndovu kwani angesombwa na maji. Ndovu ndiye anayetoa ushauri kwa Sungura. Haya yanapatikana katika mshororo $M_{1-2}$:

| | |
|---|---|
| *Kavaluku keiwe ni Nzou uyu ni usi muliku* M1 | Sungura aliambiwa na ndovu huu mto una kina kirefu |
| *Ndukatate kuinga ta Nzou M2* | Usijaribu kuvuka kama ndovu |
| *Ndukatwawe ni kiw'u M3* | Usisombwe na maji |

Ndovu ni mfano wa viongozi wa kisiasa ambao wamekomaa katika siasa. Wamo safarini kisiasa ambamo inahitaji kusafiri masafa marefu mahali kwingi. Katika safari hii, wanakumbana na changamoto nyingi. Mito yenye kina kirefu ni jazanda ya changamoto ambazo wanakumbana nazo. Kwa vile Sungura hana uwezo, basi anahitaji ushauri na msaada wa kuvuka mto. Sungura anatoa pendekezo kwa Ndovu kwamba apande juu ya mgongo wa Ndovu ili avushwe mto. Ndovu anampatia onyo kwamba iwapo angetaka kurudi ng'ambo waliyotoka, basi itabidi Sungura atafute mbinu zake. Jazanda hii inasawiri hali ambapo viongozi chipukizi wa kisiasa hupata ushauri wa viongozi wakuu wa kisiasa katika jamii na wakati mwingi kuwaomba usaidizi wao kuhusiana na masuala ya kisiasa. Wakati mwingine viongozi hawa chipukizi hawazingatii ushauri wanaopata. Suala hili huleta mgawanyiko katika jamii na kusababisha jamii kurudi nyuma. Hali hii inaweza kuepukwa iwapo wanajamii watakubaliana kuendesha shughuli zao za kijamii pamoja na kujenga utaifa wao wa kijamii.

Kuna pendekezo kuhusu namna ya kutatua masuala ya kisiasa miongoni mwa jamii ya Akamba: kuwepo kwa chama kimoja cha kisiasa ambacho kitawabeba wanajamii wote. Ndovu anambeba Sungura na wanaanza safari wakiwa pamoja kwenye njia moja wakielekea upande mmoja. Hivi ndivyo siasa za kijamii zinastahili kuwa wala si kuwa na vyama vingi vya kisiasa katika jamii moja. Iwapo wanajamii wote watakuwa katika chama kimoja cha kisiasa, itakuwa rahisi kutandarukia mahitaji yao kwani watakuwa

wanazungumza kwa sauti moja. Pendekezo ni ujenzi wa utaifa dhabiti wa kijamii ambao utaiwezesha jamii ya Akamba kutatua changamoto zinazowakumba.

Mto katika wimbo $W_6MB_{Jz}$ ni jazanda ya changamoto za kisiasa ambazo huikumba jamii katika safari yao ya kisiasa. Baada ya Sungura kuvushwa mto salama, anamsimanga Ndovu na kumwambia kuwa hakuna jambo kubwa amefanya. Changamoto hizi ni pamoja na wanasiasa chipukizi kutofuata maelekezo ya viongozi wakuu wa kisiasa, usaliti wa kisiasa, tamaa ya viongozi wa kisiasa kiasi cha kuisaliti jamii ya Akamba kwa jumla, viongozi kuyajali masilahi yao ya kibinafsi na hata uundaji wa vyama pinzani vya kisiasa vya kijamii. Hizi ni baadhi ya changamoto ambazo zinakumba utaifa wa jamii ya Akamba. Wananchi wanashauriwa kuwa ni vyema wadumishe umoja wao kama jamii iwapo wanatarajia kupata maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Anwani ya wimbo $W_3MB_{Jz}$ ni jazanda. Neno *mikorogo* limetumiwa kijazanda katika wimbo huu kubainisha namna utambulisho wa mwanamke unavyokinzana katika jamii ya Akamba. Mwanzo, mwanamke anasawiriwa kama ambaye ametumia vipodozi (mikorogo) hadi akapauka ngozi na kuwa nyeupe kama ya mtu mweupe. Msanii anashangaa iwapo kuna wazungu katika mji wa Makutano ambapo ameenda kupiga densi pamoja na mwanabendi mwenzake, Mbasu. Baada ya kufanya uchunguzi wake, anaarifiwa kuwa pale Makutano hakuna Wazungu. Wazungu ambao anawaona ni wasichana wenye asili ya Kikamba ambao wamejipodoa hadi ngozi zao zikabadilika na kuwa kama za wazungu. Inabainika kuwa msichana aliyegeuza rangi yake ya asili kwa vipodozi anaitwa Mwikali wa Kaumbulu na kwamba ni *Mukamba kivindyo* (Mkamba halisi). Wakati wanawake wanapotumia kemikali ili kuzibadilisha ngozi zao na kuzifanya ziwe kama za watu weupe, ni bayana kwamba waja hawa wanajaribu kuubadilisha utambulisho wao na kuchukua wa watu wengine.

Kwa upande mmoja, mwanamke halisi wa Kikamba anabainishwa. Huyu ni yule ambaye anazingatia mila na desturi za jamii ya Akamba, hajaathiriwa na usasa ulioletwa na mataifa ya magharibi na ambaye anaionea fahari jamii yake, asili yake, lugha yake na hata utamaduni wake. Kwa upande mwingine, kuna huyu mwanamke ambaye amejipodoa na kuchukua utambulisho wa mzungu. Anafanya hivi ili kuifanya ngozi yake kuwa nyeupe. *Mikorogo* au vipodozi anavyojipodoa ni kemikali mbaya ambazo zina uwezo wa kuathiri

ngozi yake. Huwezi ukamtambua haraka kupitia ngozi yake kwa hivyo ni lazima umchunguze kwa makini ndipo uweze kupata utambulisho wake. Baada ya uchunguzi wa makini asili yake inajulikana na inabainika kwamba huyu ni msichana Mkamba kwa jina Mwikali Kaumbulu. Majina aliyopewa mhusika huyu ni ya asili ya Kikamba na jina la anakotoka pia ni la Kikamba. Hili linajaribu kuonyesha namna ukengeushi unaotokana na utandawazi ulivyouathiri utaifa wa jamii ya Akamba kwa kiasi kikubwa. Wimbo huu ni kama unajaribu kujibu swali iwapo mwanamke ambaye ametumia mikorogo bado atasalia kuwa na utambulisho wa Kikamba. Huyu ni mwanamke ambaye ameasi mila, desturi na mienendo ya jamii ya Akamba na kufuata mienendo ya mataifa ya magharibi.

Katika mshororo $M_7$, Jamii ya Akamba inabuni istilahi ngeni ya *mikorogo* katika lugha ya Kikamba. Wanajamii wanajaribu kubainisha mikorogo ni nini katika mwonoulimwengu wa jamii ya Akamba. Dhana ya *mikorogo* ni mambo yote ambayo hayaoani na utamaduni wa jamii ya Akamba. *Mikorogo* au mchanganyiko ni istilahi ambayo inamaanisha bila uwazi; isiyoeleweka kwa uwazi, mambo ambayo yanabadili sura ya utaifa wa Akamba kwa kuingiza utamaduni wa kigeni. Wimbo huu unazungumzia tisho ambalo lipo katika utambulisho wa mwanamke Mkamba na jamii kwa jumla. Inaonekana kwamba jamii ya Akamba iko katika tishio la kupoteza utambulisho wake wa lugha, historia, dini na utamaduni na kupata utambulisho mpya wa kijinsia ambao umekuja kuvuruga mpangilio wa kifamilia. Mifano mizuri ni kama vile ushoga, usagaji na ubadilishaji wa jinsia. Hizi ni dhana ngeni kwa msanii na jamii yake ndiposa wamebuni istilahi mpya *mikorogo*. Utambulisho huu mpya wa kijinsia umeletwa na jamii za kimagharibi na jamii inaupinga. Masuala ya mikorogo yanaathiri ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba kwa njia hasi.

Mbinu ya jazanda inajitokeza pia katika wimbo $W_8MB_{Jz}$. Wimbo huu unazungumzia kuhusu mabadiliko ambayo yanaikumba jamii ya Akamba. Jamii hii imo katika harakati za kupanua mipaka yake. Wanataka kuongezea maeneo mengine ambayo awali hayakuwa yao. Katika ulimwengu wa sasa wa utandawazi, jamii ya Akamba haijaachwa nyuma. Inajaribu kujiunga na jamii zingine ili kuleta mpanuko wa kijamii. Katika mishororo $M_{1-4}$, utangamano wa jamii tatu unajitokeza: Wamaasai, Wakorea na Wakamba. Baada ya jamii hizi tatu kutagusana, kutakuwa na kupanuka kwa jamii ya Akamba kupitia ndoa mseto. Katika mshororo $M_3$ hatua ya kwanza ya kupanuka ni *Kúvanda ítumo* (kupanda mkuki).

*Kúvanda ítumo* ni jazanda ya jamii kutangaza kwamba walipo ni eneo lao, yaani kunyakua maeneo mapya. Uhusiano wa msanii na Mkorea utailetea jamii yake manufaa mengi. Maingiliano ya kijamii huweza kusababisha kupanuka katika sekta mbalimbali kama vile kielimu, kiuchumi, kiteknoloja, kisiasa na kijamii. Kiuchumi, jamii ya Akamba itaweza kushiriki biashara na nchi za nje hivyo kuleta maendeleo katika eneo la Ukambani.

Katika wimbo $W_{12}MB_{Jz,}$ mhusika Daktari Mueni ametumiwa kijazanda. Daktari Mueni anawakilisha ufanisi wa mwanamke katika jamii ya Akamba. Daktari Mueni ni msomi, ni mlezi bora na anajali maslahi ya wanajamii. Anapoitwa wakati wa dhiki yeye huja haraka na huwa hakawii. Mwanamke wa Mkamba amepewa utambulisho wake kama vile kuwa msomi, mlezi bora na mwenye utu. Jazanda hii ya mwanamke aliyepevuka na kuendelea pia inajitokeza katika nyimbo nyingine za Ken wa Maria kama vile $W_4MB_{Jz}$, $W_2MB_{Jz}$ *na Mwende* katika $W_1MB_{Jz}$. Uwezo na nguvu alizopewa mwanamke unampa nafasi ya kuchangia ujenzi utaifa wa jamii ya Akamba.

### 4.3.7 Aforisimu

Aforisimu ni kauli fupi yenye busara au ukweli wa kimsingi ambao mara nyingi hutumika kama mwongozo au ushauri mfupi. Aforisimu ni taarifa fupi ambazo zinaleta ukweli au uchunguzi wa kimsingi kuhusu maisha, mara nyingi kwa njia inayokumbukwa na fupi. Waandishi hutumia aforisimu kuwasilisha mawazo au uchunguzi wenye ugumu kwa njia ya kifupi na yenye athari. Mtindo huu wa uandishi unajumuisha kuunda taarifa fupi, zenye mvuto, zinazotoa hekima, ufahamu au mawazo juu ya mada fulani.

Mbinu ya aforisimu imetumika katika wimbo $W_9MB_{Af}$ ambapo inatoa dhana ya utaifa wa jamii. Lugha ya kimaelezo inatumiwa katika kubainisha himaya au mipaka ya jamii ya Akamba. Wimbo huu unabainisha misingi ya jamii ya Akamba ambao ni familia iliyoundwa na mume na mke. Hawa ndio waanzilishi wa jamii. Wimbo huu unasawiri usawa ulioko baina ya mume na mke katika kitengo cha familia. Wote huwa na usemi sawa kuhusu mali ya jamii husika. Vyote walivyo navyo ni vyao wote wawili. Hii inajenga dhana ya utaifa katika jamii. Msanii katika mishororo $M_{5-12}$ anasema:

| | |
|---|---|
| *Ithi ni syindu* | Hizi ni vitu |
| *Ithi ni syakwa* | Hizi ni zangu |
| *Ithi ni syaku* | Hizi ni zako |
| *Ithi ni fundamentals* | Hizi ni muhimu |

Mistari hii inaashiria hali ya mshikamano wa kijamii inayodumishwa na wanajamii ya Akamba na ambao ni utambulisho wao. Hali hii inaweza kuelezewa kwa methali *mundu ni andu*, yaani mtu ni watu na kwamba kuwepo kwa mmoja kunategemea kuwepo kwa mtu mwingine. Utaifa wa jamii ya Akamba unadhihirika kupitia ushirikiano na mshikamano wa kijamii. Mishororo hii inaashiria mazungumzo baina ya watu wawili kwa mfano, mume na mke ambao wako katika muktadha wa familia ambao kwa kiwango kikubwa wanawakilisha jamii pana ya Akamba. Mazungumzo haya yanasawiri hali ya usawa wa kijinsia ambao upo katika jamii na kwamba vilivyomo katika jamii hii ni vya watu wote; waume kwa wake. Vitu kama vile ardhi, utambulisho, lugha, historia yao na vinginevyo ni vya kila mtu na kwa manufaa yao wote. Maneno haya yanawakilisha umuhimu wa usawa katika kugawa rasilimali za jamii. Kwa hivyo kauli 'hizi ni zangu' na 'hizi ni zako', inaweza kueleweka kama nembo za utaifa wa jamii ya Akamba wakati wanaume na wanawake wanapata fursa sawa na hivyo kuchangia katika ujenzi wa utaifa wa jamii yao. Utaifa wa jamii pia unajitokeza kupitia elementi kama vile jinsia, lugha na rasilimali ambazo zipo kwa wanajamii wote kwani hivi ndivyo vitu muhimu (fundamentals) kwa wanajamii wa jamii ya Akamba.

Msemo *kúsúvía mbaí* katika wimbo $W_{11}MB_{Af}$, umetumika kiaforisimu. Msemo huu ni wa kuhimiza viongozi kutunza jamii yao ya Akamba kwa kushughulikia mahitaji pamoja na changamoto zinazowakabili. Neno *mbai* lina maana mbili: kwanza ukoo katika jamii ya Akamba na pili, linatambulisha taifa la Akamba. Mwikali (2021), anasema kuwa *mbai* ndicho kitengo cha juu kidogo baada ya familia miongoni mwa jamii ya Akamba. Kwa mujibu wa msomi huyu, *mbai* ni kikundi cha watu ambao washirika wake wanahusiana na kuunganishwa kwa kuwa na asili moja. Ukoo wa mtu au mbai huwa ni cheti cha utambulisho wa Mkamba kwa Wakamba wenzake wanapokutana. Watu wa ukoo mmoja huamini kwamba wana kitovu kimoja kwa hivyo ni wa familia moja. Majukumu ya *mbai* yamebainishwa wazi katika jamii ya Akamba. *Mbai* huweza kumsaidia mwanajamii wakati wa dhiki. Msomi huyu anabainisha baadhi ya majukumu ya mbai kama vile kuwasaidia watoto yatima katika kuendesha maisha yao ya kila siku, kumwauni mwanajamii ambaye amekumbwa na msiba pamoja na kuwasaidia wale ambao hujipata katika shida za kifedha kama vile deni. Wakati kama huu wa shida, msomi huyu anasema kwamba mbai huja

pamoja na kila mtu hutoa mchango wake ili kumsaidia mwenzao. Jambo hili huchangia ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

Katika wimbo $W_{11}MB_{Af}$, mhusika Mutua Katuku anasifiwa kwa kuchuka hatua ya kuwatunza watu wa jamii ya Akamba mjini Mombasa wakati wanapojipata katika matatizo ya kifedha. Wanajamii wa Akamba wanastahili kudumisha umoja wao kupitia taasisi hii ya mbai kwani kupitia kwake wanajamii watadumisha umoja wao na pia kuhakikisha shida za kila mwanajamii zimeshughulikiwa na wanajamii wenzake. Mshororo $M_1$ unatanguliza kwa maneno *súvía mbaí mani* ili kuhimiza viongozi wa Ukambani kuwatunza wanajamii wenzao ili kuendeleza utaifa wa jamii ya Akamba.

### 4.3.8 Taswira

Taswira ni matumizi ya lugha kwa namna inayojenga picha akilini mwa msomaji kuhusu jambo au hali fulani (Ismail, 2019). Ni vielelezo vya kufikirika vinavyoundika akilini kutokana na masimulizi au maelezo fulani katika tungo. Taswira huwa na jukumu la kutupa picha kamili ya yanayosimuliwa katika mawazo yetu. Picha hizi husimulia na kudokeza tukio fulani na hali ya mhusika au kisa fulani. Ni picha ambayo humjia mtu akilini anaposoma, kutazama au kusikiliza kazi ya kifasihi. Taswira huweza kufumbata maana fiche au ile ya kijazanda. Huweza pia kuundwa kwa tamathali za usemi kama vile sitiari, tashbihi, tashhisi, majazi na chuku. Wamitila (2008) anakuli kwamba taswira ni neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo au za ki-ishara. ni ile hali ya kurejelea hali au dhana fulani kwa kutumia picha katika kazi za kifasihi ambayo hutokana na matumizi ya lugha au maelezo ya masimulizi. Wandera (2022), anadokeza kuwa taswira ni mbinu ya lugha ambayo hutumia lugha ya picha ya kitu au mahali kwa kutumia ishara ambazo zinaweza kuwa za kihisia, za kimawazo au zile zinazoonekana. Lengo kuu la matumizi ya taswira ni kumfanya msomaji ajenge picha akilini mwake ili aweze kuona jambo au kitu kinavyoonekana na pia kutoa msisitizo.

Taswira ya mwanamume inajitokeza katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria. Taswira hii imetumiwa ili kusisitiza suala la uongozi, siasa na pia kubainisha matakwa ya jamii ya Akamba. Hali ya siasa za jamii ya Akamba inawekwa wazi kwa kuonyesha kuwa uongozi wa kisiasa umefeli katika wadhifa wake. inaonekana viongozi wa kiume wa kisiasa

wamewasaliti wanajamii kwa vile hawajali masilahi yao. Usaliti huu unatokana na kutotimizwa kwa ahadi za kisiasa ambazo viongozi hawa walitoa kwa wapiga kura wakati wa kutafuta kupigiwa kura. Katika jamii ya Akamba neno *munene* linarejelea ukubwa na uwezo wa kuongoza. Katika wimbo $W_7MB_{Ts,}$ Munene anatambulishwa kama kiongozi wa kiume ambaye anakashifiwa kwa kusahau ahadi alizozitoa wakati wa kampeni za kuomba kura wakati wa uchaguzi. Haya yapo katika mshororo $M_{3-12}$ msanii anaposema:

| | |
|---|---|
| *Munene wambiie we ukanzuvia M3* | Mkubwa ulisema utanitunza |
| *Oila kivila kiuka kwitu M4* | Utakapopata cheo kije kwetu |
| *Kivila niwoosie na nyie ndwaanzuvia M5* | Ulipata cheo na ulisahau mambo yangu |
| *Kivila ni twosie na we mwa niwaie M6* | Kiti tulipata lakini ulipotea |
| *Ninguseng'a na ngekulya ii* | Nashangaa na kujiuliza |
| *Munene we kowolilwe (wiper) M7* | mkubwa mbona hivi ulisahau |
| *Na voyaa Ngai mwa autethye M8* | Nilikuwa nakuombea Mola akusaidie |
| *Muvaka nyie ngolwa ni kwivoyea M10* | Mpaka nasahau kujiombea |
| *Ngivoya unene uke kwitu M11* | Nikiomba uongozi uje kwetu |
| *Munene we nongi ututethye M12* | Mkubwa jaribu utusaidie na uongozi |

Msanii anatuchorea picha ya mtu mwenye nguvu za kulinda na kutunza taifa la Akamba katika mishororo $M_{3-12}$, kwa kumkumbusha sababu za kuchaguliwa kwake. Katika wimbo $W_7MB_{Ts}$ msanii analalamika kwamba kiongozi *Munene* hajatimiza ahadi alizotoa wakati wa kampeni licha ya msanii kujitosa katika kumfanyia kampeni hadi akawa hana muda wa kujiendeleza mwenyewe. Hili linatupa taswira ya namna wanasiasa hutumia muda mwingi wa wafuasi wao bila kuwalipa na hivyo kuwakwamiza kimaendeleo. Kiongozi alikuwa amemweleza msanii kwamba amfanyie kampeni za kutafuta kura za uongozi ili baada ya kushinda kile kiti aangalie masilahi ya msanii. Inaelekea baada ya kupata kile kiti cha uongozi, kiongozi huyu amemkwepa msimulizi. Taswira tunayopata hapa ni ya kiongozi mwanamume ambaye anatoa ahadi ambazo hazitimizi. Msanii anawakilisha wapiga kura wa kawaida katika jamii ambao hujitolea kwa hali na mali kusudi mmoja wao apate wadhifa wa kisiasa. *Munene* naye anawakilisha tabaka la viongozi ambao pindi wanapopata nyadhifa za uongozi wa kisiasa hutoweka na kusahau ahadi walizotoa kwa wananchi. Kupitia kwa taswira hii, suala la siasa na uongozi linajitokeza katika ujenzi wa utaifa wa Akamba.

Kupitia taswira ya mwanamke mabadiliko yanayoendelea kufanyika kuhusu majukumu ya kijinsia yanabainishwa. Scott (2006) anasema kuwa katika miaka michache iliyopita kumekuwa na mabadiliko ya majukumu ya wanawake hasa katika ushiriki wao kwenye ulingo wa ajira na uongozi katika jamii. Wanaume wameanza polepole kukubali uongozi wa wanawake na ushiriki wao katika maendeleo ya jamii. Hii ni kinyume na ukweli kwamba vigezo vya kijamii na kitamaduni vina ushawishi mkubwa juu ya ushiriki wa wanawake katika maamuzi na utatuzi wa masuala nyeti yanayoathiri jamii zao. Jamii ilitarajia wanaume kuchukua jukumu la kufanya maamuzi na kutatua migogoro, huku wanawake wakiwachwa tu kama watazamaji. Hii ni kwa sababu utamaduni wa jamii nyingi za Kiafrika ikiwemo jamii ya Akamba ulikuwa na jukumu la kugawa majukumu kulingana na jinsia (Nkumbuku, 2013). Jukumu lililokabidhiwa kitamaduni kwa kuzingatia jinsia linaamua taaluma na maendeleo ya wanawake. Kupitia mabadiliko haya ya kimajukumu, utaifa wa jamii ya Akamba unaendelea kudumishwa.

Akina mama wamesawiriwa kama wazazi, wasomi, wazibuzi na wataalamu ambao hutekeleza majukumu muhimu katika jamii. Kupitia wimbo $W_{12}MB_{Ts}$, mwanamke amesawiriwa kama mjenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Anasisitiza umuhimu wa mwanamke katika jamii kupitia utoaji wa huduma za matibabu. Mhusika Mueni ni daktari ambaye anajali masilahi ya wanajamii wenzake. Anashughulikia mahitaji ya jamii yake kupitia taaluma yake. Katika mishororo $M_{1-6,}$ ambayo ni uradidi wa mshororo *Ngwéndéá kuká oyu kwa mituki mituki mituki M1* (Nakupenda kwa kuja haraka haraka haraka), msanii anatujengea taswira ya mwanamke ambaye amewajibika katika kutekeleza majukumu ya jamii kwa wepesi. Anatumia neno *mituki* (haraka) mara kadhaa kuonyesha jinsi Daktari Mueni hutatua matatizo ya jamii haraka. Mwanamke anashiriki ujenzi wa utaifa wa jamii yake kwa kuwajibika na kutatua tatizo la kijamii kama vile magonjwa kwa haraka na kiutaalamu. Katika $M_{7-11}$, anatumia mbinu ya chuku kutuchorea taswira ya mwanamke kama mtatuzi wa changamoto za kijamii kwa kusema Daktari Mueni anapofika magonjwa yake yote hutoweka. Kupitia kwa wimbo huu, msanii anasawiri nafasi muhimu inayoshikiliwa na wanawake wasomi katika ujenzi wa utaifa wa jamii kama wazalishaji mali kwa kutumia mhusika Daktari Mueni.

Katika nyimbo $W_9MB_{Ts}$, na $W_{10}MB_{Ts}$ taswira ya mwanamke imetumika kuwakilisha usawa katika jamii ya Akamba. Katika wimbo $W_9MB_{Ts}$ Msanii ametumia takriri ya virai '*The things, my things, your things'* katika lugha tatu tofauti ili kuonyesha usawa kati ya wanawake na wanaume katika ugawaji wa mali. Amerudia maneno ' hivi ni vitu' kujenga taswira ya mali inayomilikiwa na jinsia zote kwa usawa. Katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba ni dhahiri kuwa mwanamke amepewa nafasi sawa na mwanamume ya kumiliki mali. Mishororo *Ndanu lika ngalini, oino ya mutongoi* (Ndanu ingia kwa gari, hii ya kiongozi) katika wimbo $W_{10}MB_{Ts}$ inachora taswira ya mwanamke kama mpenda maendeleo na anayepaswa kushirikiana na mwanamume katika harakati za kuleta maendeleo katika jamii. Kitendo *lika* ni taswira ya kujiunga na uongozi. Mhusika Ndanu ni mwanamke ambaye anatarajiwa kujiunga na kiongozi katika kuendeleza jamii yao. Iwapo ufanisi wa kijamii utapatikana, ni sharti jinsia ya kike ihusishwe katika mchakato mzima. Taswira ya gari katika muktadha huu ni ujenzi wa taifa zima la jamii ya Akamba ambalo kila mmoja anastahili kushirikishwa. Nyimbo hizi pia zinatupa taswira ya muundo wa familia katika jamii ya Akamba. Msanii anaweka wazi kuwa kuwepo kwa mwanamume na mwanamke katika uhusiano wenye usawa ndio huunda jamii ya Akamba. Ushirikiano huu wa kijamii ndio msanii anaousisitiza katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

Taswira ya mwanamke inaendelezwa katika wimbo $W_2MB_{Ts}$ ambapo msanii anamrejelea mhusika Ngemi kama *ngethe* (msichana mrembo) kupitia mshororo M1-2: *Návíká Kibwezi nìèndà úkwíà nyíè ní nōníé ngèthé … yítàwā Ngémì* (Nilipofika Kibwezi niliona msichana mrembo … anaitwa Ngemi). Msichana *Ngemi* anasawiriwa kama aliyeumbwa akaumbika, mwenye staha, mwenye bidii kazini na kiongozi bora. Msisitizo katika usimulizi wa haiba ya msichana *Ngemi* una jukumu la kusawiri thamani na umuhimu wa mwanamke katika jamii ya Akamba. Maana ya *ngemi* ni kumetameta. Vitu vinavyometameta huwa vya thamani kuu. Mfano ni madini ya dhahabu ambayo huwa na thamani kuu katika jamii. Taswira hii imetumika kuonyesha kuwa wanawake ni nguzo muhimu katika jamii. *Ngemi* pia ni taswira ya urathi wa jamii ya Akamba kama vile ardhi, lugha, historia, imani na rasilimali zingine ambazo zinapatikana katika eneo la Ukambani. Msanii ametumia taswira ya urembo wa *Ngemi* kukuza utaifa wa jamii ya Akamba kwa kuibua fahari ya rasilimali za thamani zinazopatikana katika eneo la Ukambani.

Taswira ya mwanamke pia imetumika ili kuweka wazi mgogoro wa kinafsi kuhusu utambulisho wa kijinsia na kijamii. Katika wimbo $W_3MB_{Ts}$ msanii ametumia tamathali ya tashbihi kujenga taswira anaposema *mailye ta Asungu* (wanafanana na Wazungu). Tamathali hii inatupa picha ya sura za wasichana wa Makutano wa jamii ya Akamba ambazo zimebadilika kutoka ngozi nyeusi hadi nyeupe ya Wazungu. Msanii anasimulia kwamba baadhi ya wanawake wanajipaka kemikali kali ambazo zinafanya ngozi zao kubadili rangi kutoka nyeusi hadi iliyopiga weupe kama ya Mzungu. Huu ni mgogoro wa kinafsi wa mwanamke huyu wa jamii ya Akamba kuhusu utambulisho wake. Anajihisi kuwa ngozi yake nyeusi haipendezi hivyo anaamua kutumia vipodozi ili kuibadilisha. Anatamani kupata utambulisho mpya. Utambulisho huu unakuja pamoja na kuasi asili yake ya jamii ikiwa ni pamoja na utambulisho wake wa awali, mila na utamaduni wake, lugha na hata mazingira anamoishi. Anataka kuiga wazungu na mienendo yake. Ni bayana kwamba juhudi zake za kuchukua utambulisho mpya hazifui dafu kwani wanaomwona wanasaili uhalisia wake. Mshororo $M_{3-6.}$ msanii anakuli:

*Ngaseng'a kwani Makutano kwithaa Asungu M3*
*Ngatuma Mbasu achunguse maumaa naku M4*
*Mbasu akambia Makutano kuyingwa asungu M5*
*Eiwe ni ngethe syivakaa miio ya Asungu M6*

Nikashangaa kwani Makutano kuna Wazungu
Nilituma Mbasu achunguze wanatoka wapi
Mbasu akaniambia Makutano hakuna Wazungu
Ni wasichana wanajipaka vitu za Wazungu

Msanii anapokutana na Mwikali, msichana aliyechukua sura ya Mzungu, anashangaa iwapo katika mji ule wa Makutano kuna Wazungu wanaoishi mle. Hali hii inampelekea kufanya uchunguzi wa kina ili kubanisha ukweli wa utambulisho wa msichana huyu. Hii ni kwa sababu Mwikali hajafanikiwa kuufuta utambulisho wake wa awali wa kuwa Mkamba. Utambulisho wake u katikati ya weusi na weupe wa wazungu ambao unakanganya. Ni mkorogo ambao haueleweki. Mkorogo huu ni hatari kwa utambulisho wa kijamii. Baada ya uchunguzi wa kina, msanii na mwenzake Mbasu wanabainisha kuwa Mwikali ni *Mukamba kivindyo* (Mkamba halisi) na asili yake inajulikana ($M_{9-16}$) kwamba yeye anaitwa Mwikali wa Kaumbulu na kwao ni Kasuvilo upande wa Ndela. Kupitia taswira hii, msanii ameweza kuweka wazi migogoro ya utambulisho wa kinafsi na kijamii

ambao unaletwa na utandawazi. Ili pawepo na ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba ni lazima kusiwe na mkorogo wa aina yoyote katika jamii.

**4.3.9 Mbinu ya Ulinganuzi na Mgotanisho**

Hii ni mbinu ambayo mwandishi anaweza kuitumia katika kuwakuza na kuwaendeleza wahusika kwa kuwalinganua au kuwaweka sambamba, yaani katika muktadha sawa (Murumba (2013). Mtunzi hufanya hivyo ili kuonyesha tofauti kati ya wahusika wawili kwa uwazi zaidi. Kwa kawaida, wahusika wanaolinganuliwa hueleweka zaidi kuliko wale wasio katika mazingira hayo. Kwa njia hii, mtunzi huweza kukuza maudhui na dhamira yake. Mbinu ya ulinganuzi na mgotanisho imejitokeza katika nyimbo pendwa za msanii katika kuendeleza ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Katika wimbo $W_3MB_{Um,}$ msanii analinganisha utambulisho wa aina mbili wa mhusika Mwikali mwenye asili ya Kikamba. Kwanza, kuna mhusika Mwikali Kaumbulu akiwa hajatagusana na mikorogo. Huyu ni mwanamke wa asili ya Kikamba ambaye hajaathiriwa na usasa, anafuata mila na desturi za jamii ya Akamba, hajaiasi lugha yake wala utamaduni wake. Katika mshororo $M_{12}$, amepewa utambulisho wa kijamii kwa kuitwa *mwíítu wa Kaumbúlú* (binti ya Kaumbulu). Mhusika Mwikali anaitwa kwa jina la ukoo wake *mwíítu wa Kaumbúlú* hivyo ni mtoto halisi wa jamii ya Akamba. Utambulisho wa pili ni wa mhusika Mwikali ambaye amekengeuka kutokana na utandawazi. Amelimatia mitindo na tamaduni za kigeni kama vile maisha ya mijini pamoja na tabia na mienendo ya kigeni. *Mikorogo* au kemikali kali anazotumia ni jazanda ya mabadiliko ambayo mhusika huyu amepitia. Hata baada ya kujaribu kuuchukua utambulisho wa kigeni, bado hajafanikiwa. Msanii anasema kuwa mabadiliko haya ni hatari kwa wanajamii. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Misamu yiitwa mikorogo kemikoo nthuku M7* | Mavitu haya yanaitwa mikorogo kemikali mbaya sana |
| *Yiivakwa ni ngethe Makutano syeuve ta asungu M8* | Inapakwa na wasichana Makutano wawe weupe kama wazungu |

Msanii anaita vipodozi hivi *mísamú* (mavitu) katika hali ya kudharau na kudunisha. Hizi ni kemikali mbaya kwa hivyo zina hatari kwa watumizi wake. Wanajamii wanatahadharishwa kuhusu athari za utamaduni hasi wa kigeni. Mwikali ambaye ametumia mikorogo hampendezi msimulizi kama vile Mwikali ambaye hajatumia

mikorogo anavyomfurahisha. Kwa kuwagotanisha wahusika hawa wawili, msanii amefanikiwa kuitahadharisha jamii yake kuhusu kupapia tamaduni za kigeni bila kuchunguza athari zake ambazo ni pamoja na kusambaratisha utaifa wa jamii ya Akamba.

### 4.3.10 Majazi

Murumba (2013) anadokeza kwamba majazi ni jina ambalo aghalabu hubeba maana ambayo husawiri na kuakisi hali au tabia ya mhusika au mahali penye jina hilo. Mbuvi (2014) anadai kuwa majazi ni mbinu ya kumpa mtu au mahali jina kulingana na umbo au sifa zake. Kimsingi, ni majina ya kistiari kwani huwakilisha sifa fulani. Katika mbinu hii, mtunzi hutumia majina ambayo yanaakisi na kufumbata sifa na matokeo ya wahusika na tabia za wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi zinazohusika. Kwa njia hii, msomaji huweza kufahamu wasifu wa wahusika na mahali kwa urahisi zaidi.

Katika wimbo $W_3MB_{Mj}$, msanii anasimulia kuhusu namna alivyokutana na msichana aliyetwaa sura ya mzungu katika mji wa Makutano. Jina hili Makutano ni la kimajazi ambapo msanii anasawiri mahali ambapo watu kutoka maeneo tofauti tofauti hukutana kwa shughuli mbalimbali. Msanii anatueleza kwamba yeye pamoja na mwanamuziki mwenzake Mbasu walikuwa wamefika kule kwa shughuli za kikazi; kupiga densi. Mji wa Makutano unakuwa mahali ambapo msanii ambaye anajiona kuwa Mkamba halisi, anakutana na wasichana ambao wametumia *mikorogo* (vipodozi) hadi ngozi zao zenye asili ya Kikamba zikabadilika. Kwa maoni yake, wasichana hawa wamebadili sura zao ili kuwavutia wanaume katika vilabu. Anaona kuwa mienendo hii haifai kwa vile ngozi zao asili zinapendeza bila vipodozi hivi. Makutano ni mahali ambapo tamaduni mbili zinakutana; utamaduni wa mkamba halisi na utamaduni mpya wa Mkamba aliyekengeuka. Ni mahali ambapo wanajamii wanakutana na kutetea utaifa wa jamii yao. Katika wimbo huu mhusika Mwikali wa Kaumbulu anatambulishwa. Ni msichana wa eneo la Kasuvilo ambaye hatambuliki kama Mkamba kwa sababu ya kutumia *mikorogo*, kemikali za kujipodoa ambazo kwa dharau anaziita *misamu* (mavitu). Neno mikorogo ni jina la kimajazi likiwa na maana ya mchanganyiko wa kemikali. Msanii anaona kwamba iwapo utaifa wa jamii yake utaafikiwa, kila mwanajamii ni sharti atambue na kuufuata utamaduni wa jamii ya Akamba bila kuuchanganya.

Jina *Ngemi* katika wimbo $W_2MB_{Mj}$ ni la kimajazi lenye maana ya kushangilia. Ngemi huhusishwa na vitu vya thamani ambavyo vinapatikana katika maeneo ya Ukambani kama vile ardhi, lugha, uongozi, mila na utamaduni wao na rasilimali zingine za kijamii. Hivi ni vitu vya tunu ambavyo vinastahili kutunzwa na kuonewa fahari na jamii ya Akamba. Katika taifa la Akamba, wanajamii hushangilia wakati wanapofanikiwa katika shughuli mbalimbali. Mhusika Ngemi anashangiliwa kwa haiba na wasifu wake wa kuongoza jamii ya Akamba. Anaonekana kama mwenye uwezo wa kuongoza wadi ya Kisaayani. Mbinu hii imetumiwa kuonyesha kwamba wanawake, kama viongozi wa jamii ya Akamba wanahusika katika ujenzi wa taifa lao.

Katika wimbo $W_1MB_{MJ}$, msanii anatueleza kuhusu mpenzi wake kwa jina *Mwende* ambaye anaishi Ujerumani. Jina *Mwende* ni la kimajazi linalowakilisha wapendwa katika jamii ambao wameondoka nchini kwenda ughaibuni kujitafutia riziki. Wanawaacha wenzao wakiwa na upweke mkuu ambao unawasababishia kutaka kuchukua hatua za kutaka kuwafikia. Msanii anadhihirisha penzi lake kwa Mwende kwa kuota na yeye, na hata kuchukua hatua mbalimbali za kumtembelea Ujerumani. Njia zote za kumtembelea zinagonga mwamba na kumfanya kuamua kusafiri kwa miguu hadi Ujerumani. Jina hili pia linawakilisha rasilimali za kijamii ambazo zimeporwa na mataifa ya kimagharibi kupitia mifumo isiyo sawa ya ukoloni na ukoloni mamboleo.

Katika wimbo $W_7MB_{Mj}$, jina *Munene* ni la kimajazi. Linatokana na mzizi –nene, maana yake ukubwa na nguvu. Jina hili linawatambulisha viongozi katika ujenzi wa utaifa wa Akamba. Katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba, jamii hushirikiana kuwatambua na kuwachagua viongozi ambao huwakilisha matakwa yao katika taifa lao la kijamii na nchi ya Kenya. Msanii katika mshororo $M_{12}$, anadhihirisha matarajio ya jamii kwa viongozi waliochaguliwa kupitia mhusika *Munene*. Anaposema *Munene we nongi ututethye M12* (Mkubwa angalau utusaidie), matarajio ya wapiga kura kwa viongozi waliochaguliwa yanabainika. Wananchi wanatarajia kuletewa maendeleo katika eneo lao ili watoke kwenye lindi la umaskini. Msanii analalamika kuwa yeye bado anataabika. Jamii ya Akamba inapoungana na kuwachagua viongozi wao huwa na matarajio mbalimbali kama vile kutunzwa na kusaidiwa. Haya yanabainika katika mishororo $M_3$ na $M_{12}$, ambapo msanii

anamkumbusha mhusika *Munene* yale yaliyomfanya kumchagua kama kiongozi. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Munene wambiie we ukanzuvia M3* | Mkubwa ulisema utanitunza |
| *Munene we nongi ututethye M12* | Mkubwa angalau utusaidie |

Wanajamii wanadai haki yao kutoka kwa viongozi wao wa kisiasa ambayo ni pamoja na kuwatunza kwa kuwaletea rasilimali ambazo zitasababisha maendeleo katika maeneo yao. *Munene,* kama jina la kimajazi limetumiwa kukejeli tabaka la viongozi wa kisiasa ambao wanawatelekeza wananchi waliowaweka katika nyadhifa hizo za uongozi baada ya kuchaguliwa. Ni vielelezo vya viongozi wa kijamii ambao hugura nyumbani pindi wanapopata viti walivyokuwa wakiwania vya kisiasa. Wananchi wanahisi ya kwamba wamesalitiwa na viongozi hawa kwani ahadi za maendeleo walizotoa zimebakia hivyo; ahadi.

### 4.3.11 Matumizi ya Motifu

Motifu ni matukio yanayojirudia rudia katika kazi ya fasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kazi hiyo. Njeru (2022), akimnukuu Mulokozi (2017) anasema kwamba motifu ni kipengele cha kijadi kinachohusu kurudiwarudiwa kwa wazo au dhamira fulani katika sehemu kubwa ya kazi za fasihi hususan riwaya, tamthilia, ushairi, fasihi simulizi na nyinginezo. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), dhana ya motifu hutumiwa kurejelea wazo kuu na sehemu ya dhamira katika kazi ya fasihi. Hutumiwa pia kuelezea elementi fulani ya kimuundo au kimaudhui inayotawala kazi fulani.

Msanii ametumia motifu ya mwanamke kuendeleza maudhui ya utaifa wa jamii ya Akamba. Kupitia kwa motifu hii ya mwanamke, msanii ameweza kusawiri ustawi wa jamii ya Akamba kupitia ardhi yenye rutuba na ukuaji wa kijamii. Zaidi ya hayo, majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na mwanamke ili kuendeleza utaifa wa jamii yanabainishwa kupitia nyimbo kadhaa. Kupitia motifu ya mwanamke msanii ameweza kuwasilisha mwonoulimwengu wa jamii ya Akamba, falsafa ya jamii yao, utambulisho wao na utaifa wao. Katika wimbo $W_1MB_{MO}$, msanii anasimulia kuhusu mpenzi wake Mwende ambaye anafanya kazi Ujerumani. Mwende anawakilisha utaifa wa Akamba kama jamii ambayo inashiriki utandawazi na ambayo haijajifunga katika mazingira asilia ya kijiografia. Mwende bado amedumisha uhusiano wake na jamii yake ya nyumbani kama njia ya kuendeleza utaifa wa jamii.

Katika wimbo $W_2MB_{MO}$, Ngemi anawakilisha utamaduni wa Akamba wa posa. Mhusika Ngemi kama mwanamke ametumiwa kuendeleza utamaduni wa posa. Msanii anawatuma Mukosi na Teke pamoja na Ndivau kama washenga. Maneno katika mshororo $M_{13}$ *Na nundu aka moombiwe nundu wa aume M13* (Kwa vile wanawake waliumbwa kwa sababu ya wanaume) yanaibua falsafa ya Akamba kuhusu wanawake, kwamba waliumbwa kwa sababu ya wanaume. Katika utaifa wa jamii ya Akamba, wanawake wanachukua nafasi ya pili. Hata hivyo, wanapewa nafasi ya uongozi kwa mfano, Ngemi anatarajiwa kuwa mwakilishi wa wodi ya Kasayani. Falsafa ya jamii hii kuhusu wanawake ni kwamba ni viongozi.

Motifu ya mwanamke inajitokeza pia kupitia wimbo $W_4MB_{MO}$. Wanawake wanashirikishwa kama wenye msimamo dhabiti na wasiokiuka kaida za jamii yao. Msanii anasimulia jinsi alivyojaribu kupata penzi la Winnie kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile kuwatuma marafiki zake, kuzungumza kwa Kiingereza na kumwandama lakini Winnie akamwambia kwamba yeye ni *mali yeene* (mali ya wenyewe). Hii ina maana kuwa ameolewa. Wanawake kama wajenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba wanashiriki ndoa na wanafuata sheria zilizowekwa na jamii yao kuhusu ndoa. Suala hili linajenga utafa wa jamii ya Akamba.

Daktari Mueni katika wimbo $W_{12}MB_{MO}$ ametumiwa kama kiwakilishi cha wanawake wasomi na wanaotumikia jamii yao ili kujenga utaifa. Anakuwa katika mstari wa mbele katika kutatua baadhi ya changamoto ambazo zinakumba taifa la Akamba mojawapo ikiwa magonjwa. Msanii anapopatwa na ndwele Daktari anaenda mbio kumtibu. Wanawake wanahusishwa katika kutatua matatizo ya jamii kama vile magonjwa. Katika wimbo $W_{20}MB_{MO,}$ wanawake wanashiriki katika ndoa za mitala ambazo zinadhihirisha utamaduni wa jamii ya Akamba. Msanii ameisawiri jamii ya Akamba kama inayokubali utamaduni wa utala kwani msanii ameoa wanawake watatu; Mumo, Angela na Inyaa Mbonge (Bernedetta). Msanii anamsifu Bernedetta mamake Mbonge kwa kumzalia mtoto wa kiume ambaye ameongeza idadi ya wanaume katika familia ya Wa Maria. Hatujaelezwa iwapo Wa Maria alikuwa na watoto wengine wa kiume ila ana furaha kuu kwa kumpata mtoto huyu wa kiume kupitia ndoa yake na mke wake wa mwisho, Berndetta. Hili linadhihirisha kuwa jinsia ya kiume imepewa hadhi kuu katika jamii ya Akamba. Mama anapojifungua

mtoto wa kiume jamii yote inashangilia. Wanawake katika ndoa wanashirikiana katika shughuli za malezi. Hili linachangia katika kupanuka kwa jamii ya Akamba na hivyo kujenga utaifa wao. Msanii anatilia mkazo suala la jamii yake kufuata utamaduni wao ambao haujaathiriwa na tamaduni za kigeni. Anachukua msimamo kwamba wakati ndoa inapokosa mtoto wa kiume basi jamii inakubali mwanamume kuoa wanawake zaidi ya mmoja ili kuhakikisha kwamba kizazi chake kitaendelezwa kupitia kupatikana kwa mtoto wa kiume. Kupitia hali hii, utaifa wa jamii unakuzwa.

Mbinu ya motifu ya safari imetumika katika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba kupitia wimbo $W_6MB_{MO}$. Msanii anasawiri ushirikiano ambao unastahili kuwapo miongoni mwa wanajamii wakati wa ujenzi wa utaifa wao kupitia hurafa ya sungura na ndovu. Safari ya wanyama hawa wawili ambao inahusu kuvuka mto wenye kina kirefu inalinganishwa na safari ndefu na yenye matatizo ya aina yake ambayo jamii ya Akamba haina budi kuipitia katika azma yake ya kufikia utaifa wa jamii. Msanii anaona kwamba wanajamii wa Jamii ya Akamba ni sharti wakubaliane kuwa na kiongozi mmoja (Ndovu) ambaye atawasaidia wanajamii kutatua changamoto zinazoikumba jamii yao kwa kutoa uongozi bora.

### 4.4 Changamoto Zinazokumba Utaifa wa Jamii ya Akamba

Sehemu hii ilijibu swali la tatu la utafiti ambalo linajibiwa kwa kupambanua changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba kwa mujibu wa nyimbo pendwa za Ken wa Maria. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba kunazo changamoto ambazo zinaathiri ujenzi wa utaifa wa Akamba. Sehemu hii iliongozwa na mhimili wa tatu wa nadharia ya utaifa unaosema kwamba wananchi ambao wako katika taifa moja ni lazima wakubali mafundisho au itikadi ya taifa lao bila kuwa na uhusiano wowote na mafundisho ya taifa lingine linaloshindana na taifa lao. Maneno haya yanathibitisha kuwa utaifa wa taifa fulani unaweza kukumbwa na changamoto ambazo zinatokana na athari hasi za maingiliano ya kijamii. Mekonnen (2019) anabainisha baadhi ya changamoto zinazokumba utaifa kama vile mizozo ya siasa za uongozi, ung'ang'aniaji wa rasilimali za taifa, utengwaji, utandawazi pamoja na athari za ukoloni. Utafiti huu ulitambua baadhi ya changamoto ambazo zinakumba utaifa wa jamii ya Akamba. Hizi ni kama vile: Kuzuka kwa utambulisho mpya, athari za utandawazi, siasa za utengano, usaliti wa kisiasa na changamoto za kiuchumi.

### 4.4.1 Kuzuka kwa Utambulisho Mpya

Kutokana na data iliyochanganuliwa, utafiti huu ulibainisha kwamba kuna aina mpya za utambulisho ambao umetokea katika jamii ya Akamba unaoathiri ujenzi wa utaifa wa Akamba. Utambulisho huu unatokana na kupenya kwa tamaduni za kigeni katika jamii. Utambulisho wa awali wa jamii unaonekana kuchanganyika na utambulisho huu mpya. Matokeo yake ni hali ambapo wanajamii wanakosa utambulisho wao wa awali na pia utambulisho huu wa kigeni. Msanii anaiita hali hii *Mikorogo* yaani, mchanganyiko katika wimbo $W_3CH_{UM}$. *Mikorogo* ni jazanda ya mchanganyiko wa aina tofauti za tamaduni za kijamii.

Msanii anaitanabaisha jamii ya Akamba kwamba utambulisho wao kama jamii umo hatarini ya kuangamizwa na utambulisho mpya ambao ni tofauti na utambulisho wao. Katika wimbo $W_3$ na $W_8$ kunaibuka njia za utambulisho katika jamii kwa misingi ya rangi, majukumu na jinsia. Inaonekana kuwa suala la rangi limewalemaza wengi kiasi kwamba wako radhi kubadili rangi ngozi zao ili wachukue rangi ya watu wengine. Kubadilisha rangi ya ngozi ni matumizi ya krimu, jeli, sabuni na bidhaa nyinginezo ili kufanya ngozi iwe nyeupe kama ya mtu mwenye asili ya kizungu (Julien, 2014). Vitu vilivyomo kwenye bidhaa hizi vinaweza kuwaweka watumiaji katika hatari kubwa ya matatizo mengi ya kiafya. Moja ya sababu za waja kubadilisha rangi ya ngozi zao ni jinsi vyombo vya habari pamoja na mabango ya matangazo yanavyoonyesha mvuto wa uzuri, ambayo huchochea wanawake kuwa na motisha ya kubadilisha rangi ya ngozi yao (Hunter, 2011). Kulingana na utafiti wa Lewis na wenzake (2011), uliofanyika kwa Watanzania, kuna vichocheo sita vikuu vinavyowafanya watu, hasa wanawake, kubadilisha rangi ya ngozi zao. Waandishi wameripoti kuwa watu wanaweza kubadilisha rangi ya ngozi yao kwa sababu zifuatazo: Kuondoa kasoro za ngozi kama vipele, madoa meusi, na chunusi; kufanya au kudumisha ngozi laini zaidi; kuifanya ngozi yao iwe nyeupe ili kufikia viwango vya uzuri vya Kimagharibi, kuonekana wanavutia zaidi kwa wenzi wao wa sasa au wa baadaye na kuwavutia au kukidhi matarajio ya marafiki zao.

Matumizi ya vipodozi vya kemikali kubadilisha rangi ya ngozi ya mtu kwa sasa ni jambo lililoenea duniani na kuathiri jamii nyingi ikiwemo jamii ya Akamba. Ingawa historia ya kubadili rangi ya ngozi inaweza kufuatiliwa hadi enzi za Elizabeth wa Uingereza ambapo

poda na rangi zilitumika, kwa sura yake ya sasa, utumiaji wa vipodozi vya kupunguza rangi ya ngozi unafanyika zaidi miongoni mwa jamii za watu "wenye rangi" na kwa kiwango kikubwa zaidi kati ya watu wenye asili ya Kiafrika. Ingawa ni kweli kwamba kubadilisha rangi ya ngozi ni jambo lenye pande nyingi, likiwa na mchanganyiko wa nguvu za kihistoria, kitamaduni, kisiasa, na kisaikolojia zinazochochea tabia hiyo, watafiti wengi wanaochunguza suala hili angalau wanakubaliana kwamba taasisi za ukoloni na utumwa kihistoria, na ubabe wa watu weupe duniani kwa sasa, ni vichocheo vikuu na vinavyolaumiwa kwa tabia ya kubadilisha rangi ya ngozi (Blay, 2011).

Katika wimbo $W_3CH_{UM,}$ msanii anamsawiri mhusika Mwikali kama mwanajamii ya Akamba aliyekengeuka kwa kuibadili rangi ngozi yake kwa kujipaka kemikali hatari ili afanane na Wazungu. Anaionea fahari rangi ya ngozi ya mtu mwingine na kuidharau rangi yake. Kulingana na Kothari (2006), wakoloni kama vile Waingereza walipofika Afrika waliendeleza utaifa wao wa Kiingereza katika koloni zao. Kutokana na utaifa huu, baada ya uhuru nchi zilizotawaliwa zilichukua utamaduni wa Waingereza na kuuendeleza ndani ya taifa zao hadi wa sasa. Baadhi ya Waafrika waliochukua utamaduni wa Waingereza walianza kuacha utamaduni wao kama vile mavazi, lugha na hata tabia. Kwa sababu hiyo utaifa wa Waingereza ulianza kuyeyusha ujenzi wa utaifa wa jamii za Kiafrika. Maoni ya Kothari yanadhihirisha kwamba utaifa wa Akamba umeyeyushwa na utaifa wa Uingereza kwa sababu Waafrika kama Mwikali wameanza kuushabikia na kuuacha utaifa wao. Mwikali ameasi utambulisho wa jamii yake na kupapia utambulisho wa jamii nyingine kwa kufikiri kwamba rangi na mienendo yao ni bora zaidi kuliko ile yake. Kwa kufanya rangi ya ngozi yake kuwa nyeupe kupitia matumizi ya kemikali hatari, mhusika huyu anadhihirisha kwamba anaidharau rangi yake huku akiitukuza rangi ya jamii za Ulaya.

Blay (2011), anairejelea hali hii kama ubabe wa watu weupe. Ubabe wa watu weupe mara nyingi hufasiriwa kama neno la siri linalowahusu watu weupe. Hata hivyo, ubabe wa watu weupe ni zaidi ya mkusanyiko wa watu weupe. Kama mfumo, watu wengi hushiriki ndani yake, na kama itikadi, watu wengi hufikiria, kuhisi, kutenda, na kufanya kazi kwa mujibu wake, na kwa njia nyingi huutetea na kuuendeleza; iwe ni watu weupe au "wasiokuwa weupe." Taasisi ya ubaguzi wa rangi ya ngozi ni mfano wa jinsi "wasiokuwa weupe" wanavyoshiriki kuendeleza ubabe wa watu weupe. Mwikali, ambaye ni mwanajamii ya

Akamba anaonekana kuendeleza hali hii. Huku kujifanya mweupe kumedhalilisha utambulisho wa jamii ya Akamba kwa vile rangi ya ngozi ni mojawapo ya vitambulisho vya jamii. Kwa mujibu wa Regmi (2003), utambulisho wa jamii hujengwa kwa vipengele kama vile: imani za jamii, mila na desturi za jamii, dini, lugha pamoja na sura, rangi au maumbile ya wanajamii. Kwa hivyo rangi ni kibainishi muhimu katika ujenzi wa utaifa wa jamii yoyote ikiwemo jamii ya Akamba. Katika wimbo $W_3CH_{UM}M_{3-4}$, inakuwa vigumu kumtambua mwanamke ambaye amebadili sura yake na kuwa mweupe na itahitaji umchunguze kwa makini ili kumtambua. Katika wimbo $W_3CH_{UM}$, msanii anasema:

| | |
|---|---|
| *Ngatuma Mbasu achunguse maumaa naku M4* | Nilituma Mbasu achunguze wanatoka wapi |
| *Mbasu akambia Makutano kuyingwa Asungu M5* | Mbasu akaniambia Makutano hakuna Wazungu |
| *Eiwe ni ngethe syivakaa miio ya Asungu M6* | Alielezwa wasichana wanajipaka bidhaa za Wazungu |

Wakati mhusika huyu anajinasibisha na jamii nyingine, si rangi ya ngozi tu ambayo hubadilika. Aghalabu mhusika huyu atabadilisha tabia na mienendo yake ishabihiane na ile ya utamaduni pokezi. Lugha yake huenda ikapotea, utamaduni wake hasa mavazi na imani yake ya dini. Suala kama hili litaathiri pakubwa utaifa wa jamii ya Akamba kwa njia hasi. Mhusika kama huyu atakuwa hana utambulisho halisi wa jamii yake. Msanii anaona kwamba hatua kwa hatua, utambulisho wa jamii ya Akamba unakufa. Anwani *Mikorogo* katika wimbo $W_3CH_{UM}$, inarejelea chochote kigeni ambacho kinaingizwa katika utamaduni wa jamii ya Akamba na kuishia kuvuruga utaifa wao. Msanii anaona kwamba utamaduni wa kigeni ni tishio kwa mshikamano wa jamii ya Akamba kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Katika wimbo $W_8CH_{UM}$, suala la majukumu ya kijinsia na jinsi yanavyoathiri utambulisho wa kijinsia linajitokeza. Katika mshororo $M_{3-4}$, msanii ana wasiwasi kwamba mpenzi wake wa kike Mkorea ndiye anayemtongoza na hata kumrai washiriki mapenzi kinyume na utamaduni wa jamii ya Akamba. Haya yanadhihirika kupitia mshororo $M_{3-4}$:

| | |
|---|---|
| *Ēendã nìvãndē ítúmô M3* | Anataka nipande mshale |
| *Nã āìndēmbēsyā Korea M4* | Kisha twende Korea |

Hali hii ya mabadiliko ya majukumu ya kijinsia kutokana na utamaduni wa kigeni yanaweza kuvuruga utamaduni na ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Wanajamii hawafuati kanuni za awali za jamii ambazo zilibaini wazi majukumu ya kila jinsia. Mbondo (2006), akizungumzia kuhusu imani na shughuli za jamii ya Akamba anaweka wazi majukumu ya wanaume na wanawake wa jamii ya Akamba. Anakuli:

> Kitamaduni, wanaume katika jamii ya Akamba kwa kawaida walijihusisha na shughuli za kiuchumi kama vile uwindaji, biashara au ukulima. Wanawake nao walikuwa na jukumu la kulea watoto pamoja na kuitunza familia kwani wao walikuwa na maarifa zaidi kuhusu malezi.

Msanii ana hofu kwamba hali imebadilika kwa sasa. Majukumu katika jamii si bainifu kama ilivyokuwa awali katika jamii za kitamaduni kwa vile mambo mengi hayaeleweki. Utamaduni wa jamii ya Akamba ulizingatia ugawaji wa majukumu kijinsia (Mwikali, 2021). Kila mwanajamii alijua na kutekeleza majukumu yake kama vile utamaduni wao ulivyoelekeza. Hakukuwa na maingiliano ya majukumu kwa vile kila mwanajamii alielewa jukumu lake.

Katika wimbo $W_3CH_{UM}$, utambulisho wa kijinsia na changamoto zake katika ujenzi wa utaifa wa Akamba unasawiriwa. Katika mshororo $M_4$, msanii anasema alimtuma Mbasu afanye utafiti kuhusu utambulisho wa wahusika wenye rangi nyeupe katika mji wa Makutano. Msanii hana uhakika kuhusu utambulisho wa mhusika ambaye amemwona Makutano wakati wakipiga densi. Inabidi amtume mwanamuziki mwenzake ili amsaidie kuchunguza kwa makini ili aweze kujua utambulisho wa mhusika aliyemwona. Inaweza kuwa utambulisho uliobadilika ni wa kijinsia kupitia majukumu ya kijamii ya mhusika au utambulisho wa kijinsia kupitia tabia za mhusika. Msanii hana uhakika iwapo huyu ni mwanamke au mwanamume. Baada ya uchunguzi wa makini, wanagundua utambulisho wa msemewa. Msanii anasema:

| | |
|---|---|
| *Kwanza yo ngethe ila nonie yiilye Musungu M9* | Kwanza msichana niliyemuona akikaa Mzungu |
| *Eiwe usu ni Mwikali wa Kaumbulu M10* | Niliambiwa anaitwa Mwikali wa Kaumbulu |
| *Kwoo nonavu Kasuvilo muingo wa Ndela M11* | Kwao ni hapo Kasuvilo upande wa Ndela |

*Na ni Mukamba kivindyo mwiitu wa Kaumbulu M12* Ni Mkamba halisi msichana wa Kaumbulu

Msemewa ameweza kutambulishwa kiuana katika mshororo $M_9$ msanii anapomrejelea kama *ngethe* (msichana). Vile vile, msanii anamtambulisha Mwikali kinasaba kama *mwiitu wa Kaumbúlú* (binti ya Kaumbulu) na kijamii kama *Mukamba* (Mkamba). Hata hivyo, utambulisho huu wa kiasili umo hatarini ya kutoweka kutokana na kuingizwa kwa utamaduni wa kigeni unaovuruga utambulisho wa kijinsia, kimajukumu na rangi.

### 4.4.2 Athari za Utandawazi

Utandawazi ni suala tata na lenye sura nyingi ambalo limechangia mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali za maisha ya watu kote ulimwenguni ikiwemo katika sekta ya utamaduni. Utandawazi umeimarisha viwango vya kipekee vya binadamu kuunganishwa kwa kuruhusu tamaduni kushirikiana katika mila, imani na desturi zao bila mipaka hivyo kuongeza uelewa wa kitamaduni duniani (Gerda, 2022). Hata hivyo, utandawazi umeibua wasiwasi kuhusu uwezekano wa kudhoofisha tamaduni za kienyeji kutokana na nguvu za vyombo vya habari vya Magharibi, mifumo ya kiuchumi na desturi za kitamaduni. Hali hii inatishia kuzifunika na katika baadhi ya matukio, kuchukua nafasi ya mila za asili. Hali hii huchangia kupotea kwa utambulisho wa kitamaduni wa jamii.

Utambulisho wa kitamaduni unahusu mkusanyiko wa kipekee wa maadili, mila, lugha, na mwonoulimwengu unaofafanua kundi au jamii fulani. Unachukua nafasi muhimu katika kuunda utambulisho wa mtu binafsi na wa pamoja, ukiunganisha watu na historia yao na kuwapa hisia ya mwendelezo na kuhisi kuwa sehemu ya jamii. Utandawazi unaweza kuchangia kwenye ufanano wa kitamaduni ambapo tamaduni zenye nguvu zinalazimisha maadili yao, vyombo vyao vya habari, na tabia zao za matumizi kwa tamaduni ndogo au zile zilizoko pembezoni, na hivyo kuhatarisha kupotea kwa mila na lugha za kienyeji. Kadri utamaduni wa kimataifa unavyoendelea kuenea kupitia maendeleo ya kiteknolojia, vyombo vya habari na utalii, desturi za kitamaduni za jadi hasa katika mataifa ambayo hayajaendelea kiuchumi yanakabiliwa na hatari ya kumezwa na uzito wa matumizi yake na usafirishaji wa tamaduni kutoka Magharibi. Hali kama hii inadhihirika katika jamii ya Akamba kupitia nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Msanii amebainisha namna suala la utandawazi limekuwa tisho kwa utaifa wa jamii ya Akamba. Kutokana na utandawazi, kuna masuala ibuka ambayo yanatishia kuuangamiza utambulisho wa kitamaduni wa jamii ya Akamba. Haya ni pamoja na kupenya kwa tamaduni za kigeni ambazo zinachanganyika na utamaduni wa jamii ya Akamba. Utamaduni mseto unaibuka; hali ambayo huenda ikachangia kudidimia kwa utamaduni wa jamii ya Akamba. Katika wimbo $W_8$CH, kunaibuka hali ya utamaduni mseto ambapo tamaduni tatu zinachanganyika: utamaduni wa Wamasai, utamaduni wa Wakorea na utamaduni wa Wakamba. Hali hii inaonekana kumtia hofu msanii ambaye ana kamio kuhusu kuyeyushwa kwa utamaduni wake. Utamaduni mseto unavyazwa na ndoa mseto. Msanii anaona kwamba ndoa hizi huenda zikachangia kupotea kwa utambulisho wa kitamaduni wa jamii ya Akamba. Wakati wanajamii kutoka jamii ya Akamba wanapotangamana na wanajamii kutoka jamii zingine, kuna uwezekano wa vipengele kadhaa vya utamaduni wao kupotea. Vipengele hivi ni pamoja na mila na desturi za jamii ya Akamba pamoja na kudhoofika kwa kumbukumbu ya kitamaduni; kumbukumbu ya pamoja ya jamii ya Akamba ambayo inahifadhi uzoefu wake wa zamani, maadili, na urithi wake.

Hali kama hii inamtia hofu msanii ambaye katika mshororo $M_5$, anasema *Nākwã nōtā ngùkìā, Kãrãtá sya Kíkorea, vújo syā Kìmásãi* (Na mimi ni kama naogopa karate za Korea na fujo za Kimasai). Msemaji anaona kwamba jamii ya Akamba itachukua tabia na desturi hasi kama vile fujo za Kimasai na karate za Kikorea na hivyo kuhatarisha utamaduni wao. Karate na fujo ni jazanda ya mambo yote ambayo msanii anahofia yanaweza kuleta mabadiliko hasi ya kijamii. Mseto wa tamaduni hizi tatu unamsababishia msanii kukata kauli kutumia nguvu ili kulinda utamaduni wake. Ndoa mseto zina athari hasi kwa utamaduni wa ndoa ya Akamba kama inavyodhihirika katika mshororo $M_3$, wakati mhusika Mkorea anapochukua nafasi ya kwanza kumtongoza na hata kuomba penzi la msanii. Katika hali ya kawaida katika utamaduni wa jamii ya Akamba, shughuli ya posa na ndoa huongozwa na mwanamume kama inavyodhihirika katika wimbo $W_2CH_{MU}$. Utamaduni wa mhusika Mkorea ni wa kigeni na wenye nguvu kuliko wa msanii. Inamlazimu msanii kutumia nguvu ili amdhibiti Mkorea. Msanii anaamua kwenda kutafuta hirizi kutoka upande wa Kitui ili awe na nguvu zaidi. Hii ina maana kwamba msemaji

anahisi kwamba msemewa (Mkorea) ana nguvu zaidi kuliko yeye kwa hivyo atatumia nguvu zaidi ili aweze kushinda na kumpata kimapenzi.

Wakati wanajamii wa Akamba wanapotangamana na tamaduni zingine, kuna uwezekano wa utamaduni wao kuathiriwa na hivyo kudidimiza juhudi za ujenzi wa utaifa wao. Msanii anapozungumza kuhusu *Karata sya Korea, ngoo sya Kimasai (*Karate za Korea, na fujo za Kimasai) ana maa na kwamba kuna ushindani wa tamaduni hizi tatu, hali ambayo inamtia hofu kwamba huenda ikaathiri ujenzi wa utaifa wa jamii yake ya Akamba. Nadharia ya utaifa inadokeza kuwa iwapo taifa fulani litadumisha utaifa wake, ni sharti raia wake wakatae mafundisho ya taifa lingine ambalo linashindana na taifa lao. Msanii anabainisha kuwa utamaduni wa jamii ya Akamba una maadui aina aina, wa kweli au wa kufikirika ndiposa anaamua kutumia mbinu mbalimbali ili kuulinda. Msemo *kuvanda itumo* (kupanda mkuki) una maana kuwa atatumia mbinu mbalimbali, zingine ambazo zitakuwa hatari ili kuulinda utamaduni wa jamii yake.

Msemaji na jamii yake wamefika njia panda. Kuna hofu ya kutojua ni mwelekeo upi jamii itachukua kutokana na athari za utandawazi kwenye utamaduni wao. Msanii katika mshororo $M_5$, anasema *nākwã nōtā ngùkìā* (na mimi ni kama naogopa) kuonyesha hofu ya jamii ya Akamba kuhusu tamaduni za kigeni zinazoletwa na ndoa mseto kwani zinahatarisha utamaduni wa Akamba kupitia kupotea kwa utambulisho wao wa kitamaduni. Wakati msanii anasema kuwa ataenda ng'ambo awe anaimba kutoka huko, ana maana kuwa ameutoa utamaduni wa jamii ya Akamba na kuuweka katika utamaduni wa kimataifa. Huu ni ubidhaaishaji wa utamaduni wa jamii ya Akamba. Uwekaji wa uchumi kwenye utamaduni, ambapo desturi na alama za kitamaduni zinageuzwa kuwa bidhaa kwa matumizi ya kimataifa, unazidisha ugumu wa jamii za kienyeji kuhifadhi utambulisho wao wa kweli wa kitamaduni. Katika muktadha huu, utandawazi unaweza kuonekana kama mchakato unaodhoofisha upekee wa tamaduni za kienyeji kwa kukuza utamaduni wa kimataifa uliosanifishwa na kuendeshwa kwa maadili ya Magharibi na maslahi ya kiuchumi. Msanii atakuwa amechangia katika kudhoofisha utaifa wa jamii yake kupitia utamaduni.

### 4.4.3 Uhamiaji

Katika miongo michache iliyopita, ulimwengu umeshuhudia harakati kubwa za uhamiaji wa watu ambazo zimeanza kubadilisha muundo wa kitamaduni na taswira za kijamii za jamii nyingi. Wimbi la wakimbizi na wanaotafuta hifadhi limepunguza maadili na imani za jadi za utambulisho wa kitaifa wa jamii moja yenye umoja, likipinga itikadi za zamani za kitaifa na simulizi za kififikra kuhusu taifa lililoungana (Gellner, 1983). Uhamiaji mkubwa umebadilisha muundo wa kitamaduni wa mataifa mengi kwa njia ile ile ambayo usafiri wa umma na utalii, pamoja na mawasiliano ya setilaiti na teknolojia ya habari yameongeza uelewa wa watu wengi kuhusu tamaduni za jamii nyingine kwa viwango vipya. Matokeo yake ni kwamba uhakika wa zamani kuhusu umoja wa kitamaduni wa taifa la Akamba umevunjwa.

Uhamaji wa watu wenye ujuzi na maarifa ya hali ya juu au walioelimika kutoka nchi moja kwenda kuishi na kufanya kazi katika nchi nyingine si jambo geni katika ulimwengu wa sasa. Tunaweza kuorodhesha sababu nyingi za uhamaji wa vijana walioelimika kutoka nchi zinazoendelea kwenda katika nchi zilizoendelea kama vile: katika nchi zinazoendelea, fursa za ajira kwa watu walioelimika ni chache kwa ujumla na haziwezi kukidhi idadi kubwa ya waombaji ajira waliotarajiwa, mazingira magumu ya kufanya kazi, ajira duni isiyoambatana na ujuzi na maarifa ya waliyonayo vijana pamoja na fursa ya kupata elimu ya juu katika nchi zilizoendelea na baadaye vijana hawa kutorejea nyumbani baada ya kupata mazingira bora ya kazi na ya kuishi (Shah, 2011). Vijana wenye elimu nzuri na afya njema wana uwezekano mkubwa wa kuhama hasa wakitafuta elimu ya juu na kuboresha hali zao kiuchumi. Wakati watu wenye ujuzi wa hali ya juu na elimu bora wanapoondoka katika nchi yao kutafuta fursa bora zaidi katika nchi zilizoendelea, mara nyingi husababisha kupungua kwa uzalishaji mali katika maeneo ya kazi waliyoacha (Tyson, 2011). Kupungua kwa wanajamii katika eneo lao la kijamii huchangia kudorora kwa eneo hilo kiuchumi hivyo kuathiri juhudi za wanajamii za kujenga utaifa wao.

Msanii ametambulisha baadhi ya changamoto za kiuchumi zinazodidimiza ujenzi wa utaifa wa Akamba. Katika wimbo $W_1$ na $W_8$ msanii anaeleza jinsi watu wenye maarifa na ujuzi wanavyohamia katika nchi za kigeni hivyo kuchangia jamii ya Akamba kupoteza maarifa na wataalamu mbalimbali kupitia uchakachuaji. Katika wimbo $W_1$, msanii amemtaja Ruth

Mwende ambaye amehamia mji wa Munich nchini Ujerumani. Ingawa hatujaelezwa sababu zilizompelekea mhusika Mwende kuhamia nchini Ujerumani, lililo bayana ni kwamba utengano huu umeathiri pakubwa jamii ya Akamba kiuchumi na kijamii. Ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba unaathirika pakubwa kwa vile Mwende anaihama jamii yake na hivyo anakosa kuchangia katika kuikuza kiuchumi. Isitoshe, watumiaji wa lugha na ukuzaji wa msamiati wa lugha ya Kikamba wanapungua jambo ambalo linaathiri ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Baada ya wanajamii wa Akamba kuhamia nchi za nje, wao huchukua lugha na mitindo ya kigeni inayolemaza ujenzi wa utaifa wa Akamba. Katika wimbo $W_8$, msanii anaeleza kwamba baada ya kuhamia Korea atajifunza lugha ya Kikorea na kuimba kwa lugha hiyo. Hili litachangia kupotea kwa msamiati wa lugha ya Kikamba kutokana na kupungua kwa watumizi wake, hali ambayo itaathiri ujenzi na ukuaji wa utaifa wa jamii ya Akamba.

Katika wimbo $W_{15}$, msanii ametambua miundo misingi ya barabara na maji kama inayoathiri maendeleo ya kiuchumi ya Jamii ya Akamba. Anamkumbusha Kalonzo kwamba kama makamu wa rais kutoka taifa la Akamba ashughulikie changamoto hizi kwani anazifahamu. Akitafitia utaifa wa jamii katika jamii za bara la Marekani ya Kusini, Posern-Zielinski (2023), amezungumzia mchango wa viongozi wa kijamii katika ujenzi wa utaifa wa jamii. Ametambua viongozi mbalimbali wa kijamii wanaochangia katika ujenzi wa utaifa wa jamii kama vile wanasayansi, makasisi, walimu, wasomi wa vyuo vikuu, mawakili, waandishi wa habari na viongozi wa kisiasa. Anaeleza kwamba viongozi katika ngazi ya juu ni wale wa mashirika yasiyo ya kiserikali ya kimataifa na wanasiasa wanaoelewa sera za serikali na kuzitumia ili kufaidi jamii zao kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kwa hivyo, Kalonzo Musyoka kama kiongozi wa jamii ya Akamba amepewa jukumu la kutatua changamoto za kiuchumi na msanii kwa sababu anaelewa sera za serikali. Iwapo changamoto hizi za kiuchumi zitashughulikiwa na viongozi wa kisiasa kutoka jamii ya Akamba, basi utaifa wa jamii ya Akamba utadumishwa kwa vile wananchi hawatalazimika kuhama makwao kwenda kwingineko ambapo mahitaji yao yatashughulikiwa. Juhudi hizi za wanasiasa zitachangia ujenzi wa utaifa wa jamii yao.

### 4.4.4 Ukandamizwaji wa Ndani

Utaifa wa jamii ya Akamba unapata changamoto ya ukandamizwaji wa ndani. Hili hutokea wakati wanajamii wanawakandamiza wanajamii wenzao kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika wimbo $W_5CH_{UK}$, msanii anasawiri hali ya ukandamizwaji ambao unatekelezwa na wanajamii wenye nia mbaya kwa wanajamii wenzao. Msanii anasimulia jinsi yeye na watu wa jamii ya Akamba walivyoshauriwa kula mayai arobaini ya ndege aina ya kware kwa mpigo mmoja. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Neeiwe matumbi ma kwelo* | Niliambiwa mayai ya kware |
| *niumina mathina ma nthi ino (Forty) M1* | Yatamaliza shida za duniani |
| *Ngamelya matumbi ma* kwelo | Nikakula mayai ya kware |
| *Nanyalile muvaka namosa (Forty)M2* | Nikatoa jasho nikakonda |

Msanii mwenyewe alimeza mayai arobaini ili aweze kuondokea matatizo ya dunia. Mhusika wa pili kwa jina Ndunge alitarajia kwamba mayai arobaine yangemwongeza makalio yake. Msanii vile vile anamtaja mhusika ambaye hakuwa akipita mitihani na ambaye alihadaiwa kwamba mayai arobaine yangemsaidia kupasi mitihani yake. Mhusika wa mwisho katika wimbo huu ni ajuza ambaye alitarajia kulainisha ngozi na uso wake kwa kumeza mayai arobaini ya kware. Baada ya kufuata ushauri huu, wanajamii wanasikitika kwa sababu matokeo yanakuwa kinyume na matarajio yao. Ushauri huu potovu kutoka kwa mwanajamii mwenza unatishia ujenzi wa utaifa kwani unasababisha wanajamii kupoteza matumaini.

Masimulizi ya wimbo $W_5CH_{UK}$ yanadhihirisha utapeli unaotekelezwa kwa taifa la Akamba na wanajamii wenzao. Hadaa hizi zinafanyiwa wanajamii wote bila kusaza: wakubwa kwa wadogo, wazee kwa vijana. Huu ni ulaghai wa kiuchumi ambapo mwanajamii anawahadaa wanajamii wenzake kuhusu faida za kutumia bidhaa fulani ambayo anauza. Mayai ya kawaida yanapewa uwezo mkuu kiafya, kielimu, kiuchumi na kijamii. Haya yote yanaishia kuwa hadaa ambazo zinaleta athari chungu nzima katika jamii. Hatimaye, msanii anahitimisha kwa kuwatahadharisha wanajamii kutokana na hadaa hizi katika mshororo $M_{10}$ anaposema *kengwai matumbi ma kwelo niumina mathina ma nthi ino (*Mdanganywe $W_5$ mayai ya kware yatamaliza shida za nchi hii) na kubainisha wazi kuwa mayai ya kware ni mayai kama yale mengine. Msanii kama kipaaza sauti cha jamii anatoa kauli hii ili

kuitahadharisha jamii yake kuhusu tabia hasi ya ulaghai wa kiuchumi ambayo itachangia kuporomoka kwa utaifa wa jamii ya Akamba.

Msanii anaendeleza suala la utapeli wa kiuchumi linalokumba taifa la Akamba kupitia wimbo $W_{24}CH_{UK}$. Jamii ya Akamba inakandamizwa na wanajamii kutoka jamii zingine nchini Kenya. Anaona kuwa ujenzi wa utaifa wao umo hatarini kwa vile jamii jirani zinawaingiza katika biashara za kitapeli. Maingiliano kati ya jamii ya Akamba na jamii ya Agikuyu inaonekana kuididimiza jamii ya Akamba kiuchumi na hivyo kuathiri ujenzi wa utaifa wao. Katika wimbo huu anasimulia jinsi mhusika Wambui wa Njoroge alivyomwandama ili wafanye biashara ya kuuza stovu za mkoloni. Alimtarajia msanii atafute mtaji wa biashara hiyo ili wanunue stovu hizo Tharaka na kuziuza mjini Nairobi. Mpango huu ulitarajiwa kumletea utajiri msanii. Msanii katika $M_1$ anasema *nota wangunie kívelenge na watoloka* yaani alimwigiza kwenye mtego na akatoroka. Msanii anamlaumu mwanabiashara Wambui wa Njoroge kwa kumtapeli. Msanii anawakilisha jamii yake kwa kueleza jinsi watu nje ya taifa lao huwatapeli wanajamii wa Akamba kiuchumi na hivyo kuathiri ujenzi wa utaifa wao.

### 4.4.5 Ukosefu wa Usemi Mkuu Kisiasa

Katika wimbo $W_{18}$CHus, msanii analalamikia idadi ndogo ya wanajamii katika jamii yake. Kwa maoni yake, idadi ndogo ya wanajamii inamaanisha idadi ndogo ya wapiga kura hivyo jamii ya Akamba kukosa usemi mkuu katika siasa za kitaifa. Msanii anaona ya kwamba hali hii inaifanya jamii ya Akamba kukosa uwezo kisiasa wa kudai haki za kijamii. Uwezo huu ndio unaoiwezesha jamii kugawiwa rasilimali ambazo zinachangia maendeleo ya kijamii. Anasema:

| | |
|---|---|
| *Akamba twiiwe tuina andu M1* | Akamba, walisema, hatuna watu |
| *Mwiwie muvisi ayiumwa M2* | Mlisikia kijana wetu akitusiwa |
| *Kikavu kya siasa ndaususya M3* | Kikapu cha siasa hatuwezi jaza |

Katika wimbo huu, msanii anaona kuwa changamoto moja ya utaifa wa jamii ya Akamba ni idadi ndogo ya wapiga kura ambayo inapelekea wanajamii kukosa usemi wa kisiasa. Analalamika kuwa kiongozi wao wa kisiasa anadharauliwa kwa vile hawezi kuzoa kura nyingi za kumwezesha kuwa na usemi katika siasa za kitaifa. Iwapo kiongozi hana uungwaji mkono wa wapigaji kura, basi hawezi kuwa na usemi wa kitaifa. Iwapo wanajamii katika jamii ni wachache, basi hili lina maana kuwa hakuna uendelevu wa kizazi

kitakachoendeleza utaifa wa jamii ya Akamba. Hali hii ya idadi ndogo ya wanajamii imesababishwa na jamii kuacha utamaduni wao na kulimatia tamaduni za kigeni. Katika utamaduni wa jamii ya Akamba, watoto walichukuliwa kama utajiri wa mzee katika boma. Idadi kubwa ya watoto ilimaanisha kuwa yule mja alikuwa tajiri. Kila mwanamume alipania kupata watoto wengi ili aweze kupata heshima kuu kutoka kwa wanajamii wake. Mwanamume mwenye watoto wengi alitambulika na jamii na wakati mwingi ndiye aliyechaguliwa kuwa kiongozi wa kijamii (Mwikali, 1990). Kuwa na watoto wengi liliihakikishia jamii kuwa ilikuwa na mustakabali.

Suala la idadi chache ya watu wa jamii ya Akamba na jinsi linavyoathiri uwezo wa utaifa wao linaonekana kuwatia kiwewe wanajamii wengi akiwemo msanii. Katika mishororo $M_{9-12}$, msanii amewataja baadhi ya vigogo wa kisiasa wa Ukambani kama vile Kalonzo Musyoka (*Muvisi*), Maanzo, Muthama na Mutula wakiwarai wanajamii wa jamii ya Akamba kuzaa kwa wingi ili kuongeza nguvu za kisiasa kupitia kura. Hawa ni viongozi wa kijamii ambao wana usemi mkubwa wa kisiasa, kiuchumi na kijamii katika eneo la Ukambani. Viongozi hawa wana ufuasi mkubwa katika eneo la Ukambani. Wanasiasa hawa wanatumiwa kama kipaaza sauti katika kuwaeleza wanajamii kuhusu umuhimu wa kuongeza idadi yao ya watu. Msanii ameradidi maneno *tusyae vyu* (tuzae kabisa) ili kusisitiza umuhimu wa kuongeza idadi ya watu katika jamii ya Akamba. Msanii anataja maeneo mbalimbali ya jamii ya Akamba ili yashirikishwe katika mchakato wa kuongeza idadi ya watu ili kuimarisha ujenzi wa utaifa wao na nafasi yao katika siasa za nchi ya Kenya.

### 4.4.6 Ukosefu wa Umoja wa Kijamii

Mojawapo ya changamoto katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba ni ukosefu wa umoja katika jamii. Tamaa na ukosefu wa uaminifu katika jamii ni vyanzo vikuu vya kuvuruga utaifa wa jamii ya Akamba. Katika wimbo $W_6CH_{UJ}$, msanii anabainisha kuwa asasi za kijamii zimo katika hatari ya kusambaratika kutokana na mawi haya matatu: tamaa, ukosefu wa umoja na kudidimia kwa uaminifu miongoni mwa wanajamii. Msanii anatumia jazanda ya sungura na ndovu kuwakilisha viongozi na wanajamii wa jamii ya Akamba. Sungura anawakilisha wananchi wa kawaida katika jamii ya Akamba ambao hutegemea viongozi kutatua matatizo yao. Katika mshororo $M_1$, Sungura anaomba msaada wa Ndovu

ili avuke mto wenye kina kirefu. Hii ni jazanda ya jinsi wananchi wanavyowaomba viongozi wenye tajiriba ushauri wa kufaulu maishani. Katika mshororo $M_{2-6}$, Ndovu anamtahadharisha Sungura kwamba mto wanaouvuka una kina kirefu kisha anambeba mgongoni na kumvusha upande wa pili. Masimulizi haya yanaonyesha jinsi viongozi wenye tajiriba huwasaidia wananchi wenzao katika jamii katika kutatua matatizo ya kijamii. Katika mshororo $M_{10}$, wanapofika ng'ambo ya mto, Sungura anamkejeli Ndovu na kumweleza kwamba hakuna jambo kubwa ametanda. Sungura katika muktadha huu ni kielelezo cha wananchi ambao hukosa shukrani baada ya kupata msaada kutoka kwa wanajamii wenzao. Hali kama hii huvunja mshikamano wa kijamii, hatimaye kuathiri ujenzi wa utaifa wa jamii yao. Msanii anaitahadharisha jamii kuhusu wanajamii ambao huchangia utengano wa jamii ya Akamba. Anaona kuwa kuna wanajamii ambao huwakejeli viongozi wao hata baada ya viongozi hawa kuwasaidia. Hali hii inaweza kusababisha mgogoro baina ya viongozi na wanajamii ya Akamba na kudidimiza ujenzi wa utaifa wao.

Suala la umoja wa wanajamii katika ujenzi wa utaifa wa Akamba limezungumziwa na msanii katika wimbo $W_{22}CH_{UJ}$. Baadhi ya tabia za wanajamii ambazo zinaweza kuvunja muumano wa wanajamii na kusababisha kusambaratika kwa umoja wao zinabainishwa. Baadhi ya tabia hasi ambazo zinaweza kuwa changamoto katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba ni pamoja na chuki, ulafi, ubaguzi, vita vya wenyewe kwa wenyewe na ubinafsi wa viongozi ambazo zinajitokeza katika simulizi hii. Katika wimbo huu, msanii anasimulia sherehe ya arusi iliyofanyika katika mji wa Kangala eneo la Kamutei. Msanii anawashutumu viongozi na wageni wengine waalikwa wa jamii ya Akamba kwa kuzua vurugu katika hafla hiyo. Katika mshororo $M_{11}$, msanii anamlaumu kiongozi Teke kwa kulewa na kupigana na dereva wake Malima. Vile vile, katika mshororo $M_{16,}$ anamshtumu kiongozi mwingine, Jambo kwa kutowajibika katika sherehe hiyo.

Msanii katika mshororo $M_{21}$ amekerwa na kiongozi Tom Luusa kwa kumzaba kofi mwanamume mmoja katika sherehe hiyo na kumwonya kwamba kama kiongozi, hakustahili kuzua vurugu. Katika mshororo $M_{26}$, wahusika Kinyonyo na Mercy wanasawiriwa kama wabaguzi na walafi kwa sababu walimbagua na kumnyima nyama ya ng'ombe iliyochinjwa katika sherehe. Sherehe na ng'ombe ni jazanda ya shughuli za

kujenga utaifa na ugamvi wa rasilimali za kijamii. Msanii anaona kwamba ili shughuli hii iweze kuwa kamilifu, kila mwanajamii anafaa kushirikishwa bila kubaguliwa. Viongozi pa wanastahili kuhakikisha kuwa hawachochei vita vya wenyewe kwa wenyewe miongoni mwa wanajamii wenzao. Viongozi pia anapaswa kuhakikisha kwamba rasilimali zimewafikia wanajamii pasi na ubaguzi. Ili kujenga utaifa wa jamii, msanii anaonyesha sifa hasi kama vile ulafi, kutowajibika, ubinafsi na ubaguzi hazifai kuwepo katika jamii ya Akamba kwa vile husababisha utengano wa wananchi.

### 4.4.7 Siasa za Utengano

Wimbo $W_{17}CH_{SU,}$ ni uhakiki wa changamoto zinazoletwa na suala la siasa na uongozi nchini Kenya, hasa namna zinavyoathiri jamii ya Akamba. Msanii anajaribu kubainisha utengano ambao huchipuka pindi tu kunapokuwa na suala la uchaguzi nchini.

| | |
|---|---|
| *Sya katiba mwamina L1* | Za katiba mkamaliza |
| *Mweka nesa mwamina L2* | Mmefanya vizuri kumaliza |
| *Yes - No unai thina L3* | Ndio-La ilikuwa shida |
| *Siasa mbingi sya thina L4* | Siasa mingi za shida |
| *Katiba myau L5* | Katiba gani |
| *Thina ungi niwaambia* | Shida nyingine imeanza |
| *Tusker nimwavandia L20* | Bei ya Tusker imepanda |
| *Nzovi bar niwavandia L21* | Bei ya pombe kwenye baa imepanda |

Kunachipuka utengano unaotokana na shughuli ya kupitisha mswada wa katiba mpya nchini Kenya mwaka wa 2005. Wakenya walitakiwa kufanya maamuzi ya *Yes/No* (Ndio/La) kuhusu kupitishwa kwa mswada ambao ungekuwa katiba mpya nchini Kenya. Shughuli hii ilichangia pakubwa changamoto za kijamii, kisiasa na kiuchumi ambazo ziliathiri utaifa wa jamii ya Akamba. Akishadida kauli hii, Lynch (2006) anasema kuwa kabla ya kufanyika kwa kura ya maoni kuhusu mswada wa katiba mpya nchini Kenya, uchambuzi wa kura ya maoni ambayo ilidhibiti mijadala ya umma na ya kibinafsi mara moja ulipata mantiki ya kikabila kwani makabila yalibainishwa kama 'machungwa', 'ndizi' au kugawanywa. Picha iliyoenea ilikuwa ya jamii zikimuunga mkono na kumfuata kigogo wao wa kikabila.

Katika eneo la Ukambani, kwa mfano, Kalonzo Musyoka, ambaye alikuwa kiongozi wa chama cha (LDP) alijitokeza kupinga Charity Ngilu (NAK) ambaye alikuwa akiunga mkono rasimu ya Wako. Hata hivyo, wakati Kalonzo alidai kuwa rasimu ya Wako ilikuwa

na dosari na ingeleta athari mbaya za muda mrefu kwa Wakamba, Ngilu alitumia mbinu tofauti. Ingawa viongozi hawa wawili kutoka eneo la Ukambani waliweka maslahi ya Wakamba katika kiini cha misimamo yao, utengano mkubwa ulibainika kati ya wafuasi wao. Ngilu alifanya msururu wa mikutano na Kibaki katika Ikulu, Nairobi, ambako alijitokeza kuwa mfuasi wa wazi wa upande wa 'ndizi', huku pia akijivunia ahadi za rais kuhusu misaada ya njaa na miradi ya maendeleo kwa Ukambani, mafanikio ya moja kwa moja ya ushirikiano wa Ngilu na serikali ya Mwai Kibaki. Wale ambao hawakushirikiana na serikali walitengwa na maeneo yao kuathiriwa kimaendeleo (Lynch. 2006). Hali hii ndiyo msanii anayoirejelea kama *siasa mbingi sya thina* (siasa nyingi za shida). Umoja wa jamii ya Akamba uliathiriwa na ubabe wa kisiasa pamoja na misimamo kinzani ya kisiasa ya viongozi hawa wawili wa kisiasa kutoka eneo la Ukambani. Msanii anaeleza katika mshororo $M_{6-12}$ jinsi utengano katika jamii ya Akamba ulivyotokea kutokana na kielelezo cha katiba katika sekta mbalimbali za kijamii kama vile: makanisa, vituo vya redio, magazeti na hata kisiasa kupitia uradidi wa maneno *inai thina* (ilikuwa shida).

Jamii iliathirika kidini wakati waumini walipochukua misimamo tofauti ya kisiasa kuhusu katiba kielelezo. Kuna wale waliounga mkono upande wa serikali wa 'ndizi' na wengine upande wa upinzani wa 'chungwa'. Wakati mwingine makabiliano makali yangetoea hata katika sehemu za kuabidu. Utengano baina ya wanajamii ya Akamba ulidhihirika kupitia matamshi ya viongozi wa kisiasa na vyombo vya habari. Badala ya viongozi hawa na vyombo vya habari kueneza upendo naumoja wa wanajamii, wao walichochea chuki na uhasama ambao ulikwamiza ujenzi wa utaifa wa jaii ya Akamba. Kilikuwa kipindi kigumu sana kisiasa kwa wanajamii wa Ukambani ambao walitenganishwa kutegemea ni kigogo yupi waliyemwuuga mkono. Chuki ilipenya baina ya wanajamii na wakati mwingine miongoni mwa ndugu katika familia, watu ambao hapo awali walikuwa wameshikana kwa upendo wakatenganishwa na siasa za kura ya maoni kuhusu katiba mpya. Utaifa wa jamii ya Akamba ukayumbishwa pakubwa na misimamo tofauti tofauti ya kisiasa ya wanajamii.

Anwani ya wimbo $W_{17}CH_{SU}$ ni kejeli kwa shughuli nzima ya kupigia kura katiba kielelezo. Maneno *katiba myau*? yanaonyesha kwamba jamii ya Akamba haikuhusishwa katika mchakato wa kuandika katiba kielelezo. Wale viongozi kutoka jamii ya Akamba walioipendekeza wameisaliti jamii yao na kusababisha mgawanyiko wa jamii ya Akamba.

Jamii yenye utaifa hushiriki shughuli za kikatiba kwa pamoja bila ubaguzi. Katiba ya nchi yoyote inastahili kuwaunganisha watu. Huwa ni mojawapo wa mambo yanayochangia utaifa wa taifa. Iwapo suala la kupitisha katiba mpya litaleta utengano wa jamii, basi huwa halina manufaa yoyote na ni shughuli ambayo inastahili kukoma mara moja. Kutokana na kampeni za *Yes/No*, jamii ya Akamba imeathirika kiuchumi. Katika mshororo $M_{20-21}$ bei ya bidhaa muhimu kwa wananchi kama vile pombe aina ya Tusker imepanda. Hili linaathiri jamii yake kwani hawana uwezo wa kununua bidhaa nyingi. Msanii anabainisha kuwa biashara za kibinafsi hazikusazwa na utengano huu kwa mfano, katika $M_{21}$ biashara ya baa iliathirika. Hili ni kutokana na mlengo wa kisiasa ambao biashara hizo zilikuwa zinaunga mkono. Wakati hali ya kiuchumi ya jamii inadorora basi utaifa wa jamii hiyo huwa katika hatari ya kuangamizwa. Misimamo tofauti kuhusu katiba kielelezo ilisababisha utengano baina yao na kuipelekea jamii ya Akamba kukosa utaifa wa jamii.

### 4.4.8 Usaliti wa Kisiasa

Utaifa wa jamii ya Akamba unadhalilishwa na usaliti wa kisiasa. Wanajamii wanaona kwamba wamesalitiwa na viongozi wa kisiasa ambao waliwachagua. Katika wimbo $W_7CH_{SL}$, msanii anachukua nafasi ya kuwa kipaaza sauti cha jamii yake. Anamsuta kiongozi huyu kwa kuwatelekeza waliompigia kura. Anasema kuwa kiongozi huyu alitoa ahadi chungu nzima ambazo alisema angetekeleza mara tu baada ya kuchaguliwa na wananchi ila hajatimiza hata moja. Msanii analalamikia hali hii kwamba wanajamii walimchagua ili alete maendeleo kwao lakini bado wanateseka. Anasema katika mishororo $M_{1-8}$:

| | |
|---|---|
| *Munene wambiie tukambeini M1* | Mkubwa ulisema tufanye kampeni |
| *Nikenda kivila kyuke kwitu M2* | Ndio tupate uongozi |
| *Munene wambiie we ukanzuvia M3* | Mkubwa ulisema utanitunza |
| *Oila kivila kiuka kwitu M4* | Utakapopata cheo kije kwetu |
| *Kivila niwoosie na nyie ndwanzuvia M5* | Ulipata cheo na ukasahau mambo yangu |
| *Kivila ni twosie na we mwa niwaie M6* | Kiti tulichukua na wewe hupatikani |
| *Ninguseng'a na ngekulya ii munene weM7* | Nashangaa na kujiuliza mkubwa mbona hivi |
| *Kowolilwe (wiper) M8* | Kwani ulisahau (wiper) |

Suala la utaifa wa jamii ya Akamba limewasilishwa kupitia mshororo $M_6$ ambapo anatumia nafsi ya kwanza wingi kuonyesha kwamba walishirikiana katika kumchagua kiongozi

ambaye anawasaliti kwa kuwatoroka. Baadhi ya ahadi ambazo kiongozi huyu alitoa ni kwamba angewatunza wanajamii katika mshororo $M_3$. Kutunza jamii ni kuhakikisha kwamba mahitaji yao ya kimsingi yameshughulikiwa kama vile kuwepo kwa miundo misingi, huduma za kiafya na kielimu karibu nao. Katika mshororo $M_4$, kiongozi huyu aliwaahidi kuwa haya yote yangepatikana iwapo hicho cheo kingekuja kwa jamii ya Akamba. Anahimiza jamii yake kumchagua kwani kungewaletea yeye na jamii ya Akamba nguvu nyingi za kisiasa. Msanii analalamika kwamba baada ya kiongozi kupata ule wadhifa wananchi hawajafaidika na bado wanateseka. Msanii anahisi kwamba jamii ya Akamba imesalitiwa na kiongozi ambaye hajatimiza ahadi alizotolea wananchi. Baada ya kuchaguliwa, kiongozi aliwasahau wananchi, akawatoroka na hajawatunza hivyo wananchi wanaendelea kuteseka. Katika matini hii, mpiga kura ameamua kusemezana moja kwa moja na uongozi wa kisiasa. Badala ya kutoa lawama kwa serikali kuu, ameona chanzo cha masaibu yake ni viongozi ambao alichagua. Anawakumbusha viongozi kuhusu majukumu yao kwa wanajamii ambao waliwapa nyadhifa wanazofurahia. Msanii anabainisha usaliti wa viongozi kwa kutowajibika kama njia ya kuzuia ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inajadili muhtasari wa tasnifu na matokeo ya utafiti. Vile vile, katika sura hii, mapendekezo kuhusu tafiti ambazo zinaweza kufanywa baadaye yametolewa. Katika tasnifu hii, tulidhamiria kuhakiki na kuchambua nyimbo pendwa za Ken wa Maria ili kubainisha namna utaifa wa jamii ya Akamba unavyojitokeza. Isitoshe, tasnifu hii ilishughulikia madhumuni matatu ambayo ni kuchunguza arki za utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria, kuhakiki mbinu za kimtindo zinazotumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria na kupambanua changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba kwa mujibu wa nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria. Uchunguzi huu uliongozwa na nadharia ya utaifa pamoja na nadharia ya umitindo. Mihimili ya nadharia ya utaifa iliyoongoza utafiti huu ni: wananchi katika taifa ni lazima wawe na uhusiano wa kitamaduni na kutumia lugha moja, wananchi ni lazima wakubali mafundisho au itikadi ya taifa lao bila kuwa na uhusiano wowote na mafundisho ya taifa lingine linaloshindana na taifa lao pamoja na wananchi katika taifa kuwa na imani moja kwa mizimu na miungu. Kiwango cha semantiki katika nadharia ya umitindo kiliwezesha utafiti huu kuhakiki mbinu za kimtindo alizotumia msanii kujenga utaifa wa jamii ya Akamba. Katika juhudi za kushughulikia suala hili, tasnifu hii imegawika katika sura tano. Sura ya kwanza imefafanua usuli wa suala la utafiti. Aidha, sura hii imeangazia madhumuni na maswali yaliyoongoza utafiti huu pamoja na dhima ya utafiti. Aidha, upeo na mipaka ya utafiti ilibainishwa.

Sura ya pili inahusu maandishi na tafiti zinazohusiana na mada ya utafiti. Kazi mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti huu zilihakikiwa katika sura hii. Kupitia uhakiki wa kazi hizi, ilibainika kuwa tafiti tangulizi zilizoshughulikia utaifa pamoja na nyimbo pendwa zimejikita katika uhakiki wa maudhui, dhamira, mtindo na lugha kama mada mahususi. Hakukuwa na data ya kutosha kuhusu tafiti zilizozingatia nyimbo za msanii Ken wa Maria

zikiwa na nia ya kubainisha utaifa wa jamii ya Akamba. Hivyo basi, utafiti huu ulifidia pengo hilo. Katika sura hii, nadharia ambazo ziliongoza utafiti huu zilifafanuliwa. Mihimili ya nadharia hizi ambazo utafiti huu uliegemea ziliwekwa wazi.

Sura ya tatu nayo iliangazia mbinu za utafiti zilizotumiwa katika ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Aidha, iliangazia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti pamoja na shughuli ya usampulishaji. Vile vile, maadili wakati wa utafiti yalishughulikiwa.

Katika sura ya nne, nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria zilichanganuliwa. Katika kufanya hivi, nyimbo zilihakikiwa kulingana na malengo ya utafiti. Nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria ziliandikwa kwa lugha asili ya Kikamba kisha kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Malengo ya utafiti huu yalikuwa matatu: kuchunguza arki za utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria, kuhakiki mbinu za kimtindo zinazotumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria na kupambanua changamoto zinazokumba utaifa wa jamii ya Akamba kwa mujibu wa nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria.

Sura ya tano inahusu muhtasari wa tasnifu, muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo ya utafiti yametolewa katika nyanja za fasihi simulizi hasa utaifa wa jamii katika nyimbo pendwa. Muhtasari wa kila madhumuni umetolewa pamoja na masuala muhimu yaliyoibuka katika mijadala ya sura hizo. Matokeo ya utafiti yametolewa kwa mujibu wa malengo ya utafiti na misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu.

### 5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria. Baada ya kuchanganua nyimbo teule za msanii huyu, madhumuni pamoja na maswali yaliyoongoza utafiti yalijibiwa. Madhumuni ya kwanza yalikuwa kuchunguza arki za utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo teule za Ken wa Maria. Baada ya kuchanganua maudhui ya nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria, ilibainika kwamba nyimbo hizi zilisheheni arki za utaifa wa jamii ya Akamba. Baadhi ya arki za utaifa wa jamii ya Akamba zilizobainika ni pamoja na arki ya utamaduni wa jamii ya Akamba, arki ya utambulisho, arki ya siasa na uongozi, arki ya jiografia na arki ya historia.

Kuhusu arki ya utamaduni wa jamii ya Akamba, utafiti huu ulibaini kwamba kupitia kwa nyimbo pendwa za Ken wa Maria, tamaduni zifuatazo zilijitokeza: ndoa, itikadi za jamii, utamaduni wa vyakula pamoja na shughuli za kiuchumi. Kuhusu ndoa, utafiti huu ulibaini kuwa kuna hatua muhimu ambazo zinastahili kuzingatiwa wakati wa kufunga ndoa. Kuna sheria ambazo zimewekwa na wanajamii wa jamii ya Akamba kuhusu posa na ndoa. Sheria hizi zimekuwapo tangu awali na zinastahili kudumishwa. Namna ya kuendesha shughuli hii muhimu ya posa na ndoa imewekwa wazi kupitia nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria. Aidha, aina za ndoa ambazo zinakubalika katika jamii hii pia zimewekwa wazi.

Utafiti huu ulibaini kuwa jamii ya Akamba ina itikadi zake. Wakamba walikuwa na dini yao hata kabla ya majilio ya wakoloni. Walikuwa na imani katika mizimu na miungu. Walikuwa na imani na itikadi zao ambazo walizingatia. Ushirikina ni taasisi iliyo hai katika utamaduni wa jamii ya Akamba. Jamii ya Akamba inaamini kuwepo kwa nguvu kuu ambazo huendesha ulimwengu. Nguvu hii ni ya kiajabu na hupatikana tu kupitia mizimu na binadamu wateule ambao huwa na uwezo wa kuzidhibiti nguvu hizi.

Utamaduni mwingine wa jamii ya Akamba ambao ulijitokeza katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria ni wa vyakula. Ilibainika kwamba kuna vyakula spesheli ambavyo huandaliwa na wanajamii wa jamii hii wakati wa sherehe muhimu. Vyakula hivi ni pamoja na *muthokoi* na pombe ya kiamaduni aina ya *kaluvu*. Sherehe ambazo zilioanishwa na matumizi ya vyakula hivi ni pamoja na ndoa na mazishi. Si kila mwanajamii ambaye alikuwa na ruhusa ya kushiriki vyakula hivi.

Utamaduni wa shughuli za kiuchumi pia ulibainika katika nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria. Kabla ya majilio ya wakoloni, jamii ya Akamba ilishiriki katika shughuli nyingi za kiuchumi kama vile uchongaji, utengenezaji wa mizinga ya nyuki, utengenezaji wa mapambo wakitumia madini aina ya chuma na pia biashara ya uhunzi. Shughuli hizi za kiuchumi bado zinaendelea kutekelezwa hadi sasa. Jamii ya Akamba ingali inashiriki katika biashara na makabila jirani hasa uuzaji wa vyuma vikuukuu.

Arki ya utambulisho ilibainika katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria. Utafiti huu ulibaini aina mbili za uambulisho: utambulisho wa kijamii na utambulisho wa kiuana. Utambulisho wa kijamii ni ule upekee wa jamii ambao unabainishwa kwa misingi ya

kitamaduni ambayo iko tofauti na misingi ya tamaduni zingine. Utambulisho wa jamii ya Akamba unajitokeza kupitia nyimbo teule za Ken wa Maria. Msanii ametumia nyimbo zake kujenga taadhima ya jamii ya Akamba, umoja miongoni mwao na kutambulisha kundi hilo huku akichangia ujenzi wa utaifa wa kitamaduni wa jamii yake. Utambulisho wa kiuana pia unabainika. Msanii anampa mwanamke utambulisho katika jamii ambayo inaongozwa na mfumo dume. Anawasawiri wahusika wanawake ambao wanashiriki katika ujenzi wa taifa lao. Anawakoleza sifa chanya sufufu kama vile wenye bidii kazini, wenye msimamo thabiti, wanaotunza familia zao na hata kuleta mshikamano wa kijamii. Wanawake wanakuwa kichocheo cha mabadiliko chanya katika jamii ya Akamba.

Kupitia kwa kazi yake, msanii amesawiri michakato yote ya kisiasa katika jamii yake. Msanii amebainisha wanasiasa ambao wamechangia pakubwa mfumo wa kisiasa wa jamii ya Akamba. Ameweka wazi siasa na historia ya jamii ya Akamba na mchango wao katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba na taifa la Kenya kwa jumla.

Arki ya jiografia ya taifa la Akamba inajitokeza katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria. Uhusiano kati ya ikolojia ya awali na ya sasa na athari zake kwa jamii ya Akamba unawekwa wazi. Isitoshe, historia ya jamii na shughuli walizoshiriki kihistoria inasimuliwa kupitia nyimbo pendwa za Ken wa Maria. Msanii anarejelea nyakati muhimu katika historia ya jamii ya Akamba. Kwa mfano, wakati Kalonzo Musyoka, ambaye ni kiongozi wa Kisiasa wa jamii ya Akamba anapoteuliwa naibu wa rais nchini Kenya mwaka wa 2007/2008 na kuchangia kupungua kwa joto la kisiasa ambalo lilikuwa limesababisha vita vya kikabila nchini. Kipindi kingine cha kihistoria ambacho kilikuwa na athari kubwa kwa utaifa wa jamii ya Akamba na ambacho msanii amekiangazia ni kile cha kupitisha mswada wa katiba mpya nchini Kenya, cha mwaka wa 2005. Msanii anaona kwamba umoja wa jamii ya Akamba ulitiwa kwenye mizani na kuyumbishwa kwani kuliimbuka utengano mkuu katika kila sekta ya jamii ya Akamba. Msanii anaona kwamba shughuli muhimu kama hii ya kitaifa ya uundaji wa katiba mpya haifai kuwatenganisha wanajamii bali inapaswa kuwaunganisha.

Madhumuni ya pili yalikuwa kuhakiki mbinu za kimtindo zinazotumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria. Utafiti huu ulibaini kuwa msanii amehusisha mbinu anuwai ambazo zimetumika katika kupitisha ujumbe kuhusu

ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Mbinu hizi ni pamoja na usimulizi, takriri, chuku, misemo, methali na jazanda. Mbinu zingine za kimtindo ambazo zimetumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba ni aforisimu, taswira, ulinganuzi na mgotanisho, majazi na motifu.

